

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HALI YA UCHUMI WA
TAIFA KATIKA MWAKA
2019**

Kimetolewa na:
Wizara ya Fedha na Mipango
DODOMA - TANZANIA
Mei, 2020

HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2019

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI	IX
KIREFU/TAFSIRI YA MANENO	XV
SURA YA I.....	1
HALI YA UCHUMI WA TAIFA.....	1
UKUAJI WA UCHUMI.....	1
MWENENDO WA BEI.....	7
UKUZAJI RASILIMALI	10
SURA YA 2	36
FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA	36
UJAZI WA FEDHA.....	36
MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA	38
MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF).....	41
MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF).....	41
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)	42
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)	43
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA TANZANIA (TIRA)	44
MWENENDO WA SOKO LA MIKOPO YA NYUMBA TANZANIA	46
BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO TANZANIA	47
BENKI YA TPB	48
SOKO LA BIDHAA TANZANIA.....	48
SURA YA 3	54
FEDHA ZA SERIKALI	54
UTANGULIZI	54
MAPATO YA NDANI.....	55
MISAADA NA MIKOPO NAFUU.....	55
MIKOPO YA NDANI.....	56
MIKOPO YENYE MASHARTI YA KIBIASHARA.....	56
MATUMIZI	56
DENI LA SERIKALI	58
DENI LA NJE	59
DENI LA NDANI	60
TATHMINI YA UHIMILIVU WA DENI	61
SURA YA 4	67
SEKTA YA NJE	67
BIDHAA ZILIZOUZWA NJE	67
BIDHAA ASILIA	67
BIDHAA ZISIZO ASILIA	69
MAPATO YA HUDUMA	71
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE	71
MALIPO YA HUDUMA	72
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI DUNIANI	72

MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE	76
SURA YA 5	92
HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA	92
UKUAIJI WA UCHUMI.....	92
MWENENDO WA BEI.....	93
USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA.....	94
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI	95
JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA.....	96
UMOJA WA AFRIKA	96
SURA YA 6	97
RASILIMALI WATU	97
IDADI YA WATU	97
MGAWANYIKO WA WATU KIMKOA.....	97
NGUVU KAZI NA AJIRA	98
WAKALA WA HUDUMA ZA AJIRA TANZANIA	99
SURA YA 7	103
UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI	103
USAJILI WA MIRADI YA UWEKEZAJI.....	103
MGAWANYIKO WA USAJILI WA MIRADI KISEKTA	103
MGAWANYIKO WA MIRADI KIMKOA.....	104
UWEKEZAJI BINAFSI KUTOKA NJE	105
UWEKEZAJI WA MOJA KWA MOJA NA HISI.....	106
UWEKEZAJI MWINGINE	106
AJIRA KUTOKANA NA UWEKEZAJI WA MOJA KWA MOJA	106
URAHISI WA KUWEKEZA NA KUFANYA BIASHARA NCHINI	107
UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI	107
USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI.....	108
UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI.....	109
SURA YA 8	111
MASUALA MTAMBUKA	111
UKIMWI	111
MAZINGIRA	111
ULINZI NA USALAMA WA RAIA	113
MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA	115
WAKALA WA USAJILI, UFLILISI NA UDHAMINI.....	116
UTAWALA BORA	116
SURA YA 9	118
HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU	118
UTANGULIZI	118
VIASHIRIA VYA UMASKINI	118
UMASKINI WA KIPATO.....	118
UMASKINI USIO WA KIPATO.....	118
UMILIKI WA AKAUNTI ZA BENKI.....	119

HALI YA MAKAZI	119
UMILIKI WA MALI	119
HUDUMA YA MAJI.....	120
MATUMIZI YA NISHATI.....	121
MAENDELEO YA WATU	122
SURA YA 10	124
UTANGULIZI	124
TAFITI ZILIZOWAHI KUFANYIKA	124
UTAFITI WA SEKTA ISIYO RASMI WA MWAKA 2019 KWA MKOA WA DAR ES SALAAM	125
MGAWANYIKO WA WAMILIKI KATIKA SEKTA ISIYO RASMI.....	126
MAENEKO YA KUFANYIA BIASHARA	129
UWEKEZAJI WA MITAJI.....	129
AJIRA KATIKA SEKTA ISIYO RASMI	130
PATO GHIFI NA ONGEZEO LA THAMANI.....	131
MCHANGO WA SEKTA ISIYO RASMI KWENYE PATO LA MKOA WA DAR ES SALAAM	132
UHUSIANO KATI YA SEKTA ISIYO RASMI NA SEKTA NYINGINE	134
CHANGAMOTO KATIKA SEKTA ISIYO RASMI NA NAMNA YA KUZITATUA.....	136
HITIMISHO.....	138
SURA YA 11	141
KILIMO NA USHIRIKA	141
KILIMO	141
UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA.....	141
UZALISHAJI WA MAZAO YA BIASHARA	142
UZALISHAJI WA MAZAO YA BUSTANI.....	142
UZALISHAJI WA MAZAO YA MBEGU ZA MAFUTA.....	143
MWENENDO WA BEI NA MASOKO YA MAZAO YA KILIMO	143
UWEKEZAJI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA KILIMO.....	144
VYUO VYA MAFUNZO YA KILIMO	144
UTAFITI	145
MFUKO WA PEMBEJEZO.....	145
UMWAGILIAJI	145
MIFUGO	146
UZALISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE.....	146
UZALISHAJI WA MALISHO NA UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA MIFUGO	147
BIASHARA YA MIFUGO NA MAZAO YAKE	148
VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO	150
UTAFITI WA MIFUGO	151
HUDUMA ZA UGANI KATIKA KILIMO NA MIFUGO	151
MAENDELEO YA USHIRIKA	152
UVUVI.....	152
USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI.....	153
UZALISHAJI WA SAMAKI, VIFARANGA VYA SAMAKI NA VIUMBWE WAKUZWAO KWENYE MAJI	153

MWENENDO WA UVUNAJI WA RASILIMALI ZA UVUVI.....	154
UDHIBITI WA UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI	155
UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI	155
MWENENDO WA UUZAJI NA UINGIZAJI WA MAZAO YA UVUVI NJE YA NCHI	156
SURA YA 12	169
MALIASILI NA UTALII	169
MISITU NA NYUKI	169
WANYAMAPORI.....	170
UTALII.....	171
MALIKALE.....	173
SURA YA 13	181
MADINI	181
UTAFUTAJI MADINI.....	181
UUZAJI WA MADINI.....	181
ALMASI	181
DHAHABU.....	181
VITO VYA THAMANI.....	182
MAKAA YA MAWE	182
TANZANITE GHAFI.....	183
MADINI MENGINE	183
UONGEZAJI THAMANI MADINI	184
MASOKO YA MADINI.....	184
SURA YA 14	187
VIWANDA NA BIASHARA	187
UZALISHAJI KATIKA BAADHI YA VIWANDA NCHINI.....	187
UENDELEZAJI WA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO.....	187
MIUNDOMBINU YA MASOKO YA BIDHAA ZA MAZAO NA MIFUGO	188
USAJILI WA BIASHARA NA VIWANDA	189
MAONESHO YA KIBIASHARA YA KIMATAIFA	189
UDHIBITI WA UBORA WA VIWANGO NA VIPIMO.....	190
UDHIBITI WA BIDHAA BANDIA	191
SHIRIKA LA MAENDELEO LA TAIFA (NDC)	191
MAMLAKA YA MAENEKO MAALUM YA UWEKEZAJI	191
SURA YA 15	200
UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI.....	200
UJENZI.....	200
MTANDAO WA BARABARA NCHINI.....	200
MATENGENEZYO YA BARABARA, MADARAJA, VIVUKO NA MAGARI	201
MTANDAO WA BARABARA ZILIZO CHINI YA TARURA	202
BODI YA MFUKO WA BARABARA	203
WAKALA WA NYUMBA NA MAJENGZO YA SERIKALI	203
BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI	204
BODI YA USAJILI WA WAHANDISI	204

BODI YA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI	205
BARAZA LA TAIFA LA UJENZI.....	206
MAENDELEO YA ARDHI.....	206
UTAYARISHAJI WA HATIMILIKI, UKAGUZI, NA UHAKIKI MILKI	206
USAJILI WA HATIMILIKI NA NYARAKA ZA KISHERIA.....	207
UTHAMINI WA MALI KWA MADHUMUNI MBALIMBALI	208
UPIMAJI WA MASHAMBA NA VIWANJA	208
MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI.....	209
URASIMISHAJI MAKAZI HOLELA	210
MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA.....	210
MAENDELEO YA MAKAZI	210
UJENZI WA NYUMBA ZA MAKAZI NA BIASHARA	210
SURA YA 16	211
MAWASILIANO NA UCHUKUZI	211
UCHUKUZI.....	211
USAFIRI WA BARABARA	211
USAFIRI WA MAJINI.....	212
USAFIRI WA RELI.....	213
SHIRIKA LA RELI TANZANIA.....	213
MAMLAKA YA RELI YA TANZANIA NA ZAMBIA.....	213
USAFIRI WA ANGA.....	214
MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA	214
KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA	216
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA	217
MUDA WA MELI KUKAA BANDARINI	219
SHEHENNA ZA NCHI JIRANI	219
UCHUKUZI KWENYE MAZIWA.....	220
KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI	220
KAMPUNI YA MELI YA CHINA NA TANZANIA	220
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA	220
UDHIBITI WA MIONZI	221
HUDUMA ZA MAWASILIANO.....	222
HUDUMA ZA POSTA.....	222
HUDUMA ZA SIMU	223
HUDUMA ZA INTANETI	223
HUDUMA ZA UTANGAZAJI.....	224
UTOAJI WA LESENI ZA MAWASILIANO	224
MKONGO WA TAIFA WA MAWASILIANO.....	225
SEKTA YA HABARI	225
MAENDELEO YA SANA'A	226
BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA.....	226
MAENDELEO YA MICHEZO	227
SURA YA 17	237

NISHATI	237
UFUAJI WA UMEME	237
UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI.....	240
GESI ASILIA.....	240
UAGIZAJI MAFUTA	242
MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA.....	244
NISHATI JADIDIFU	246
NISHATI MBADALA YA LPG.....	246
NISHATI YA MIONZI YA JUA	247
SURA YA 18	248
MAJI.....	248
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI.....	248
HUDUMA YA MAJI VIJJINI	249
HUDUMA ZA MAJI MIJINI	250
UCHIMBAJI WA VISIMA	250
UONDOAJI WA MAJITAKA.....	251
SURA YA 19	254
ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA.....	254
ELIMU YA AWALI	254
ELIMU YA MSINGI	254
ELIMU YA SEKONDARI.....	255
ELIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU	255
UKAGUZI WA SHULE NA VYUO VYA UALIMU.....	256
ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO	256
ELIMU YA UFUNDI STADI NA VYUO VYA MAENDELEO YA WANANCHI.....	256
ELIMU YA JUU	257
TEKNOLOJIA NA UBUNIFU	257
SURA YA 20	264
AFYA NA MAENDELEO YA JAMII.....	264
AFYA	264
VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA.....	264
HUDUMA ZA AFYA KWA WATOTO CHINI YA MWAKA MMOJA.....	264
UPATIKANAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA	265
AFYA YA UZAZI NA MTOTO	265
UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA	266
UDHIBITI WA MALARIA	267
MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA KIFUA KIKUU	267
LISHE.....	268
MAFUNZO KWA WATUMISHI WA KADA YA AFYA	268
MAENDELEO YA JAMII	268
MAFUNZO YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII	268
MAENDELEO YA WANAWAKE	269
HUDUMA ZA USTAWI NA MAENDELEO YA WATOTO	270

HUDUMA ZA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO	271
HUDUMA ZA USTAWI KWA WAZEE	271
MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI	271

Ukurasa**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali A:	Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara	xviii
Jedwali B:	Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2013 – 2019.....	xix
Jedwali 1:	Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika)	12
Jedwali 1A	Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika)	13
Jedwali 2:	Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika).....	14
Jedwali 2A:	Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko- Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika)	15
Jedwali 2B:	Pato la Taifa (PLT) na Matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za miaka inayohusika)	16
Jedwali 3:	Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015)	17
Jedwali 3A:	Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Kwa Bei za mwaka 2015)	18
Jedwali 4:	Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015)	19
Jedwali 4A:	Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za mwaka 2015).....	21
Jedwali 4B:	Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za mwaka 2015).....	22
Jedwali 5:	Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (bei za miaka inayohusika).....	23

Jedwali 6:	Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (Bei za mwaka 2015).24
Jedwali 7A:	Mchango katika Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya Shughuli (Kwa Bei za Miaka inayohusika) 25
Jedwali 7B:	Ukuzaji wa Rasilimali katika Sehemu za Uchumi wa Kitaifa na Binafsi (Kwa bei za Miaka inayohusika)..... 25
Jedwali 8:	Fahirisi za bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (Des. 2015=100)..... 26
Jedwali 9:	Fahirisi za Bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini D'Salaam (Des. 2015=100) ... 27
Jedwali 10:	Fahirisi za bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (Des. 2015=100) 28
Jedwali 11:	Fahirisi ya Bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa kima cha kati D'Salaam (Des. 2015=100)..... 29
Jedwali 12:	Fahirisi ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100) 30
Jedwali 13:	Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100)..... 31
Jedwali 14:	Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2015=100) 32
Jedwali 15:	Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (Des. 2015=100) 33
Jedwali 16:	Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (Des. 2015=100) 35
Jedwali 17:	Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara 50
Jedwali 18:	Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara..... 51

Jedwali 19:	Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani	52
Jedwali 20:	Mikopo ya benki za biashara kwa Shughuli za Kiuchumi...	52
Jedwali 21:	Mwenendo wa amana katika benki za biashara	53
Jedwali 22:	Viwango vya wastani vya riba (asilimia)	53
Jedwali 23:	Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali.....	63
Jedwali 24:	Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma za Serikali (Sh. Milioni)	65
Jedwali 25:	Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (Sh. Milioni)	80
Jedwali 26:	Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh. Milioni)	81
Jedwali 27:	Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje	82
Jedwali 28:	Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh./tani).....	86
Jedwali 29:	Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US \$/tani)	87
Jedwali 30:	Aina na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za nje (Sh. Milioni)	89
Jedwali 31:	Mizania ya malipo na nchi za nje (US\$ milioni)	90
Jedwali 32:	Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa (2011-2019).....	101
Jedwali 33:	Kituo cha Uwekezaji Tanzania(TIC): Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa	110
Jedwali 34:	Uzalishaji wa miwa na sukari nchini.....	157
Jedwali 35:	Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini.....	158

Jedwali 36:	Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana.....	159
Jedwali 37:	Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini	160
Jedwali 38:	Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana.....	161
Jedwali 39:	Tumbaku iliyonunuliwa na mauzo nchini	162
Jedwali 40:	Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto nchini.....	163
Jedwali 41:	Korosho zilizonunuliwa na mauzo nchini.	164
Jedwali 42:	Muhtasari wa kiasi cha mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa	165
Jedwali 43:	Uzalishaji katika sekta ya uvuvi (2000-2019).....	166
Jedwali 44:	Mauzo ya mazao ya uvuvi nchi za nje.....	167
Jedwali 44A:	Muhtasari wa Mauzo ya Mazao ya Uvuvi Nchi za Nje....	168
Jedwali 44B:	Mwelekeo wa Mauzo ya Sangara Nje ya Nchi	168
Jedwali 45:	Idadi ya wageni walitembelea Hifadhi za Taifa na Mapato yaliyopatikana	175
Jedwali 46:	Mauzo ya bidhaa za misitu katika masoko ya nje	175
Jedwali 47:	Idadi na Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii.....	176
Jedwali 48:	Mwenendo wa Biashara ya Utalii	177
Jedwali 49:	Idadi ya watalii walioingia nchini na kiasi cha fedha kilichopatikana.....	178
Jedwali 50:	Watalii walitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.....	179

Jedwali 51:	Idadi ya wageni walitembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2015-2019	180
Jedwali 52:	Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana	185
Jedwali 53:	Madini yaliyouzwa nchi za nje (2015-2019).....	186
Jedwali 54:	Matumizi ya saruji nchini.....	193
Jedwali 55:	Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani	194
Jedwali 56:	Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa.....	195
Jedwali 57:	Viwanda - Gharama za kazi	196
Jedwali 58:	Viwanda - Muhtasari wa Matokeo	197
Jedwali 59:	Viwanda - Muhtasari wa Matokeo Kimkao	198
Jedwali 60:	Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda	199
Jedwali 61:	Shirika la Reli Tanzania (TRL)	229
Jedwali 62:	Reli ya Uhuru (TAZARA).....	230
Jedwali 63A:	Usafirishaji kwa Meli: Dar Es Salaam	231
Jedwali 63B:	Usafirishaji kwa Meli: Tanga	232
Jedwali 63C:	Usafirishaji kwa Meli: Mtwara.....	233
Jedwali 64:	Huduma za Posta	234
Jedwali 65:	Idadi ya Wanaotumia Simu za Mezani na Viganjani.....	235
Jedwali 66:	Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)	236
Jedwali 67:	Uwezo wa Mitambo ya Umeme na Kiasi cha Umeme Uliotengenezwa kwa Vituo.....	238
Jedwali 68:	Mauzo ya Umeme kwa Watumiaji Mbalimbali	239

Jedwali 69:	Mauzo ya Umeme kwa Mikoa	240
Jedwali 70:	Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji Mijini..	252
Jedwali 71:	Mahitaji na Upatikanaji wa Maji katika Miji	253
Jedwali 72:	Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato	259
Jedwali 72A:	Idadi ya wanafunzi na walimu katika shule za msingi na sekondari kwa jinsia.....	260
Jedwali 72B:	Idadi ya taasisi za elimu.....	260
Jedwali 72C:	Mafunzo ya walimu katika vyuo vya ualimu.....	261
Jedwali 72D:	Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika taasisi za elimu ya juu.....	262
Jedwali 73:	Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato	263
Jedwali 74:	Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za afya nchini	273
Jedwali 75:	Idadi ya Wagonjwa katika Vituo vya Afya.....	274
Jedwali 76:	Idadi ya Vitanda katika Hospitali zote Nchini.....	275

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

ACP	- African Caribbean and Pacific Group of State (Nchi Wanachama wa Kundi la Afrika, Karibiani na Pacific)
ART	- Antiretroviral Therapy (Dawa za Kufubaza Virusi vya Ukimwi)
ASDP	- Agricultural Sector Development Programme (Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo)
ATCL	- Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania)
BAKITA	- Baraza la Kiswahili Tanzania
BRELA	- Business Registration and Licencing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni)
COMESA	- Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika)
CHF	- Community Health Fund (Mfuko wa Jamii wa Afya)
AfCFTA	- Afican Continental Free Trade Areas (Eneo Huru la Biashara kwa Umoja wa Afrika)
EAC	- East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki)
EMS	- Express Mail Service (Huduma ya Kutuma Fedha, Nyaraka na Vifurushi vya Haraka)
EPZ	- Export Processing Zones (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje)
FAO	- Food and Agriculture Organisation (Shirika la Chakula Duniani)
f.o.b	- free on board (Thamani ya Bidhaa bila Kujumuisha Gharama za Usafiri na Bima)
HBS	- Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya)
HDI	- Human Development Index (Fahirisi ya Maendeleo ya Watu)
JICA	- Japan International Cooperation Agency (Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Japani)
IMF	- International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa)
JKT	- Jeshi la Kujenga Taifa
LPG	- Liquified Petroleum Gas (Gesi ya Kupikia Majumbani)
M ₁	- Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu)
M ₂	- Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana)
M ₃	- Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi)
MSD	- Medical Stores Department (Bohari Kuu ya Dawa)
MW	- Megawatts
NSSF	- National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii)
NDC	- National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa)
NHIF	- National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya)
NMB	- National Microfinance Bank (Benki ya Taifa ya Mikopo Midogo)
PSSSF	- Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa

	Watumishi wa Umma)
REA	- Rural Electrification Agency (Wakala wa Nishati Vijijini)
SIDO	- Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo)
SADC	- Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika)
TAKUKU RU	- Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TaESA	- Tanzania Employment Service Agency (Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania)
TAM	- Tathmini ya Athari kwa Mazingira
TANESCO	- Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Umeme Tanzania)
TANROA DS	- Tanzania Roads Agency (Mamlaka ya Barabara Tanzania)
TAWA	- Tanzania Wildlife Authority (Mamlaka ya Uhifadhi Wanyamapori)
TARURA	- Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini)
TAZARA	- Tanzania Zambia Railways Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia)
TEHAMA	- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMESA	- Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency
TEUs	- (Wakala wa Ufundis na Umeme Tanzania)
TIRA	- Twenty Equivalent Units
TICTS	- Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania)
TBS	- Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam)
TRL	- Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzani)
UKIMWI	- Tanzania Railways Company Limited (Kampuni ya Reli Tanzania)
UTT	- Unit Trust of Tanzania
VVU	- Virusi Vya Ukimwi
WCF	- Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi)
WE0	- World Economic Organisation (Shirika la Kiuchumi Duniani)

MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2019

TAREHE	MWEZI	MATUKIO
9	Februari	Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikutana na wachimbaji wa madini kusikiliza kero zao.
15	Aprili	Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizindua Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.
26	Julai	Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliweka jiwe la msingi kwenye mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere wa katika bonde la Mto Rufiji.
1	Agosti	Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizindua Jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.
14	Desemba	Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alizindua programu ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha.

TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

Jedwali Na. A

Maelezo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019p	2018/19 Badiiko (%)
Idadi ya Watu (Milioni)	44.8	46.1	47.4	48.7	51.0	52.6	54.3	3.2
Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni)	72,977,200	82,603,388	94,349,316	108,362,324	118,744,498	129,043,901	139,893,804	8.4
Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni)	83,268,117	88,874,111	94,349,316	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,175,839	7.0
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.)	1,628,955	1,793,387	1,990,492	2,225,099	2,327,395	2,452,406	2,577,967	5.1
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2015 (Sh.)	1,858,663	1,929,529	1,990,492	2,070,398	2,110,088	2,188,195	2,269,888	3.7
Kasi ya Upandaji Bei (asilimia)	7.9	6.1	5.6	5.2	5.3	3.5	3.4	-3.1
Urari wa Biashara ya Bidhaa (US\$ milioni)	-5771.1	-5723.7	-5016.3	-3589.8	-3040.95	-3853.51	-3095.86	-19.7
Urari wa Bidhaa,Huduma na Uhamisho wa Mali (US\$ milioni)	-4,988.5	-5,048.6	-4,477.4	-2,740.5	-1,827.1	-1,897.8	-1,111.9	-41.4
Sarufi Iliyotumika (Tani '000)	3,433,791	4,082,681	4,404,187	6,028,794	4,359,163	4,577,117	6,104,108	33.4
Umemu Ulipuzwa (GWH)	4,806.7	5,051.5	5,297.1	5,871.5	5,956.2	6,290.7	6,642.8	5.6
Utalii (Mapato US\$ milioni)	1,853.3	1,983.0	1,901.9	2,131.6	2,199.8	2,432.9	2,604.5	7.1
Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000)	430.0	160.0	363.6	198.0	341.0	625.0	529.0	-15.4
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) *	8231.9	8222.7	8298.3	8639.2	9317.8	10,112	10,605	4.9
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) *	1804.1	1947.3	1774.4	1807.0	1908.9	2,149	2,338	8.8
Hospitali: Idadi ya Vitanda	70,906	50,670	-	59,757	60,952	62,203	80,164	28.9
Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US\$)								
Bidhaa Asilia								
Kahawa	171.00	130.52	160.88	153.69	126.27	148.00	153.39	3.6
Pamba	111.70	52.31	28.16	46.76	36.76	68.38	91.77	34.2
Katani	16.90	16.76	26.53	17.23	28.73	32.54	34.92	7.3
Chai	56.90	57.10	47.21	44.79	49.13	45.82	45.72	-0.2
Tumbaku	307.00	137.79	214.79	339.20	195.81	269.95	146.52	-45.7
Korosho	162.40	212.09	196.42	320.24	529.70	109.56	353.12	222.3
Karaafuu	43.00	15.91	25.49	10.47	55.42	0.36	9.14	2419.8
Bidhaa zisizo Asilia								
Madini	1782.10	1926.32	1893.92	1930.02	1694.48	1615.40	2326.68	44.0
Bidhaa za Viwanda	1072.10	1139.10	785.44	684.86	676.27	894.29	805.21	-10.0
Samaki na Mazao ya Samaki	130.60	167.91	161.48	143.70	193.01	181.85	168.03	-7.6
Mazao ya Mboga na Maua	28.10	19.29	193.27	274.10	148.65	147.70	176.04	19.2
Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export)	172.80	219.77	339.08	194.07	143.16	186.71	242.86	30.1
Bidhaa nyinginezo	517.60	500.68	315.25	271.64	223.29	340.40	450.38	32.3
Ujazi wa Fedha								
Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni) *	16,106.8	18,614.2	22,115.3	22,877.8	24,714.3	25,823.5	28,313.1	9.6
Karadha (Sh. bilioni)	16,293.0	18,863.7	22,505.5	23,775.8	24,977.2	26,249.3	28,103.3	7.1
Fedha za serikali								
2013/14	2014/15	2015/16p	2016/17	2017/18	2018/19p	2019/20p	2019/20	
Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni)	10,182,454.7	10,957,765.3	14,048,034.0	16,639,831.5	17,944,887.0	18,529,558.0	23,045,337.5	24.4
Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni)	10,032,119.7	10,893,486.1	13,420,045.1	11,625,865.8	12,852,304.0	13,806,788.9	15,420,491.5	11.7
Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni)	3,926,042.2	3,710,228.2	4,339,552.9	7,272,824.3	7,615,768.3	8,493,838.5	12,248,602.3	44.2

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

* Kwa shule za Serikali na binafsi

¹ Kwa tafsiri pana (M3)

- Takwimu hazikupatikana

**JEDWALI B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA
BAJETI**

JEDWALI B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI (2012 - 2019)							
Mwaka wa Kalenda	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
PATO LA TAIFA							
Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp)	6.8%	6.7%	6.2%	6.9%	6.8%	7.0%	7.0%
Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp)	17.1%	13.2%	14.2%	14.9%	9.6%	8.7%	7.3%
Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP)	37.5%	37.7%	32.8%	32.2%	34.0%	38.4%	39.7%
Uwiano wa Akiba kwenye Benki na Pato la Taifa (Savings/GDP)	10.7%	13.0%	13.2%	17.2%	15.8%	16.2%	18.0%
MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA							
Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi)	5.6%	4.8%	6.8%	6.5%	4.0%	3.3%	3.8%
Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka)	7.9%	6.1%	5.6%	5.2%	5.3%	3.5%	3.4%
GDP deflator Inflation (bp)	10.7%	4.8%	6.1%	7.1%	2.5%	2.0%	0.7%
GDP deflator Inflation (MP)	9.7%	6.1%	7.6%	7.5%	2.6%	1.8%	0.7%
Riba za Mikopo (mwaka mmoja)	14.0%	14.7%	14.2%	13.7%	18.3%	18.2%	16.7%
Riba za Amana za muda maalum (miezi 12)	11.6%	10.8%	10.8%	11.5%	11.7%	8.8%	8.8%
Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka)	2.4%	3.9%	3.4%	2.2%	6.6%	9.4%	7.9%
Kiwango cha ubadilishanaji fedha kwa Dola (wastani wa mwaka)	1,598.7	1,652.5	1,985.4	2,177.1	2,228.9	2,264.1	2,288.6
UJAZI WA FEDHA							
Kiwango cha ukuaji wa M3	10.0%	15.6%	18.8%	3.4%	8.0%	4.5%	9.6%
Kiwango cha ukuaji wa M2	10.9%	17.0%	13.4%	5.3%	10.4%	3.8%	11.8%
Mikopo Chechefu	6.6%	6.8%	6.6%	10.3%	11.5%	10.7%	9.8%
Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi	15.3%	19.4%	24.8%	7.2%	1.7%	4.9%	11.1%
UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA							
Bidhaa zilizouzwa nje	11.5%	10.3%	11.2%	9.9%	8.5%	7.7%	9.2%
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	18.5%	17.2%	18.4%	17.2%	15.7%	14.7%	16.1%
Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje	24.2%	21.9%	20.6%	17.0%	14.2%	14.2%	14.7%
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	29.6%	27.2%	26.2%	21.4%	18.0%	17.9%	17.9%
Urari wa malipo ya kawaida	-10.9%	-10.1%	-8.3%	-5.4%	-3.4%	-3.4%	-2.4%
Akiba ya fedha za kigeni (miezi)	4.1	4.0	4.3	4.9	7.4	6.0	6.2
UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA							
Mwaka wa fedha	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19
Mapato ya ndani	12.5%	13.1%	12.4%	13.9%	14.7%	14.6%	14.0%
Mapato ya kodi	11.4%	11.9%	11.2%	12.2%	12.4%	12.3%	11.7%
Matumizi (Bila rollover)	18.8%	17.9%	16.5%	17.5%	16.6%	16.7%	16.9%
Matumizi ya kawaida	13.4%	12.9%	12.3%	13.2%	10.2%	10.5%	10.5%
Matumizi ya maendeleo	5.4%	5.0%	4.2%	4.3%	6.4%	6.2%	6.5%
Misaada	2.0%	2.0%	1.2%	0.5%	1.0%	0.8%	0.7%
Nakisi (kabla ya misaada)	-6.2%	-5.3%	-4.3%	-3.9%	-2.4%	-2.6%	-3.9%
Nakisi (baada ya misaada)	-4.1%	-3.2%	-3.2%	-3.4%	-1.4%	-1.9%	-3.2%
Mikopo ya nje	2.6%	2.9%	2.3%	1.1%	1.5%	1.4%	0.9%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SEHEMU YA KWANZA

MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA


SURA YA I

HALI YA UCHUMI WA TAIFA

Ukuaji wa Uchumi

1. Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa asilimia 7.0 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuimarika kwa sekta ya madini, kuboreshwa kwa huduma za usafiri na usafirishaji, pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege, miradi ya nishati ya umeme pamoja na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji mwaka 2019 ni pamoja na: madini iliyokua kwa asilimia 17.7; ujenzi (asilimia 14.8); sanaa na burudani (asilimia 11.2); na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.7).

Kielelezo Na.1.1: Mwenendo wa Ukuaji kwa Baadhi ya Sekta



2. Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika lilikuwa shilingi milioni 139,893,804 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi milioni 129,043,901 mwaka 2018. Aidha, mwaka 2019, Tanzania Bara ilikadirwa kuwa na watu 54,265,158 ambapo Pato la Wastani la Kila Mtu lilitifika shilingi 2,577,967 kutoka shilingi

2,452,406 mwaka 2018, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 5.1. Kiasi hicho cha Pato la Wastani kwa Kila Mtu kwa mwaka 2019 ni sawa na dola za Marekani 1,126.4 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,083.2 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 4.0.

3. Mwaka 2019, shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilikua kwa asilimia 4.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4 mwaka 2018. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyopelekea kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Shughuli ndogo za uzalishaji mazao zilikua kwa asilimia 4.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2018 na zilichangia asilimia 14.8 katika Pato la Taifa mwaka 2019. Aidha, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za mifugo kilikuwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2018 na zilichangia asilimia 7.4 katika Pato la Taifa mwaka 2019. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za misitu na uvuvi kilipungua kufikia asilimia 4.8 na 1.5 mwaka 2019 kutoka asilimia 4.9 na 9.2 mwaka 2018 na mchango katika Pato la Taifa uliendelea kubaki asilimia 2.7 na 1.7 mtawalia mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

4. Shughuli za kilimo sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 4.4 mwaka 2019 wakati sehemu isiyouzika ilikua kwa asilimia 4.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4 na 6.4 mwaka 2018 mtawalia. Kiwango cha ukuaji wa shughuli ndogo za kiuchumi za uvuvi, misitu na mazao sehemu inayouzika kilipungua kufikia asilimia 1.5, asilimia 4.8 na asilimia 4.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.2, asilimia 5.2 na asilimia 5.6 mwaka 2018 mtawalia. Hata hivyo, kasi ya ukuaji kwa shughuli ndogo za kiuchumi za mifugo sehemu inayouzika iliongezeka na kuwa asilimia 5.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2018. Kwa upande wa sehemu isiyouzika, shughuli ndogo za kiuchumi za mazao na misitu zilikua kwa asilimia 4.4 na asilimia 4.8 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.1 na asilimia 1.7 mwaka 2018 mtawalia. Aidha, kiwango cha ukuaji kwa shughuli ndogo za kiuchumi za uvuvi na mifugo sehemu isiyouzika kilipungua na kufikia asilimia 1.5 na asilimia 5.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 9.2 na asilimia 9.8 mwaka 2018 mtawalia. Mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa kwa ujumla wake ulipungua na kufikia asilimia 26.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 27.9 mwaka 2018.

5. Shughuli za kiuchumi za uchimbaji madini na mawe ndizo ziliongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa asilimia 17.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.5 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na gesi asilia pamoja na kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini nchini. Aidha, mchangano wa shughuli za uchimbaji madini na mawe katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2018.
6. Mwaka 2019, kasi ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani ilikuwa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2018. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za nguo, bia na ngano pamoja na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kufuatia kuongezeka kwa bei za malighafi za viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, mchangano wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 8.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2018.
7. Shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme zilikua kwa asilimia 7.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.8 mwaka 2018. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu za maji na gesi asilia. Mchangano wa shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.3 kwa mwaka wa tatu mfululizo.
8. Mwaka 2019, shughuli za usambazaji maji na udhibiti maji taka zilikua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na juhudhi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuimarisha miundombinu ya maji safi na maji taka na kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu kuzalisha na kusambaza maji. Mchangano wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa umeendelea kubaki asilimia 0.4 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Shughuli za usambazaji maji na udhibiti wa maji taka sehemu inayouzika na isiyouzika zilikua kwa kiwango sawa cha asilimia 6.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.6 na asilimia 14.1 mwaka 2018 mtawalia.

9. Shughuli za kiuchumi za ujenzi kwa mwaka 2019 zilikua kwa asilimia 14.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 13.8 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kuendelea kwa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, madaraja, viwanja vya ndege, na reli. Aidha, shughuli za ujenzi sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 14.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 13.7 mwaka 2018 wakati ambapo sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 12.5 mwaka 2018. Shughuli za kiuchumi za ujenzi zilichangia asilimia 14.3 katika Pato la Taifa mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 13.1 mwaka 2018.
10. Shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka 2018. Aidha, shughuli za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 8.8 katika Pato la Taifa mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2018.
11. Shughuli za uchukuzi na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 8.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 11.8 mwaka 2018. Ukuaji huo ultokana na kuongezeka kwa idadi ya mizigo na abiria iliyosafirishwa kwa njia ya anga, reli na barabara. Mchango wa huduma za uchukuzi na uhifadhi mizigo katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 6.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2018.
12. Shughuli za malazi na huduma ya chakula zilikua kwa asilimia 3.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kupungua kwa idadi ya wageni wa ndani na nje walipata huduma za malazi, chakula na vinywaji nchini. Aidha, sekta hii ilibaki na mchango wa asilimia 1.3 katika Pato la Taifa kwa mwaka wa tatu mfululizo.
13. Shughuli za kiuchumi za huduma za habari na mawasiliano ambazo zinajumuisha huduma za utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa taarifa mbalimbali kuititia vyombo vya habari kama vile radio, magazeti, luninga, tovuti pamoja na huduma za mawasiliano kwa njia ya simu zilikua kwa kiwango cha asilimia 7.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za simu za viganjani na mitandao ya kijamii nchini katika kuwasiliana na kupata habari na matukio mbalimbali. Mchango wa shughuli za huduma za habari na

mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

14. Mwaka 2019, shughuli za kiuchumi katika huduma za fedha na bima zilikua kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.5 mwaka 2018. Ongezeko hili lilitokana na juhudzi za Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zilizokuwa zinaikabili sekta hii ikiwemo ongezeko la mikopo chechefu. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 3.8 mwaka 2018 hadi asilimia 3.5 mwaka 2019.

15. Mwaka 2019, kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba kilikuwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi, biashara na ofisi, hususan maeneo ya mijini. Aidha, ukuaji wa shughuli za upangishaji wa nyumba sehemu inayouzika uliongezeka kufikia asilimia 4.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2018. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa shughuli za upangishaji wa nyumba sehemu isiyouzika ilipungua na kufikia asilimia 4.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 mwaka 2018. Mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba katika Pato la Taifa ulipungua kufikia asilimia 2.7 mwaka 2019 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2018.

16. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi kilikua kwa asilimia 7.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 9.9 mwaka 2018. Shughuli hizi za kitaaluma, kisayansi na kiufundi zimekuwa na mchango sawa wa asilimia 0.6 katika Pato la Taifa kwa mwaka 2018 na 2019. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za huduma zinazohusiana na utawala zikiwemo ukodishaji wa vifaa, mashine na mitambo, utafutaji wa ajira, huduma za utalii, ulinzi wa mali na watu, utoaji huduma ofisini, na haki ya kutumia matokeo ya kitaaluma kiliongezeka kufikia asilimia 8.4 mwaka 2019 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2018. Aidha, mchango wa shughuli hizi uliendelea kuwa asilimia 2.6 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

17. Shughuli za utawala na ulinzi zinajumuisha shughuli zinazofanywa na Serikali kwa maana ya sekta ya umma, shughuli za mahakama, uhamiaji,


mambo ya nje, ulinzi na usalama na usimamizi wa programu za Serikali. Shughuli za kiuchumi za utawala na ulinzi zilikua kwa asilimia 3.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 mwaka 2018. Sekta hii ilikuwa na mchango wa asilimia 3.8 katika Pato la Taifa mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2018.

18. Shughuli za utoaji huduma za elimu zilikua kwa asilimia 6.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.6 mwaka 2018. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa udahili hasa katika shule za msingi kufuatia kuendelea kwa utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Mchango wa shughuli za huduma za elimu katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 2.4 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Aidha, ukuaji wa shughuli za afya na huduma za ustawi wa jamii kwa mwaka 2019 ulifikia asilimia 5.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.4 mwaka 2018. Mchango wa shughuli za afya na utoaji huduma kwa jamii katika Pato la Taifa umeendelea kubaki asilimia 1.4 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

19. Kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi za sanaa na burudani ilipungua na kufikia asilimia 11.2 mwaka 2019 kutoka ukuaji wa asilimia 13.7 mwaka 2018. Mchango wa sekta hii bado umebaki kuwa asilimia 0.3 ya Pato la Taifa mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

20. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri kiliendelea kubaki asilimia 3.1 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Shughuli za kaya binafsi katika kuajiri hujumuisha shughuli zinazofanywa na wafanyakazi walioajiriwa katika kaya binafsi hususan walinzi, wapishi, wahudumu wa ndani, na madereva. Mwaka 2019, mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.2.

Kielelezo Na. 1.2: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa (Asilimia)



Mwenendo wa Bei

21. Katika kipindi cha miaka saba mfululizo, mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2018 hadi asilimia 3.4 mwaka 2019. Kiwango cha chini cha mfumuko wa bei kilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: Kuendelea na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti; kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika soko la ndani; na kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani.

22. Uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma unaonesha kuwa yapo makundi yaliyokuwa na ongezeko dogo la bei na mengine yaliyokuwa na ongezeko kubwa la bei kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018. Makundi ambayo mfumuko wa bei uliongezeka mwaka 2019 ni pamoja na hoteli na migahawa; samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba; usafirishaji; na mavazi ya nguo na viatu. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei, kundi la nishati, maji na malazi ndilo lililokuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei cha asilimia 7.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 12 mwaka 2018. Hii inatokana na kuimarika kwa bei za mafuta katika

soko la dunia pamoja na jitihada za Serikali za kuimarisha huduma za maji mijini na vijijini. Aidha, kundi la mawasiliano liliendelea kuwa na mwenendo wa kupungua kwa kasi ya upandaji bei kwa mwaka wa nne mfululizo ambapo kwa mwaka 2019 ulipungua kwa asilimia 0.2 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2018. **Jedwali Na. 1.1.**

Jedwali Na. 1.1: Fahirisi na Mfululizo wa Bei ya Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Wakazi wa Mijini – Tanzania Bara (2001-100)

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji wenyewe kilevi na tumbaku	Mavazi na viatu	Nishati na Makazi	Samani, vifaa ya nyumbani ukarabati wa nyumba za Afya	Gharama Usafirishaji	Mawasili ni na arno	Utamadu Burudani	Hoteli na Elimu	Bidhaa na nyngine zo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE			
2014	FAHIRISI ZA BEI	89.1	95.8	94.5	99.3	96.7	95.0	99.4	99.6	96.8	96.8	94.7	95.6	92.7
2015		96.8	99.2	98.4	100.9	98.2	97.9	98.8	99.8	98.4	99.6	99.1	98.4	97.9
2016		103.8	103.2	102.2	107.3	101.7	103.4	99.5	99.1	101.1	102.3	103.1	101.7	102.9
2017		113.3	106.6	105.8	115.4	104.7	106.0	99.9	98.2	102.3	103.2	104.4	105.0	108.4
2018		116.6	108.4	108.9	129.2	107.4	107.4	102.5	96.6	102.8	105.8	105.7	106.7	112.2
2019		120.0	111.0	112.1	139.4	111.5	109.3	105.7	96.5	104.3	107.6	110.2	109.3	116.1
2015	MWEENDO WA BEI	8.7%	3.6%	4.1%	1.6%	1.6%	3.0%	-0.6%	0.3%	1.6%	2.9%	4.6%	2.9%	5.6%
2016		7.2%	4.0%	3.9%	6.3%	3.6%	5.6%	0.6%	-0.7%	2.7%	2.7%	4.1%	3.4%	5.2%
2017		9.1%	3.3%	3.5%	7.6%	2.9%	2.6%	0.5%	-0.9%	1.3%	0.9%	1.2%	3.2%	5.3%
2018		3.0%	1.6%	2.9%	12.0%	2.5%	1.3%	2.5%	-1.6%	0.5%	2.4%	1.3%	1.6%	3.5%
2019		2.9%	2.4%	3.0%	7.9%	3.9%	1.8%	3.1%	-0.2%	1.5%	1.8%	4.2%	2.4%	3.4%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

23. Uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi mengine maalum unaonesha kuwa wastani wa ongezeko la bei ya chakula kinachojumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na hotelini ulikuwa asilimia 4.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa chakula kwa nchi jirani na hivyo kusababisha bei ya chakula nchini kupanda. Aidha, wastani wa ongezeko la bei ya bidhaa zisizokuwa za chakula ulipungua na kufikia asilimia 4.0 mwaka 2019 kutoka asilimia 4.3 mwaka 2018. Mwenendo wa bei ya nishati unaonesha kuwa wastani wa ongezeko la bei umepungua kufikia asilimia 9.0 mwaka 2019 kutoka asilimia 17.2 mwaka 2018. Hii ni kutokana na kuimarika kwa bei za petroli, dizeli na mafuta ya taa katika soko la ndani kufuatia kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji. Mfumuko wa bei ambao haujumuishi chakula na nishati (core inflation) uliongezeka kwa asilimia 3.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na

asilimia 1.9 mwaka 2018. Kundi hili limechangia asilimia 54.3 katika kapu la walaji na ndilo ambalo linaweza kudhibitiwa kwa kutumia nyenzo za sera za fedha.

24. Mwaka 2019, fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa makundi ya watu wa tabaka la kipato cha chini na kati iliongezeka na kufikia asilimia 3.8 na asilimia 4.5 kutoka asilimia 2.0 na asilimia 1.9 mwaka 2018 kwa mtiririko huo. Hii ilitokana na ongezeko la wastani wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika kwa wingi na makundi hayo zikiwemo vyakula na vinywaji baridi, gharama za afya, nishati, maji na makazi. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa kundi la watu wa tabaka la kipato cha juu ilipungua na kufikia asilimia 3.6 mwaka 2019 kutoka asilimia 4.7 mwaka 2018. Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma nyingine ilikuwa na mwenendo unaoendana na mahitaji ya kundi husika kimapato kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.2**. Aidha, **majedwali Na. 8 – 16** yanaonesha mwenendo wa fahirisi ya bei kwa makundi na sehemu mbalimbali.

Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Walaji Kulingana na Tabaka la Kipato

Mwaka	Tabaka la Kipato	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji wenyewe kilev na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifa ya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasilini na Burudani	Utamadu	Elimu	Hoteli na Migahawa zo	Bidhaa na huduma nyingine	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2014	KIPATO CHA JUU	6.7%	8.1%	2.1%	7.5%	1.3%	2.4%	5.3%	0.0%	3.8%	15.9%	4.5%	3.2%	6.0%
2015		8.8%	6.5%	0.9%	7.1%	0.7%	1.2%	3.6%	2.9%	0.8%	2.1%	8.4%	-0.7%	6.5%
2016		8.6%	3.3%	1.8%	8.8%	3.3%	14.1%	-2.3%	2.4%	1.1%	-1.6%	5.1%	3.5%	4.8%
2017		9.2%	2.1%	1.8%	1.3%	5.4%	2.5%	4.9%	0.6%	-1.2%	-0.1%	0.8%	3.2%	4.2%
2018		7.0%	0.2%	2.5%	5.6%	1.1%	0.1%	6.4%	0.4%	0.8%	7.8%	1.0%	0.6%	4.7%
2019		4.4%	0.0%	2.4%	8.1%	2.0%	4.1%	2.8%	1.5%	0.7%	1.5%	3.7%	0.4%	3.6%
2014	KIPATO CHA KATI	3.9%	8.1%	2.1%	13.9%	5.1%	5.2%	12.5%	0.7%	3.7%	11.0%	7.1%	6.2%	6.2%
2015		2.9%	7.4%	2.1%	14.6%	4.5%	3.1%	4.4%	0.5%	3.9%	5.5%	11.4%	5.0%	5.6%
2016		3.3%	2.5%	1.1%	12.4%	1.4%	13.4%	0.3%	0.6%	2.9%	-2.3%	8.3%	5.4%	4.5%
2017		4.6%	2.3%	1.4%	2.2%	3.3%	2.4%	0.7%	0.5%	0.5%	-0.1%	1.2%	1.1%	2.6%
2018		7.0%	-0.5%	2.1%	4.1%	1.3%	0.3%	-18.8%	-0.1%	0.1%	8.6%	-0.5%	1.5%	1.9%
2019		5.6%	0.4%	3.5%	6.6%	2.2%	4.5%	5.6%	1.4%	2.0%	0.0%	2.7%	2.6%	4.5%
2014	KIPATO CHA CHINI	7.3%	8.4%	9.2%	7.0%	4.0%	0.7%	15.9%	0.0%	4.3%	0.0%	7.8%	11.5%	7.7%
2015		5.9%	14.2%	9.0%	3.4%	6.0%	5.6%	-0.2%	0.0%	5.6%	-0.3%	7.1%	2.7%	5.4%
2016		3.6%	8.2%	-2.4%	7.1%	2.7%	12.1%	0.9%	0.6%	1.2%	-5.2%	6.8%	6.0%	4.3%
2017		3.4%	2.9%	1.3%	0.9%	3.1%	1.6%	-0.1%	0.4%	1.7%	3.9%	0.5%	0.9%	1.9%
2018		4.5%	0.0%	3.1%	5.7%	1.9%	0.1%	-12.5%	-0.1%	1.1%	5.5%	0.1%	1.6%	2.0%
2019		4.6%	0.8%	4.0%	5.6%	1.9%	3.1%	4.9%	1.0%	2.3%	-0.1%	2.2%	2.5%	3.8%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ukuzaji Rasilimali

25. Ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi bilioni 55,474.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 49,493.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 9.9 na kufikia shilingi bilioni 49,095.4 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 44,669.6 mwaka 2018. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulifikia asilimia 39.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 38.4 mwaka 2018.

26. Ukuzaji rasilimali za kudumu unaojumuisha majengo: vifaa vya usafiri; mitambo na vifaa vingine; rasilimali za mazao na mifugo; haki za umiliki, utafiti na maendeleo; na huduma za kitaalamu ulifikia shilingi bilioni 53,873.1 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 46,705.5 mwaka 2018 kwa bei za mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika nao uliongezeka kwa asilimia 18.1 kutoka shilingi bilioni 50,387.1 mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 59,530.0 mwaka 2019. Thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 4,777.8 mwaka 2019 ikilinganishwa na upungufu wa shilingi bilioni 2,035.9 mwaka 2018. Aidha, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za miaka husika ilipungua kwa shilingi bilioni 4055.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na upungufu wa shilingi bilioni 867.5 mwaka 2018.

27. Ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo uliongezeka kwa asilimia 17.3 kufikia shilingi bilioni 45,285.9 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 38,591.0 mwaka 2018 kwa bei za mwaka 2015. Vile vile, ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 20.5 kufikia shilingi bilioni 50,257.5 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 41694.7 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba za makazi na biashara. Thamani ya uagizaji wa vifaa vya usafiri kwa bei za mwaka 2015 iliongezeka kwa asilimia 19.9 na kufikia shilingi bilioni 2,131.9 wakati kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa asilimia 9.8 kufikia shilingi bilioni 1,936.1 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, thamani ya ununuzi wa mitambo na vifaa vingine kwa ujumla wake kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa asilimia 4.2 kufikia shilingi bilioni 5,301.2 na kwa bei za mwaka 2015 thamani ilipungua kwa asilimia 0.3 kufikia shilingi bilioni 4,647.5 mwaka 2019.

28. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma inayojumuisha Serikali kuu, mashirika na taasisi za Serikali ulifiki shilingi bilioni 17,680.4 mwaka 2019 kwa bei za miaka husika ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,287.1 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi ulifiki shilingi bilioni 41,849.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 35,100 mwaka 2018 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Sekta ya umma ilichangia asilimia 29.7 katika rasilimali za kudumu na sekta binafsi ilichangia asilimia 70.3 mwaka 2019.

PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)								
Jedwali Na.1							Shs.Milioni	
	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	19,551,225	21,313,803	25,234,560	29,739,111	34,154,594	35,962,728	37,136,790
	Kilimo cha Mazao	10,500,528	11,562,090	13,279,392	16,474,729	19,703,004	21,003,720	20,632,396
	Mifugo	5,579,312	5,585,211	7,158,457	8,205,007	8,857,939	9,240,100	10,344,727
	Misitu	2,069,113	2,477,897	2,920,425	3,094,767	3,310,076	3,459,581	3,738,360
	Uvubi	1,375,790	1,658,605	1,843,401	1,929,747	2,245,558	2,218,731	2,379,172
	Huduma katika shughuli za Kilimo	26,483	30,000	32,886	34,861	38,017	40,596	42,136
	Viwanda na Ujenzi	18,570,322	20,767,734	23,103,647	26,937,139	29,735,584	34,851,874	40,037,880
B	Uchimbaji Madini na Mawe	3,125,480	3,097,933	4,055,619	5,299,362	5,206,217	6,573,059	7,219,118
C	Viwanda	6,648,876	7,533,519	7,411,672	8,467,126	9,102,282	10,418,776	11,872,086
D	Umeme	550,300	818,693	798,801	472,868	413,351	348,527	374,002
E	Maji safi na Maji taka	324,028	371,581	390,758	433,132	519,909	566,562	628,187
F	Ujenzi	7,921,637	8,946,007	10,446,797	12,264,650	14,493,826	16,944,950	19,944,486
	Huduma	29,384,671	34,111,643	38,146,529	42,747,407	45,066,596	48,059,561	51,433,592
G	Biashara na Matengenezo	7,063,673	8,045,702	8,747,862	9,861,678	10,843,499	11,793,201	12,264,410
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	5,246,333	6,167,366	6,929,895	7,549,484	7,897,993	8,381,276	9,621,651
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,317,191	1,330,371	1,421,916	1,523,035	1,602,543	1,653,792	1,770,670
J	Habari na Mawasiliano	1,433,179	1,598,597	1,681,098	1,739,556	1,829,360	1,948,180	2,052,241
K	Fedha na Bima	2,541,198	3,614,991	4,189,021	5,268,866	4,789,632	4,947,301	4,927,613
L	Upangishaji Majengo	2,551,029	2,721,061	2,949,598	3,162,290	3,334,171	3,553,630	3,831,113
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundu	353,038	433,939	518,123	617,914	726,707	817,442	903,234
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	1,522,884	1,914,456	2,183,917	2,661,978	3,027,384	3,306,554	3,640,720
O	Utawala na Ulinzi	3,615,292	3,973,787	4,548,604	4,846,491	4,986,287	5,131,630	5,357,235
P	Elimu	1,728,376	2,027,225	2,413,306	2,673,289	2,864,290	3,081,718	3,322,488
Q	Afyu na Huduma za Jamii	1,113,563	1,233,077	1,419,090	1,540,484	1,681,353	1,816,738	1,932,659
R	Sanaa na Burudani	194,938	223,468	248,510	285,626	322,353	374,924	427,887
S	Huduma nyingine za Kijamii	555,957	661,939	717,898	831,216	959,152	1,037,612	1,140,424
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	148,022	165,666	177,691	185,501	201,872	215,564	241,246
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	67,506,219	76,193,180	86,484,736	99,423,658	108,956,774	118,874,163	128,608,262
	Ongeza kodi katika bidhaa	5,470,981	6,410,208	7,864,579	8,938,667	9,787,724	10,169,738	11,285,542
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	72,977,200	82,603,388	94,349,316	108,362,324	118,744,498	129,043,901	139,893,804
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA
(KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)

Jedwali Na. 1A								Shs.Milioni
	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A:SEHEMU INAYOUZIKA								
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	64,901,865	73,572,807	84,275,963	97,295,383	106,025,246	114,220,803	124,768,533	
Kilimo, Misitu na Uvubi	12,100,550	13,008,318	16,020,386	19,628,661	22,561,096	22,410,625	23,341,415	
Kilimo cha Mazao	5,416,553	5,828,361	7,176,326	9,729,649	11,822,710	11,350,635	11,149,968	
Mifugo	3,944,325	3,866,240	5,160,608	6,322,457	6,877,739	6,661,287	7,457,625	
Misitu	1,388,640	1,685,505	1,882,033	1,706,926	1,680,599	2,229,486	2,409,141	
Uvubi	1,324,549	1,598,212	1,768,534	1,834,769	2,142,032	2,128,621	2,282,546	
Huduma katika shughuli za Kilimo	26,483	30,000	32,886	34,861	38,017	40,596	42,136	
Viwanda na Ujenzi	18,096,470	20,188,806	22,361,768	26,111,436	28,749,158	33,722,200	38,860,340	
B: Uchimbaji Madini na Mawe								
Viwanda	6,648,876	7,533,519	7,411,672	8,467,126	9,102,282	10,418,776	11,872,086	
Umeme	550,300	818,693	798,801	472,868	413,351	348,527	374,002	
Maj safi na Maji taka	222,978	261,504	272,990	301,821	372,032	395,810	438,862	
Ujenzi	7,548,836	8,477,157	9,822,685	11,570,259	13,655,276	15,986,029	18,956,271	
Huduma	29,233,864	33,965,476	38,029,229	42,616,618	44,927,268	47,918,240	51,281,236	
Biashara na Matengenezo	7,063,673	8,045,702	8,747,862	9,861,678	10,843,499	11,793,201	12,264,410	
Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	5,246,333	6,167,366	6,929,895	7,549,484	7,897,993	8,381,276	9,621,651	
Malazi na Huduma ya chakula	1,317,191	1,330,371	1,421,916	1,523,035	1,602,543	1,653,792	1,770,670	
Habari na Mawasiliano	1,433,179	1,598,597	1,681,098	1,739,556	1,829,360	1,948,180	2,052,241	
Fedha na Birma	2,541,198	3,614,991	4,189,021	5,268,866	4,789,632	4,947,301	4,927,613	
Upangishaji Majengo	2,400,221	2,574,893	2,832,298	3,031,501	3,194,842	3,412,309	3,678,758	
Misitu za kitaakuma, Sayansi na Ufundu	353,038	433,939	518,123	617,914	726,707	817,442	903,234	
Huduma zinazohusiana na Utawala	1,522,884	1,914,456	2,183,917	2,661,978	3,027,384	3,306,554	3,640,720	
Utwala na Ulinzi	3,615,292	3,973,787	4,548,604	4,846,491	4,986,287	5,131,630	5,357,235	
Elimu	1,728,376	2,027,225	2,413,306	2,673,289	2,864,290	3,081,718	3,322,488	
Afya na Huduma za Jamii	1,113,563	1,233,077	1,419,090	1,540,484	1,681,353	1,816,738	1,932,659	
Sanaa na Burudani	194,938	223,468	248,510	285,626	322,353	374,924	427,887	
Huduma nyngine za Kijamii	555,957	661,939	717,898	831,216	959,152	1,037,612	1,140,424	
Shughuli za Kaya katika kuajiri	148,022	165,666	177,691	185,501	201,872	215,564	241,246	
Jumla ya Ongezeko la Thamani	59,430,884	67,162,600	76,411,383	88,356,716	96,237,522	104,051,065	113,482,991	
Ongeza kodi katika bidhaa								
B: SEHEMU ISIYOUZIKA								
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	8,075,334	9,030,580	10,073,353	11,066,941	12,719,252	14,823,098	15,125,271	
Kilimo, Misitu na Uvubi								
Kilimo	7,450,675	8,305,485	9,214,174	10,110,449	11,593,497	13,552,103	13,795,375	
Mazao	5,083,974	5,733,729	6,103,066	6,745,080	7,880,294	9,653,085	9,482,428	
Mifugo	1,634,987	1,718,971	1,997,848	1,882,549	1,980,200	2,578,812	2,887,102	
Misitu	680,473	792,392	1,038,392	1,387,841	1,629,477	1,230,096	1,329,219	
Uvubi	51,240	60,393	74,867	94,978	103,526	90,110	96,626	
Viwanda na Ujenzi	473,852	578,928	741,880	825,703	986,427	1,129,674	1,177,540	
Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	101,050	110,077	117,768	131,311	147,877	170,752	189,325	
Ujenzi	372,802	468,851	624,112	694,392	838,550	958,922	988,215	
Huduma	150,808	146,168	117,300	130,789	139,328	141,321	152,356	
Upangishaji Majengo	150,808	146,168	117,300	130,789	139,328	141,321	152,356	
Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	72,977,200	82,603,388	94,349,316	108,362,324	118,744,498	129,043,901	139,893,804	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)								
	Jedwali Na.2	Asilimia						
	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A	Kilimo, Misitu na Uvvi	26.8	25.8	26.7	27.4	28.8	27.9	26.6
	Kilimo cha Mazao	14.4	14.0	14.1	15.2	16.6	16.3	14.8
	Mifugo	7.6	6.8	7.6	7.6	7.5	7.2	7.4
	Misitu	2.8	3.0	3.1	2.9	2.8	2.7	2.7
	Uvvi	1.9	2.0	2.0	1.8	1.9	1.7	1.7
	Huduma katika shughuli za Kilimo	0.04	0.04	0.03	0.03	0.03	0.03	0.03
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4.3	3.8	4.3	4.9	4.4	5.1	5.2
C	Viwanda	9.1	9.1	7.9	7.8	7.7	8.1	8.5
D	Umeme	0.8	1.0	0.8	0.4	0.3	0.3	0.3
E	Maji safi na Maji taka	0.4	0.4	0.4	0.4	0.4	0.4	0.4
F	Ujenzi	10.9	10.8	11.1	11.3	12.2	13.1	14.3
G	Biashara na Matengenezo	9.7	9.7	9.3	9.1	9.1	9.1	8.8
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7.2	7.5	7.3	7.0	6.7	6.5	6.9
I	Malazi na Huduma ya chakula	1.8	1.6	1.5	1.4	1.3	1.3	1.3
J	Habari na Mawasiliano	2.0	1.9	1.8	1.6	1.5	1.5	1.5
K	Fedha na Bima	3.5	4.4	4.4	4.9	4.0	3.8	3.5
L	Upangishaji Majengo	3.5	3.3	3.1	2.9	2.8	2.8	2.7
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundu	0.5	0.5	0.5	0.6	0.6	0.6	0.6
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2.1	2.3	2.3	2.5	2.5	2.6	2.6
O	Utawala na Ulinzi	5.0	4.8	4.8	4.5	4.2	4.0	3.8
P	Elimu	2.4	2.5	2.6	2.5	2.4	2.4	2.4
Q	Afya na Huduma za Jamii	1.5	1.5	1.5	1.4	1.4	1.4	1.4
R	Sanaa na Burudani	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3
S	Huduma nyingine za Kijamii	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	92.5	92.2	91.7	91.8	91.8	92.1	91.9
	Ongeza kodi katika bidhaa	7.5	7.8	8.3	8.2	8.2	7.9	8.1
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	100.0						
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)							
Jedwali Na. 2A	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2013	2014	2015	2016	2017	Asilimia 2019
A:SEHEMU INAYOUZIKA							
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)							
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	16.6	15.7	17.0	18.1	19.0	17.4
	Kilimo cha Mazao	7.4	7.1	7.6	9.0	10.0	8.8
	Mifugo	5.4	4.7	5.5	5.8	5.8	5.2
	Misitu	1.9	2.0	2.0	1.6	1.4	1.7
	Uvubi	1.8	1.9	1.9	1.7	1.8	1.6
	Huduma katika shughuli za Kilimo	0.04	0.04	0.03	0.03	0.03	0.03
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4.3	3.8	4.3	4.9	4.4	5.1
C	Viwanda	9.1	9.1	7.9	7.8	7.7	8.1
D	Umeme	0.8	1.0	0.8	0.4	0.3	0.3
E	Maji safi na Maji taka	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3
F	Ujenzi	10.3	10.3	10.4	10.7	11.5	12.4
G	Biasara na Matengenezo	9.7	9.7	9.3	9.1	9.1	9.1
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	7.2	7.5	7.3	7.0	6.7	6.5
I	Malazi na Huduma ya chakula	1.8	1.6	1.5	1.4	1.3	1.3
J	Habari na Mawasiliano	2.0	1.9	1.8	1.6	1.5	1.5
K	Fedha na Bima	3.5	4.4	4.4	4.9	4.0	3.8
L	Upangishaji Majengo	3.3	3.1	3.0	2.8	2.7	2.6
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundu	0.5	0.5	0.5	0.6	0.6	0.6
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2.1	2.3	2.3	2.5	2.5	2.6
O	Utawala na Ulinzi	5.0	4.8	4.8	4.5	4.2	4.0
P	Elimu	2.4	2.5	2.6	2.5	2.4	2.4
Q	Afya na Huduma za Jamii	1.5	1.5	1.5	1.4	1.4	1.4
R	Sanaa na Burudani	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3
S	Huduma nyingine za Kijamii	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	81.4	81.3	81.0	81.5	81.0	80.6
	Ongeza kodi katika bidhaa	7.5	7.8	8.3	8.2	8.2	7.9
B: SEHEMU ISIYOUZIKA							
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)							
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	11.1	10.9	10.7	10.2	10.7	11.5
	Kilimo, Misitu na Uvubi	10.2	10.1	9.8	9.3	9.8	10.5
	Mazao	7.0	6.9	6.5	6.2	6.6	7.5
	Mifugo	2.2	2.1	2.1	1.7	1.7	2.0
	Misitu	0.9	1.0	1.1	1.3	1.4	1.0
	Uvubi	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1
F	Ujenzi	0.5	0.6	0.7	0.6	0.7	0.7
L	Upangishaji Majengo	0.2	0.2	0.1	0.1	0.1	0.1
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu						

PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)							
Jedwali Na. 2B	2013	2014	2015	2016	2017	2018	Shs.Milioni 2019
Aina ya Matumizi							
Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)	72,977,200	82,603,388	94,349,316	108,362,324	118,744,498	129,043,901	139,893,804
Matumizi ya Mwisho(Final consumption)	56,171,499	62,297,764	69,619,572	74,761,715	81,577,249	87,731,958	92,780,273
Serikali	7,330,733	8,151,130	9,366,334	9,824,677	10,097,404	10,468,798	10,867,505
Binafsi	48,675,221	53,954,463	60,047,089	64,699,505	71,211,545	76,966,654	81,601,115
Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii	165,545	192,171	206,149	237,532	268,299	296,506	311,653
Ukuzaji rasilimali	27,344,522	31,103,452	30,907,602	34,865,346	40,427,427	49,493,556	55,474,690
Rasilimali za kudumu	24,780,897	27,399,832	30,070,195	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,529,980
Ongezeko la limbikizo la Vito ya Thamani (changes in Valuables)	766,581	756,477	903,043	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337
Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories)	1,797,044	2,947,143	- 65,636	- 1,732,887	- 2,720,674	- 2,108,634	- 5,328,628
Mauzo nje	13,874,574	14,925,779	16,138,367	17,717,213	17,993,324	19,160,137	22,394,010
Bidhaa-fob	8,403,257	8,441,487	8,708,690	9,177,377	8,924,522	10,066,069	12,597,462
Huduma	5,471,317	6,484,292	7,429,677	8,539,835	9,068,803	9,094,069	9,796,547
Uagizaji	21,614,687	22,539,832	22,316,226	20,665,232	20,320,749	23,103,332	23,713,761
Bidhaa-fob	17,628,319	18,054,008	16,955,419	15,602,694	15,816,338	18,797,200	19,681,869
Huduma	3,986,369	4,485,823	5,360,807	5,062,538	4,504,411	4,306,132	4,031,891
Makosa na Mapungufu	- 2,798,709	- 3,183,776	-	1,683,283	- 932,752	- 4,238,418	- 7,041,408
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (KWA BEI ZA MWAKA 2015)									
Jedwali NA.3								Shs.Milioni	
	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	21,807,030	22,408,192	23,952,077	25,234,560	26,436,338	28,008,976	29,504,198	30,801,226
	Kilimo cha Mazao	10,806,678	11,283,264	12,344,014	13,279,392	13,996,348	14,895,622	15,659,175	16,351,012
	Mifugo	6,204,980	6,503,187	6,820,846	7,158,457	7,506,593	7,876,592	8,266,049	8,676,074
	Misitu	2,578,779	2,695,825	2,825,341	2,920,425	3,034,569	3,180,379	3,334,791	3,495,187
	Uvubi	2,187,669	1,896,254	1,930,394	1,843,401	1,864,627	2,020,292	2,206,242	2,240,163
	Huduma katika shughuli za Kilimo	28,925	29,661	31,482	32,886	34,201	36,091	37,941	38,790
	Viwanda na Ujenzi	17,987,423	19,872,086	21,057,206	23,103,647	25,817,955	28,565,774	31,344,128	35,042,891
B	Uchimbaji Madini na Mawe	3,314,742	3,464,721	3,687,273	4,055,619	4,356,709	4,588,624	4,659,195	5,486,097
C	Viwanda	6,066,989	6,292,514	6,919,794	7,411,672	8,213,364	8,889,818	9,623,501	10,184,558
D	Umeme	669,069	723,608	815,297	798,801	869,262	877,667	928,174	994,820
E	Maji safi na Maji taka	358,361	367,890	381,760	390,758	417,899	444,660	477,510	510,411
F	Ujenzi	7,578,263	9,023,353	9,253,082	10,446,797	11,960,720	13,765,005	15,655,747	17,867,005
	Huduma	31,223,623	32,808,710	35,863,739	38,146,529	40,549,564	42,689,011	45,369,789	48,118,368
G	Biashara na Matengenezo	7,371,411	7,682,286	8,444,243	8,747,862	9,260,703	9,821,248	10,396,691	10,963,963
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	5,710,466	6,050,976	6,577,706	6,929,895	7,324,856	7,815,845	8,736,561	9,493,191
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,343,924	1,356,204	1,397,782	1,421,916	1,480,052	1,525,619	1,604,391	1,651,794
J	Habari na Mawasiliano	1,266,747	1,414,116	1,560,064	1,681,098	1,718,548	1,824,471	1,989,717	2,133,313
K	Fedha na Bima	3,444,161	3,405,940	3,764,113	4,189,021	4,235,515	4,115,393	4,094,972	4,281,167
L	Upangishaji Majengo	2,606,439	2,714,775	2,828,970	2,949,598	3,077,086	3,211,895	3,354,518	3,505,485
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundu	322,260	385,090	447,921	518,123	606,207	694,291	763,332	821,636
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	1,417,467	1,660,994	1,976,260	2,183,917	2,611,498	2,892,463	3,054,288	3,311,753
O	Utawala na Ulinzi	3,623,123	3,974,206	4,242,164	4,548,604	4,793,820	4,907,113	5,064,968	5,236,678
P	Elimu	1,922,643	1,927,633	2,186,260	2,413,306	2,665,336	2,859,171	3,046,789	3,257,866
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,284,594	1,245,030	1,349,941	1,419,090	1,497,896	1,611,999	1,746,731	1,834,012
R	Sanaa na Burudani	198,470	212,502	230,652	248,510	280,131	307,907	350,027	389,225
S	Huduma nyingine za Kijamii	550,177	612,079	685,475	717,898	814,529	912,404	971,690	1,037,083
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	161,741	166,880	172,190	177,691	183,387	189,193	195,113	201,203
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	71,018,077	75,088,988	80,873,021	86,484,736	92,803,857	99,263,761	106,218,115	113,962,485
	Ongeza kodi katika bidhaa	6,961,771	8,179,129	8,001,090	7,864,579	8,024,535	8,393,644	8,923,215	9,213,354
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	77,979,847	83,268,117	88,874,111	94,349,316	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,175,839
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu								


PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA
(KWA BEI ZA MWAKA 2015)

Jedwali Na.3A								Shs. Milioni
SHUGHULI YA KUCHUMI		2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A: SEHEMU INAYOUZIKA								
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	79,294,951	84,760,925	90,262,677	96,464,568	103,029,270	110,210,543	118,030,637
A	Kilimo, Misitu na Uvuvu	19,105,967	20,538,538	21,953,873	22,914,869	24,357,439	25,671,332	26,791,784
	Kilimo cha Mazao	9,308,881	10,267,229	11,330,959	11,852,633	12,666,159	13,361,566	13,951,892
	Mifugo	5,465,006	5,788,062	6,131,537	6,458,453	6,797,008	7,080,239	7,431,444
	Misitu	2,421,026	2,536,530	2,629,474	2,720,412	2,853,656	3,002,559	3,146,975
	Uvuvu	1,881,393	1,915,235	1,829,018	1,849,169	2,004,525	2,189,028	2,222,684
	Huduma katika shughuli za Kilimo	29,661	31,482	32,886	34,201	36,091	37,941	38,790
	Viwanda na Ujenzi	19,292,729	20,449,621	22,391,185	25,070,677	27,685,960	30,352,531	34,018,239
B	Uchimbaji Madini na Mawe	3,464,721	3,687,273	4,055,619	4,356,709	4,588,624	4,659,195	5,486,097
C	Viwanda	6,292,514	6,919,794	7,411,672	8,213,364	8,889,818	9,623,501	10,184,558
D	Umerme	723,608	815,297	798,801	869,262	877,667	928,174	994,820
E	Maji safi na Maji taka	285,538	296,333	302,407	326,898	350,019	369,545	395,006
F	Ujenzi	8,526,348	8,730,924	9,822,685	11,304,444	12,979,833	14,772,116	16,957,757
	Huduma	32,717,125	35,771,676	38,053,040	40,454,486	42,592,227	45,263,466	48,007,260
G	Biashara na Matengenezo	7,682,286	8,444,243	8,747,862	9,260,703	9,821,248	10,396,691	10,963,963
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	6,050,976	6,577,706	6,929,895	7,324,856	7,815,845	8,736,561	9,493,191
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,356,204	1,397,782	1,421,916	1,480,052	1,525,619	1,604,391	1,651,794
J	Habari na Mawasiliano	1,414,116	1,560,064	1,681,098	1,718,548	1,824,471	1,989,717	2,133,313
K	Fedha na Bima	3,405,940	3,764,113	4,189,021	4,235,515	4,115,393	4,094,972	4,281,167
L	Upangishaji Majengo	2,623,190	2,736,907	2,856,109	2,982,008	3,115,112	3,248,194	3,394,377
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundu	385,090	447,921	518,123	606,207	694,291	763,332	821,636
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	1,660,994	1,976,260	2,183,917	2,611,498	2,892,463	3,054,288	3,311,752.9
O	Utawala na Ulinzi	3,974,206	4,242,164	4,548,604	4,793,820	4,907,113	5,064,968	5,236,678
P	Elimu	1,927,633	2,186,260	2,413,306	2,665,336	2,859,171	3,046,789	3,257,866
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,245,030	1,349,941	1,419,090	1,497,896	1,611,999	1,746,731	1,834,012
R	Sanaa na Burudani	212,502	230,652	248,510	280,131	307,907	350,027	389,225
S	Huduma nyingine za Kijamii	612,079	685,475	717,898	814,529	912,404	971,690	1,037,083
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	166,880	172,190	177,691	183,387	189,193	195,113	201,203
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	71,115,822	76,759,835	82,398,098	88,440,032	94,635,626	101,287,328	108,817,283
	Ongeza kodi katika bidhaa	8,179,129	8,001,090	7,864,579	8,024,535	8,393,644	8,923,215	9,213,354
B: SEHEMU ISIYOUZIKA								
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	3,973,166	4,113,187	4,086,638	4,363,825	4,628,135	4,930,787	5,145,201
A	Kilimo, Misitu na Uvuvu	3,302,224	3,413,539	3,280,687	3,521,469	3,651,537	3,832,866	4,009,441
	Mazao	1,974,383	2,076,785	1,948,433	2,143,714	2,229,463	2,297,609	2,399,120
	Mifugo	1,038,181	1,032,784	1,026,920	1,048,140	1,079,584	1,185,810	1,244,630
	Misitu	274,799	288,811	290,951	314,157	326,723	332,233	348,212
	Uvuvu	14,861	15,159	14,383	15,458	15,767	17,214	17,479
	Viwanda na Ujenzi	579,357	607,585	712,462	747,278	879,814	991,597	1,024,652
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	82,352	85,427	88,351	91,001	94,641	107,966	115,404
F	Ujenzi	497,005	522,159	624,112	656,276	785,173	883,632	909,247
	Huduma	91,585	92,063	93,489	95,078	96,783	106,323	111,108
L	Upangishaji Majengo	91,585	92,063	93,489	95,078	96,783	106,323	111,108
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	83,268,117	88,874,111	94,349,316	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,175,839

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (Kwa Bei za Mwaka 2015)									
	Jedwali Na.4	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2014	2015	2016	2017	2018	Asilimia	2019
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	6.9	5.4	4.8	5.9	5.4	4.4		
	Kilimo cha Mazao	9.4	7.6	5.4	6.4	5.2	4.4		
	Mifugo	4.9	4.9	4.9	4.9	4.9	5.0		
	Misitu	4.8	3.4	3.9	4.8	4.9	4.8		
	Uvubi	1.8	-4.5	1.2	8.4	9.2	1.5		
	Huduma katika shughuli za Kilimo	6.1	4.5	4.0	5.5	5.2	2.2		
B	Uchimbaji Madini na Mawe	6.4	10.0	7.4	5.3	1.5	17.7		
C	Viwanda	10.0	7.1	10.8	8.2	8.3	5.8		
D	Umeme	12.7	-2.0	8.8	1.0	5.8	7.2		
E	Maji safi na Maji taka	3.8	2.4	6.9	6.4	7.4	6.9		
F	Ujenzi	2.5	12.9	14.5	15.1	13.8	14.8		
G	Biashara na Matengenezo	9.9	3.6	5.9	6.1	5.9	5.5		
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	8.7	5.4	5.7	6.7	11.8	8.7		
I	Malazi na Huduma ya chakula	3.1	1.7	4.1	3.1	5.2	3.0		
J	Habari na Mawasiliano	10.3	7.8	2.2	6.2	9.1	7.2		
K	Fedha na Bima	10.5	11.3	1.1	-2.8	-0.5	4.5		
L	Upangishaji Majengo	4.2	4.3	4.3	4.4	4.4	4.5		
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundji	16.3	15.7	17.0	14.5	9.9	7.6		
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	19.0	10.5	19.6	10.8	5.6	8.4		
O	Utawala na Ulinzi	6.7	7.2	5.4	2.4	3.2	3.4		
P	Elimu	13.4	10.4	10.4	7.3	6.6	6.9		
Q	Afya na Huduma za Jamii	8.4	5.1	5.6	7.6	8.4	5.0		
R	Sanaa na Burudani	8.5	7.7	12.7	9.9	13.7	11.2		
S	Huduma nyingine za Kijamii	12.0	4.7	13.5	12.0	6.5	6.7		
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	3.2	3.2	3.2	3.2	3.1	3.1		
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	7.7	6.9	7.3	7.0	6.9	7.2		
	Ongeza kodi katika bidhaa	-2.2	-1.7	2.0	4.6	6.3	3.3		
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	6.7	6.2	6.9	6.8	7.0	7.0		
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu								

UKUAJI HALISI WA PATO LA TAIFA - Kwa bei za mwaka 2015



**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA
(KWA BEI ZA MWAKA 2015)**

Jedwali Na.4A		Asilimia						
SHUGHULI YA KIUCHUMI		2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
A: SEHEMU INAYOUZIKA								
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)								
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	2.9	7.5	6.9	4.4	6.3	5.4	4.4
	Kilimo cha Mazao	5.1	10.3	10.4	4.6	6.9	5.6	4.4
	Mifugo	5.4	5.9	5.9	5.3	5.2	4.2	5.0
	Misitu	4.5	4.8	3.7	3.5	4.9	5.2	4.8
	Uvubi	-13.4	1.8	-4.5	1.1	8.4	9.2	1.5
	Huduma katika shughuli za Kilimo	2.5	6.1	4.5	4.0	5.5	5.2	2.2
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4.5	6.4	10.0	7.4	5.3	1.5	17.7
C	Viwanda	3.7	10.0	7.1	10.8	8.2	8.3	5.8
D	Urnerme	8.2	12.7	-2.0	8.8	1.0	5.8	7.2
E	Maji safi na Maji taka	2.7	3.8	2.0	8.1	7.1	5.6	6.9
F	Ujenzi	19.0	2.4	12.5	15.1	14.8	13.7	14.1
G	Biashara na Matengenezo	4.2	9.9	3.6	5.9	6.1	5.9	5.5
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	6.0	8.7	5.4	5.7	6.7	11.8	8.7
I	Malazi na Huduma ya chakula	0.9	3.1	1.7	4.1	3.1	5.2	3.0
J	Habari na Mawasiliano	11.6	10.3	7.8	2.2	6.2	9.1	7.2
K	Fedha na Birna	-1.1	10.5	11.3	1.1	-2.8	-0.5	4.5
L	Upangishaji Majengo	4.3	4.3	4.4	4.4	4.5	4.3	4.5
M	Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundji	19.5	16.3	15.7	17.0	14.5	9.9	7.6
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	17.2	19.0	10.5	19.6	10.8	5.6	8.4
O	Utawala na Ulinzi	9.7	6.7	7.2	5.4	2.4	3.2	3.4
P	Elimu	0.3	13.4	10.4	10.4	7.3	6.6	6.9
Q	Afya na Huduma za Jamii	-3.1	8.4	5.1	5.6	7.6	8.4	5.0
R	Sanaa na Burudani	7.1	8.5	7.7	12.7	9.9	13.7	11.2
S	Huduma nyingine za Kijamii	11.3	12.0	4.7	13.5	12.0	6.5	6.7
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	3.2	3.2	3.2	3.2	3.2	3.1	3.1
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	5.9	7.9	7.3	7.3	7.0	6.9	7.4
	Ongeza kodi katika bidhaa	17.5	-2.2	-1.7	2.0	4.5	6.3	3.3
B: SEHEMU ISIYOUZIKA								
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)								
A	Kilimo, Misitu na Uvubi	1.7	3.4	-3.9	7.3	3.7	5.0	4.6
	Kilimo cha Mazao	1.3	5.2	-6.2	10.0	4.0	3.1	4.4
	Mifugo	1.7	-0.5	-0.6	2.1	3.0	9.8	5.0
	Misitu	4.7	5.1	0.7	8.0	4.0	1.7	4.8
	Uvubi	4.9	2.0	-5.1	7.5	2.0	9.2	1.5
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	2.7	3.7	3.4	3.0	4.0	14.1	6.9
F	Ujenzi	19.6	5.1	19.5	5.2	19.6	12.5	2.9
L	Upangishaji Majengo	0.4	0.5	1.5	1.7	1.8	9.9	4.5
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	6.8	6.7	6.2	6.9	6.8	7.0	7.0
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu								

PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MWAKA 2015)								
Jedwali Na. 4B								Shs.Milioni
Aina ya Matumizi	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	
Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)	75,088,988	80,873,021	86,484,736	92,803,857	99,263,761	106,218,115	113,962,485	
Kodi za uzalishaji	8,179,129	8,001,090	7,864,579	8,024,535	8,393,644	8,923,215	9,213,354	
Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)	83,268,117	88,874,111	94,349,316	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,175,839	
MATUMIZI YA PATO LA TAIFA								
Pato la Taifa kwa Bei za Soko(GDPmp)	83,268,117	88,874,111	94,349,316	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,175,839	
Matumizi ya Mwisho(Final consumption)	61,881,807	65,250,580	69,619,572	70,594,782	73,603,189	77,376,434	79,728,362	
Serikali	8,058,996	8,548,398	9,366,334	9,667,251	9,771,806	9,965,992	10,199,718	
Binafsi	53,641,790	56,500,911	60,047,089	60,697,766	63,578,381	67,135,273	69,243,571	
Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii	181,021	201,271	206,149	229,766	253,003	275,169	285,073	
Ukuzaaji rasilimali	29,019,243	31,803,806	30,907,602	33,795,169	38,338,123	44,669,633	49,095,353	
Rasilimali za kudumu	26,190,461	28,081,728	30,070,195	34,878,462	40,376,858	46,705,540	53,873,143	
Ongezeko la limbikizo la Vito wa Thamani (changes in Valuables)	775,566	820,886	903,043	902,490	858,566	776,123	925,034	
Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories)	2,053,216	2,901,191	- 65,636	- 1,985,783	- 2,897,301	- 2,812,030	- 5,702,825	
Mauzo nje	14,674,503	15,923,654	16,138,367	16,137,713	15,480,491	15,316,635	18,099,201	
Bidhaa-fob	8,406,652	8,815,465	8,708,690	8,060,826	7,805,507	7,608,448	10,033,375	
Huduma	6,267,851	7,108,189	7,429,677	8,076,886	7,674,984	7,708,187	8,065,826	
Uagizaji	22,796,325	23,545,813	22,316,226	20,331,252	18,879,441	22,025,703	21,719,228	
Bidhaa-fob	17,946,005	18,354,816	16,955,419	15,631,116	15,311,240	18,593,941	18,609,070	
Huduma	4,850,319	5,190,997	5,360,807	4,700,136	3,568,202	3,431,761	3,110,158	
Makosa na Mapungufu	488,889	-558,115	0	631,981	-884,958	- 195,670	- 2,027,849	
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu								

UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Kwa bei za miaka inayohusika)

Jedwali Na. 5

Shs. Milioni

Aina	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Majengo	17,908,862	19,195,447	22,807,556	27,721,670	33,872,241	41,694,655	50,257,469
Vifaa vya Usafiri	1,395,037	1,828,607	1,663,027	1,514,772	1,413,888	1,763,519	1,936,053
Mitambo na Vifaa	3,599,450	4,154,298	3,194,486	3,430,297	3,756,643	3,400,915	3,513,381
Mitambo na Vifaa vingine	987,752	1,156,588	1,172,391	1,366,982	1,441,018	1,688,577	1,787,804
Rasilimali za Mazao ya Mifugo	297,937	330,525	375,399	425,361	461,511	510,723	567,597
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu	591,860	734,368	857,335	1,033,744	1,196,620	1,328,698	1,467,676
Rasilimali za Kudumu	24,780,897	27,399,832	30,070,195	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,529,980
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables)	766,581	756,477	903,043	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337
Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories)	1,797,044	2,947,143	-65,636	-1,732,887	-2,720,674	-2,108,634	-5,328,628
Jumla ya Ukuzaji Rasilimali	27,344,522	31,103,452	30,907,602	34,865,346	40,427,427	49,493,556	55,474,690

Chanzo:Ofisi ya Taifa ya Taktamu

UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Bei za Mwaka 2015)							
Jedwali Na.6	Shs.Milioni						
Aina	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Majengo	19,218,436	19,485,103	22,807,556	27,512,753	32,836,681	38,590,978	45,285,927
Vifaa vya Usafiri	1,218,733	2,044,517	1,663,027	1,373,682	1,173,050	1,778,192	2,131,925
Mitambo na Vifaa	3,713,748	4,229,095	3,194,486	3,268,709	3,473,892	3,136,401	3,081,417
Mitambo na Vifaa vingine	1,061,609	1,200,328	1,172,391	1,323,953	1,335,724	1,525,517	1,566,066
Raslimali za Mazao ya Mifugo	332,936	364,963	375,399	385,150	414,428	434,150	473,265
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu	645,000	757,723	857,335	1,014,215	1,143,083	1,240,303	1,334,543
Raslimali za Kudumu	26,190,461	28,081,728	30,070,195	34,878,462	40,376,858	46,705,540	53,873,143
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables)	775,566	820,886	903,043	902,490	858,566	776,123	925,034
Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories)	2,053,216	2,901,191	-65,636	-1,985,783	-2,897,301	-2,812,030	-5,702,825
Jumla ya Ukuzaji Raslimali	29,019,243	31,803,806	30,907,602	33,795,169	38,338,123	44,669,633	49,095,353
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Kwa bei za miaka inayohusika)							Asilimia
Jedwali Na. 7A	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Aina							
Majengo	65.5	61.7	73.8	79.5	83.8	84.2	90.6
Vifaa vya Usafiri	5.1	5.9	5.4	4.3	3.5	3.6	3.5
Mitambo na Vifaa	13.2	13.4	10.3	9.8	9.3	6.9	6.3
Mitambo na Vifaa vingine	3.6	3.7	3.8	3.9	3.6	3.4	3.2
Raslimali za Mazao ya Mifugo	1.1	1.1	1.2	1.2	1.1	1.0	1.0
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu	2.2	2.4	2.8	3.0	3.0	2.7	2.6
Raslimali za Kudumu	90.6	88.1	97.3	101.8	104.2	101.8	107.3
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables)	2.8	2.4	2.9	3.2	2.5	2.5	2.3
Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories)	6.6	9.5	-0.2	-5.0	-6.7	-4.3	-9.6
Jumla ya Ukuzaji Raslimali	100	100	100	100	100	100	100
Chanzo:Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI (Kwa bei za miaka inayohusika)							Shs. Milioni
Jedwali Na.7B	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Sekta							
A. Raslimali za Kudumu	24,780,897	27,399,832	30,070,195	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,529,980
1. Serikali kuu	5,451,797	6,549,213	7,219,843	8,944,186	10,914,757	13,124,780	15,001,545
2. Mashirika	545,180	534,350	589,169	745,349	1,011,406	1,106,303	1,250,128
3. Taasisi	545,180	586,415	812,232	851,827	1,095,690	1,056,017	1,428,718
4. Sekta binafsi	18,238,741	19,729,853	21,448,950	24,951,465	29,120,067	35,099,986	41,849,589
B: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables)	766,581	756,477	903,043	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337
C. Ongezeko la Limbikizo	1,797,044	2,947,143	-65,636	-1,732,887	-2,720,674	-2,108,634	-5,328,628
D. Jumla ya Ukuzaji Raslimali	27,344,522	31,103,452	30,907,602	34,865,346	40,427,427	49,493,556	55,474,690
Chanzo:Ofisi ya Taifa ya Takwimu							

**FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO
NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Des.2015=100)**

Jedwali Na.8

MWAKA	BIDHAA ZOTE		CHAKULA	
	FAHIRISI	BADILIKO ASILIMIA	FAHIRISI	BADILIKO ASILIMIA
2001	25.9	8.5	24.0	8.9
2002	26.9	3.8	24.9	4.0
2003	28.4	5.8	26.3	5.4
2004	30.2	6.4	28.1	6.8
2005	32.7	8.3	30.1	7.3
2006	36.5	11.5	33.2	10.3
2007	39.9	9.3	36.3	9.3
2008	46.8	17.3	41.9	15.2
2009	54.7	16.8	50.0	19.4
2010	61.9	13.2	59.0	18.0
2011	66.5	7.4	63.2	7.1
2012	79.0	18.8	77.8	23.2
2013	86.3	9.3	86.0	10.5
2014	93.0	7.7	92.2	7.3
2015*	98.0	5.4	97.7	5.9
2016	102.2	4.3	101.2	3.6
2017	104.1	1.9	104.7	3.4
2018	106.1	2.0	109.4	4.5
2019	110.1	3.8	114.4	4.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (2001= 100)

Jedwali Na.9

Mwaka	Chakula	Vinywaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha, Vyombo Vya Nyumbani	Huduma Mahitaji ya Nyumbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote
2004	123.5	122.9	100.0	142.0	97.2	137.4	80.5	85.1	99.4	104.1	191.1	123.0	121.9
2005	125.7	120.0	113.6	162.3	108.7	115.7	110.0	113.6	110.4	109.8	115.0	121.1	126.5
2006	138.6	141.8	132.8	193.7	108.0	115.4	109.6	118.8	113.5	134.0	93.3	139.3	141.1
2007	151.5	159.5	146.1	209.1	124.1	131.7	119.1	114.8	148.5	114.9	104.0	128.4	154.2
2008	174.6	175.1	199.3	269.8	139.3	160.5	138.4	134.0	110.8	179.5	99.2	137.2	180.9
2009	208.5	210.8	206.6	276.6	152.8	173.3	167.1	163.8	124.7	225.9	111.3	147.7	211.3
FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Des. 2015 = 100)													
	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa ya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2011	63.16	61.31	68.58	73.79	83.74	82.85	73.17	99.72	68.03	102.59	67.21	69.09	66.48
2012	77.83	66.34	75.61	86.46	86.26	88.38	83.22	100.00	81.74	103.20	73.61	76.41	78.96
2013	85.98	75.34	85.60	88.69	88.81	90.62	86.32	100.00	90.84	102.73	85.16	84.36	86.34
2014	92.22	81.64	93.45	94.93	92.39	91.24	100.08	100.00	94.70	102.72	91.76	94.05	92.95
2015*	97.67	93.26	101.90	98.12	97.91	96.35	99.91	100.00	100.00	102.40	98.24	96.61	97.97
2016	101.19	100.89	99.41	105.13	100.55	108.05	100.84	100.57	101.22	97.07	104.92	102.41	102.21
2017	104.67	103.85	100.71	106.08	103.70	109.73	100.74	100.95	102.92	100.84	105.48	103.38	104.10
2018	109.36	103.85	103.87	112.15	105.67	109.80	88.19	100.86	104.08	106.36	105.60	105.01	106.15
2019	114.38	104.67	107.98	118.42	107.72	113.26	92.54	101.84	106.52	106.25	107.91	107.62	110.13

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Taktamu

NB. Wastani (Average) wa mwaka (kuanzia mwaka 2003, Fahirisi (Index) imekuwa ikitolewa kila mwezi katika miezi yote 12 ya mwaka

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya

Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizenzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA
WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Des.2015 =100)**

Jedwali Na.10

Mwaka	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne	Wastani	Badiliko Asilimia
2001	30.5	28.9	28.7	28.4	29.1	4.5
2002	30.0	30.0	30.2	30.4	30.2	3.5
2003	30.4	30.4	30.9	31.7	30.8	2.3
2004	32.8	33.1	33.5	34.2	33.4	8.2
2005	34.9	35.3	36.7	37.3	36.0	7.9
2006	38.3	39.4	39.5	40.2	39.3	9.2
2007	41.7	43.3	44.4	46.0	43.9	11.5
2008	48.5	49.9	51.2	52.7	50.6	15.3
2009	55.7	57.3	60.3	62.3	58.9	16.4
2010	63.9	64.6	65.1	65.6	64.8	10.0
2011	67.9	69.3	70.3	72.1	69.9	7.9
2012	78.4	81.6	82.7	83.4	81.5	16.6
2013	87.6	88.6	88.5	88.4	88.3	8.3
2014	92.8	94.2	94.5	93.5	93.7	6.2
2015*	96.5	98.9	100.6	100.0	99.0	5.6
2016	102.05	104.35	103.81	103.79	103.50	4.5
2017	104.48	106.72	106.65	107.02	106.22	2.6
2018	105.75	108.50	108.73	109.82	108.20	1.9
2019	111.91	113.48	112.96	113.96	113.08	4.5

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Jedwali Na.11

FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI DAR ES SALAAM (DES. 2015 = 100)

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji wenyewe kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa ya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirish aji	Mawasili ano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
Robo ya nne	66.7	68.9	72.1	51.7	75.9	77.1	68.8	97.3	75.2	67.4	69.4	69.1	65.6
2011 Robo ya kwanza	69.8	69.5	74.0	54.2	78.8	79.0	70.2	97.3	75.8	67.1	68.6	70.9	67.9
Robo ya pili	70.9	70.1	75.9	56.5	81.3	80.6	71.0	97.3	76.8	67.0	69.5	73.4	69.3
Robo ya tatu	72.1	71.3	75.9	57.6	82.0	80.8	71.1	97.4	77.0	67.2	70.0	75.1	70.3
Robo ya nne	75.1	72.0	76.3	58.1	82.5	80.8	71.6	97.6	77.7	67.3	70.0	75.9	72.1
2012 Robo ya kwanza	82.9	76.0	84.8	64.1	83.8	83.0	73.6	97.9	81.3	73.8	74.4	79.5	78.4
Robo ya pili	85.9	78.7	87.6	67.5	87.9	87.0	78.2	98.3	86.3	79.1	77.0	81.9	81.6
Robo ya tatu	87.1	81.2	89.5	68.4	89.0	87.9	78.5	98.4	89.2	81.3	78.6	83.1	82.7
Robo ya nne	87.6	82.2	91.9	69.4	89.6	88.8	78.1	98.5	89.4	82.7	79.5	84.6	83.4
2013 Robo ya kwanza	94.6	82.5	94.0	70.7	90.1	90.0	78.0	98.7	90.0	83.5	80.0	85.4	87.6
Robo ya pili	94.6	83.5	94.7	73.7	90.4	90.1	83.6	99.0	90.8	84.2	80.7	86.0	88.6
Robo ya tatu	92.7	86.2	95.6	76.2	90.8	91.3	88.0	99.2	91.5	85.9	81.6	88.2	88.5
Robo ya nne	91.7	88.0	95.7	77.5	91.3	91.7	89.5	99.2	92.2	86.8	82.5	88.8	88.4
2014 Robo ya kwanza	98.1	88.8	96.0	80.3	92.1	92.2	93.5	99.3	92.6	91.8	83.5	90.2	92.8
Robo ya pili	99.1	89.0	96.6	82.8	93.2	94.8	94.2	99.5	93.2	94.3	85.8	90.6	94.2
Robo ya tatu	97.3	92.9	97.3	86.8	96.7	97.0	96.3	100.0	95.0	95.9	88.0	93.6	94.5
Robo ya nne	93.7	97.0	98.0	89.6	99.0	97.8	97.7	100.0	97.2	95.9	90.5	95.7	93.5
2015* Robo ya kwanza	97.3	97.9	98.5	93.4	99.6	97.8	98.6	100.2	97.2	99.0	93.8	96.0	96.5
Robo ya pili	100.1	98.1	98.9	96.7	99.3	97.8	99.3	100.3	97.3	99.9	96.4	96.6	98.9
Robo ya tatu	101.8	98.9	99.0	99.4	99.4	98.4	100.5	100.2	98.2	100.0	98.0	96.7	100.6
Robo ya nne	100.4	100.0	99.8	99.5	99.9	99.6	100.1	100.0	100.1	100.0	99.0	99.2	100.0
2016 Robo ya kwanza	101.81	100.94	99.84	108.37	99.89	106.44	99.44	100.00	100.34	97.77	100.70	101.37	102.05
Robo ya pili	104.35	100.23	100.67	111.35	101.13	111.18	99.79	100.65	100.98	97.34	105.93	102.20	104.35
Robo ya tatu	103.90	101.28	99.83	107.36	100.24	113.92	100.57	101.22	101.05	97.34	106.92	102.16	103.81
Robo ya nne	102.52	102.55	100.25	110.34	102.43	114.81	99.94	101.34	101.94	97.34	105.83	103.52	103.79
2017 Robo ya kwanza	105.73	103.07	100.93	105.30	104.32	114.49	101.20	101.35	101.16	97.34	106.10	102.99	104.48
Robo ya pili	110.22	103.61	101.49	108.85	104.02	114.00	102.03	101.35	101.70	97.34	105.91	103.44	106.72
Robo ya tatu	107.86	103.86	101.84	115.20	104.13	114.10	99.40	101.34	101.41	97.34	106.27	103.89	106.65
Robo ya nne	107.75	103.85	101.95	117.53	104.36	114.48	99.98	101.28	101.91	97.34	106.27	103.25	107.02
2018 Robo ya kwanza	111.38	103.06	101.58	112.37	104.56	114.41	80.57	101.28	101.05	105.74	104.96	103.43	105.75
Robo ya pili	117.46	103.06	102.80	114.81	105.34	114.57	80.87	101.18	101.75	105.74	104.97	104.92	108.50
Robo ya tatu	116.84	103.06	104.34	116.35	105.73	114.65	81.26	101.12	101.55	105.74	105.55	105.35	108.73
Robo ya nne	115.96	103.21	106.12	121.73	106.68	114.80	84.15	101.17	102.12	105.74	106.91	106.24	109.82
2019 Robo ya kwanza	119.35	103.50	106.54	123.10	107.69	118.59	85.96	102.55	103.36	105.74	108.48	107.91	111.91
Robo ya pili	123.24	103.50	107.13	122.92	107.94	120.09	86.49	103.03	103.56	105.74	108.62	108.00	113.48
Robo ya tatu	121.21	103.50	107.82	124.54	107.77	120.10	86.49	102.29	104.49	105.74	108.59	107.40	112.96
Robo ya nne	123.84	103.50	107.79	125.41	108.11	120.21	86.11	102.45	103.13	105.74	108.15	107.64	113.96

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

Jedwali Na.12

FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Des. 2015=100)													
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji wenyewe kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa wya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasili ano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2011 Robo ya kwanza	61.1	73.8	80.7	70.9	86.7	85.2	70.8	94.9	89.3	82.1	67.5	83.9	68.7
Robo ya pili	62.4	74.8	83.8	72.0	89.5	87.7	77.2	94.9	91.2	82.1	72.2	85.6	70.8
Robo ya tatu	64.5	76.7	84.2	74.4	88.9	87.7	80.5	95.2	91.8	82.5	76.4	86.9	72.8
Robo ya nne	68.8	77.3	85.7	76.4	90.3	89.5	82.9	95.4	92.0	82.7	77.2	88.4	75.7
2012 Robo ya kwanza	72.8	78.2	88.7	77.3	92.9	91.5	82.4	95.4	92.8	82.7	78.7	91.3	78.0
Robo ya pili	74.2	78.6	89.2	79.8	94.2	91.9	83.3	95.4	93.0	82.7	79.6	95.4	79.5
Robo ya tatu	74.9	80.5	91.0	81.8	95.0	92.0	83.3	95.5	93.3	82.7	81.5	95.7	80.4
Robo ya nne	77.3	81.4	93.0	83.1	95.7	93.3	85.2	95.6	93.4	82.7	82.9	96.1	82.2
2013 Robo ya kwanza	83.1	81.4	93.8	83.9	96.1	94.8	86.4	95.5	93.9	84.4	84.9	96.4	85.5
Robo ya pili	81.7	82.1	95.2	83.4	96.3	94.8	94.1	95.7	96.1	84.4	85.3	96.8	85.6
Robo ya tatu	82.8	87.7	96.3	84.3	97.1	94.8	95.6	95.7	96.3	84.4	85.8	97.2	86.6
Robo ya nne	84.2	90.4	96.4	86.4	97.7	94.8	96.2	95.7	96.0	84.7	87.4	97.2	87.9
2014 Robo ya kwanza	88.5	90.4	97.5	87.6	97.7	95.5	96.6	95.7	98.8	95.7	87.9	99.0	90.6
Robo ya pili	87.9	90.4	97.6	88.1	98.5	97.7	97.6	95.7	98.9	98.6	88.0	99.8	90.7
Robo ya tatu	88.0	92.9	97.5	92.7	97.8	97.5	98.7	95.7	99.3	98.6	90.4	101.2	91.8
Robo ya nne	89.7	95.6	97.3	95.1	98.2	97.3	99.3	95.6	99.8	98.6	92.5	99.9	93.3
2015* Robo ya kwanza	92.5	96.7	97.8	95.2	98.3	97.5	101.2	97.6	99.7	100.0	95.4	100.2	95.1
Robo ya pili	95.1	98.1	97.8	96.0	98.2	97.5	102.5	97.7	100.0	100.0	97.5	98.6	96.8
Robo ya tatu	97.6	99.0	98.5	97.1	98.7	98.4	102.6	98.5	100.2	100.0	97.5	98.7	98.3
Robo ya nne	100.0	99.6	99.3	101.1	99.6	99.3	99.9	100.0	100.1	100.0	98.4	99.6	100.0
2016 Robo ya kwanza	102.6	100.4	99.8	105.2	100.2	107.3	98.6	100.0	100.4	98.6	100.4	101.4	101.0
Robo ya pili	105.3	100.9	100.7	107.2	103.0	111.9	98.9	100.6	101.3	98.4	103.1	102.0	102.5
Robo ya tatu	106.0	102.3	99.7	104.3	100.1	114.0	99.7	101.2	101.0	98.4	102.9	102.7	102.4
Robo ya nne	104.4	102.8	100.2	106.9	104.4	115.0	99.8	101.3	101.9	98.4	102.4	105.0	102.8
2017 Robo ya kwanza	107.4	102.9	101.3	105.5	107.3	115.2	101.7	101.3	100.1	98.4	102.5	105.3	104.0
Robo ya pili	112.6	103.8	102.0	105.8	107.7	114.7	103.2	101.3	100.6	98.4	103.1	105.4	105.8
Robo ya tatu	116.9	104.1	102.1	107.7	107.3	114.2	104.8	101.3	99.4	98.4	103.4	106.3	107.4
Robo ya nne	119.9	104.1	102.4	110.0	107.2	115.2	106.8	101.5	99.8	98.4	103.0	107.3	108.9
2018 Robo ya kwanza	120.6	104.1	102.8	110.4	107.6	115.1	107.8	101.7	100.4	101.4	103.0	105.2	109.5
Robo ya pili	121.9	104.1	103.9	112.9	108.6	115.1	110.4	101.8	100.9	107.6	103.2	106.6	111.2
Robo ya tatu	123.3	103.8	105.2	113.8	108.9	115.0	111.6	101.8	101.3	107.6	103.9	107.5	112.1
Robo ya nne	122.9	103.8	105.9	115.9	109.2	114.9	113.4	101.8	100.7	107.6	106.1	107.7	113.0
2019 Robo ya kwanza	124.8	103.9	106.1	116.4	110.4	118.4	113.5	103.3	101.3	107.6	108.2	107.7	113.9
Robo ya pili	128.5	103.9	106.8	123.5	110.8	120.1	114.4	103.8	101.8	107.6	108.3	107.7	116.0
Robo ya tatu	127.5	103.9	107.4	124.5	110.6	120.0	114.1	103.0	102.5	107.6	107.5	107.3	115.7
Robo ya nne	129.4	103.9	107.5	125.4	110.9	120.1	113.6	103.2	100.7	107.6	107.8	105.9	116.1

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo

FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WATU WENYE KIPATO
CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100)

Jedwali Na. 13

Mwaka	M I E Z I				Wastani	Badiliko Asilimia
	Machi	Juni	Sept.	Desemba		
2001	30.87	28.15	27.03	25.83	27.97	12.5
2002	28.96	28.88	28.93	28.89	28.91	6.6
2003	29.92	30.22	30.19	30.24	30.14	4.2
2004	30.98	31.77	32.30	33.02	32.02	6.2
2005	33.62	33.88	34.76	36.80	34.77	8.6
2006	37.88	38.51	38.90	40.13	38.86	11.8
2007	42.19	43.45	44.68	45.76	44.02	13.3
2008	48.86	50.13	53.91	55.41	52.08	18.3
2009	57.72	58.40	61.62	63.21	60.24	15.7
2010	63.41	64.89	65.82	66.29	65.10	8.1
2011	68.73	70.77	72.83	75.67	72.00	10.6
2012	78.04	79.50	80.40	82.20	80.04	11.2
2013	85.48	85.58	86.64	87.93	86.41	8.0
2014	90.61	90.68	91.84	93.27	91.60	6.0
2015*	95.14	96.78	98.27	100.00	97.55	6.5
2016	101.02	102.52	102.43	102.81	102.20	4.8
2017	104.01	105.76	107.37	108.93	106.52	4.2
2018	109.52	111.24	112.15	113.00	111.48	4.7
2019	113.92	115.99	115.74	116.09	115.44	3.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Jedwali Na.14

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDDUMA ZITUMIAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2015=100)

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vitaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Alya	Usaliris haji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2011 Robo ya kwanza	59.0	67.7	73.6	61.9	80.5	85.7	80.4	100.2	84.7	85.6	72.4	74.6	65.8
Robo ya pili	61.2	68.7	75.0	66.2	83.1	86.2	84.5	99.9	85.2	85.9	73.9	75.4	68.2
Robo ya tatu	64.4	69.7	76.9	70.3	84.6	86.5	86.6	100.7	86.1	85.9	75.9	77.9	71.0
Robo ya nne	69.0	70.3	79.5	71.8	86.1	87.6	88.1	100.7	86.3	85.9	78.0	80.3	74.2
2012 Robo ya kwanza	74.7	73.1	83.8	73.4	88.9	88.2	88.8	99.6	90.9	89.2	83.7	82.9	78.6
Robo ya pili	76.3	75.5	86.5	76.3	90.7	89.0	90.4	99.1	93.7	90.0	87.3	85.2	80.5
Robo ya tatu	76.3	83.3	87.8	80.4	91.8	89.4	90.5	99.1	96.0	90.0	88.5	85.9	81.4
Robo ya nne	78.5	85.4	89.0	84.1	93.1	90.1	90.5	98.9	95.7	90.0	90.5	87.1	83.4
2013 Robo ya kwanza	83.4	87.6	90.5	86.1	94.4	91.0	90.7	98.7	95.6	91.7	91.8	88.6	86.7
Robo ya pili	82.9	88.3	91.2	90.1	94.6	91.7	96.1	98.5	96.0	91.9	92.2	89.4	87.3
Robo ya tatu	81.6	92.4	92.3	90.7	95.0	91.9	97.8	99.0	96.4	92.1	92.3	90.9	86.9
Robo ya nne	83.7	93.5	92.8	92.0	95.6	92.0	98.4	99.1	96.4	92.1	92.9	91.7	88.4
2014 Robo ya kwanza	88.9	93.8	93.8	96.8	96.1	92.8	98.8	99.2	96.6	96.8	93.3	92.6	91.9
Robo ya pili	89.7	93.8	94.1	98.7	96.8	95.2	99.4	99.5	96.7	96.8	94.5	96.6	92.9
Robo ya tatu	88.6	96.8	94.5	100.5	96.9	95.8	100.0	99.9	96.9	96.8	95.2	96.6	92.7
Robo ya nne	89.2	98.6	96.5	101.1	96.9	96.2	99.6	99.7	97.0	96.8	96.1	96.7	93.3
2015* Robo ya kwanza	93.5	98.8	97.0	101.6	97.4	96.6	97.5	99.8	97.1	98.6	97.6	97.4	95.7
Robo ya pili	97.3	98.8	97.8	99.8	97.4	97.1	97.6	99.8	97.5	100.0	98.9	97.8	97.8
Robo ya tatu	97.5	99.4	99.1	101.1	98.7	98.4	100.3	99.7	98.9	100.0	99.8	98.5	98.5
Robo ya nne	98.9	99.8	99.7	100.9	99.3	99.5	99.8	100.0	100.1	100.0	100.0	99.8	99.4
2016 Robo ya kwanza	102.1	100.4	101.0	103.8	100.5	101.6	99.1	99.5	100.4	101.8	100.5	100.8	101.4
Robo ya pili	104.2	103.2	101.9	107.3	101.5	103.2	98.9	98.8	100.9	102.3	103.6	101.4	103.0
Robo ya tatu	103.9	104.4	102.8	107.8	101.9	104.0	99.8	99.1	101.2	102.6	104.4	101.9	103.3
Robo ya nne	105.1	104.9	103.3	110.1	103.1	104.6	100.0	99.1	101.7	102.6	104.1	102.6	104.2
2017 Robo ya kwanza	111.4	105.5	104.4	112.5	104.2	105.3	100.0	98.7	101.5	102.9	104.3	103.4	107.1
Robo ya pili	115.7	106.5	105.8	113.6	104.7	105.8	100.1	98.1	102.0	103.1	104.4	105.5	109.1
Robo ya tatu	113.2	107.0	106.4	116.7	104.8	106.2	99.5	98.1	102.7	103.4	104.4	105.7	108.6
Robo ya nne	112.9	107.5	106.5	118.8	105.1	106.7	100.1	98.1	103.2	103.5	104.5	105.4	108.9
2018 Robo ya kwanza	117.4	107.9	107.6	122.3	106.1	107.0	101.2	98.2	103.1	105.5	105.2	105.7	111.4
Robo ya pili	119.4	107.6	108.3	128.7	107.1	107.3	101.9	97.3	102.8	105.6	105.3	106.8	113.1
Robo ya tatu	115.9	108.4	109.4	131.4	107.8	107.5	102.4	95.5	102.7	106.0	105.7	107.0	112.2
Robo ya nne	113.9	109.6	110.2	134.4	108.5	107.7	104.5	95.5	102.6	106.0	106.7	107.5	112.3
2019 Robo ya kwanza	118.0	110.8	111.4	137.4	110.4	108.6	105.0	96.3	103.3	107.5	109.1	108.6	114.7
Robo ya pili	121.5	111.5	112.0	141.2	111.6	109.5	106.1	96.9	105.3	107.7	110.4	109.5	117.0
Robo ya tatu	119.9	110.9	112.3	139.6	111.9	109.5	105.8	96.3	104.6	107.7	110.5	109.6	116.2
Robo ya nne	120.5	110.7	112.7	139.6	112.2	109.5	105.8	96.4	104.1	107.7	110.7	109.7	116.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilisha na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitafifa (National Classification) hivyo

fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonia mwaka 2010 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa mifumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Des 2015=100)**


Jedwali Na.15

Mwaka	R o b o y a M w a k a				Wastani wa Fahirisi	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
2001	35.0	34.7	33.4	33.8	34.2	5.1
2002	35.4	35.6	35.5	36.3	35.7	4.3
2003	37.1	37.6	37.4	38.3	37.6	5.3
2004	39.0	39.0	39.1	40.4	39.4	4.7
2005	40.6	41.2	41.3	42.4	41.4	5.0
2006	43.8	44.9	43.7	45.1	44.4	7.3
2007	46.9	47.5	47.4	48.2	47.5	7.0
2008	51.1	51.9	52.3	54.2	52.4	10.3
2009	57.7	57.8	58.4	61.0	58.7	12.1
2010	61.3	62.1	61.9	62.4	61.9	5.5
2011	65.8	68.2	71.0	74.2	69.8	12.7
2012	78.6	80.5	81.4	83.4	81.0	16.0
2013	86.7	87.3	86.9	88.4	87.3	7.9
2014	91.9	92.9	92.7	93.3	92.7	6.1
2015*	95.7	97.8	98.5	99.4	97.9	5.6
2016	101.4	103.0	103.3	104.2	102.9	5.2
2017	107.1	109.1	108.6	108.9	108.4	5.3
2018	111.4	113.1	112.2	112.3	112.2	3.5
2019	114.7	117.0	116.2	116.4	116.1	3.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

MWENENDO WA KASI YA UPANDAJI BEI - Tanzania Bara



**FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (Des.2015=100)**

Jedwali Na.16

Mwaka	F A H I R I S I			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA	B A D I L I K O %			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA		
	KIPATO C H A				KIPATO C H A					
	CHINI	KATI	JUU		CHINI	KATI	JUU			
2001	25.9	29.1	28.0	34.2	8.5	4.5	12.5	5.1		
2002	26.9	30.2	28.9	35.7	3.8	3.5	3.3	4.3		
2003	28.4	30.8	30.1	37.6	5.8	2.3	4.3	5.3		
2004	30.2	33.4	32.0	39.4	6.4	8.2	6.2	4.7		
2005	32.7	36.0	34.8	41.4	8.3	7.9	8.6	5.0		
2006	36.5	39.3	38.9	44.4	11.5	9.2	11.8	7.3		
2007	39.9	43.9	44.0	47.5	9.3	11.5	13.3	7.0		
2008	46.8	50.6	52.1	52.4	17.3	15.3	18.3	10.3		
2009	54.7	58.9	60.2	58.7	16.8	16.4	15.7	12.1		
2010*	61.9	64.8	65.1	61.9	13.2	10.0	8.1	5.5		
2011	66.5	69.9	72.0	69.8	7.4	7.9	10.6	12.7		
2012	79.0	81.5	80.0	81.0	18.8	16.6	11.2	16.0		
2013	86.3	88.3	86.4	87.3	9.3	8.3	8.0	7.9		
2014	93.0	93.7	91.6	92.7	7.7	6.2	6.0	6.1		
2015*	98.0	99.0	97.5	97.9	5.4	5.6	6.5	5.6		
2016	102.2	103.5	102.2	102.9	4.3	4.5	4.8	5.2		
2017	104.1	106.2	106.5	108.4	1.9	2.6	4.2	5.3		
2018	106.1	108.2	111.5	112.2	2.0	1.9	4.7	3.5		
2019	110.1	113.1	115.4	116.1	3.8	4.5	3.6	3.4		

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Tawkimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

SURA YA 2

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

Ujazi wa Fedha

29. Mwaka 2019, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenyе lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi kwa ajili ya kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na ukuaji wa uchumi. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ilitumia nyenzo mbalimbali za utekelezaji wa sera ya fedha ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara hadi asilimia 7.0 kutoka asilimia 8.0. Aidha, Benki Kuu iliongeza wigo wa benki kutumia amana hizo kutoka asilimia 10 hadi asilimia 20 mwaka 2019. Vile vile, Benki Kuu iliendelea kuongeza ukwasi katika sekta ya kibenki kwa kutoa mikopo ya muda mfupi na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara na taasisi za Serikali.

30. Ujazi wa fedha uliendelea kuongezeka kwa kasi inayoendana na mahitaji mbalimbali ya shughuli za kiuchumi. Hadi Desemba 2019, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 9.6 na kufikia shilingi bilioni 28,313.1 kutoka shilingi bilioni 25,823.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 11.8 kutoka shilingi bilioni 19,040.4 Desemba 2018 na kufikia shilingi bilioni 21,280.3 Desemba 2019. Ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 13.7 na kufikia shilingi bilioni 13,325.1 kutoka shilingi bilioni 11,723.7 Desemba 2018. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi pamoja na rasilimali fedha za kigeni katika sekta ya benki.

Mwenendo wa Mikopo kwa Serikali Kuu na Sekta Binafsi

31. Mwaka 2019, mikopo kwa Serikali Kuu kutoka katika sekta ya benki ilipungua kwa asilimia 13.1 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 36.8 mwaka 2018. Kupungua kwa mikopo kulitokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na hivyo kuongeza amana za Serikali. Kwa upande mwingine, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 11.1 na kufikia shilingi bilioni 19,695.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2018. Ukuaji wa mikopo kwenye sekta ya kilimo, ujenzi na madini uliongezeka kwa asilimia 90.1,

asilimia 72.6 na asilimia 17.7 kwa mtiririko huo. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulitokana na usimamizi thabiti wa sera ya fedha, utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kupungua kwa mikopo chechefu kulikochangiwa na matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa zaidi katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 27.8 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 17.1.

Amana Katika Benki za Biashara

32. Amana katika benki za biashara ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 22,758.9 mwaka 2019 kutoka bilioni 20,921.3 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na jitihada za benki za biashara kuhamasisha wananchi kutunza fedha katika mfumo rasmi wa benki, kuongezeka kwa matawi ya benki na matumizi ya wakala wa benki. Amana za sekta binafsi ziliwuwa shilingi bilioni 21,777.5, sawa na asilimia 95.7 ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni ukilinganishwa na amana zote ulipungua na kufikia asilimia 27.1 mwaka 2019 kutoka asilimia 30.5 mwaka 2018.

Mwenendo wa Viwango vya Riba

33. Mwaka 2019, wastani wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki uliongezeka na kufikia asilimia 5.13 kutoka asilimia 2.21 mwaka 2018. Vile vile, riba za dhamana za Serikali ziliongezeka hadi asilimia 7.71 mwaka 2019 kutoka asilimia 6.43 mwaka 2018. Ongezeko hilo linaakisi uhitaji wa ukwasi katika mabenki kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mikopo kwa sekta binafsi kulikotokana na kupanuka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

34. Riba za mikopo kwa ujumla zilipungua hadi wastani wa asilimia 16.97 mwaka 2019 kutoka wastani wa asilimia 17.43 mwaka 2018. Riba za mikopo ya mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 16.69 kutoka asilimia 18.25 mwaka 2018. Kupungua kwa riba za mikopo kulitokana na jitihada za Serikali kuitia Benki Kuu katika kupunguza mikopo chechefu, uwepo wa ukwasi wa kutosha katika benki za biashara na kuboresha mazingira ya kufanya biashara. Aidha, riba za amana za muda maalumu kwa ujumla zilipungua hadi asilimia 7.25 mwaka 2019 kutoka asilimia 8.24 mwaka 2018. Riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 8.80 mwaka 2019 kutoka asilimia 8.78 mwaka 2018

MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki

35. Mwaka 2019, sekta ya benki iliendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha juu ya ukomo unaohitajika kisheria. Uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi ulifikia asilimia 32.4 Desemba 2019 kutoka asilimia 35.2 Desemba 2018 ikilinganishwa na uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20. Uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ulipungua hadi asilimia 16.7 Desemba 2019 kutoka asilimia 17.0 Desemba 2018, kiasi ambacho ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 10.

36. Hadi Desemba 2019, idadi ya benki na taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu zilifikia 60 (benki 51 na taasisi nyingine za fedha 9) ikilinganishwa na benki na taasisi za fedha 62 mwaka 2018. Hii ilitokana na benki ya UBL kuchukuliwa na benki ya Exim, na Bank M kuchukuliwa na benki ya Azania baada ya kuridhiwa na Benki Kuu. Aidha, benki ziliendelea kuongeza idadi ya matawi kutoka matawi 878 mwaka 2018 na kufikia matawi 941 mwaka 2019.

37. Katika kuimarisha huduma jumuishi za kifedha, idadi ya benki zinazotoa huduma kwa njia ya uwakala iliongezeka na kufikia benki 21 mwaka 2019 kutoka benki 17 mwaka 2018. Aidha, idadi ya mawakala wa utoaji huduma za kibenki iliongezeka kwa asilimia 50.6 na kufikia mawakala 28,358 mwaka 2019 kutoka mawakala 18,827 mwaka 2018. Miamala ya kuweka amana kuitia huduma za benki kwa njia ya uwakala iliongezeka kwa asilimia 57.9 na kufikia miamala 28,469,139 yenye thamani ya shilingi bilioni 18,938.7 mwaka 2019 kutoka miamala 18,034,023 yenye thamani ya shilingi bilioni 10,278.3 mwaka 2018. Vile vile, idadi ya miamala ya kutoa fedha ilifikia 17,460,891 mwaka 2019 ikilinganishwa na miamala 9,784,192 mwaka 2018. Kutokana na miamala hiyo, fedha taslimu zilizotolewa kwa mwaka 2019 zilikuwa shilingi bilioni 5,929.5 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 3,070.5 mwaka 2018.

38. Rasilimali za sekta ya benki ziliimarika kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kutoka asilimia 10.7 Desemba 2018 na kufikia asilimia 9.8 Desemba 2019. Hii ilitokana na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwa ni pamoja na kuhimiza benki za biashara kupeleka taarifa za mikopo kwenye kanzidata na kutumia taarifa za historia za wakopaji zilizo kwenye

kanzidata kabla ya utoaji wa mikopo na kuzihimiza benki na taasisi za fedha kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo.

Huduma Ndogo za Fedha

39. Mwaka 2019, Serikali ilitunga Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018. Serikali iliandaa Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017 baada ya mapitio ya Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000. Lengo kuu la Sera hiyo ni kuimarisha huduma jumuishi kwenye sekta ndogo ya fedha kwa kujenga mazingira wezeshi yatakayoleta ufanisi wa utoaji huduma za fedha kwa wananchi. Sera hiyo ilielekeza kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ili kulinda watumiaji wa huduma hizo pamoja na kuondoa changamoto zilizokuwepo katika kusimamia sekta hiyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 ili kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha na kuhamasisha ukuaji na uendelezaji wa sekta hiyo. Aidha, Sheria hiyo imeipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

40. Mwaka 2019, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilitoa leseni kwa watendaji na washauri wa uwekezaji katika masoko ya mitaji ambapo hadi Desemba 2019 leseni 76 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 74 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Aidha, Mamlaka kupitia masoko ya awali iliidhinisha maombi ya kuuza hatifungani za Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania zenye thamani ya shilingi bilioni 120.0. Vile vile, Mamlaka iliidhinisha maombi ya kuuza hisa 33,913,948 za benki ya biashara ya DCB zenye thamani ya shilingi bilioni 8.98.

41. Mwaka 2019, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yalikuwa shilingi bilioni 624.82 ikilinganishwa na shilingi bilioni 504.82 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya hisa katika kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, Tanzania Breweries Limited na CRDB Bank PLC. Aidha, mtaji wa soko ulikuwa shilingi trilioni 17.10 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi trilioni 19.68 mwaka 2018. Kupungua kwa mtaji wa soko kulichangiwa na kuondolewa kwa kampuni ya Acacia katika Soko la Hisa la Dar es Salaam baada ya kampuni hiyo kuondolewa katika Soko la Hisa la London.

42. Hadi Desemba 2019, hatifungani za Serikali zenyenye thamani ya shilingi trilioni 10.28 ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na hatifungani zenyenye thamani ya shilingi trilioni 9.11 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 12.8. Mauzo ya hatifungani za Serikali katika soko yalifikia shilingi trilioni 1.10 Desemba 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 965.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Aidha, hatifungani za kampuni zenyenye thamani ya shilingi bilioni 704.81 ziliorodheshwa ikilinganishwa na hatifungani zenyenye thamani ya shilingi milioni 682.67 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Mauzo ya hatifungani za kampuni yalifikia shilingi milioni 757.36 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi milioni 677.87 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 11.7. Kwa upande mwingine, idadi ya wawekezaji katika soko la mitaji na dhamana ilifikia 689,495 ikilinganishwa na wawekezaji 672,209 Desemba 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Kulingana na fahirisi ya soko la hisa, Soko la Hisa la Dar es Salaam lilipata alama 2,059.21 mwaka 2019 ikilinganishwa na alama 2,041.39 mwaka 2018. Kuongezeka kwa alama ya fahirisi kunaashiria ufanisi wa soko hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

43. Mwaka 2019, Kampuni ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS iliendesha Mfuko wa Ukwasi, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Jikimu na Mfuko wa Umoja. Katika kipindi hicho, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilikuwa shilingi bilioni 304.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 281.7 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya vipande katika mifuko hiyo. Aidha, thamani ya kipande katika Mfuko wa Ukwasi iliongezeka hadi shilingi 227.77 mwaka 2019 kutoka shilingi 199.88 mwaka 2018. Thamani ya kipande katika Mfuko wa Jikimu ilifikia shilingi 130.24 kutoka shilingi 128.75 mwaka 2018. Vile vile, thamani ya kipande katika Mfuko wa Watoto iliongezeka na kufikia shilingi 353.55 kutoka shilingi 332.0 mwaka 2018. Vile vile, thamani za vipande katika mifuko ya Wekeza Maisha na Umoja ziliongezeka na kufikia shilingi 426.28 na shilingi 601.49 mwaka 2019 kutoka shilingi 377.69 na shilingi 570.17 mwaka 2018 kwa mtiririko huo. Ongezeko la thamani ya vipande lilitokana na kuhamasika kwa wananchi kufuatia elimu iliyotolewa kuhusu faida za kuwekeza katika vipande. Mchanganuo wa thamani ya mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.1**.

Jedwali Na. 2.1: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Shilingi Milioni)

Aina ya Uwekezaji	2017	2018	2019	Ukuaji (asilimia)
Umoja	214,658.83	218,809.27	217,343.59	-0.7
Jikimu	21,687.04	20,280.46	19,775.64	-2.5
Wekeza	1,488.96	1,193.82	1,175.29	-1.6
Watoto	3,532.13	3,154.30	3,205.69	1.6
Ukwasi	15,113.44	38,230.54	62,690.47	64.0
Jumla	256,480.40	281,668.39	304,190.68	8.0

Chanzo: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)

44. Mwaka 2019, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulisajili wanachama wapya 12,809 ikilinganishwa na wanachama 6,705 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 91.0. Kati ya hao, wanachama 11,528 walisa jiliwa kutoka kwenye sekta ya umma na wanachama 1,281 kutoka sekta binafsi. Aidha, Mfuko ulikusanya shilingi trilioni 1.3 mwaka 2019 kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.7 mwaka 2018. Upungufu wa makusanyo ultokana na baadhi ya wanachama wa sekta binafsi waliokuwa wakichangia kwenye mfuko kuhamia mfuko wa NSSF. Kwa upande mwingine, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 1,500.9 kwa wanachama 23,504 mwaka 2019, ikilinganishwa na mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 321.4 yaliyolipwa kwa wanachama 12,124 mwaka 2018.

45. Mwaka 2019, mapato yaliyotokana na uwekezaji wa Mfuko yalikuwa shilingi bilioni 429.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,119.8 mwaka 2018. Kupungua kwa mapato kulitokana na kupungua kwa uwekezaji uliosababishwa na ongezeko la malipo ya mafao ikilinganishwa na mapato ya Mfuko. Hadi Desemba 2019, thamani ya Mfuko ilikuwa shilingi trilioni 5.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 6.3 mwaka 2018. Kupungua kwa thamani ya Mfuko kulitokana na kuendelea na ulipaji wa madeni hususan madeni ya wanachama.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

46. Wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii waliongezeka na kufikia 1,348,210 mwaka 2018/19 kutoka wanachama 1,297,499 mwaka 2017/18. Kati ya hao, wanachama waliokuwa wakichangia walikuwa 520,708

sawa na asilimia 38.6 ya wanachama wote. Michango iliyokusanya kutoka kwa wanachama ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 926,002.08 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na shilingi milioni 728,736.26 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 27.1. Aidha, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalikuwa na thamani ya shilingi milioni 375,726.07 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na shilingi milioni 401,758.58 zilizolipwa mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Upungufu huo ilitokana na kusimamishwa kwa ulipaji wa fao la kujitoa.

47. Thamani ya uwekezaji katika vitega-uchumi iliongezeka kwa asilimia 11.1 na kufikia shilingi bilioni 2,502.54 mwaka 2018/19 kutoka shilingi bilioni 2,252.60 mwaka 2017/18. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye dhamana za Serikali kutoka shilingi bilioni 325.42 mwaka 2017/18 hadi shilingi bilioni 655.20 mwaka 2018/19. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji katika vitegauchumi yalipungua kwa asilimia 8.5 kutoka shilingi bilioni 185.23 mwaka 2017/18 hadi shilingi bilioni 169.53 mwaka 2018/19. Kwa upande mwingine, rasilimali za Mfuko ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 3,909.19 mwaka 2018/19 kutoka shilingi bilioni 3,462.93 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Rasilimali halisi za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 3,665.32 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,191.99 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 14.8.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

48. Hadi Desemba 2019, waajiri waliosajiliwa na Mfuko waliongezeka kwa asilimia 35.5 na kufikia waajiri 20,102 mwaka 2019 kutoka waajiri 14,836 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na utoaji elimu kwa waajiri, wafanyakazi na wadau mbalimbali pamoja na kufanya kaguzi. Katika kipindi hicho, michango ya wanachama ilikuwa shilingi bilioni 108.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 116.7 Desemba 2018.

49. Mapato ya Uwekezaji wa Mfuko yaliongezeka hadi shilingi bilioni 25.02 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 17.9 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 39.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa michango ya waajiri na Mfuko kuwekeza kiwango kikubwa kwenye hatifungani za Serikali za muda mrefu zenye faida kubwa.

50. Mfuko ultumia shilingi bilioni 4.69 kulpia matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.85 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asimilia 64.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa madai ya wafanyakazi walioumia, kuugua au kufariki wakiwa kazini. Aidha, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilima 29.2 na kufikia shilingi bilioni 278.13 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 215.29 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa makusanyo ya michango ya waajiri pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na uwekezaji.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

51. Idadi ya wanachama wachangiaji katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliongezeka na kufikia wanachama 966,792 mwaka 2018/19 kutoka wanachama 858,446 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Ongezeko hilo lilitokana na utoaji elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kujiunga na bima ya afya pamoja na kujumuisha wakulima na makundi mengine kutoka sekta isiyo rasmi kwenye huduma ya bima ya afya. Mwaka 2018/19, Mfuko ulihudumia wanufaika 16,825,479 ikilinganishwa na wanufaika 17,425,329 mwaka 2017/18. Kati ya hao, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa na wanufaika 4,025,693 sawa na asilimia 7.4 ya watu Tanzania Bara na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na wanufaika 12,799,786 sawa na asilimia 23.6 ya watanzania wote.

Jedwali Na. 2.2: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Wanachama (NHIF)	Wanufaika NHIF	Wanufaika CHF	Jumla ya wanufaika (NHIF na CHF)
2016/17	753,892	3,491,400	12,183,996	15,675,396
2017/18	858,446	3,918,999	13,506,330	17,425,329
2018/19	966,792	4,025,693	12,799,786	16,825,479
Ukuaji (Asilimia)	12.6	2.7	-5.2	-3.4

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

52. Aidha, vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na Mfuko vilikuwa 7,606 mwaka 2019 ikilinganishwa na vituo 7,031 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Kati ya hivyo, vituo 5,596 sawa na asilimia 74 vilikuwa vya Serikali, vituo 758 sawa na asilimia 10 vilikuwa vya mashirika ya dini na vituo binafsi vilikuwa 1,252 sawa na asilimia 16.

Jedwali Na. 2.3: Mchanganuo wa Vituo vya Afya Vilivyosajiliwa

Aina ya Kituo	2017/18	2018/19	Ukuaji (Asilimia)
Zahanati	5,401	5,753	6.5
Vituo vya Afya	713	766	7.4
Hospitali	286	298	4.2
Maduka ya dawa	349	449	28.7
Maduka ya dawa maalum	202	200	-1.0
Kliniki maalum	73	130	78.1
Vituo vya uchunguzi	6	9	50.0
Vituo vya uokozi	1	1	0
Jumla	7,031	7,606	8.2

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

53. Mwaka 2018/19, mapato ya Mfuko yalipungua na kufikia shilingi milioni 502,880.44 kutoka shilingi milioni 503,801.68 mwaka 2017/18. Hii ilichangiwa na kupungua kwa mapato ya uwekezaji kutokana na kushuka kwa riba kwenye masoko ya fedha. Aidha, thamani ya rasilimali za Mfuko ilikuwa shilingi bilioni 1,343.7 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,382.8 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 2.8. Upungufu huo ulichangiwa na ongezeko la malipo kwa watoa huduma kutokana na kupanda kwa gharama za huduma na dawa

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA)

54. Hadi Desemba 2019, kampuni za bima zilizosajiliwa kufanya biashara ya bima nchini zilifikia 32 ikilinganishwa na kampuni 31 mwaka 2018. Aidha, Mamlaka ilisajili kampuni za udalali wa bima 101, mawakala 643 na wakadiriaji hasara 58 ikilinganishwa na kampuni za udalali wa bima 109, mawakala 635 na wakadiriaji hasara 55 mwaka 2018. Vile vile, mikataba ya bima iliyotolewa na kampuni za bima iliongezeka kwa asilimia 32.9 na kufikia 4,054,711 mwaka 2019 kutoka mikataba 3,050,167 mwaka 2018.

55. Mauzo katika soko la bima yaliongezeka kwa asilimia 17.3 na kufikia shilingi bilioni 811.6 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 691.9 mwaka 2018. Hii ilitokana na utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kuhakiki bima ya vyombo vya moto, kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya bima na kampuni

za ndani kutoa huduma ya bima kwenye miradi mikubwa ya ujenzi. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 693.4 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 687.6 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bima za uhandisi katika miradi mikubwa ya ujenzi pamoja na bima za anga katika ununuvi wa ndege za kampuni za hapa nchini. Vile vile, mauzo ya bima za maisha yaliongezeka kwa asilimia 13.2 hadi shilingi bilioni 118.1 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 104.3 mwaka 2018. Bima za kawaida zilichangia asilimia 85.4 ya mauzo yote ya bima mwaka 2019 na bima za maisha zilichangia asilimia 14.6.

56. Mwaka 2019, thamani ya mali za kampuni za bima zilifikia shilingi bilioni 1,045.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 936.0 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 11.7. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bima. Aidha, uwekezaji wa kampuni za bima ulikuwa shilingi bilioni 729.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 647.3 mwaka 2018. Uwekezaji huo ulijumuisha amana katika taasisi za fedha, fedha taslimu na amana za benki (asilimia 52.4), dhamana za Serikali (asilimia 22.7), mali zisizohamishika (asilimia 11.5), hisa (asilimia 11.2) na uwekezaji mwingine wa fedha (asilimia 2.1). Madeni ya kampuni za bima yalifikia shilingi bilioni 729.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 655.2 mwaka 2018. Tofauti kati ya mali na madeni ya makampuni iliongezeka kwa asilimia 12.7 na kufikia shilingi bilioni 316.7 mwaka 2019 kutoka shilingi bilioni 280.9 mwaka 2018.

Jedwali Na. 2.4: Thamani ya Mali na Madeni ya Kampuni za Bima (Shilingi Milioni)

Mali na Madeni	2018	2019	Ongezeko (asilimia)
Jumla ya Mali	936,026	1,045,896	11.7
Jumla ya Madeni	655,184	729,210	11.3
Ziada ya Mali	280,911	316,687	12.7
Uwekezaji wa Kampuni	647,294	729,452	12.7

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima

57. Mwaka 2018/19, Shirika la Bima la Taifa liliendelea kutoa huduma za bima ya maisha na bima nyingine kupitia matawi na wakala waliopo nchi nzima. Katika kipindi hicho, jumla ya wateja 440,552 walihudumiwa ambao walijumuisha wateja 394,906 wa bima ya maisha, wateja 45,005 wa bima za vyombo vy'a moto na wateja 641 wa bima nyingine.

58. Mwaka 2018/19, mapato ya Shirika yalifikia shilingi bilioni 75.2 ikilinganishwa shilingi bilioni 61.2 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 22.9. Aidha, thamani ya mali za Shirika iliongezeka na kufikia shilingi milioni 281.7 mwaka 2018/19, kutoka shilingi milioni 257.0 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bima zilizotolewa na Shirika (*underwritten policies*). Vile vile, thamani ya fidia iliyotolewa na Shirika iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 12.3 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.8 mwaka 2017/18. Kuongezeka kwa kiwango cha fidia iliyolipwa kulitokana na utekelezaji wa mkakati wa Shirika uliolenga kupunguza malimbikizo ya madai na hivyo kuongeza imani katika soko na kuvutia wateja.

Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania

59. Mwaka 2019, mikopo 5,411 ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni 432.3 ilitolewa ikilinganishwa na mikopo 4,996 yenye thamani ya shilingi bilioni 421.07 mwaka 2018. Kati ya mikopo hiyo, Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47.4 kwa benki saba (7) zinazota mikopo ya nyumba na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa hadi Desemba 2019 kufikia shilingi bilioni 149.5. Kuongezeka kwa mikopo ya nyumba iliyotolewa kulitokana na kushuka kwa riba za mikopo kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.5 kwa benki wanachama na asilimia 10 hadi asilimia 8.5 kwa benki zisizo wanachama. Kupungua kwa riba kulitokana na Serikali kupitia Benki Kuu kupunguza riba ya mikopo kwa Kampuni ya Mikopo ya Nyumba kwa asilimia 1.5.

Jedwali Na.2.5: Mikopo iliyotolewa na Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania

Benki	Thamani ya mkopo (Shilingi Milioni)	Asilimia
CRDB Bank Plc	27,000	18
Azania Bank Limited	18,500	12
National Bank of Commerce Limited	13,000	9
Barclays Bank (T) Limited	12,000	8
NMB Bank Plc	11,700	8
Bank of Africa (T) Limited	10,750	7
Commercial Bank of Africa (T) Limited	10,000	7
KCB Bank (T) Limited	10,000	7
African Banking Corporation (T) Limited	6,400	4
Exim Bank (T) Limited	6,000	4
Mkombozi Commercial Bank Plc	6,000	4
Stanbic Bank (T) Limited	5,900	4
DCB Commercial Bank Plc	3,500	2
I & M Bank (T) Limited	3,250	2
Peoples Bank of Zanzibar	3,000	2
First National Bank (T) Limited	2,500	2
Jumla	149,500	100

Chanzo: Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania

60. Mwaka 2019, thamani ya mali za Kampuni ya Mikopo ya Nyumba ilikuwa shilingi bilioni 201 ikilinganishwa na shilingi bilioni 136 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 47.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mikopo mipy ya nyumba, utoaji wa hatifungani za taasisi/kampuni kwenye soko la mitaji, ongezeko la mtaji kutoka kwa wanahisa na limbikizo la faida. Aidha, Kampuni ilipata faida ya shilingi bilioni 1.01 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.1 mwaka 2018. Wananchi 923 walinufaika na mikopo iliyotolewa kuititia benki zilizokopeshwa na Kampuni. Kati ya hao, wanaume walikuwa 604, wanawake 264 na waliokopa kwa pamoja (mwanaume na mwanamke) walikuwa 55.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

61. Mwaka 2019, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 59.59. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 13.14 zilitolewa kwa miradi sita (6) ya umwagiliaji inayofanywa na vyama vya

wakulima wadogo wadogo katika mikoa ya Iringa, Njombe, Pwani, Morogoro na Tanga pamoja na mradi mkubwa wa mazao ya nafaka uliopo Kagera. Mwaka 2019, wakulima 2,130,849 walinufaika na mikopo ikilinganishwa na wakulima 1,994,726 mwaka 2018.

62. Mwaka 2019, Benki ilipata faida ya shilingi bilioni 3.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.9 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 63.2. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya uwekezaji. Hadi Desemba 2019, Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo unaosimamiwa na Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 36.4 kwa wanufaika 5,808.

Benki ya TPB

63. Mwaka 2019, amana za wateja katika benki ya TPB zilifikia shilingi milioni 498,200 kutoka shilingi milioni 453,531 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wateja 51,322 na kufikia jumla ya wateja 581,586 Desemba 2019. Aidha, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 420,200 ikilinganishwa na shilingi milioni 412,769 mwaka 2018. Uwekezaji wa Benki katika dhamana za Serikali uliongezeka kwa asilimia 77.0 na kufikia shilingi milioni 100,588 mwaka 2019 kutoka shilingi milioni 56,819 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa amana za wateja. Kwa upande mwingine, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia asilimia 5.4 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2018. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na ufuutiliaji wa mikopo iliyotolewa kwa wateja pamoja na utumiaji wa kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo. Pato ghafi la Benki liliongezeka kwa asilimia 10.6 na kufikia shilingi milioni 129,800 kutoka shilingi milioni 117,400 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika dhamana za Serikali.

Soko la Bidhaa Tanzania

64. Mwaka 2018/19, Soko la Bidhaa Tanzania lilitoa elimu kwa wadau 13,285 katika mikoa mbalimbali nchini ambapo wananchi 6,502 walinufaika kwa kushiriki kwenye minada. Katika kipindi hicho, wakulima wa ufuta kupitia vyama vya ushirika waliwezesha kufanya mauzo kwa njia ya kielektroniki katika Soko la Bidhaa. Mwaka 2018/19, bei ya ufuta iliongezeka na kufikia shilingi 3,000 kwa kilo ikilinganishwa na shilingi 1,500 kwa kilo kabla ya zao hilo kuanza kuuzwa kupitia Soko hilo. Aidha, minada minne ilikamilika ambapo

jumla ya shilingi bilioni 1.47 zililipwa kwa wakulima kupitia akaunti zao za benki na vyama vyaa ushirika.

MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 17

Sh. Bilioni

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba							Badiliko 2016/17	
	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Kiasi	%
Fedha ya msingi (M0)	5,027.8	5,909.5	6,833.1	6,854.4	6,954.4	6,992.9	7,466.4	473.5	6.8
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	7,218.1	8,284.2	9,575.7	10,083.8	11,155.3	11,723.7	13,325.1	1,601.4	13.7
Amana za Akiba na za muda maalum	4,672.4	5,632.9	6,204.4	6,536.5	7,194.6	7,316.7	7,955.1	638.4	8.7
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	11,890.6	13,917.0	15,780.1	16,620.3	18,349.9	19,040.4	21,280.3	2,239.9	11.8
Amana za fedha za kigeni	4,216.2	4,697.1	6,335.2	6,257.5	6,364.4	6,783.06	7,032.89	249.8	3.7
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	16,106.8	18,614.2	22,115.3	22,877.8	24,714.3	25,823.5	28,313.1	2,489.7	9.6
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	6,576.3	6,551.5	8,244.0	8186.3	11596.1	10629.8	12034.5	1,404.7	13.2
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	9,530.4	12,062.6	13,871.3	14,691.6	13,118.2	15,193.7	16,278.6	1,084.9	7.1
Karadha Nchini	16,293.0	18,863.7	22,505.5	23,775.8	24,977.2	26,249.3	28,103.3	1,854.0	7.1
Madai halisi kwa serikali kuu	2,554.6	3,651.6	4,881.6	4,282.0	3,275.7	4,481.6	3,893.9	-587.7	-13.1
Mikopo kwa serikali kuu	5,900.4	6,451.5	7,012.8	7,166.9	8,081.8	8,522.5	8,408.0	-114.5	-1.3
Mikopo kwa sekta binafsi	10,392.7	12,412.3	15,492.7	16,608.9	16,895.4	17,726.8	19,695.4	1,968.6	11.1
Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara	3345.8	2799.8	2131.1	2,884.9	4,806.1	4,040.9	4,514.1	473.2	11.7
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	-3,416.8	-4,001.3	-6,503.1	-6,199.3	-7,052.9	-7,014.7	-7,310.7	-296.0	4.2

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 18

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba						
	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Fedha ya msingi (M0)	11.1%	17.5%	15.6%	0.3%	1.5%	0.6%	6.8%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	10.4%	14.8%	15.6%	5.3%	10.6%	5.1%	13.7%
Amana za Akiba na za muda maalum	11.6%	20.6%	10.1%	5.4%	10.1%	1.7%	8.7%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	10.9%	17.0%	13.4%	5.3%	10.4%	3.8%	11.8%
Amana za fedha za kigeni	7.5%	11.4%	34.9%	-1.2%	1.7%	6.6%	3.7%
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	10.0%	15.6%	18.8%	3.4%	8.0%	4.5%	9.6%
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	2.8%	-0.4%	25.8%	-0.7%	41.7%	-8.3%	13.2%
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	15.5%	26.6%	15.0%	5.9%	-10.7%	15.8%	7.1%
Karadha Nchini	18.8%	15.8%	19.3%	5.6%	5.1%	5.1%	7.1%
Madai halisi kwa serikali kuu	26.5%	42.9%	33.7%	-12.3%	-23.5%	36.8%	-13.1%
Mikopo kwa serikali kuu	25.3%	9.3%	8.7%	2.2%	12.8%	5.5%	-1.3%
Mikopo kwa sekta Binafsi	15.3%	19.4%	24.8%	7.2%	1.7%	4.9%	11.1%
Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara	24.4%	-16.3%	-23.9%	35.4%	66.6%	-15.9%	11.7%
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	23.0%	17.1%	62.5%	-4.7%	13.8%	-0.5%	4.2%

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.19

	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Shs/Dola mwisho wa mwaka	1,605.35	1,578.41	1,600.46	1,723.69	2,148.52	2,172.62	2,230.07	2,281.23	2,287.93
Badiliko la thamani ya shilingi (%)	9.74	-1.68	1.40	7.70	24.65	1.12	2.64	2.29	0.29
Shs/Dola wastani wa mwaka	1,572.22	1,583.00	1,605.39	1,652.51	1,985.39	2,177.07	2,228.86	2,264.14	2,288.56
Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%)	11.6	0.7	1.4	2.9	20.1	9.7	2.4	1.6	1.1

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 20

Aina ya Shughuli	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Billioni)							Ukuaji (%)	Mchango (%)
	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019		
Uzalishaji katika Kilimo	965	1,057	1,174	1,108	1,135	953	1,811	90.1	9.2
Huduma za Kifedha Madini na Uchimbaji	251	311	405	389	292	173	202	16.6	1.0
Mawendo Viwanda	97	166	275	329	293	361	425	17.7	2.2
Majengo na Ujenzi	1,161	1,386	1,696	1,628	1,778	1,938	2,071	6.9	10.5
Uchukuzi na Mawasiliano	514	660	741	741	837	643	1,110	72.6	5.6
Biashara	728	926	1,232	1,181	976	930	1,052	13.2	5.3
Utalii	2,162	2,652	3,078	3,349	3,307	3,277	3,375	3.0	17.1
Mahoteli na Migahawa	113	129	177	198	176	141	144	2.1	0.7
Umeme	371	436	515	526	595	583	534	-8.4	2.7
Watu Binafsi	403	441	440	430	335	356	183	-48.7	0.9
Sekta Nyinginezo	1,745	2,104	2,732	2,982	3,259	4,923	5,484	11.4	27.8
Jumla	10,392.7	12,412.3	15,492.7	16,608.9	16,895.4	17,726.8	19,695.4	11.1	100.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA							Sh. Bilioni
Jedwali Na.21	Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba						
	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2018/19 (%)
Amana za Sekta Binafsi							
Amana za Hundu/Zinazaohamishika	5,026.6	5,772.1	5,941.5	6,685.3	7,031.7	7,866.5	11.9
Amana za Akiba na za Muda Maalum	5,498.9	6,086.8	6,415.6	7,052.2	7,154.7	7,750.4	8.3
Amana za fedha za kigeni	4,670.4	6,301.8	5,831.5	6,087.1	6,376.3	6,160.6	-3.4
Jumla	15,195.9	18,160.7	18,188.7	19,824.6	20,562.8	21,777.5	5.9
Amana za Serikali	808.9	857.0	577.8	560.6	358.5	981.3	173.7
Jumla za Amana zote	16,004.8	19,017.7	18,766.5	20,385.1	20,921.3	22,758.9	8.8
Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania							

VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA						
Jedwali Na. 22	Asilimia					
Aina ya Riba	Wastani wa mwaka					
	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Riba ya Benki kuu (Discount rate)	16.00	16.00	16.00	16.00	7.00	7.00
Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla	9.12	11.23	13.47	6.00	2.21	5.13
Riba za dhamana za serikali kwa ujumla	13.56	12.91	16.17	11.10	6.43	7.71
Siku 91	12.08	8.80	7.85	5.49	2.89	4.17
Siku 182	13.66	13.04	15.84	10.01	4.13	5.07
Siku 364	13.98	13.92	16.56	11.79	7.08	8.04
Riba za amana						
Amana za akiba	3.13	3.45	3.35	3.03	2.52	2.44
Amana za muda maalum kwa ujumla	8.44	8.89	9.19	10.04	8.24	7.25
Mwaka mmoja	10.85	10.80	11.47	11.66	8.78	8.80
Riba za mikopo						
Mikopo kwa ujumla	16.29	16.10	15.96	17.77	17.43	16.97
Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja	14.70	14.25	13.66	18.30	18.25	16.69
Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania						

SURA YA 3

FEDHA ZA SERIKALI

Utangulizi

65. Bajeti ya mwaka 2019/20 iliandaliwa kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya kuwainua wananchi kiuchumi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini. Bajeti hii imeendelea kufungamanisha juhudzi za kuimarishe sekta ya viwanda na uendelezaji wa sekta ya kilimo inayoajiri wananchi wengi na hasa waishio vijijini na kuimarishe huduma za jamii. Dhima kuu ya bajeti ya mwaka 2019/20 iliendelea kuwa "**kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii**".

66. Katika bajeti ya mwaka 2019/20, Serikali ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: Kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini; kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na ziada kwa ajili ya kuuza nje, pamoja na kuongeza fursa za ajira; kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili (ASDP II); kuimarishe upatikanaji wa huduma za jamii; kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya nishati na uchukuzi; kutekeleza mpangokazi wa kuboresha mazingira ya biashara; na kuimarishe ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote.

67. Shabaha za bajeti ya mwaka 2019/20 zililenga kuwa na ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 7.1 mwaka 2019; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kuwa asilimia 15.8 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 22.7 ya Pato la Taifa; na nakisi ya bajeti kufikia asilimia 2.3 ya Pato la Taifa.

68. Mwaka 2019/20, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 33, 105.4 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 23,045.3 sawa na asilimia 69.6 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo ya ndani, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 19,100.9 sawa na asilimia 12.9 ya Pato la

Taifa. Mapato yasiyo ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 3,178.9 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 765.5.

Mwenendo wa Mapato

Mapato ya Ndani

69. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, makusanyo ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 16,075.0 sawa na asilimia 92.5 ya lengo la shilingi bilioni 17,375.9. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 14.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14,071.1 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Ukuaji huo umetokana na: Kuongezeka kwa utoaji wa elimu kwa walipakodi; wananchi kuhamasika kulipa kodi kutokana na kuimarika kwa utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii ikijumuisha maji, elimu, afya, miundombinu wezeshi ya barabara na umeme; kuongezeka kwa uwazi katika usimamizi wa sheria za kodi; maboresho ya huduma kwa mlipakodi; na usimamizi wa matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki.

70. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 13,465.9 sawa na asilimia 94.7 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 14,224.5. Kiasi kilichokusanywa ni sawa na ongezeko la asilimia 14.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,720.8 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

71. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, makusanyo ya maduhuli yalifikia shilingi bilioni 2,071.4 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 2,576.1 sawa na asilimia 80.4 ya lengo. Aidha, hadi Machi 2020, mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yaliwa shilingi bilioni 538.6, sawa na asilimia 93.7 ya lengo la shilingi bilioni 575.3.

Misaada na Mikopo Nafuu

72. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 2,039.4, sawa na asilimia 93.1 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 197.7 ikiwa ni asilimia 72.5 ya makadirio ya kipindi hicho; mifuko ya kisekta shilingi bilioni 242.4 ambayo ni asilimia 174.4 ya makadirio katika kipindi hicho; na miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 1,599.3, sawa na asilimia 89.9 ya makadirio.

73. Mwenendo huu mzuri wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo umetokana na juhudzi za Serikali katika kutekeleza hatua mbalimbali za ushirikiano kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework – DCF). Mwongozo huo unatoa fursa mbalimbali za majadiliano yanayowezesha kufikia makubaliano ya utoaji fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, sababu nyingine ni kuimarika kwa upatikanaji wa taarifa za fedha za Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii ni baada ya Serikali kujenga Mfumo wa kuratibu fedha za washirika wa maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi (D-Fund).

Mikopo ya Ndani

74. Hadi Machi 2020, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 3,886.0 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 101.8 ya shilingi bilioni 3,815.6 zilizopangwa kukopwa mwaka 2019/20. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,933.7 zilikopwa kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 952.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mikopo yenyé Masharti ya Kibiashara

75. Kwa mwaka 2019/20, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 2,316.4 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi Machi 2020, Serikali iliweza kukopa kiasi cha shilingi bilioni 1,822.1 sawa na asilimia 78.7 ya lengo la mwaka. Kiasi kilichobaki kinatarajiwaa kukopwa katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka.

Matumizi

76. Katika mwaka 2019/20, Serikali iliendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi hususan katika miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali iliendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia kuongezeka kwa malimbikizo ya madai. Vile vile, Serikali iliendelea kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yenyé kuchochea ukuaji wa uchumi. Lengo kuu likiwa ni kuwa na matumizi bora ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha. Ili kutimiza azma hiyo, sera za matumizi zililenga kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 wenye maeneo makuu manne ya vipaumbele, ambayo ni: Viwanda na kilimo; ukuaji wa uchumi na maendeleo ya

watu; uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na ufuatiliaji na tathmini.

77. Katika mwaka 2019/20, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 33,105.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20,856.8 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.0 ya bajeti na kiasi cha shilingi bilioni 12,248.6 kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37.0 ya bajeti. Aidha, katika bajeti ya fedha za maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 9,737.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,510.9 ni fedha za nje.

78. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya ridhaa ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 22,328.03 sawa na asilimia 92.4 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 15,479.63 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8,290.38 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 5,874.85 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,415.53 ni fedha za nje. Kiasi cha fedha za maendeleo zilizotolewa kinajumuisha fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

79. Kati ya kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 1,841.0 ambayo ni asilimia 98.3 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,873.8 kwa kipindi hicho. Aidha, malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 4,482.3 sawa na asilimia 97.2 ya lengo la shilingi bilioni 4,609.6. Kati ya malipo hayo, shilingi bilioni 3,066.3 zilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya dhamana na amana za Serikali zilizoiva. Matumizi mengine ya Mfuko Mkuu yalikuwa shilingi bilioni 1,174.7.

80. Matumizi ya kawaida yalijumuisha malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 5,232.6 sawa na asilimia 93.4 ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 5,600.5. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,741.8 zililipa kwa watumishi wa Serikali Kuu, shilingi bilioni 54.8 kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,657.2 kwa watumishi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 778.8.


81. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 9,413.30 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 6,295.4 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 1,917.9 fedha za nje. Hadi Machi, 2020, ridhaa ya matumizi ya maendeleo ya shilingi bilioni 8,290.38 ilitolewa sawa na asilimia 88.1 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,874.85 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2,415.53 fedha za nje

82. Baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ni pamoja na: Utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege ambapo jumla ya shilingi trilioni 2.09 zilitolewa; kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, uimarishaji wa vyuo vya VETA na kukuza ujuzi kwa vijana shilingi bilioni 431.8; ununuzi wa ndege mpya na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania shilingi bilioni 315.2; Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) shilingi bilioni 259.6; Mradi wa kufua umeme utokanao na nguvu za maji katika Mto Rufiji shilingi bilioni 235.3; kugharamia elimu msingi bila ada shilingi bilioni 190.5; utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini shilingi bilioni 106.9; kuendeleza ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu shilingi bilioni 53.5; na kugharamia shughuli za Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo shilingi bilioni 11.

Deni la Serikali

83. Hadi Machi 2020, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 54,976.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 50,772.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 14,730.7 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 40,245.4. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mpya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, madaraja ya juu na miradi ya barabara. **Kielelezo Na. 3.1** kinaonesha mwenendo wa Deni la Serikali.

Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2011 - Machi 2020 (Shilingi Bilioni)



Deni la Nje

84. Deni la Serikali la nje liliongezeka kwa asilimia 6.9 kutoka dola za Marekani milioni 16,358.6 Machi 2019 na kufikia dola milioni 17,488.2 Machi 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipyka kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Deni la Nje kwa Wakopeshaji

85. Mchanganuo wa deni la nje ulionesha kuwa, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 57.7 ya deni la nje kwa Machi 2020 ikilinganishwa na asilimia 58.2 Machi 2019, mikopo yenyeye masharti ya kibiasara ilichangia asilimia 30.6 na mikopo kutoka nchi wahisani ilichangia asilimia 11.7 ya mikopo yote ya nje. Vilevile, Serikali imedhamiria kuendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumika kugharamia miradi ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha mchanganuo wa deni la nje kwa wakopeshaji.

Jedwali Na.3.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji


Taasisi	Machi 2018	Mchango kwa Asilimia	Machi 2019	Mchango kwa asilimia	Machi 2020	Mchango kwa Asilimia
Mashirika ya Fedha	9,305.8	59.5	9,561.9	58.2	10,091.5	57.70
Washirika wa Mendeleo	1,876.6	12.0	1,930.8	11.9	2,038.5	11.66
Benki za kibiashara	4,460.5	28.5	4,865.8	29.9	5,358.2	30.64
Jumla	15,642.9	100.0	16,358.6	100.0	17,488.2	100.00

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Deni la Ndani

86. Deni la ndani liliongezeka kutoka shilingi bilioni 13,133.1 Machi 2019 na kufikia shilingi bilioni 14,730.7 Machi 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kukopa kutoka kwenye soko la ndani ili kulipia mikopo ya ndani iliyoiva pamoja na kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, sehemu kubwa ya deni la ndani ilikuwa ni mikopo ya hati fungani ambayo ilikuwa ni asilimia 73.1 ya deni lote la ndani ikifuatiwa na dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 18.1, hati fungani maalum asilimia 8.7 na madeni mengine asilimia 0.1. **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha mwenendo wa madeni ya ndani.

Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Ndani (Shilingi Bilioni)



Deni la Ndani kwa Wakopeshaji

87. Hadi kufikia Machi 2020, benki za biashara ziliongoza kwa kuhodhi asilimia 40.7 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 42.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Aidha, mifuko ya hifadhi ya jamii ilihodhi asilimia 32.9 ikifuatiwa na kampuni za bima asilimia 10.0. **Jedwali Na. 3.2** linaonesha mchanganuo wa deni la ndani kwa wakopeshaji.

Jedwali Na. 3.2: Mchanganuo wa Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2020

Taasisi	Machi 2018	Mchango kwa %	Machi 2019	Mchang o kwa %	Machi 2020	Mchan go kwa %
Benki za Biashara	5,417.34	48.7	4,866.29	42.4	5,346.48	40.7
Taasisi za Fedha	128.10	1.2	139.04	1.2	189.47	1.4
Mifuko ya Jamii	3,805.4	34.2	3,782.05	32.9	4,318.34	32.9
Kampuni za Bima	1,123.77	10.1	1,310.64	11.4	1,305.30	10.0
Taasisi za Kigeni	-	-	502.40	4.4	877.24	6.7
Mashirika Madogo	245.82	2.2	230.32	2.0	296.64	2.3
Watu binafsi	397.92	3.6	656.88	5.7	790.65	6.0
Jumla	11,118.35	100.0	11,487.63	100.0	13,278.57	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

88. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa iliyofanyika Desemba, 2019 yilibainisha kuwa deni ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo viashiria vya deni vilionesha kuwa: katika mwaka 2019/20 thamani ya sasa ya deni lote kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 16.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 103.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240. Viashiria hivyo vinapima uwezo wa nchi kukopa bila kuathiri uhimilivu wa deni.

89. Aidha, kwa upande wa viashiria vinavyopima uwezo wa nchi kulipa deni, matokeo yalibainisha kuwa: uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 11.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 11.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 21. **Jedwali Na. 3.3** linaonesha matokeo ya uhimilivu.


Jedwali Na.3.3: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa

VIASHIRIA VYA DENI LA NJE	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24	2029/30	2039/40	Ukomo
Deni (PV(1))/pato la taifa	16.3	16.8	17.6	18.2	18.0	13.7	9.1	55
Deni (PV)/uuzaaji wa bidhaa nje	103.9	105.5	110.9	116.7	105.4	83.9	53.5	240
Ulipaji wa deni la nje/Uuzaaji wa bidhaa nje	11.9	11.1	9.5	10.3	11.2	11.7	8.1	21
Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani	11.9	11.9	10.1	10.7	11.6	11.8	7.9	23
VIASHIRIA VYA DENI LA NJE NA NDANI	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24	2029/30	2039/40	Ukomo
Deni (PV)/ Pato la Taifa	27.1	27.5	28.1	29.2	29.6	33.2	28.2	70
Deni (PV)/ Mapato ya ndani	163.7	175.6	178.4	185.3	187.8	202.5	160.9	
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	33.4	29.7	27.5	29.3	29.9	46.8	44.8	

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Jedwali Na. 23	MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI						Shilingi milioni
	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2019/20	
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matokeo hadi Machi	
A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)	14,048,034.02	16,639,831.46	17,944,886.98	18,529,557.99	23,045,337.46	16,074,950.43	21,146,768.22
MAPATO YA NDANI	13,622,181.80	16,128,113.46	17,403,387.93	17,868,194.98	22,279,854.08	15,536,350.43	20,381,284.85
1. Mapato yatokanayo na Kodi Ushuru wa Forodha na Excise Duty	12,410,950.84	14,055,172.60	15,191,421.33	15,511,330.10	19,100,932.25	13,465,878.88	17,614,959.53
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	3,090,109.60	3,116,298.10	3,313,671.46	3,585,509.02	4,363,696.35	2,995,245.81	3,902,828.81
Bidhaa toka nje	3,553,636.70	3,979,473.00	4,478,850.59	4,781,633.01	6,159,344.30	3,988,781.52	5,282,099.36
Bidhaa za ndani	1,717,902.00	1,803,666.90	2,054,675.39	2,259,827.38	2,756,738.70	1,849,956.47	2,471,164.43
Bidhaa za ndani	1,835,734.70	2,175,806.10	2,424,175.20	2,521,805.63	3,402,605.60	2,138,825.04	2,810,934.93
Kodi ya Mapato	4,608,244.50	4,832,759.00	5,157,886.30	5,148,191.50	6,322,811.70	4,726,058.51	6,130,702.16
Kodi nyngine	1,921,459.14	2,216,356.98	2,299,242.38	2,130,594.49	2,392,980.10	1,918,424.00	2,449,860.15
Marejesho (Refunds Accounts)	(762,499.10)	(89,714.48)	(58,229.40)	(134,597.92)	(137,900.20)	(162,630.95)	(150,530.96)
2. Mapato yasiyotokana na Kodi	1,211,230.96	2,072,940.86	2,211,966.60	2,356,864.88	3,178,921.83	2,070,471.55	2,766,325.32
3. Mapato ya Halmashauri	425,852.22	511,717.99	541,499.05	661,363.01	765,483.38	538,600.00	765,483.38
B. JUMLA YA MATUMIZI	17,759,598.00	18,898,690.06	20,468,072.32	22,300,627.38	27,669,093.81	17,765,066.72	24,573,891.95
1. Matumizi ya Kawaida	13,420,045.07	11,625,865.77	12,852,304.02	13,806,788.92	15,420,491.53	9,474,683.63	14,649,466.96
2. Matumizi ya Maendeleo	4,339,552.93	7,272,824.29	7,615,768.31	8,493,838.46	12,248,602.28	8,290,383.09	9,924,425.00
Fedha za ndani	2,904,529.72	5,141,450.67	5,397,033.55	6,535,879.18	9,737,738.81	5,874,853.33	7,790,191.05
Fedha za nje	1,435,023.21	2,131,373.62	2,218,734.76	1,957,959.29	2,510,863.47	2,415,529.76	2,134,233.95
C. NAKISI/SALIO (A-B)	(3,711,563.98)	(2,258,858.60)	(2,523,185.35)	(3,771,069.39)	(4,623,756.36)	(1,690,116.29)	(3,427,123.73)
D. KUZIBA NAKISI	3,711,563.98	2,258,858.60	2,523,185.35	3,771,069.39	4,623,755.63	856,438.48	2,358,610.92
1. Fedha kutoka nje	3,982,100.45	2,797,487.94	2,632,730.66	1,569,325.67	3,123,981.45	2,364,841.17	2,672,217.80
Ruzuku	1,349,799.03	923,511.57	813,482.95	285,340.00	1,043,809.60	650,063.08	900,650.28
Basket support	81,073.46	168,983.82	117,165.44	92,162.52	164,713.49	202,992.61	164,713.49
Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL	546,845.75	257,473.16	71,077.78	169,676.95	160,736.49	39,406.93	64,294.60
Mikopo ya miradi	344,800.00	1,124,190.38	1,464,294.03	1,452,477.00	1,414,416.28	1,146,948.73	1,202,253.84
Mikopo ya masharti ya kibia shara	2,142,468.90	1,226,759.77	1,474,281.58	1,144,822.29	2,316,403.59	1,822,093.10	2,316,403.59
Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign)	(482,886.69)	(903,430.76)	(1,307,571.11)	(1,575,153.09)	(1,976,098.00)	(1,496,663.28)	(1,976,098.00)
2. Fedha za Ndani	(270,536.46)	(538,629.34)	(109,545.32)	2,201,743.72	1,499,774.18	(1,508,402.69)	(313,606.88)
Mikopo isiyo ya mabenki	776,944.86	989,282.97	(343,325.54)	653,774.14	456,236.67	728,129.23	456,236.67
Mikopo ya mabenki	1,522,206.56	(1,100,144.97)	941,973.00	2,383,403.31	1,043,537.51	(2,495,398.76)	1,043,537.51
Mikopo ya ndani (Rollover)	2,600,000.00	4,615,670.38	4,835,199.26	3,718,008.34	3,460,218.00	3,066,300.00	3,460,218.00
Mapato ya Ubinafsishaji	-	-	-	-	-	-	-
Marekebisho (Adjustment to Cash)	(2,500,269.58)	(368,120.19)	(636,424.90)	(835,433.73)	-	273,321.34	(1,798,926.55)
Kulipia madeni ya ndani (amortization)	(2,600,000.00)	(4,615,670.38)	(4,835,199.26)	(3,718,008.34)	(3,460,218.00)	(3,066,300.00)	(3,460,218.00)
Expenditure float	(69,418.30)	(59,647.14)	(71,767.88)	-	-	(14,454.51)	(14,454.51)

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango



MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

Jedwali Na. 24

Fungu	Maelezo	2018/2019 (Bajeti)			2019/2020 (Makadirio)		
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
701	Huduma za Kawaida	12,603,274.6	2,420,933.8	15,024,208.4	13,359,498.1	1,830,078.3	15,189,576.4
70111	Utwala na Shughuli za Bunge	859,070.2	128,741.7	987,812.0	855,515.0	88,330.7	943,845.8
70112	Fedha na Masuala ya Kodi	388,420.7	1,260,768.4	1,649,189.1	1,213,791.1	650,119.5	1,863,910.5
70113	Mambo ya Nje	136,718.9	-	136,718.9	147,407.9	-	147,407.9
70121	Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje	-	-	-	-	-	-
70122	Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa	-	-	-	-	-	-
70131	Huduma za Umma	59,080.4	6,648.9	65,729.2	48,208.6	24,540.3	72,749.0
70132	Huduma za Mipango na Takwimu	408,374.6	454,640.6	863,015.2	443,901.1	522,071.7	965,972.7
70133	Huduma nyngine za Kawaida	49,996.5	349,868.7	399,865.2	164,739.1	380,099.5	544,838.6
70140	Utafiti wa Msingi	-	-	-	-	-	-
70150	Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma	709.5	20,988.8	21,698.4	480.4	100.0	580.4
70160	Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu	22,482.1	20,128.5	42,610.6	20,802.4	7,890.8	28,693.2
70170	Deni la Taifa	10,013,706.1	-	10,013,706.1	9,730,012.7	-	9,730,012.7
70180	Uhamishajii Fedha Ndani ya Serikali	664,715.5	179,148.2	843,863.8	734,639.7	156,925.9	891,565.6
702	Ulinzi	1,656,396.8	183,011.2	1,839,408.0	1,705,687.0	124,000.0	1,829,687.0
70210	Huduma za Ulinzi wa Kijeshi	1,656,172.9	29,668.0	1,685,840.9	1,705,463.1	9,000.0	1,714,463.1
70220	Huduma za Ulinzi wa Kiraa	-	-	-	-	-	-
70230	Misaada ya Nje ya Ulinzi	-	-	-	-	-	-
70240	Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi	-	223.9	153,343.2	153,567.1	223.9	115,000.0
70250	Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu	-	-	-	-	-	115,223.9
703	Usalama wa Raia	834,900.5	69,632.3	904,532.7	849,663.7	54,601.3	904,265.0
70310	Huduma za Polisi	592,511.3	3,749.9	596,261.2	601,076.2	2,792.9	603,869.1
70320	Huduma za Zimamoto	32,515.8	4,500.0	37,015.8	34,755.7	4,500.0	39,255.7
70330	Mahakama	147,603.5	41,382.4	188,985.9	151,323.6	22,662.9	173,986.5
70340	Magereza	42,744.2	5,000.0	47,744.2	42,191.3	5,000.0	47,191.3
70350	Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia	245.9	-	245.9	428.0	-	428.0
70360	Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu	19,279.7	15,000.0	34,279.7	19,889.0	19,645.5	39,534.5
704	Shughuli za Kiuchumi	593,792.4	6,539,459.3	7,133,251.6	672,996.7	7,596,023.5	8,269,020.2
70411	Shughuli za Kiuchumi na Biashara	38,224.3	214,563.6	252,787.9	39,573.7	148,417.5	187,991.2
70412	Masuala ya Kazi	8,697.2	16,200.0	24,897.2	11,484.2	20,052.0	31,536.1
70421	Kilimo	240,167.6	124,090.2	364,257.8	225,107.0	163,392.9	388,499.9
70422	Misitu	42,176.5	11,263.4	53,439.9	21,782.5	13,530.8	35,313.4
70423	Uvuuvi na Uwindaji	35,167.3	21,590.3	56,757.6	32,564.8	29,254.6	61,819.4
70431	Makaa ya Mawe na Nishati nyngine	-	-	-	-	-	-
70432	Petrolji na Gesi Asilia	20,030.5	1,663,483.0	1,683,513.5	18,164.1	2,112,204.0	2,130,368.1
70433	Nishati ya Nyukilia	-	-	-	-	-	-
70434	Nishati nyngine	-	-	-	-	-	-
70435	Urmeeme	-	-	-	-	-	-
70436	Nishati isiyo ya umeme	-	-	-	-	-	-
70441	Uchimbaji Madini yasiyo Nishati	30,907.8	19,621.0	50,528.8	34,702.9	7,039.8	41,742.8
70442	Uzalishajii Viwandani	10,065.7	89,450.0	99,515.7	12,211.9	43,160.0	55,371.9
70443	Ujenzi	13,307.0	32,929.0	46,236.0	15,163.4	54,917.0	70,080.4
70451	Usafiri wa Barabara	17,025.2	1,573,893.3	1,590,918.5	18,210.0	1,136,667.2	1,154,877.2
70452	Usafiri wa Majini	-	-	-	-	-	-
70453	Usafiri wa Reli	77,212.1	2,294,739.9	2,371,952.0	76,363.8	3,517,722.2	3,594,086.1
70454	Usafiri wa Anga	108.2	215,000.0	215,108.2	123.8	102,192.4	102,316.2
70455	Usafirishajii kwa njia ya Bomba na njia nyngine za usafiri	-	-	-	-	-	-
70460	Mawasiliano	1,713.0	14,650.0	16,363.0	2,069.5	-	2,069.5
70471	Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo	-	-	-	-	-	-
70472	Hoteli na Migawahwa	-	-	-	-	-	-
70473	Utalii	13,074.4	1,000.0	14,074.4	10,380.6	20,300.0	30,680.6
70474	Miradi ya Maendeleo	-	-	-	-	-	-
70481	Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi	-	-	-	-	-	-
70482	Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuuvi na Uwindaji	32.9	-	32.9	66.0	-	66.0
70483	Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati	-	-	-	-	-	-
70484	Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishajii Viwandani na Ujenzi	-	-	-	-	-	-
70485	Utafiti na Maendeleo ya Usafiri	-	-	-	-	-	-
70486	Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano	-	-	-	-	-	-
70487	Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine	-	-	-	-	-	-
70490	Shughuli nyngine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu	45,882.6	246,985.6	292,868.2	155,028.5	227,172.9	382,201.4
Jedwali linaendelea ukurasa unaofuata							

Jedwali Na. 24 linaendelea

Fungu	Maelezo	2018/2019 (Bajeti)			2019/2020 (Makadirio)		
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
705 Hifadhi ya Mazingira		9,953.8	6,551.3	16,505.1	10,129.6	21,575.3	31,704.9
70510 Hifadhi ya Taka	-	-	-	-	-	-	-
70520 Hifadhi ya Maji Taka	-	-	-	-	-	-	-
70530 Kupunguza Uharibifu wa Mazingira	-	-	-	-	-	-	-
70540 Hifadhi ya Viumbhai na Mazingira	-	-	-	-	-	-	-
70550 Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira	-	-	-	-	-	-	-
70560 Huduma nyininge za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu	9,953.8	6,551.3	16,505.1	10,129.6	21,575.3	31,704.9	
706 Nyumba na Huduma za Jamii		112,398.2	875,043.0	987,441.1	91,194.4	647,102.0	738,296.4
70610 Maendeleo ya Nyumba	31,404.8	85,492.3	116,897.1	28,197.5	27,877.7	56,075.2	
70620 Maendeleo ya Jamii	26,487.0	23,656.2	50,143.2	17,482.2	26,159.2	43,641.3	
70630 Usambazaji Maji	52,173.2	760,894.5	813,067.6	43,081.1	590,065.1	633,146.2	
70640 Taa za Barabarani	-	-	-	-	-	-	-
70650 Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii	254.2	-	254.2	114.9	-	114.9	
70660 Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	2,079.0	5,000.0	7,079.0	2,318.8	3,000.0	5,318.8	
707 Afya		1,019,803.3	787,457.2	1,807,260.5	973,065.3	749,644.7	1,722,710.1
70711 Madawa	185.5	240,000.0	240,185.5	385.1	200,000.0	200,385.1	
70712 Bidhaa nyininge za madawa	-	-	-	-	-	-	-
70713 Huduma za Tiba na Vifa ya Tiba	-	-	-	-	-	-	-
70721 Huduma za Tiba za Jumla	353,435.6	29,894.0	383,329.6	307,951.0	27,171.7	335,122.6	
70722 Huduma Maalumu za Tiba	-	-	-	-	-	-	-
70723 Huduma za Meno	-	-	-	-	-	-	-
70724 Huduma za Wakunga Wasaidizi	-	-	-	-	-	-	-
70731 Huduma za Hospitali	145,929.1	22,551.3	168,480.4	172,271.9	7,527.2	179,799.1	
70732 Huduma za Hospitali Maalumu	-	-	-	-	-	-	-
70733 Huduma za Vifa ya Kujifungulia Wajawazito	-	-	-	-	-	-	-
70734 Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi	390.2	-	390.2	552.9	-	552.9	
70740 Huduma za Afya	226,871.2	373,598.6	600,469.6	213,643.9	465,763.2	679,407.1	
70750 Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya	-	-	-	-	-	-	-
70760 Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu	292,991.6	121,413.3	414,405.0	278,260.6	49,182.6	327,443.3	
708 Burudani, Utamaduni na Dini		23,390.7	8,700.0	32,090.7	21,905.1	6,000.0	27,905.1
70810 Huduma za Burudani na Michemo	2,253.5	1,650.0	3,903.5	1,846.6	-	1,846.6	
70820 Huduma za Utamaduni	8,104.3	1,000.0	9,104.3	6,389.8	-	6,389.8	
70830 Huduma za Utangazaji na Uchapishaji	12,921.5	6,050.0	18,971.5	13,550.1	6,000.0	19,550.1	
70840 Dini na Huduma nyininge za Kijamii	-	-	-	-	-	-	-
70850 Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini	-	-	-	-	-	-	-
70860 Huduma nyininge za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu	111.4	-	111.4	-	-	-	-
709 Elimu		3,441,131.6	1,111,220.2	4,552,351.8	3,016,101.9	1,218,182.7	4,234,284.6
70911 Elimu ya Awali	-	-	-	-	-	-	-
70912 Elimu ya Msingi	1,940,613.0	187,404.4	2,128,017.5	1,618,494.0	205,088.8	1,823,582.9	
70921 Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV)	997,193.3	171,990.4	1,169,183.6	824,822.3	162,859.4	987,681.6	
70922 Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI)	-	-	-	-	-	-	-
70930 Elimu baada ya Sekondari isio ya Chuo Kikuu	-	-	-	-	-	-	-
70941 Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu	-	-	-	-	-	-	-
70942 Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu	5,306.9	8,500.0	13,806.9	23,796.6	18,348.1	42,144.7	
70950 Elimu isiyopambanuliwa	616.9	-	616.9	-	-	-	-
70960 Huduma za Ziada kwa Elimu	497,401.5	743,325.4	1,240,726.9	548,989.1	831,886.4	1,380,875.5	
70970 Utafiti na Maendeleo ya Elimu	-	-	-	-	-	-	-
70980 Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu	-	-	-	-	-	-	-
710 Kinga ya Jamii		173,634.2	5,244.2	178,878.5	156,565.7	1,394.6	157,960.2
71011 Ugonjwa	-	-	-	-	-	-	-
71012 Ulemavu	-	-	-	-	-	-	-
71020 Wazeen	-	-	-	-	-	-	-
71030 Waathirika	-	-	-	-	-	-	-
71040 Familia na Watoto	167,111.9	2,494.2	169,606.2	149,849.9	949.9	150,799.8	
71050 Ukosefu wa Ajira	-	-	-	-	-	-	-
71060 Nyumba	-	-	-	-	-	-	-
71070 Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	-	-	-	-	-	-	-
71080 Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii	-	-	-	-	-	-	-
71090 Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu	6,522.3	2,750.0	9,272.3	6,715.7	444.7	7,160.4	
Jumla Kuu		20,468,676.0	12,007,252.5	32,475,928.5	20,856,807.5	12,248,602.3	33,105,409.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Taktamu

CS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni watu wote

IS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni wanakaya

SURA YA 4

SEKTA YA NJE

Bidhaa Zilizouzwa Nje

90. Thamani ya bidhaa zilizouzwa nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 5,504.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 4,445.1 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kukua kwa mapato yatokanayo na bidhaa zisizo asilia hususan dhahabu na bidhaa za viwandani.

Bidhaa Asilia

91. Mwaka 2019, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 834.6 ikilinganishwa na dola milioni 674.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, pamba, katani na kahawa katika soko la dunia. Aidha, bidhaa asilia zilichangia asilimia 24.3 ya mapato ya mauzo nje mwaka 2019.

Korosho

92. Mwaka 2019, thamani ya mauzo ya korosho nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 353.1 ikilinganishwa na dola milioni 109.6 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kutoka tani 70,100 mwaka 2018 hadi tani 295,600 mwaka 2019. Aidha, bei ya korosho kwa tani katika soko la dunia ilipungua kwa asilimia 23.5 kutoka dola za Marekani 1,562.5 mwaka 2018 hadi dola za Marekani 1,194.6 mwaka 2019.

Kahawa

93. Thamani ya mauzo ya kahawa nje iliongezeka kwa asilimia 3.6 na kufikia dola za Marekani milioni 153.4 mwaka 2019 kutoka dola milioni 148.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya kahawa nje ambapo tani 76,500 ziliuzwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 56,700 mwaka 2018. Hata hivyo, wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 23.2 mwaka 2019.

Pamba

94. Thamani ya pamba iliyouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 91.8 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 68.4 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 34.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje kutoka tani 47,400 mwaka 2018 hadi tani 79,000 mwaka 2019. Aidha, wastani wa bei ya pamba kwa tani katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 19.5 na kufikia dola 1,162.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,443.9 mwaka 2018.

Katani

95. Thamani ya mauzo ya katani nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 34.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 32.5 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kutoka tani 20,300 mwaka 2018 hadi tani 21,100 mwaka 2019. Aidha, wastani wa bei ya katani katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 3.1 na kufikia dola za Marekani 1,654.0 kwa tani mwaka 2019 ikilinganishwa na dola 1,604.5 kwa tani mwaka 2018.

Chai

96. Thamani ya mauzo ya chai nje ilikuwa dola za Marekani milioni 45.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 45.8 mwaka 2018. Kupungua kwa thamani ya mauzo kulitokana na kushuka kwa bei ya chai katika soko la dunia kwa asilimia 15.4 na kufikia dola 1,444.2 kwa tani mwaka 2019 kutoka dola za Marekani 1,707.4 kwa tani mwaka 2018. Hata hivyo, kiasi cha chai kilichouzwa nje kiliongezeka hadi tani 31,700 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 26,800 mwaka 2018.

Tumbaku

97. Thamani ya mauzo ya tumbaku ilipungua kwa asilimia 45.7 na kufikia dola za Marekani milioni 146.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 269.9 mwaka 2018. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kutoka tani 72,200 mwaka 2018 hadi tani 42,600 mwaka 2019. Aidha, wastani wa bei ya tumbaku kwa tani katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 8.0 kutoka dola za Marekani 3,740.1 mwaka 2018 hadi dola 3,440.9 mwaka 2019.

Bidhaa Zisizo Asilia

98. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilikuwa dola za Marekani milioni 4,169.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 3,366.4 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini, bidhaa zilizouzwa tena, mazao ya mboga na maua na bidhaa nyinginezo. Aidha, bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 75.7 ya mauzo ya bidhaa nje.

Madini

99. Thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa dola za Marekani milioni 2,326.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 1,615.4 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 44.4. Hii ilitokana kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu nje ya nchi pamoja na madini mengine. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 45.3 na kufikia dola za Marekani milioni 2,215.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 1,524.1 mwaka 2018. Mapato ya mauzo ya madini yalichangia asilimia 55.8 ya mapato yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2019.

Bidhaa za Viwandani

100. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani ilipungua kwa asilimia 10.0 na kufikia dola za Marekani milioni 805.2 mwaka 2019 kutoka dola milioni 894.3 mwaka 2018. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi hususan, karatasi na bidhaa za karatasi, bidhaa za plastiki na mafuta ya kupikia. Aidha, bidhaa za viwandani zilichangia asilimia 19.3 ya mapato yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2019.

Samaki na Mazao ya Samaki

101. Mwaka 2019, thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake ilipungua kwa asilimia 7.6 na kufikia dola za Marekani milioni 168.0 kutoka dola milioni 181.9 mwaka 2018. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje ya nchi.

Mazao ya Mboga na Maua

102. Mauzo ya mazao ya mboga na maua yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 176.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 147.7 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mazao ya mboga na maua kilichouzwa nje.

Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje

103. Thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje iliongezeka kwa asilimia 32.3 na kufikia dola za Marekani milioni 450.4 mwaka 2019 kutoka dola milioni 340.4 mwaka 2018. Miogoni mwa bidhaa zinazojumuishwa katika kundi hili ni mbegu za mafuta, kakao, ngozi na nafaka.

Jedwali Na. 4.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje

Bidhaa	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	In USD Million Badiliko, %
Bidhaa Asilia									
Kahawa									
Thamani (US\$ milioni)	186.6	171.0	130.5	160.9	153.7	126.3	148.0	153.4	3.6
Kiasi ('000 tani)	54.8	59.5	46.7	58.7	58.7	41.8	56.7	76.5	34.9
Bei (US\$ kwa tani)	3,403.2	2,872.7	2,796.2	2,740.3	2,616.8	3,019.2	2,610.7	2,005.4	-23.2
Pamba									
Thamani (US\$ milioni)	164.9	111.7	52.3	28.2	46.8	36.8	68.4	91.8	34.2
Kiasi ('000 tani)	132.0	89.0	81.8	30.9	33.0	25.3	47.4	79.0	66.8
Bei (US\$ kwa tani)	1,249.7	1,256.0	639.4	911.8	1,416.1	1,450.3	1,443.9	1,162.2	-19.5
Katani									
Thamani (US\$ milioni)	18.4	16.9	16.8	26.5	17.2	28.7	32.5	34.9	7.3
Kiasi ('000 tani)	13.5	12.6	11.5	15.2	8.6	17.0	20.3	21.1	4.1
Bei (US\$ kwa tani)	1,357.1	1,341.6	1,459.7	1,748.8	2,002.1	1,686.7	1,604.5	1,654.0	3.1
Chai									
Thamani (US\$ milioni)	56.1	56.9	57.1	47.2	44.8	49.1	45.8	45.7	-0.2
Kiasi ('000 tani)	27.2	28.8	29.2	29.3	26.3	27.5	26.8	31.7	18.0
Bei (US\$ kwa tani)	2,061.2	1,977.9	1,952.9	1,611.8	1,700.8	1,783.6	1,707.3	1,444.2	-15.4
Tumbaku									
Thamani (US\$ milioni)	350.1	307.0	137.8	214.8	339.2	195.8	269.9	146.5	-45.7
Kiasi ('000 tani)	105.6	67.8	73.2	65.9	74.3	48.3	72.2	42.6	-41.0
Bei (US\$ kwa tani)	3,316.0	4,526.1	1,882.7	3,258.1	4,562.7	4,055.6	3,740.1	3,440.9	-8.0
Korosho									
Thamani (US\$ milioni)	142.6	162.4	212.1	196.4	320.2	529.7	109.6	353.1	222.3
Kiasi ('000 tani)	130.9	147.3	194.4	171.2	217.5	329.5	70.1	295.6	321.6
Bei (US\$ kwa tani)	1,089.3	1,102.5	1,091.0	1,147.3	1,472.4	1,607.5	1,562.5	1,194.6	-23.5
Karafuu									
Thamani (US\$ milioni)	38.1	43.0	15.9	25.5	10.5	55.4	0.4	9.1	2,419.8
Kiasi ('000 tani)	3.4	4.1	1.6	3.1	1.3	7.0	0.1	1.8	2,548.2
Bei (US\$ kwa tani)	11,198.5	10,562.8	10,227.6	8,285.0	7,989.3	7,865.1	5,305.0	5,047.8	-4.8
Jumla (Bidhaa Asilia)	956.7	868.9	622.5	699.5	932.4	1,021.8	674.6	834.6	23.7
Bidhaa Zisizo Asilia (US\$ millioni)									
Madini	2,197.8	1,782.1	1,926.3	1,893.9	1,930.0	1,694.5	1,615.4	2,326.7	44.0
Dhababu	2,117.4	1,644.8	1,288.4	1,374.6	1,508.8	1,541.1	1,524.1	2,215.1	45.3
Almasi	30.2	48.8	0.7	2.3	38.9	64.4	81.8	81.3	-0.6
Madini mengine	50.2	88.5	637.2	517.0	382.3	88.9	9.5	30.3	219.7
Bidhaa za Viwandani	1,037.3	1,072.1	1,139.1	785.4	684.9	676.3	894.3	805.2	-10.0
Nyuzi za Pamba	5.8	10.9	10.4	13.4	16.8	16.1	28.8	6.7	-76.7
Kahawa iliyozaleshwa	1.0	1.1	0.9	0.9	0.5	1.2	2.0	0.2	-92.2
Tumbaku iliyozaleshwa	24.6	32.2	31.9	35.3	31.6	22.3	21.6	24.5	13.4
Mazao ya Katani	9.1	9.7	9.2	21.9	22.3	26.3	21.4	23.9	11.6
Mazao mengine ya Viwandani	996.8	1,018.2	1,086.8	714.0	613.7	610.4	820.5	750.0	-8.6
Samaki na Mazao ya Samaki	160.6	130.6	167.9	161.5	143.7	193.0	181.9	168.0	-7.6
Mazao ya Mboga na Maua	31.3	28.1	19.3	193.3	274.1	148.7	147.7	176.0	19.2
Bidhaa zilitouzwa tena (re-exports)	181.7	172.8	219.8	339.1	194.1	143.2	186.7	242.9	30.1
Bidhaa nyinginezo	555.7	517.6	500.7	315.3	271.6	223.3	340.4	450.4	32.3
Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)	4,164.4	3,703.3	3,973.1	3,688.5	3,498.4	3,078.9	3,366.4	4,169.2	23.8
Bidhaa zisizo rekodiwa	768.2	685.8	564.8	438.8	443.1	410.1	404.1	500.4	23.8
JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)	5,889.2	5,258.1	5,160.3	4,826.7	4,873.9	4,510.8	4,445.1	5,504.2	23.8

Chanzo: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

Mapato ya Huduma

104. Mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 4,280.6 ikilinganishwa na dola milioni 4,014.7, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii, huduma za usafirishaji na mawasiliano. Aidha, mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yaliongezeka kwa asilimia 6.3 na kufikia dola za Marekani milioni 2,604.5 ikilinganishwa na dola milioni 2,449.4 mwaka 2018. Hii ilitokana na juhudzi za Serikali kuendelea kutangaza vivutio vya utalii. Mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,349.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 1,222.1 mwaka 2018. Vile vile, mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano yalikuwa dola za Marekani milioni 28.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 27.1 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.6.

Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje

105. Mwaka 2019, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 3.6 na kufikia dola za Marekani milioni 8,600.0 ikilinganishwa na dola milioni 8,298.6 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za kati, bidhaa za matumizi ya kawaida pamoja na bidhaa za kukuza mitaji hususan bidhaa za majengo na ujenzi pamoja na mitambo.

Bidhaa za Kukuza Mitaji

106. Thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilikuwa dola za Marekani milioni 3,712.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 3,500.7 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za majengo na ujenzi kwa asilimia 16.1 pamoja na mitambo (asilimia 14.2) iliyoagizwa kutoka nje ya nchi.

Bidhaa za Kati

107. Thamani ya bidhaa za kati zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 1.7 na kufikia dola za Marekani milioni 2,662.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 2,618.3 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli na malighafi za viwandani. Thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 7.4 kufikia dola za Marekani milioni 1,801.2 ikilinganishwa na dola milioni 1,677.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mafuta kilichoagizwa.

Bidhaa za Matumizi ya Kawaida

108. Bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa nje ya nchi ziliwu na thamani ya dola za Marekani milioni 2,225.1 ikilinganishwa na dola milioni 2,179.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida zisizohusisha bidhaa za chakula. Thamani ya bidhaa za chakula zilizoagizwa nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 18.7 kutokana na kuimarika kwa uzalishaji ndani ya nchi.

Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje (Dola za Marekani)

Bidhaa	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko, %
Bidhaa za Kukuza Mitaji	3,598.1	3,813.0	3,497.4	2,688.4	3,500.7	3,712.9	6.1
Vifaa vya Usafirishaji	1,214.8	1,096.5	907.7	694.2	1,195.3	1,064.3	-11.0
Majengo na Ujenzi	1,032.4	908.0	817.2	581.8	860.0	998.5	16.1
Mitambo	1,351.0	1,808.4	1,772.5	1,412.5	1,445.4	1,650.1	14.2
Bidhaa za Kati	4,663.6	3,696.6	2,863.2	2,704.4	2,618.3	2,662.0	1.7
Uagizaji Mafuta	3,656.8	2,760.7	1,807.7	1,850.6	1,677.0	1,801.2	7.4
Mbolea	122.8	145.6	118.6	124.9	166.2	118.8	-28.5
Malighafi za Viwanda	884.0	790.4	937.0	728.9	775.2	742.0	-4.3
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	2,656.1	2,333.5	2,103.0	2,158.9	2,179.6	2,225.1	2.1
Bidhaa za Vyakula	632.6	541.7	445.5	405.3	262.3	213.2	-18.7
Bidhaa Nyingine	2,023.4	1,791.8	1,657.5	1,753.6	1,917.3	2,011.9	4.9
Jumla (FoB)	10,917.8	9,843.1	8,463.6	7,551.7	8,298.6	8,600.0	3.6

Chanzo: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

Malipo ya Huduma

109. Mwaka 2019, thamani ya malipo ya huduma ilikuwa dola za Marekani milioni 1,761.7 ikilinganishwa na dola milioni 1,902.3 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 7.4. Hii ilitokana na kupungua kwa malipo ya huduma za usafiri, huduma za mawasiliano, huduma ya ujenzi, huduma za kifedha na huduma nyingine za biashara.


Mwenendo wa Biashara Bainya Tanzania na Nchi Mbalimbali Duniani

110. Mwaka 2019, Tanzania iliendelea kuwa na mahusiano mazuri ya kibashara na nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko la Jumuia ya Afrika Mashariki iliongezeka kwa asilimia 51.8 na kufikia dola za Marekani milioni 674.4 ikilinganishwa na dola milioni 444.3

mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka. Bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,350.9 ikilinganishwa na dola milioni 993.6 kwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 36.0. Sehemu kubwa ya bidhaa hizo ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Malawi. Bidhaa zilizouzwa ni pamoja na madini, pamba, chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), *petroleum coke*, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka.

111. Mwaka 2019, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mauzo kwenda nchi za India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Kenya, Uswisi na Vietnam ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 62.8 ya bidhaa zote zilizouzwa nje ya nchi. Aidha, bidhaa zilizouzwa Umoja wa Falme za Kiarabu, India na Vietnam ni pamoja na mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho. Kwa upande mwingine, dhahabu iliuzwa Afrika Kusini, India na Uswisi. Bidhaa za mahindi, maharage, vyandarua, mboga mboga na nafaka ziliuzwa zaidi Kenya. Mwenendo wa bidhaa zilizouzwa katika nchi hizo ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.1**

Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Mauzo ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi Mwaka 2019



Jedwali Na. 4.3: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali Duniani (Dola Milioni)

JUMUIYA/ NCHI	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	791.7	615.4	629.8	510.5	657.3	725.9	10.4
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	77.5	176.4	784.7	26.2	92.7	98.0	5.7
JUMLA- BARA LA ULAYA	869.2	791.8	1,414.5	536.7	750.1	823.9	9.8
AFRIKA							
JUMUIYA YA MAENDELEO KKUSINI MWA AFRIKA (SADC)							
Afrika ya Kusini	689.1	673.2	692.2	693.3	730.6	971.6	33.0
Zambia	135.3	44.1	35.7	48.3	50.2	63.6	26.7
Swaziland	1.2	9.1	0.1	0.5	2.0	5.9	195.0
Zimbabwe	7.1	6.3	7.0	8.3	8.7	18.8	116.1
Msumbiji	68.1	18.6	13.5	13.0	6.8	32.6	379.4
Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	281.5	197.7	319.8	101.4	133.7	164.1	22.7
Nchi nyingine za SADC	53.7	79.1	44.4	89.7	61.7	94.3	52.8
Jumla-SADC	1,236.0	1,028.1	1,112.7	954.6	993.6	1,350.9	36.0
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)							
Burundi	43.0	39.1	52.1	50.5	47.4	87.9	85.4
Kenya	445.9	731.4	313.8	174.4	212.0	269.9	27.3
Rwanda	35.8	41.2	6.5	60.1	79.0	190.9	141.6
Uganda	73.3	50.3	58.2	104.9	104.9	123.7	17.9
Sudan ya Kusini	-	-	-	1.0	1.0	2.0	100.0
JUMLA-EAC	598.0	862.0	430.6	590.9	444.3	674.4	51.8
Nchi nyingine za Afrika	219.1	337.5	202.8	24.8	102.7	59.5	-42.1
JUMLA-AFRICA	2,053.1	2,227.6	1,746.1	1,570.3	1,540.6	2,084.8	35.3
BARA LA AMERIKA							
Marekani	143.0	50.6	57.0	61.7	59.7	52.4	-12.2
Canada	7.1	6.0	4.7	3.6	6.9	3.7	-46.4
Nchi nyingine za bara la Amerika	6.2	84.7	9.3	98.7	69.0	69.7	1.0
JUMLA - BARA LA AMERIKA	156.3	77.1	71.0	164.0	135.5	125.8	-7.2
BARA LA ASIA							
China	583.9	560.5	354.1	141.0	143.0	233.7	63.4
India	1,084.1	1,145.8	702.8	974.1	727.1	867.8	19.4
Japan	247.8	229.7	138.5	73.9	66.0	64.2	-2.7
Umoj wa falme za kiarabu	85.5	157.1	63.5	87.3	84.9	395.1	365.4
Honkong	35.6	33.9	30.0	42.9	38.7	49.6	28.2
Singapore	15.9	6.6	10.5	5.4	2.8	7.6	171.4
Nchi nyingine za Asia	121.9	160.2	193.0	811.8	288.3	289.1	0.3
JUMLA-ASIA	2,174.7	2,293.8	1,492.4	2,136.5	1,350.8	1,906.9	41.2
Nchi nyinginez	65.5	12.0	964.8	783.7	668.1	562.8	-15.8
JUMLA KUU	5,318.8	5,402.3	5,688.8	5,191.2	4,445.1	5,504.2	23.8


Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

112. Mwaka 2019, bidhaa zenyenye thamani ya dola za Marekani milioni 329.2 ziliagizwa kutoka Jumuia ya Afrika Mashariki mwaka 2019 ikilinganishwa na bidhaa zenyenye thamani ya dola milioni 302.8 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 594.0 ikilinganishwa na dola milioni 604.2 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 1.7. Upungufu huo ultokana na kuimariika kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha

bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nchi wanachama zikiwemo juisi mchanganyiko, mabati na bidhaa za chuma.

113. Mwaka 2019, Bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za China, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Afrika Kusini na Japani zilichangia asilimia 30.7 ya thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa nje ya nchi. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa zilijumuisha: mafuta ya petroli kutoka nchi za Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu; magari na chuma kutoka India, Japani na Afrika Kusini; na mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China.

Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Uagizaji Bidhaa kutoka Nje ya Nchi Mwaka 2019



**Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani
(Dola Milioni)**

JUMUIYA/NCHI	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	2,795.0	1,007.0	977.8	1,085.6	982.4	1,069.9	8.9
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	499.1	673.6	323.6	311.5	442.5	422.4	-4.5
JUMLA - ULAYA	3,294.0	1,680.0	1,301.4	1,397.1	1,424.9	1,492.3	4.7
AFRIKA							
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)							
Afrika ya Kusini	603.3	514.1	472.2	414.7	437.2	438.8	0.4
Zambia	63.3	32.6	2.1	53.7	51.0	47.3	-7.3
Swaziland	47.1	37.3	33.5	37.1	38.5	48.7	26.5
Zimbabwe	4.8	5.7	41.2	1.1	1.2	1.0	-16.7
Msumbiji	18.3	33.3	12.0	9.2	24.0	8.4	-65.0
Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	0.8	0.6	0.4	1.0	0.6	1.3	116.7
Nchi nyingine za SADC	35.3	45.6	54.2	45.6	51.7	48.5	-6.2
JUMLA-SADC	772.9	669.2	615.6	562.5	604.2	594.0	-1.7
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)							
Burundi	0.6	1.1	0.8	0.2	1.0	0.4	-60.0
Kenya	379.6	238.6	267.7	201.0	247.5	267.0	7.9
Rwanda	3.2	1.1	1.1	1.3	1.4	1.5	7.1
Uganda	48.0	39.4	30.7	34.1	52.7	60.3	14.4
Sudan ya Kusini	-	-	-	-	0.2	-	-100.0
JUMLA-EAC	431.4	280.2	300.3	236.6	302.8	329.2	8.7
Nchi nyingine za Afrika	53.3	62.7	69.0	88.6	83.8	113.7	35.7
JUMLA-AFRIKA	1,258.0	1,012.0	984.9	887.7	990.8	1,037.0	4.7
BARA LA AMERIKA							
Marekani	269.8	323.3	252.0	201.8	237.7	320.6	34.9
Canada	93.7	60.2	100.9	39.5	34.7	30.3	-12.7
Nchi nyingine za bara la Amerika	44.4	47.3	48.6	95.3	50.3	100.3	99.4
JUMLA - BARA LA AMERIKA	407.9	430.8	401.5	336.7	322.6	451.2	39.9
ASIA							
China	1,571.0	1,700.0	1,638.4	1,499.6	1,762.0	1,987.7	12.8
India	1,749.0	1,154.0	1,428.7	1,165.0	1,217.3	1,258.5	3.4
Japan	559.3	363.0	371.0	410.6	398.0	485.2	21.9
Umoja wa falme za kiarabu	1,095.0	769.0	592.3	592.2	871.6	949.9	9.0
Honkong	53.2	41.6	51.6	51.3	60.0	47.6	-20.7
Singapore	39.2	84.3	52.6	61.5	30.2	65.6	117.2
Nchi nyingine za Asia	1,052.0	2,497.0	1,566.6	961.0	822.4	848.5	3.2
JUMLA-ASIA	6,119.0	6,609.0	5,701.2	4,741.2	5,161.6	5,643.0	9.3
Nchi nyinginez	3.4	111.3	74.6	189.1	482.5	90.3	34.7
JUMLA KUU	11,082.0	9,843.0	8,463.6	7,551.7	8,298.6	8,600.0	3.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

Urari wa Malipo Yote

114. Urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 587.0 ikilinganishwa na nakisi ya kiasi cha dola za Marekani milioni 790.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje.

Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma Nje

115. Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 577.0 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 1,741.2 mwaka 2018, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 66.7. Kupungua kwa nakisi kulitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kutoka dola za Marekani milioni 8,459.8 mwaka 2018 hadi dola milioni 9,784.8 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilifikia kiasi cha dola za Marekani milioni 10,361.7 kutoka dola za Marekani milioni 10,200.9 mwaka 2018.

Urari wa Biashara ya Bidhaa

116. Mwaka 2019, urari wa biashara ya bidhaa ulipungua na kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 3,095.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 3,853.5 mwaka 2018, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 19.7. Upungufu huo ultokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

Urari wa Biashara ya Huduma

117. Urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,518.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 2,112.3 mwaka 2018, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 19.2. Hii ilitokana na kupungua kwa malipo ya huduma za safari nje ya nchi pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma hususan katika biashara ya utalii.

Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

118. Urari wa mapato ya vitega uchumi yanayojuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 953.4 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 625.2 mwaka 2018.

Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

119. Mwaka 2019, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 418.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 468.5 mwaka 2018, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 10.7. Upungufu huo ultokana na kupungua kwa misaada.

Urari wa Malipo ya Kawaida

120. Mwaka 2019, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,111.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 1,897.8 mwaka 2018, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 41.4. Hii ilitokana na kupungua kwa nakisi ya biashara ya bidhaa na huduma.

Urari wa Uhamisho wa Mitaji

121. Urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 420.5 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 255.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Urari wa Rasilimali ya Kifedha

122. Mwaka 2019, urari wa malipo katika rasilimali ya kifedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,369.4 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 1,668.1 mwaka 2018, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 42.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.

Akiba ya Fedha za Kigeni

123. Mwaka 2019, akiba ya fedha za kigeni iliendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Desemba 2019, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,567.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,044.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 6.4. Aidha, kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.0. Vile vile, kiwango hicho ni zaidi ya lengo la miezi 4.5 na miezi 6.0 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika kwa mtiririko huo.

Soko la Fedha za Kigeni kwa Mabenki

124. Mwaka 2019, viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni viliendelea kuamuliwa na nguvu ya soko huria ambapo kiasi cha dola za Marekani milioni 1,280.4 ziliuzwa katika soko la jumla la fedha za kigeni ikilinganishwa na dola milioni 1,302.8 mwaka 2018. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kushiriki katika soko hilo kama moja ya nyenzo za utekelezaji wa sera ya fedha. Katika kipindi hicho, Benki Kuu iliuza jumla ya dola za Marekani milioni 153.8 sawa na asilimia 12.0 ya mauzo yote na kununua dola za Marekani milioni 466.9.

Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania

125. Mwaka 2019, thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu ambapo dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,288.6 ikilinganishwa na shilingi 2,264.1 mwaka 2018. Utulivu wa thamani ya shilingi ulitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, usimamizi thabiti wa mapato na matumizi ya Serikali, kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali, na mfumuko wa bei kuendelea kuwa chini ya asilimia 5. Aidha, dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,287.9 mwishoni mwa mwaka 2019 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,281.2 mwishoni mwa mwaka 2018.

THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE								Shs. Milioni
Jedwali Na.25	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	
Aina ya Bidhaa								2019
Zilizouzwa Nje	8,653,372	8,223,206	8,527,450	9,582,943	10,610,721	10,053,844	10,064,249	12,596,598
Bidhaa Halisi	8,363,496	7,012,100	7,060,772	7,979,691	9,303,457	8,779,726	8,307,170	10,824,002
Zilizouzwa Tena	289,875	1,211,106	363,174	673,214	422,502	319,086	422,733	555,799
Zilizoagizwa	18,275,893	19,904,472	18,041,771	19,542,294	18,425,925	16,831,696	18,789,124	19,681,659
Jumla	26,929,265	28,127,678	26,569,220	29,125,237	29,036,647	26,885,540	28,853,373	32,278,257
Urari	-9,622,521	-11,681,266	-9,514,321	-9,959,352	-7,815,204	-6,777,852	-8,724,875	-7,085,061
Thamani ya Fedha (Shs/US\$)	1,571.71	1,605.40	1,652.51	1,985.39	2,177.07	2,228.86	2,264.14	2,288.56
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya forodha na Benki Kuu ya Tanzania								

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 26

Bidhaa	Kiasi(000 th Tani)							Thamani(sh. Milioni)						
	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko(%)	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (%)
Kahawa	46.7	58.7	58.7	41.8	56.7	76.5	34.9	215,688	319,408	334,594	281,441	335,102	351,045	4.8
Pamba	81.8	30.9	33.0	25.3	47.4	79.0	66.8	86,440	55,911	101,792	81,940	154,811	210,024	35.7
Katani	11.5	15.2	8.6	17.0	20.3	21.1	4.1	27,698	52,680	37,509	64,046	73,686	79,920	8.5
Chai	29.2	29.3	26.3	27.5	26.8	31.7	18.0	94,366	93,738	97,512	109,515	103,745	104,622	0.8
Tumbaku	73.2	65.9	74.3	48.3	72.2	42.6	-41.0	227,700	426,450	738,458	436,423	611,201	335,310	-45.1
Korosho	194.4	171.2	217.5	329.5	70.1	295.6	321.6	350,477	389,966	697,193	1,180,627	248,063	808,135	225.8
Karafuu	1.6	3.1	1.3	7.0	0.1	1.8	2548.2	26,286	50,601	22,801	123,518	821	20,910	2447.0
Almasi (Carat)	241,709	185,873	235,951	282,032	408,656	590,000	44.4	1,225	4,542	84,625	143,628	185,166	186,027	0.5
Dhahabu(gms)	41,813,100	48,394,953	81,561,000	54,660,377	60,784,383	81,098,466	33.4	2,129,076	2,729,082	3,284,790	3,434,956	3,450,863	5,069,370	46.9


Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE


Jedwali Na. 27

Bidhaa	Kiasi (000" Tani)					Badiliko(%)		Thamani (Milioni US\$)						Badiliko (%)	
	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2018/19	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2018/19	
Bidhaa Asilia:															
Kahawa	46.7	58.7	58.7	41.8	56.7	76.5	34.9	130.5	160.9	153.7	126.3	148.0	153.4	3.6	
Pamba	81.8	30.9	33.0	25.3	47.4	79.0	66.8	52.3	28.2	46.8	36.8	68.4	91.8	34.2	
Katani	11.5	15.2	8.6	17.0	20.3	21.1	4.1	16.8	26.5	17.2	28.7	32.5	34.9	7.3	
Chai	29.2	29.3	26.3	27.5	26.8	31.7	18.0	57.1	47.2	44.8	49.1	45.8	45.7	-0.2	
Tumbaku	73.2	65.9	74.3	48.3	72.2	42.6	-41.0	137.8	214.8	339.2	195.8	269.9	146.5	-45.7	
Korosho	194.4	171.2	217.5	329.5	70.1	295.6	321.6	212.1	196.4	320.2	529.7	109.6	353.1	222.3	
Karafuu	1.6	3.1	1.3	7.0	0.1	1.8	2,548.2	15.9	25.5	10.5	55.4	0.4	9.1	2419.8	
Jumla								622.5	699.5	932.4	1021.8	674.6	834.6	23.7	
Bidhaa zisizo asilia:															
Madini								1,926.3	1,893.9	1,930.0	1,694.5	1,615.4	2,326.7	44.0	
Bidhaa za Viwanda								1139.1	785.4	684.9	676.3	894.3	805.2	-10.0	
Samaki na Mazao ya Samaki								167.9	161.5	143.7	193.0	181.9	168.0	-7.6	
Mazao ya Mboga na Maua								19.3	193.3	274.1	148.7	147.7	176.0	19.2	
Bidhaa zilizouzwa tena								219.8	339.1	194.1	143.2	186.7	242.9	30.1	
Bidhaa nyingezeo								500.7	315.3	271.6	223.3	340.4	450.4	32.3	
Jumla								3,973.1	3,688.5	3,498.4	3,078.9	3,366.4	4,169.2	23.8	
Bidhaa Zisizorekodiwa								564.8	438.8	443.1	410.1	404.1	500.4	23.8	
JUMLA KUBWA								5,160.3	4,826.7	4,873.9	4,510.8	4,445.1	5,504.2	23.8	


I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US\$ Milioni)



II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)



III: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2019



WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 28

Sh./Tani*

Bidhaa	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (%) 2018/19
Kahawa	5,580,087	5,400,679	4,135,909	4,620,772	5,440,481	5,696,882	6,729,323	5,910,939	4,589,421	-22.4
Pamba	1,431,997	1,724,164	2,016,331	1,056,627	1,810,254	3,082,925	3,232,598	3,269,171	2,659,695	-18.6
Katani	2,091,121	2,102,332	2,129,059	2,412,232	3,471,979	4,358,643	3,759,421	3,632,793	3,785,245	4.2
Chai	2,664,933	3,144,333	3,392,989	3,227,164	3,199,976	3,702,858	3,975,372	3,865,620	3,305,024	-14.5
Tumbaku	2,564,562	3,145,641	2,237,711	3,111,126	6,468,558	9,933,320	9,039,462	8,468,137	7,874,684	-7.0
Korosho	1,636,560	1,695,963	1,943,340	1,802,912	2,277,753	3,205,456	3,582,971	3,537,608	2,733,869	-22.7
Karafuu	20,972,246	9,783,616	16,735,615	16,901,202	16,449,051	17,393,365	17,530,187	12,011,337	11,552,255	-3.8
Almasi (kwa carat)	40,709	99,809	353,966	309,019	353,121	786,301	507,080	453,109	315,300	-30.4
Dhahabu (kwa gramu)	85,738	89,993	78,874	62,795	56,146	37,527	62,555	56,767	62,509	10.1

Chanzo Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania


WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 29

Bidhaa	US\$/Tani*									
	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko(%) 2018/19
Kahawa	3,655	3,403	2,873	2,796	2,740	2,617	3,019	2,611	2,005	-23.2
Pamba	1,529	1,250	1,256	639	912	1,416	1,450	1,444	1,162	-19.5
Katani	1,224	1,357	1,342	1,460	1,749	2,002	1,687	1,604	1,654	3.1
Chai	1,740	2,061	1,978	1,953	1,612	1,701	1,784	1,707	1,444	-15.4
Tumbaku	3,839	3,316	4,526	1,883	3,258	4,563	4,056	3,740	3,441	-8.0
Korosho	1,110	1,089	1,103	1,091	1,147	1,472	1,608	1,562	1,195	-23.5
Karafuu	13,163	11,199	10,563	10,228	8,285	7,989	7,865	5,305	5,048	-4.8
Almasi (kwa carat)	2,395	2,188	208	187	178	361	228	200	138	-31.2
Dhahabu (kwa gramu)	55	57	35	38	28	17	28	25	27	8.9

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu



AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 30

Sh. Milioni

Mwaka	Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	Bidhaa za Kati	Bidhaa za Viwanda	Jumla
2002	499,346	408,872	697,209	1,605,426
2003	654,630	705,729	846,251	2,206,610
2004	917,953	1,024,705	1,029,389	2,972,046
2005	937,031	1,451,062	1,341,462	3,729,555
2006	1,068,550	1,977,695	1,799,855	4,846,100
2007	1,393,799	2,441,781	2,186,910	6,022,490
2008	1,703,932	3,217,747	3,537,543	8,459,222
2009	1,836,142	2,471,066	3,319,331	7,626,538
2010	2,395,883	3,842,560	3,806,106	10,044,549
2011	3,345,668	6,507,436	5,597,904	15,451,009
2012	3,660,616	6,838,826	5,835,734	16,335,176
2013	3,794,301	8,356,425	5,555,358	17,706,084
2014	4,389,198	7,706,705	5,945,868	18,041,771
2015	4,632,842	7,339,252	7,570,201	19,542,294
2016	4,578,423	6,233,493	7,614,010	18,425,925
2017	4,811,915	6,027,694	5,992,087	16,831,696
2018	4,934,915	5,928,160	7,926,048	18,789,124
2019	5,092,244	6,092,176	8,497,239	19,681,659

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.


MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 31

US \$ milioni

	2014 Halisi	2015 Halisi	2016 Halisi	2017 Halisi	2018 Halisi	2019 Halisi
Urari wa Biashara	-5723.7	-5016.3	-3589.8	-3041.0	-3853.5	-3095.9
Zilizouzwa nje (fob)	5194.1	4826.7	4873.9	4510.8	4445.1	5504.2
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	10917.8	9843.1	8463.6	7551.7	8298.6	8600.0
Urari wa Huduma	727.3	783.3	1422.9	1792.0	2112.3	2518.9
Mapato	3396.0	3412.4	3599.3	3831.9	4014.7	4280.6
Malipo	2668.7	2629.1	2176.4	2039.9	1902.3	1761.7
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-529.5	-724.3	-955.1	-980.1	-625.2	-953.4
Yaliyoingia	118.4	110.3	98.5	125.3	155.9	261.7
Yaliyotoka	647.9	834.6	1053.6	1105.4	781.1	1215.1
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	477.3	479.9	381.5	402.0	468.5	418.5
Iliyoingia	535.5	560.1	452.7	485.2	535.8	474.9
Serikalini	177.9	194.8	81.1	121.8	170.3	103.5
Sekta nyngine	357.6	365.3	371.6	363.4	365.5	371.4
Iliyotoka	58.2	80.2	71.2	83.2	67.3	56.4
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-5048.6	-4477.4	-2740.5	-1827.1	-1897.8	-1111.9
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	547.9	380.1	446.2	376.8	255.0	420.5
Iliyoingia	547.9	380.1	446.2	376.8	255.0	420.5
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	3218.1	2586.0	1734.9	1811.1	1668.1	2369.4
Uwekezaji katika miradi	1416.1	1506.0	864.0	937.7	971.6	990.6
Uwekezaji katika hisa	11.5	27.6	-5.0	2.9	-3.7	33.2
Uwekezaji aina nyngine	1790.5	1052.3	875.8	870.4	700.3	1345.5
Makosa na Masahihisho	1035.1	1286.5	839.3	1283.1	-815.4	-1091.0
Urari wa Malipo yote	-247.5	-224.8	279.8	1643.9	-790.0	587.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



SURA YA 5

HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

HALI YA UCHUMI WA DUNIA

Ukuaji wa Uchumi

126. Mwaka 2019, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 2.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.6 mwaka 2018. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kilitokana na mivutano ya kisiasa, kuongezeka kwa machafuko ya kijamii pamoja na majanga yanayohusiana na hali ya hewa kama vile kimbunga cha *hurricane* huko Caribbean, ukame na kuungua kwa misitu Australia, mafuriko maeneo ya mashariki ya Afrika na ukame maeneo ya kusini ya Afrika.

127. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea ulikuwa asilimia 1.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.2 mwaka 2018. Kasi ya ukuaji ilipungua kutokana na kupungua kwa shughuli za uzalishaji viwandani na mivutano ya kibiashara na kushuka kwa kasi ya uwekezaji hususan katika nchi ya Marekani.

128. Ukuaji wa Pato la nchi zinazoendelea ulikuwa asilimia 3.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.5 mwaka 2018. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa uzalishaji viwandani, kupungua kwa uwekezaji na mivutano ya kibiashara hususan katika nchi za Asia na Ulaya. Aidha, uwepo wa masharti magumu ya mikopo katika sekta isiyo ya kibenki nchini India ulichangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha mahitaji ya ndani, wakati nchini Pakistan shughuli za uzalishaji zilipungua kutokana na sera za fedha zilizolenga kurejesha mizania ya ndani na nje katika hali ya kawaida. Nchi nyininge kama Guatemala na Papua New Guinea zilipata athari za majanga ya asilia yaliyoharibu miundombinu mbalimbali. Kutokana na hayo, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India ilipungua na kufikia asilimia 5.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2018.

129. Kasi ya ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ilikuwa asilimia 3.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2018. Hii ilitokana na kupungua kwa shughuli za kibiashara baina ya nchi washirika, mafuriko maeneo ya Mashariki ya Afrika na ukame maeneo ya Kusini ya Afrika.

Jedwali Na 5.1: Pato la Dunia 2015 – 2019 (Asilimia)

	2015	2016	2017	2018	2019
Ukuaji					
Pato la Dunia	3.2	3.1	3.8	3.6	2.9
Nchi zilizoendelea	2.1	1.6	2.4	2.2	1.7
Nchi zinazoendelea	4.1	4.1	4.8	4.5	3.7
Nchi za Asia Zinazoendelea	6.7	6.3	6.6	6.3	5.5
Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara	3.4	1.6	2.9	3.3	3.1

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2020

Mwenendo wa Bei

130. Mwaka 2019, mfumuko wa bei wa dunia ulikuwa asilimia 3.6 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulifikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2018. Sababu ya kupungua kwa mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ni pamoja na kuimarika kwa sera za fedha na kupungua kwa bei za madini ya chuma na nishati kutokana na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa hizo. Mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2018. Aidha, kasi ya ukuaji wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2018. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kulitokana na mafuriko maeneo ya mashariki ya Afrika na ukame maeneo ya kusini ya Afrika.

Mwenendo wa Biashara Duniani

131. Ukuaji wa shughuli za biashara duniani uliendelea kudhoofika ambapo kasi yake ilikuwa asilimia 1.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2018. Mwenendo huo ulitokana na kuendelea kwa mvutano wa biashara baina ya Marekani na China na kutotabirika kwa athari za kujitoa kwa Uingereza kwenye Umoja wa Ulaya. Aidha, mvutano huo ulisababisha kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa baaadhi ya nchi zilizoendelea, hali tete katika masoko ya fedha na masharti magumu ya kifedha na hivyo kusababisha kuwepo kwa kasi ndogo ya uwekezaji unaoongeza tija ambao ni muhimu katika kukuza uchumi.

USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

132. Tanzania imeendelea kuwa na mahusiano mazuri kimataifa katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama, kijamii na kiuchumi. Mwaka 2019, Tanzania ilikua mwenyeji wa Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika na Nordic, uliofanyika jijini Dar es Salaam. Lengo la mkutano huo lilikua ni kutoa nafasi kwa nchi za Afrika na Nordic kujadiliana masuala ya ushirikiano kati ya pande hizo mbili na kuainisha vipaumbele na mikakati ya ushirikiano kwenye sekta za biashara na uwekezaji kwa maendeleo ya pande zote mbili.

133. Mwaka 2019, ziara ya ujumbe wa Taasisi ya *China-Africa Development Fund (CADF)* na *Huaxin Cement Co. Ltd* ilifanyika hapa nchini. Lengo la ziara hiyo lilikua ni kuangalia fursa za uwekezaji kwa Kampuni ya Huaxin Cement Co. Ltd kwenye saruji pamoja na kufahamu mfumo mzima wa sera, kanuni, sheria na taratibu za uwekezaji nchini. Uwekezaji huo unatarajiwa kuzalisha ajira kwa watanzania kati ya 400 hadi 500. Aidha, yalifanyika mazungumzo na Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO) ili kufahamu hali halisi ya upatikanaji umeme mkoani Tanga. Vile vile, ujumbe ulitembelea kiwanda cha *Maweni Limestones Ltd* kilichopo Tanga kwa lengo la kuwekeza katika kiwanda hicho. Taasisi ya CADF imejidhatiti kusaidia uwekezaji wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni 52.0 katika miradi ya kilimo, vyombo vyaya habari kidijitali, viwanda na madini.

134. Mwaka 2019, Tanzania ilishiriki katika mikutano mitatu ya Tume za pamoja za kudumu za ushirikiano na nchi nyingine. Kupitia mikutano hiyo, Tanzania ilisaini makubaliano ya ushirikiano kati yake na nchi za Zimbabwe, Uganda na Namibia katika masuala ya biashara, uchukuzi, nishati, ulinzi na huduma za kijamii. Kwa upande mwingine, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 9 wa Wakuu wa nchi na Serikali kwa Nchi Wanachama wa Kundi la Afrika, Karibeani na Pasifikasi (ACP) uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Katika mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi nchi wanachama kukubali: kuingizwa kwa mazao ya korosho na mahindi kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ya ACP na hivyo kuwa sehemu ya mazao yatakayonufaika na ufadhili wa Euro milioni 140.0 zilizotolewa kwa ajili ya programu ya kuboresha uzalishaji wa mazao hayo ikiwemo kuyaongezea thamani; kufanyika maboresho muhimu katika mkatiba wa *Georgetown* kwa kuondoa vifungu visivyokua na maslahi kwa Tanzania na ACP

kwa ujumla; kufanya mawasiliano na mashauriano ya kina na nchi husika kabla ya kufanya mabadiliko yoyote katika fedha zilizotengwa kwa nchi husika hivyo kupunguza athari za kibajeti zinazotokana na uamuzi wa kuhamisha sehemu ya fedha zilizopitishwa; na kuingiza suala la kuondolewa vikwazo vyta kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe kwenye Azimio la Nairobi na hivyo kuongeza msukumo na mshikamano wa kimataifa.

Jumuiya ya Afrika Mashariki

135. Ushirikiano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki umeendelea kuimarika kutokana na mahusiano mazuri ya nchi hizo pamoja na kufanya mikutano na warsha mbalimbali ili kujadili na kufanya maamuzi ya pamoja katika kuimarisha ushirikiano katika nyanja za kiuchumi na kijamii. Mwaka 2019, Mkutano wa 36 wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji Afrika Mashariki ulifanyika jijini Arusha, Tanzania. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kujadili utekelezaji wa mpango wa sekta ya viwanda hususan bidhaa za dawa, pamba na nguo, na ngozi na bidhaa zake. Aidha, nchi wanachama zilijadili taarifa ya mapitio ya wigo wa pamoja wa forodha wa Afrika Mashariki na taarifa ya maandalizi ya wigo wa forodha kwa nchi za Afrika Mashariki katika majadiliano ya Eneo huru la Biashara la Afrika. Katika Mkutano huo, ulipitishwa mkakati wa kuendeleza sekta ya pamba na nguo unaolenga kuongeza uzalishaji wa mbegu za pamba kutoka tani za ujazo 290,0000 kwa mwaka hadi tani za ujazo 1,000,000 kwa mwaka na kuongeza uwezo wa kuchakata pamba kutoka urefu wa mita milioni 6.9 hadi kufikia urefu wa mita milioni 37.3. Vile vile, nchi wanachama zilikubaliana kuwa ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati (*wet blue*) inayouzwa nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itozwe ushuru wa asilimia 10 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10 ili kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vyta ngozi na bidhaa za ngozi Afrika Mashariki.

136. Katika kuendelea kuimarisha uchumi wa nchi za Jumuiya, mwaka 2019 Tanzania ilishiriki kwenye maonesho ya 20 ya wajasiriamali Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Kigali, Rwanda. Katika Maonesho hayo wajasiriamali wapatao 1,500 kutoka nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki walishiriki ambapo wajasiriamali 160 walitoka Tanzania. Maonesho yalilenga kukuza ajira, kupanua wigo wa masoko ya bidhaa za wajasiriamali, kukuza biashara na kuwezesha urasimishaji wa shughuli za sekta zisizo rasmi pamoja na kuwapatia

wajasiriamali hao fursa za kubadilishana taarifa za kibashara, ujuzi pamoja na huduma katika ukanda wa Afrika Mashariki.

137. Mwaka 2019, Tanzania ilishiriki kwenye majadiliano ya Programu ya kuwezesha sekta ya uchukuzi na biashara kwa Nchi Wanachama wa Utatu wa EAC - SADC - COMESA yaliyofanyika Kigali, Rwanda. Majadiliano hayo yalijikita katika jitihada za kuboresha: mifumo ya kitaasisi na kuwezesha utekelezaji wa mpango wa kuendeleza miundombinu; mifumo ya usajili na leseni za vyombo vya barabarani; utoaji wa huduma za uchukuzi; na tafiti za usalama barabarani.

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

138. Mwaka 2019, Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulifanyika jijini Dar es Salaam, Tanzania na kuhudhuriwa na nchi zote 16 wanachama. Katika Mkutano huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikabidhiwa jukumu la Uenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kufuatia hilo, Tanzania itakuwa mwenyeji na mwenyekiti wa mikutano yote ya kisekta ya Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Pamoja na masuala mengine, mkutano uliridhia Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne itakayotumika kwenye Jumuiya hiyo pamoja na kuhimiza mshikamano na nchi za magharibi. Aidha, Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC waliagiza suala la Zimbabwe kuondolewa vikwazo lizungumzwe katika majukwaa yote ya kikanda na kimataifa.

Umoja wa Afrika

Mwaka 2019, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri kutoka Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanaosimamia biashara uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Lengo la Mkutano huo lilikua ni kujadili namna ya kuanza utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) baada ya Mkataba huo kupata nguvu ya kisheria. Aidha, uzinduzi wa eneo hilo ulifanywa na Wakuu wa Nchi na Serikali jijini Niamey Niger. Masuala yaliyojadiliwa katika Mkutano huo ni pamoja na uanzishwaji wa Sekretarieti ya Mpito na ya kudumu ambayo itakua Accra, Ghana, bajeti ya Sekretarieti na Mpango kazi wa utekelezaji wake. Vile vile, Mkutano huo ulijadili masuala yanayotakiwa kutekelezwa kabla ya kufungua rasmi biashara mwezi Julai, 2020.

SURA YA 6

RASILIMALI WATU

Idadi ya Watu

139. Mwaka 2019, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 55,890,747 ikilinganishwa na watu 54,199,163 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 54,265,158 sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikadiriwa kuwa na watu 1,625,589. Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 28,534,558 sawa na asilimia 51.1 ya watu wote na wanaume walikadiriwa kuwa 27,356,189. Makadirio haya yalitokana na maoteo ya idadi ya watu kwa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 pamoja na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu vikijumuisha uzazi, vifo na uhamiaji.

Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

140. Mwaka 2019, mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine. Katika kipindi hicho, mkoa wa Dar es Salaam ulikadiriwa kuwa na watu 5,275,315 sawa na asilimia 9.7 ya watu wote Tanzania Bara ukifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokadiriwa kuwa na watu 3,676,300 sawa na asilimia 6.8. Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na fursa za kiuchumi zilizopelekea watu kuhamia kutoka mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 771,287 ukifuatiwa na mkoa wa Njombe uliokuwa na watu 820,355 na Lindi watu 1,004,439. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 717,468, sawa na asilimia 44.1 ya watu wote. Mkoa wa Kaskazini Pemba ulikadiriwa kuwa na watu 282,716 (asilimia 17.4) na mkoa wa Kusini Unguja ulikadiriwa kuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 136,235, sawa na asilimia 8.4.

141. Msongamano wa watu kwa Tanzania ulikuwa wastani wa watu 63 kwa kila kilometra ya mraba mwaka 2019 ikilinganishwa na wastani wa watu 61 mwaka 2018. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa wastani wa watu 61 kwa kila kilometra ya mraba. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi ukiwa na wastani wa watu 3,787 kwa kila kilometra ya mraba,

ukifuatiwa na Mwanza (wastani wa watu 388), Kagera (wastani wa watu 124), na Kilimanjaro (wastani wa watu 144). Mkoa wa Lindi ulikuwa na msongamano mdogo zaidi ukiwa na wastani wa watu 15 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na mkoa wa Katavi ulikuwa na wastani wa watu 17 na Ruvuma wastani wa watu 25 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,119 kwa kila kilometa ya mraba ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani wa watu 160 kwa kila kilometa ya mraba.

142. Mwaka 2019, idadi ya watoto wenyewe umri chini ya miaka mitano ilikuwa 9,628,845 sawa na asilimia 17.2 ya watu wote Tanzania. Watu wenyewe umri wa miaka mitano (5) hadi 14 walikuwa 14,725,639 sawa na asilimia 26.3. Aidha, watu wenyewe umri wa miaka 15 hadi 24 walikuwa 10,882,410 sawa na asilimia 19.5. Vile vile, idadi ya watu wenyewe umri wa miaka 25 hadi 64 ilikuwa 18,919,802 sawa na asilimia 33.9 ya watu wote na watu wenyewe umri zaidi ya miaka 64 walikuwa 1,734,051 sawa na asilimia 3.1. Katika kipindi hicho, watu wenyewe umri wa miaka 15 hadi 64 amba ni nguvukazi ya Taifa walikuwa 29,802,212 sawa na asilimia 53.3 ya watu wote Tanzania.

Jedwali Na.6.1 Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi kwa Mwaka 2019

Umri	Jinsi			Asilimia
	Wanaume	Wanawake	Jumla	
<5	4,860,093	4,768,752	9,628,845	17.2
5-14	7,390,368	7,335,271	14,725,639	26.3
15-24	5,406,712	5,475,698	10,882,410	19.5
25-64	8,892,852	10,026,950	18,919,802	33.9
65+	806,164	927,887	1,734,051	3.1
Jumla	27,356,189	28,534,558	55,890,747	100

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Nguvu Kazi na Ajira

143. Mwaka 2019, jumla ya ajira 1,577,622 zilizalishwa nchini kutokana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikilinganishwa na ajira 1,555,960 mwaka 2018. Kati ya hizo, ajira 579,518 zilizalishwa katika sekta rasmi na ajira 998,104 zilizalishwa katika sekta isiyo rasmi. Kwa upande wa ajira

zilizozalishwa na sekta rasmi: ajira 421,624 zilitokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Serikali; ajira 145,551 zilitokana na uwekezaji wa sekta binafsi; na ajira 12,343 zilikuwa za Serikali.

Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Ajira Zilizozalishwa Mwaka 2016 - 2019

	2016	2017	2018	2019	Jumla
Sekta Rasmi					
Serikali	71,496	82,302	18,000	12,343	184,141
Miradi ya maendeleo ya Serikali	124,178	132,147	397,009	421,624	1,074,958
Sekta binafsi	195,002	239,017	137,054	145,551	716,624
Jumla Ndogo	390,676	453,466	552,063	579,518	1,975,723
Sekta Isiyo Rasmi	1,018,095	1,036,480	1,003,897	998,104	4,056,576
Jumla Kuu	1,408,771	1,489,946	1,555,960	1,577,622	6,032,299

Chanzo: Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

144. Mwaka 2019, Serikali kuitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi iliawezesha vijana 23,755 kupata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili waweze kujiajiri na kuajirika. Kati ya hao, vijana 5,875 walipata mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi; wahitimu 2,115 walipata mafunzo ya uzoefu mahali pa kazi; vijana 5,395 walipata mafunzo ya ufundi stadi na kurasimishwa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi; vijana 8,980 walipata mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba; na wajasiriamali 1,390 wa sekta isiyo rasmi walipata mafunzo ya ujasiriamali na urasimishaji wa biashara.

Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania

145. Mwaka 2019, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania ulisajili na kutoa ushauri kwa watafutakazi 14,884 kuhusu uchaguzi wa kazi kulingana na fani zao ikilinganishwa na watafutakazi 21,684 mwaka 2018. Kati ya watafutakazi waliosajiliwa, wanaume walikuwa 8,296 na wanawake 6,588. Aidha, watafutakazi 7,979 (wanaume 4,276 na wanawake 3,703) walipatiwa mafunzo mwaka 2019 ikilinganishwa na watafutakazi 2,253 mwaka 2018. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa kutafuta kazi, kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kujenga maadili ya kazi yanayohitajika na waajiri mbalimbali.

146. Mwaka 2019, Wakala uliunganisha watafutakazi 698 (wanaume 511 na wanawake 187) katika nafasi za kazi za kudumu ikilinganishwa na watafutakazi 607 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Ongezeko hilo lilitokana na zoezi la kuwafikia waajiri mbalimbali mikoani lililofanywa na Wakala na hivyo kuwezesha kupatikana kwa fursa za kazi. Aidha, watafutakazi 2,268 wakiwemo wanaume 1,069 na wanawake 1,199 waliunganishwa na waajiri mbalimbali kufanya mafunzo ya vitendo na kujenga uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2011-2019

Jedwali Na. 32

Mkoa	2011	2012**	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Dodoma	2,163,817	2,083,588	2,127,416	2,172,165	2,217,856	2,264,508	2,419,941	2,492,989	2,568,514
Arusha	1,711,624	1,694,310	1,741,396	1,789,791	1,839,531	1,890,653	1,948,219	1,999,907	2,051,852
Kilimanjaro	1,669,174	1,640,087	1,669,051	1,698,526	1,728,522	1,759,048	1,823,151	1,864,329	1,906,978
Tanga	2,010,480	2,045,205	2,091,341	2,138,517	2,186,757	2,236,086	2,284,712	2,337,053	2,391,791
Morogoro	2,162,197	2,218,492	2,271,310	2,325,386	2,380,750	2,437,431	2,531,268	2,596,287	2,662,468
Pwani	1,086,658	1,098,668	1,122,685	1,147,227	1,172,306	1,197,933	1,236,481	1,265,504	1,295,267
Dar es Salaam	3,194,903	4,364,541	4,617,000	4,884,061	5,166,570	5,465,420	5,017,294	5,147,070	5,275,315
Lindi	941,884	864,652	872,758	880,939	889,197	897,533	963,465	983,738	1,004,439
Mtewara	1,349,235	1,270,854	1,286,501	1,302,340	1,318,374	1,334,606	1,397,723	1,424,083	1,451,078
Ruvuma	1,412,084	1,376,891	1,406,411	1,436,563	1,467,362	1,498,821	1,543,869	1,579,811	1,616,991
Iringa	1,764,285	941,238	951,964	962,813	973,784	984,882	1,068,695	1,095,172	1,122,131
Mbeya	2,743,084	2,707,410	2,781,971	2,858,585	2,937,310	1,883,024	2,006,072	2,070,412	2,136,614
Singida	1,404,065	1,370,637	1,402,820	1,435,758	1,469,469	1,503,972	1,569,304	1,612,854	1,658,086
Tabora	2,443,049	2,291,623	2,359,642	2,429,679	2,501,796	2,576,053	2,769,093	2,870,522	2,974,427
Rukwa	1,558,200	1,004,539	1,037,259	1,071,044	1,105,931	1,141,953	1,160,568	1,195,550	1,231,959
Kigoma	1,891,173	2,127,930	2,179,598	2,232,520	2,286,727	2,342,250	2,528,708	2,616,200	2,706,831
Shinyanga	3,998,664	1,534,808	1,566,734	1,599,325	1,632,593	1,666,554	1,816,316	1,874,709	1,933,768
Kagera	2,661,671	2,458,023	2,537,021	2,618,558	2,702,715	2,789,577	2,919,942	3,022,037	3,127,908
Mwanza	3,669,380	2,772,509	2,856,258	2,942,537	3,031,422	3,122,992	3,393,620	3,532,378	3,676,300
Mara	1,891,907	1,743,830	1,787,279	1,831,810	1,877,451	1,924,230	2,123,683	2,209,143	2,298,317
Manyara	1,441,771	1,425,131	1,471,083	1,518,516	1,567,479	1,618,020	1,692,667	1,750,864	1,810,929
Njombe	-	702,097	707,698	713,345	719,036	724,772	786,347	803,299	820,355
Katavi	-	564,604	583,160	602,325	622,121	642,567	706,472	738,237	771,287
Simiyu	-	1,584,157	1,613,580	1,643,549	1,674,075	1,705,168	1,998,224	2,094,798	2,196,449
Geita	-	1,739,530	1,785,824	1,833,350	1,882,141	1,932,230	2,148,409	2,239,949	2,335,134
Songwe	-					1,136,415	1,166,094	1,202,419	1,239,970
Tanzania Bara	43,169,305	43,625,354	44,827,757	46,069,230	47,351,275	48,676,698	51,020,337	52,619,314	54,265,158
Kaskazini Unguja	183,209	187,455	193,551	199,844	206,343	213,053	216,697	222,066	227,317
Kusini Unguja	115,035	115,588	117,923	120,305	122,736	125,215	131,162	133,767	136,235
Mjini Magharibi	495,054	593,678	619,144	645,701	673,398	702,283	683,833	700,791	717,468
Kaskazini Pemba	264,677	211,732	214,502	217,309	220,153	223,033	260,884	271,594	282,716
Kusini Pemba	257,577	195,116	197,274	199,456	201,662	203,893	241,715	251,631	261,853
Zanzibar	1,315,552	1,303,569	1,342,394	1,382,616	1,424,292	1,467,477	1,534,291	1,579,849	1,625,589
Tanzania	44,484,857	44,928,923	46,170,151	47,451,847	48,775,567	50,144,175	52,554,628	54,199,163	55,890,747

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

SEHEMU YA PILI UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

SURA YA 7

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

147. Mwaka 2019, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili miradi 269 ikilinganishwa na miradi 215 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 25.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuhakikisha huduma zote zinazohusiana na uwekezaji zinapatikana katika Kituo cha Uwekezaji. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 86 ilikuwa ya watanzania, miradi 107 ya wageni na miradi 76 ya ubia kati ya watanzania na wageni ikilinganishwa na miradi 132 ya watanzania, 69 ya wageni na miradi 14 ya ubia mwaka 2018. Aidha, thamani ya miradi iliyosajiliwa ilipungua kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.82 mwaka 2018 hadi dola bilioni 2.62 mwaka 2019. Vile vile, miradi iliyosajiliwa mwaka 2019 ilitoa fursa za ajira 46,703 ikilinganishwa na fursa za ajira 27,469 mwaka 2018.

Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta

148. Mwaka 2019, sekta ya uzalishaji viwandani ilivutia uwekezaji wenyе thamani ya dola za Marekani milioni 1,159.01 ikifuatiwa na kilimo dola milioni 462.73, usafirishaji dola milioni 374.78, mawasiliano dola milioni 253.80; na majengo ya biashara dola milioni 158.75. Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani ilisajili idadi kubwa ya miradi (miradi 156) ikifuatiwa na usafirishaji mizigo miradi 34, huduma za kibiashara miradi 19, kilimo miradi 18, utalii miradi 16 na majengo ya biashara miradi 11. **Jedwali Na. 7.1** linaonesha mgawanyo wa miradi iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji.

Jedwali Na. 7.1. Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2019

Sekta	Miradi yote	Miradi mipyä	Miradi ya mwendelezo	Miradi ya wazawa	Miradi ya wageni	Miradi ya ubia	Ajira	Thamani dola za Marekani milioni
Kilimo	18	18	0	6	6	6	19,428	462.73
Maliasili	2	2	0	0	0	2	195	1.57
Utalii	16	16	0	7	7	2	1,260	60.29
Uzalishaji Viwandani	156	156	0	41	70	45	17,713	1,159.01
Madini	0	0	0	0	0	0	-	-
Majengo ya Biashara	11	11	0	2	6	3	1,101	158.75
Usafirishaji	34	34	0	22	7	5	3,876	374.78
Huduma	19	19	0	1	9	9	1,828	38.30
Kompyuta	0	0	0	0	0	0	-	-
Taasisi za Kifedha	2	2	0	0	0	2	52	9.34
Raslimali Watu	2	2	0	2	0	0	308	64.00
Mawasiliano	2	2	0	0	0	2	61	253.80
Nishati	6	6	0	4	2	0	669	27.85
Miundombinu	0	0	0	0	0	0	-	-
Utangazaji	1	1	0	1	0	0	212	12.40
Jumla	269	269	0	86	107	76	46,703	2,622.82

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2019

Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa

149. Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kuvutia miradi ya uwekezaji ambapo miradi 151 ilisajiliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na miradi 109 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuwepo kwa mazingira wezeshi ya uwekezaji hasa miundombinu bora ikilinganishwa na mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Pwani ulisajili miradi 36, Mwanza miradi 12, Arusha miradi 11, Morogoro miradi 8 na Dodoma miradi 6. Mchanganuo wa usajili wa miradi kimkoa ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 7.2.**

Jedwali Na. 7.2: Mgawanyiko wa Miradi iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2019

Mkoa/Sekta	Kilimo	Maliasili	Utalii	Uzalishaji Viwandani	Madini	Majengo ya Biashara	Usafirishaji	Huduma	Kompyuta	Tasisisi za Fedha	Rasimali Watu	Mawasiliano	Nishati	Miundombinu	Utangazaji	Jumla
Arusha	0	0	6	3	0	1	0	1	0	0	0	0	0	0	0	11
Pwani	3	0	1	29	0	0	2	1	0	0	0	0	0	0	0	36
D'Salaam	5	0	6	79	0	10	26	14	0	2	6	2	0	0	1	151
Dodoma	0	0	0	5	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	6
Geita	0	0	0	3	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	4
Iringa	3	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	1	0	0	5
Kagera	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Katavi	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Kigoma	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
K'Njaro	0	0	0	4	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	4
Lindi	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Manyara	1	0	0	3	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	4
Mbeya	0	0	0	4	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	4
Morogoro	2	0	0	3	0	0	2	0	0	0	1	0	0	0	0	8
Mtwara	1	0	0	2	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	3
Mwanza	0	0	1	8	0	0	2	0	0	0	1	0	0	0	0	12
Njombe	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1	0	0	2
Mara	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Rukwa	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Ruvuma	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Shinyanga	0	0	0	5	0	0	1	1	0	0	0	0	0	0	0	7
Simiyu	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Singida	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Songwe	0	0	0	2	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	2
Tabora	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Tanga	1	0	1	1	0	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	4
Jumla	18	0	16	156	0	11	34	19	0	2	8	2	2	0	1	269

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2019

Uwekezaji Binafsi Kutoka Nje

150. Mwaka 2019, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliendelea kuimarika na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi. Kwa mujibu wa Ripoti ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2019, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje ya nchi ulifikia dola za Marekani milioni 16,204.8 mwaka 2018 kutoka dola 15,509.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulifikia dola za Marekani milioni 13,869.1 sawa na asilimia 85.6

ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa dola milioni 214.2 na uwekezaji mwingine dola milioni 2,121.5. Aidha, thamani ya mitaji iliyowekezwa kwenye sekta binafsi kutoka nje ya nchi mwaka 2018 ilikuwa dola za Marekani milioni 1,214.4 ikilinganishwa na dola milioni 1,051.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Hii ilitokana kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kulikochangiwa na sera madhubuti za uchumi pamoja na uwepo wa amani na utulivu nchini.

Uwekezaji wa Moja kwa Moja na Hisa

151. Kulingana na Ripoti ya Uwekezaji ya Mwaka 2019, Tanzania ilipokea uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi wenyewe thamani ya dola za Marekani milioni 971.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 937.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji hususan kwenye miradi ya miundombinu ya barabara, reli na umeme. Jitihada hizo zilisababisha kuongezeka kwa uwekezaji kwenye viwanda vya kuzalisha saruji, vifaa vya plastiki na chuma. Kwa upande wa uwekezaji wa hisa, Tanzania ilipokea dola za Marekani milioni 1.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 0.8 mwaka 2017. Uwekezaji wa hisa unahusisha uwekezaji kwenye kampuni usiozidi asilimia kumi ya hisa.

Uwekezaji Mwingine

152. Uwekezaji mwingine unahusisha mikopo ya muda mrefu na mfupi pamoja na mikopo ya kibiashara kutoka kwenye taasisi na kampuni zisizokuwa na uhusiano wa hisa na kampuni au taasisi zilizowekeza moja kwa moja. Mwaka 2018, Tanzania ilipokea dola za Marekani milioni 241.3 kupitia uwekezaji mwingine ikilinganishwa na dola milioni 113.2 mwaka 2017. Uwekezaji mwingine ulijikita zaidi kwenye sekta za viwanda, fedha na bima na usafirishaji.

Ajira kutokana na Uwekezaji wa Moja kwa Moja

153. Mwaka 2018, ajira zilizotokana na uwekezaji wa moja kwa moja zilikuwa 140,256 ikilinganishwa na ajira 134,653 mwaka 2017. Aidha, wafanyakazi wataalamu walikuwa asilimia 37 ya waajiriwa wote na wasiokuwa wataalamu walikuwa asilimia 63. Wafanyakazi Wataalamu walijiriwa zaidi katika sekta za fedha na bima pamoja na mawasiliano kutokana na utaalamu unaohitajika katika sekta hizo.

Jedwali Na.7.3: Uwekezaji kwenye Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani, Milioni)

Aina ya Uwekezaji	Kiasi kilichowekezwa					Limbikizo lililowekezwa		
	2015	2016	2017	2018	2015	2016	2017	2018
Uwekezaji wa Moja kwa Moja	1,560.6	755	937.7	971.6	12,572.6	12,839.2	13,274.4	13,869.1
Uwekezaji wa Hisa	1.5	2.8	0.8	1.6	31.4	128	176.6	214.2
Uwekezaji Mwingine	2.7	237.7	113.2	241.3	1100.7	1667.1	2058.7	2121.5
Jumla	1,564.8	995.5	1,051.7	1,214.4	13,704.7	14,634.3	15,509.7	16,204.8

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Urahisi wa kuwekeza na Kufanya Biashara Nchini

154. Taarifa ya Mazingira ya Biashara Duniani ya Mwaka 2020 ilionesa kuwa Tanzania ilishika nafasi ya 141 kati ya nchi 190 zilizofanyiwa tathmini mwaka 2019 ikilinganishwa na nafasi ya 144 mwaka 2018. Kupanda kwa nafasi ya Tanzania kulitokana na juhudzi za Serikali kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, Tanzania ilishika nafasi ya 182 katika viashiria vya wepesi wa kusafirisha bidhaa zinazopita bandarini kwenda nchi jirani, nafasi ya 165 katika taratibu za kulipa kodi na nafasi ya 162 katika taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara ikilinganishwa na nafasi ya 183, nafasi ya 167 na nafasi ya 163 mwaka 2018 mtawalia. Viashiria ambavyo Tanzania haikufanya vizuri ni pamoja na wepesi wa kupata mikopo nafasi ya 67, kuheshimu utekelezaji wa mikataba na ubora wa utatuza wa migogoro ya kibiashara nafasi ya 71 na upatikanaji wa umeme nafasi 85. Serikali inaendelea kutekeleza Mpango Kazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini kwa lengo la kupunguza kodi, tozo na ucheleweshaji wa shughuli za kibiashara. Kulunganana na taarifa ya Absa-Africa ya mwaka 2019 Tanzania ilishika nafasi ya saba (7) kati ya nchi 54 za Afrika katika ukomavu wa masoko ya fedha mwaka 2019 ikilinganishwa na nafasi ya 15 mwaka 2018.

Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi

155. Mwaka 2019, Serikali kuitia Baraza la Taifa la Uvezeshaji iliendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kuitia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi. Hadi Desemba 2019, mifuko ya uvezeshaji

wananchi kiuchumi inayotoa mikopo moja kwa moja kwa kushirikiana na mifuko inayotoa dhamana ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.24 kwa wajasiriamali 1,150,741. Kati ya hao, wanawake walikuwa 677,404 sawa na asilimia 59.0 na wanaume walikuwa 473,337. Katika kuhakikisha wananchi wanufaika na uwepo wa mifuko ya uwezeshaji, Serikali ilifanya makongamano katika halmashauri tisa (9) nchini ambapo wajasiriamali 6,516 walishiriki. Aidha, Serikali ilianda mwongozo wa uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji kwa kila mkoa kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa na huduma za uwezeshaji ambapo vituo sita (6) vilianzishwa katika mkoa wa Kigoma na kituo kimoja katika mkoa wa Shinyanga.

156. Katika kutekeleza Programu ya Taifa ya Ukuza Ujuzi, Baraza lilitoa mafunzo kwa vijana wajasiriamali 1,408 (wanawake 566 na wanaume 842) wakiwemo walemovu 90 katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Lindi, Tanga, Arusha, Mwanza, Geita na Ruvuma. Mafunzo hayo yalilenga kutoa ujuzi wa jinsi ya kuanzisha na kusimamia biashara, urasimishaji wa biashara, umuhimu wa kuunda vikundi, utafutaji masoko pamoja na kuunganisha wajasiriamali na fursa za mitaji kutoka mifuko ya uwezeshaji, benki na taasisi za fedha. **Jedwali Na.7.4** linaonesha mchanganuo wa wajasiriamali waliopatiwa mafunzo.

Jedwali Na. 7.4: Wajasiriamali waliopatiwa Mafunzo Mwaka 2019

Mkoa	Me	Ke	Jumla
Dodoma	135	78	213
Ruvuma	94	67	161
Geita	125	36	161
Mwanza	87	68	155
Mbeya	123	88	211
Lindi	61	106	167
Tanga	110	61	171
Arusha	107	62	169
Jumla kuu	842	566	1,408

Chanzo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji wananchi Kiuchumi

Ushiriki wa Watanzania katika Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati

157. Mwaka 2019, Serikali ilianda na kuzindua Mwongozo wa Uratibu wa Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati kwa lengo la kuhakikisha watanzania wanashiriki na kunufaika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika kipindi hicho, watanzania walajiriwa katika miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwemo: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ulioajiri watanzania 987 na wageni 373; Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki ulioajiri watanzania 115 na wageni 41; Mradi wa Ujenzi wa Jengo la III la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ulioajiri watanzania 997 na wageni 59; Mradi wa Reli ya Kisasa ulioajiri watazania 13,117 na wageni 813; na Mradi wa Barabara za Mapishano Ubungo ulioajiri watanzania 845 na wageni 100.

158. Mwaka 2019, miradi mingine ya maendeleo iliyoajiri watanzania ni pamoja na: mradi wa Ujenzi wa Daraja la Selander ulioajiri watanzania 677 ikilinganishwa na wageni 51; na mradi wa ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) ulioajiri watanzania 180 ikilinganishwa na wageni 18. Aidha, kampuni za ndani 71 zilipewa kazi katika kandarasi ndogo ikilinganishwa na kampuni 9 za kigeni.

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

159. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kupokea na kuchambua miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, miradi iliyopokelewa na kuchambuliwa ilikuwa: mradi wa Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA); miradi ya Maji kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar Es Salaam, Moshi, Mwanza, Tanga na Mbozi – Songwe; na miradi ya Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano, Ujenzi wa Jengo la Abiria na Ujenzi wa Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro.

160. Mwaka 2019, maandiko ya miradi yaliyopo katika hatua mbalimbali za uchambuzi ni pamoja na: Miradi ya Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma) na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini; Ujenzi wa Hospitali ya Taifa ya Saratani Mloganzila; Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Ujenzi wa Kituo cha biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; Mradi wa Kuzalisha Dawa Muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Dawa; Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; Ujenzi wa Reli ya Mtwara-Mchuchuma/Liganga kwa kiwango cha kisasa; na Ujenzi wa Reli ya Tanga-Arusha-Musoma kwa kiwango cha kisasa.

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA

Jedwali Na.33

Sekta	2018								2019							
	A	B	C	D	E	F	G	H	A	B	C	D	E	F	G	H
Kilimo	12	12	-	6	6	-	6,151	507	18	18	-	6	6	6	19,428	463
Maliasili	4	4	-	2	1	1	157	2	2	2	-	-	-	2	195	2
Uzalishaji Viwandani	108	108	-	68	38	2	10,893	639	156	156	-	41	70	45	17,713	1,159
Majengo ya biashara	26	26	-	13	13	-	2,580	245	11	11	-	2	6	3	1,101	159
Usafirishaji Mizigo	16	16	-	12	3	1	2,235	166	34	34	-	22	7	5	3,876	375
Huduma za Biashara	16	16	-	11	4	1	1,746	1,017	19	19	-	1	9	9	1,828	38
Komputa	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Taasisi za fedha	3	3	-	-	-	3	442	61	2	2	-	-	-	2	52	9
Mawasiliano	1	1	-	1	-	-	955	37	2	2	-	-	-	2	61	254
Nishati	3	3	-	1	2	-	36	52	6	6	-	4	2	-	669	28
Rasilimali watu	7	7	-	6	1	-	431	5	2	2	-	2	-	-	308	64
Utalii	18	18	-	11	1	6	1,817	91	16	16	-	7	7	2	1,260	60
miundombinu	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Utangazaji	1	1	-	1	-	-	26	0	1	1	-	1	-	-	212	12
Jumla	215	215	-	132	69	14	27,469	2,823	269	269	-	86	107	76	46,703	2,623

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

- A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
- B Miradi Mipyä
- C Miradi ya Maendeleo
- D Miradi ya Wazawa
- E Miradi ya Wageni
- F Miradi ya Ubia
- G Jumla ya Ajira
- H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 8

MASUALA MTAMBUKA

UKIMWI

Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI

161. Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI iliendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na UKIMWI ili kuweza kufikia Malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI Tanzania (2018/19-2022/23). Mojawapo ya malengo hayo ni kuhakikisha Nchi inatimiza Lengo la 90-90-90 kufikia Desemba 2020. Hadi Desemba 2019, watu 1,289,125 sawa na asilimia 80.6 ya watu 1,600,000 wanaokadiriwa kuwa na VVU walikuwa wanatambua hali zao ikilinganishwa na asilimia 75 ya watu 1,500,000 mwaka 2018 waliokuwa wanatambua hali zao. Aidha, watu 1,271,666 sawa na asilimia 98.6 ya watu 1,289,125 waliokua wanatambua hali zao walikuwa wanatumia dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI yaani ARV ikilinganishwa na asilimia 98 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, asilimia 91 ya watu walioanzishiwa dawa za ARV kinga zao za mwili ziliimarika na wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini na hivyo kupunguza uwezekano wa kuweza kuwaambukiza wenzi wao ikilinganishwa na asilimia 88 mwaka 2018.

162. Mwaka 2019, Serikali iliongeza mashine za kupima wingi wa virusi vya UKIMWI kufikia 40 kutoka mashine 17 mwaka 2018. Aidha, mashine nyingine 38 zinazoitwa “Point of Care (GeneXpert)” ambazo zinasaidia kupima wingi wa virusi vya UKIMWI kwenye vituo vidogo ambavyo vinatoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU ziliongezwa. Vile vile, vituo vinavyotoa huduma na tiba ya kufubaza VVU viliongezeka na kufikia 6,529 kutoka vituo 6,206 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vituo vya matunzo na matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI vilikuwa 2,861 na vituo vya huduma ya afya ya mama na mtoto vilikuwa 3,668.

Mazingira

163. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo unazingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ikiwa ni pamoja na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Katika kipindi hicho, miradi 720 ilipata hati za TAM baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na miradi 412 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia

74.8. Ongezeko hilo lilitokana na: Serikali kufanya uhamasishaji kwa njia ya redio na runinga kuhusu umuhimu wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa kila mradi utakaoteklezwa nchini na kutoa maelekezo kwa taasisi za fedha kutotoa mikopo kwa kampuni ambazo hazina vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira. Aidha, Serikali ilitoa hati tatu (3) za Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati mwaka 2019. Hati hizo zilitolewa katika: Sera, Mkakati, Sheria na Kanunu za Uvuvi wa Bahari Kuu; Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma; na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere.

164. Serikali iliendelea kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa kampeni ya kupanda miti ambapo mwaka 2019, miti 608,494,464 ilipandwa katika mikoa yote nchini. Kati ya hiyo, miti 382,134,523 sawa na asilimia 62.8 ya miti ilistawi.

165. Mwaka 2019, Serikali ilifanya marekebisho ya Kanuni ya Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi ya Mwaka 2009 kwa lengo la kuweka utaratibu wenyewe tija wa kusimamia taka hatarishi zikiwemo vyuma chakavu, mafuta machafu na betri zisizotumika. Marekebisho hayo yalitoa fursa kwa wadau wanaojihusisha na biashara ya ukusanyaji wa taka hizo kupata huduma kwa urahisi. Katika kipindi hicho, vibali 20 vilitolewa kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na ukusanyaji wa taka hatarishi ambazo hurejelezwa na kutumika kama malighafi katika shughuli za uzalishaji viwandani. **Jedwali Na. 8.1** linaonesha idadi ya vibali vilivyotolewa kwa kila aina ya taka hatarishi.

Jedwali Na. 8.1: Vibali Vilivyotolewa Mwaka 2019

Aina ya taka hatarishi	Idadi
Chuma chakavu	9
Mafuta machafu	5
Betri zilizotumika	3
Taka za kielektroniki	3
Jumla	20

Chanzo: Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

166. Mwaka 2019, Serikali ilizuia uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini kwa lengo la kulinda afya ya jamii, wanyama na mazingira dhidi ya athari zinazotokana na matumizi ya mifuko ya plastiki. Kutokana na zuio hilo, tani 890 za mifuko mbadala aina ya *non-woven* ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 192 zilizoingizwa kabla ya zuio. Aidha, zuio la mifuko ya plastiki liliibua fursa za biashara ikiwemo uzalishaji wa mifuko mbadala ambapo hadi Desemba 2019

kulikuwa na viwanda 14 vilivyozalisha mifuko mbadala. Kati ya hivyo, viwanda saba (7) vilizalisha mifuko mbadala aina ya *non-woven* na viwanda saba (7) vilizalisha mifuko ya karatasi. Vile vile, zuo hilo liliibua fursa za ajira ambapo takribani watu 345 walajiriwa katika uzalishaji wa mifuko mbadala na uzalishaji wa malighafi za kutengeneza mifuko hiyo.

167. Bioanuwai na ikolojia nchini huathiriwa na ongezeko la viumbe-vamizi vinavyojumuisha mimea na wanyama pamoja na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu ikiwemo kilimo, ufugaji na uvuvi. Tathmini ya viumbe-vamizi ya mwaka 2019, ilionesha uwepo wa takribani aina 198 za viumbe vamizi nchini. Katika kukabiliana na viumbe-vamizi, Serikali iliandaa mkakati wa miaka 10 (2019-2029) wa kukabiliana na athari zinazosababishwa na viumbe vamizi katika mazingira na katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, utalii, afya, uvuvi na mifugo.

Ulinzi na Usalama wa Raia

168. Mwaka 2019, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia na mataifa mengine liliendelea kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara haramu ya madawa ya kulevyta na usafirishaji haramu wa binadamu. Katika kipindi hicho, Jeshi lilifanya operesheni nne (4) za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na jumuiya za kikanda. Operesheni hizo zilifanyika katika nchi za Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kati na Lebanon.

169. Mwaka 2019, Serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ilitoa mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi na uzalendo kwa vijana 31,512 ambapo vijana 20,413 walipata mafunzo kwa mujibu wa sheria na vijana 11,099 walikuwa wa kujitolea. Aidha, kati ya vijana waliopatiwa mafunzo, 23,558 walikuwa wanaume na 7,954 walikuwa wanawake. Aidha, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMA JKT) lilitoa ajira kwa vijana 9,912 waliota huduma ya ulinzi kwa kampuni za umma na binafsi 408.

170. Mwaka 2019, makosa ya jinai 58,590 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 60,108 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Kati ya hayo, makosa dhidi ya binadamu yalikuwa 12,223 mwaka 2019 ikilinganishwa na makosa 11,759 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Makosa hayo yalijumuisha ya mauaji, ubakaji, ulawiti, wizi wa watoto, utupaji wa watoto,

unajisi na usafirishaji haramu wa binadamu. Aidha, makosa ya kuwania mali yalikuwa 28,853 mwaka 2019 ikilinganishwa na makosa 29,596 mwaka 2018. Makosa hayo yalijumuisha unyang'anyi, uvunjaji, wizi, kuchoma nyumba moto na uhalifu wa kifedha. Vile vile, makosa 17,514 dhidi ya maadili ya jamii yaliripotiwa mwaka 2019 ikilinganishwa na makosa 18,753 mwaka 2018. Makosa hayo yalihuisha rushwa, magendo, uhamiaji haramu pamoja na kupatikana na dawa za kulevya, nyara za Serikali, silaha, risasi, pombe ya moshi na mazao ya misitu.

171. Mwaka 2019, matukio makubwa ya usalama barabarani yaliyoripotiwa yalipungua kwa asilimia 26.7 na kufikia 2,924 ikilinganishwa na matukio 3,988 mwaka 2018. Upungufu huo ilitokana na kuongezeka kwa utii wa sheria bila shuruti kwa watumiaji wa vyombo vya moto barabarani na kampeni za uhamasishaji wa umma kuhusu umuhimu wa kutii sheria za usalama barabarani. Katika matukio hayo, kulikuwa na ajali 1,208 zilizosababisha vifo vya watu 1,536 mwaka 2019 ikilinganishwa na ajali 1,449 zilizosababisha vifo vya watu 1,912 mwaka 2018. Aidha, watu 3,123 walijeruhiwa mwaka 2019 ikilinganishwa na watu 4,194 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 25.5.

172. Mwaka 2019, idadi ya wafungwa katika magereza yote nchini ilikuwa 14,503 ikilinganishwa na wafungwa 18,661 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 22.3. Aidha, idadi ya mahabusu ilikuwa 17,845 ikilinganishwa na mahabusu 19,113 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 6.6. Hata hivyo, idadi hiyo ya wafungwa na mahabusu amba ni 32,348 ni kubwa ikilinganishwa na uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Aidha, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza msongamano magerezani ikiwemo kutoa adhabu ya vifungo vya nje kwa wafungwa 483 na kutumia vikao vya Bodi ya Parole ambapo wafungwa 91 walinufaika pamoja na ukarabati wa mabweni yaliyochakaa na ujenzi wa magereza kumi na nne ambayo ni mahabusu Morogoro, mahabusu Sumbawanga, Masasi, Handeni, Lindi, Kahama, Bariadi, Ruanda, Nzega, Ushora, Babati, Ngudu, Tarime na Biharamulo.

173. Mwaka 2019, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji iliendelea kukabiliana na majanga ya moto na majanga mengine. Katika kipindi hicho, miito 2,023 ya matukio ya moto ilipokelewa ikilinganishwa na miito 1,633 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.9. Hii ilitokana na namba ya dharura ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuanza kutumika kwenye mitandao yote ya simu pamoja

na kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu tahadhari na kinga ya moto. Aidha, Jeshi lilifanya maokozi katika matukio 853 mwaka 2019 ikilinganishwa na matukio 471 mwaka 2018. Vile vile, Jeshi liliendelea kutoa elimu kwa umma na kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali ambapo maeneo 93,963 yalikaguliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na maeneo 62,675 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 49.9. Ongezeko hilo lilitokana na kufanyika kwa kaguzi katika maeneo yenyе mikusanyiko ya watu wengi pamoja na kuanzishwa kwa ukaguzi wa magari katika vituo vya mabasi.

174. Mwaka 2019, wageni walioingia nchini kwa vibali halali walikuwa 1,457,597 ikilinganishwa na wageni 1,376,228 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Kwa upande mwingine, wageni 1,174,411 waliondoka nchini mwaka 2019 ikilinganishwa na wageni 1,555,273 mwaka 2018. Aidha, vibali vya ukaazi 20,844 vilitolewa mwaka 2019 ikilinganishwa na vibali vya ukaazi 15,769 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 32.2. Ongezeko hilo lilitokana na idara kuzindua mfumo wa utoaji huduma kielektroniki pamoja na utendaji wa karibu baina ya idara ya kazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara ya Uhamiaji. Kati ya vibali hivyo, vibali 2,219 vilikua vya daraja A, vibali 11,682 daraja B na vibali 6,943 daraja C. Vile vile, jumla ya hati za kusafiria 198,209 zilitolewa kwa watanzania mwaka 2019 ikilinganishwa na hati 74,896 mwaka 2018. Wahamiaji haramu 12,687 walikamatwa mwaka 2019 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 13,691 mwaka 2018.

175. Mwaka 2019, Tanzania ilihifadhi wakimbizi 291,647 kutoka mataifa mbalimbali ikilinganishwa na wakimbizi 326,941 mwaka 2018. Kati ya hao, wakimbizi 216,072 walitoka Burundi, 75,217 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, 150 Somalia na wakimbizi 208 kutoka mataifa mengine. Aidha, wakimbizi 20,936 walirejeshwa katika nchi zao kwa hiari kutoptana na kuimarika kwa hali ya amani katika nchi hizo. Vile vile, wakimbizi 4,078 walihamishiwa nchi ya tatu katika nchi za Marekani, Canada, Australia, Uhlanzi na Ireland.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

176. Mwaka 2019, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa wananchi katika mikoa yote Tanzania. Hadi Desemba 2019, jumla ya wananchi 21,511,321 walitambuliwa na kusajiliwa ikilinganishwa na wananchi 19,648,857 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Aidha, Mamlaka ilisajili wageni wakaazi 19,311 na wakimbizi 200,074 waliokuwa katika kambi za Mtendeli, Nduta na Nyarugusu

(Kigoma), makazi ya Katumba na Mishamo (Katavi), kambi ya Ulyankulu (Tabora) pamoja na wakimbizi wenyе vibali vya kuishi katika jiji la Dar es Salaam.

177. Hadi Desemba 2019, Mamlaka ilizalisha namba za utambulisho 16,211,654. Katika kipindi hicho, vitambulisho vilivyotolewa na Mamlaka viliongezeka na kufikia 5,787,869 kutoka vitambulisho 4,494,790 Desemba 2018. Ongezeko hilo lilitokana na hitaji la kuwa na namba ya utambulisho wa Taifa katika usajili wa laini za simu pamoja na ongezekoko la taasisi na kampuni zinazohitaji wateja wao kuwa na namba za utambulisho ili kupata huduma. Aidha, Mamlaka iliziunganisha ofisi 126 za usajili za wilaya na huduma ya mtandao wa mawasiliano ili kurahisisha usafirishaji wa taarifa baina ya ofisi hizo na makao makuu ya Mamlaka. Vile vile, Mamlaka iliziunganisha taasisi 57 katika mfumo wake wa utambuzi mwaka 2019 ikilinganishwa na taasisi 45 mwaka 2018.

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini

178. Mwaka 2019, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ulisajili vizazi 2,164,982, vifo 35,708, ndoa 44,562, talaka 295, hati 34 za watoto wa kuasili na hati 98 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na usajili wa vizazi 1,409,206, vifo 22,938, ndoa 24,490, talaka 3,923 hati 32 za watoto wa kuasili na hati 71 za miunganisho ya wadhamini mwaka 2018. Ongezeko la usajili wa vizazi lilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya usajili wa vitambulisho vya Taifa na kampeni za usajili wa watoto wenyе umri chini ya miaka mitano zilizofanyika katika mikoa ya Dodoma, Singida, Pwani na Morogoro. Aidha, Wakala ulifunga Mfumo wa Usajili wa Vizazi – Toleo la Nne katika wilaya za Chemba, Malinyi, Bahi, Buhigwe, Kakonko na Kalambo na hivyo kukamilisha ufungwaji wa mfumo huo katika wilaya zote Tanzania Bara.

Utawala Bora

179. Mwaka 2019, Serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliendelea kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Katika kipindi hicho, uchunguzi wa majalada 916 ulikamilika ambapo majalada 51 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani ikilinganishwa na majalada 163 mwaka 2018. Aidha, kesi mpya 331 zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa kufikia 718 mwaka 2019. Vile vile, kesi 324 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 137 watuhumiwa wake

waliachiwa huru na kesi 187 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini.

180. Mwaka 2019, Serikali iliendesha Mashauri 59 ya usuluhishi ya kitaifa na kimataifa ambapo mashauri 40 yalikuwa ya kitaifa na mashauri 19 ya kimataifa. Katika kipindi hicho, Mashauri 15 yalihitimishwa, kati ya hayo Mashauri mawili (2) ni ya kimataifa na Mashauri 13 ni ya kitaifa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 6424.3 kiliokolewa.

181. Mwaka 2019, Mahakama ya Tanzania ilisikiliza mashauri 225,308 kati ya mashauri 228,152 yaliyofunguliwa katika ngazi zote za Mahakama. Aidha, Mahakama ilishughulikia malalamiko 994 kati ya malalamiko 1,080 yaliyokuwepo, sawa na asilimia 92 ya malalamiko yote. Katika kipindi hicho, Mahakama iliendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa haki nchini na kuwezesha utambuzi wa taarifa na takwimu mbalimbali za Mahakama katika kutafsiri sheria. Kwa upande mwingine, Serikali iliendesha kesi 25,163 katika Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi mwaka 2019 ambapo kesi 8,330 zilisikilizwa na kutolewa hukumu. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Sheria (Sura Na. 21) kwa kusajili watoa huduma ya msaada wa sheria 126 na wasaidizi wa kisheria 498. Aidha, Serikali iliteua Wasajili Wasaidizi 185 katika kila mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kusajili, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria. Kupitia huduma hii wananchi walipata huduma za haki kwa gharama nafuu na kwa wakati.

SURA YA 9

HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU

Utangulizi

182. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati mbalimbali ya kuimarisha maendeleo ya watu, kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza umaskini. Utekelezaji huo utawezesha nchi kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

Viashiria vya Umaskini

183. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS) wa Mwaka 2017/18 ni utafiti wa tano katika mfululizo wa tafiti za mapato na matumizi ya kaya zilizofanyika Tanzania Bara tangu mwaka 1991/92. Lengo kuu la HBS 2017/18 ni kutoa taarifa mpya za makadirio ya viwango vya umaskini na viashiria vinavyohusiana na umaskini kwa ajili ya kufuatilia, kupima na kutathmini mipango mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na kupima maendeleo yaliyofikiwa katika kuimarisha hali ya maisha ya watu. Utafiti huu unajumuisha viashiria vya umaskini wa kipato na usio wa kipato.

Umaskini wa Kipato

184. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18, unaonesha kuwa umaskini umepungua hadi asilimia 26.4 kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12. Katika maeneo ya mijini umaskini umepungua kutoka asilimia 21.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 15.8 mwaka 2017/18. Kwa upande wa maeneo ya vijijini, umaskini umepungua kutoka asilimia 33.3 mwaka 2011/12 hadi asilimia 31.3 mwaka 2017/18. Kupungua kwa umaskini kumechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa kaya zilizounganishwa na umeme, kuboreshwa kwa hali ya makazi na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za kijamii kama maji, elimu na afya.

Umaskini Usio wa Kipato

185. Hali ya umaskini inaweza kupimwa kwa kutumia kigezo/kiashiria zaidi ya kimoja ili kutoa picha pana ya hali ya umaskini. Kutokana na hilo, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi hujumuisha viashiria vya umaskini usio wa kipato katika kupima hali ya umaskini. Viashiria hivyo ni pamoja na umiliki wa

akaunti za benki, hali ya makazi, umiliki wa mali, huduma ya maji na matumizi ya nishati.

Umiliki wa Akaunti za Benki

186. Umiliki wa akaunti za benki ni muhimu katika kukuza shughuli za uchumi na biashara na kuboresha ustawi wa jamii. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, umiliki wa akaunti za benki katika kaya umeongezeka ambapo kaya zenyne angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti benki zimefikia asilimia 12.3 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 10 mwaka 2007. Kasi ndogo ya ongezeko la umiliki wa akaunti inachangiwa na kuongezeka kwa wigo wa utoaji wa huduma za fedha kuptitua sekta rasmi isiyo ya kibenki inayojumuisha huduma za fedha kwa simu za kiganjani inayomuwezesha mwananchi kuhifadhi fedha na kufanya miamala ya kifedha. Katika maeneo ya mijini, kuna kiwango kikubwa cha watu wanaomiliki akaunti za benki ambapo asilimia 23.8 ya kaya zina angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti benki. Kiwango hiki ni takribani mara nne ya kiwango cha kaya za vijijini ambapo asilimia 6.1 ya kaya zina angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti benki. Hii inamaanisha kuwa asilimia kubwa ya watu wanaoishi vijijini wanapata huduma za fedha kuptitua VICOBA, ushirika wa akiba na mikopo vijijini pamoja na ushirika wa kuweka akiba na kukopa kwa zamu.

Hali ya Makazi

187. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18 unaonesha kuwa makazi yaliyojengwa kwa paa za kisasa yamefikia asilimia 84.1 ya makazi yote Tanzania Bara mwaka 2017/18 kutoka asilimia 68 mwaka 2011/12. Aidha, kaya zinazoishi kwenye makazi yaliyojengwa kwa kuta imara zimefikia asilimia 78.8 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 46 mwaka 2011/12. Vile vile, kaya zinazoishi kwenye makazi yaliyojengwa kwa sakafu za kisasa zimeongezeka hadi asilimia 50.1 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 40 mwaka 2011/12. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa kipato cha kaya na kuimarika kwa ubora wa maisha ya watanzania. Kwa upande mwengine, makazi ya vijijini yaliyojengwa kwa kutumia paa, kuta na sakafu za kisasa ni asilimia 76.6, asilimia 70.5 na asilimia 32.1 ikilinganishwa na asilimia 97.6, asilimia 94.0 na asilimia 85.6 katika maeneo ya mijini kwa mtiririko huo.

Umiliki wa Mali

188. Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi hususan wenye kipato cha chini kuweza kumiliki mali. Kulingana na Utafiti wa Mapato na

Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18, kumekuwa na ongezeko la umiliki wa simu za mkononi, pikipiki na runinga. Kaya zinazomiliki simu za mkononi zimeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2011/12 hadi asilimia 78 mwaka 2017/18. Hii imetokana na kuongezeka kwa matumizi ya simu katika shughuli za kiuchumi na kufanya miamala ya kifedha. Kaya zinazomiliki pikipiki zimeongezeka hadi asilimia 11 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 4.0 mwaka 2011/12. Hii imetokana na kuongezeka kwa matumizi ya pikipiki katika shughuli za biashara hususan usafirishaji wa abiria. Aidha, kaya zinazomiliki runinga zimeongezeka kutoka asilimia 16 mwaka 2011/12 hadi asilimia 24 mwaka 2017/18. **Jedwali Na. 9.1** linaonesha kiwango cha umiliki wa mali kwa mwaka 2017/18.

Jedwali Na. 9.1: Kiwango cha Umiliki wa Mali (Asilimia)


Mwaka	2011/12	2017/18
Simu za mkononi	57	78
Runinga	16	24
Pikipiki	4	11
Redio	55	43
Simu za Mezani	1	0.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu - Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi

Huduma ya Maji

189. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18, takriban kaya 9 kati ya 10 (asilimia 87.8) zinatumia maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshw wakati wa msimu wa mvua ikilinganishwa na takriban kaya 7 kati ya 10 (asilimia 69.1) mwaka 2011/12. Katika msimu wa kiangazi, kaya zinazotumia maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshw kilikuwa asilimia 73.0 ikilinganishwa na asilimia 60.5 mwaka 2011/12. Kwa upande mwingine, kaya zinazotumia maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshw wakati wa msimu wa mvua katika maeneo ya mjini na vijiji zimeongezeka na kufikia asilimia 95.6 na asilimia 83.5 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 85.0 na asilimia 62.4 mwaka 2011/12 kwa mtiririko huo. Katika msimu wa kiangazi, kaya zinazotumia maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshw katika maeneo ya mijini na vijiji zimeongezeka na kufikia asilimia 87.6 na asilimia 65.0 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 78.0 na asilimia 52.5 mwaka 2011/12 kwa mtiririko huo.

Kielelezo Na. 9.1: Upatikanaji wa Maji katika Misimu ya Mvua na Kiangazi mwaka 2017/18



Matumizi ya Nishati

190. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18, asilimia 29.0 ya kaya za Tanzania Bara zinatumia nishati ya umeme wa TANESCO kama chanzo kikuu cha kuangazia ikifuatiwa na kurunzi/taa ya kuchaji (asilimia 27.5), umeme wa mionzi ya jua (asilimia 26.5) na vyanzo vingine (asilimia 17). Aidha, asilimia 63.8 ya kaya za mijini zinatumia umeme kwa kuangazia ikilinganishwa na asilimia 10.0 ya kaya za vijijini. Kwa upande wa nishati ya kupikia, asilimia 60.9 ya kaya za Tanzania Bara zinatumia kuni kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia ikilinganishwa na asilimia 66.3 ya kaya mwaka 2011/12. Matumizi ya kuni ni makubwa zaidi maeneo ya vijijini (asilimia 84.8) ikilinganishwa na maeneo ya mjini (asilimia 17.4). Kaya zinazotumia mkaa zimeongezeka kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 28.8 mwaka 2017/18. Vile vile, gesi ya viwandani inatumiwa na asilimia 3.2 ya kaya, umeme asilimia 2.1, mafuta ya taa asilimia 1.3 na umeme wa mionzi ya jua asilimia 1.1. Kwa ujumla, takwimu hizi zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 89 ya kaya za Tanzania Bara zinategemea kuni na mkaa kama chazo kikuu cha nishati. Matumizi ya nishati hizi ni makubwa kwa kuwa zinapatikana kwa urahisi na gharama zake ni ndogo ikilinganishwa na nishati mbadala kama umeme na gesi ya viwandani. Hata hivyo, ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unaharibu ikolojia ya misitu na kusababisha uharibifu wa mazingira. Hivyo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wabunifu kuendelea kuibua nishati

mbalimbali zenyenye gharama nafuu na zitakazowezwa kutumika badala ya mkaa na kuni.

Maendeleo ya Watu

191. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za msingi hususan afya na elimu pamoja na upatikanaji wa huduma hizo kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya watu. Kutokana na hilo, umri wa kuishi mtanzania ambao ni kigezo muhimu katika kupima maendeleo ya watu umeongezeka kutoka wastani wa miaka 65.0 mwaka 2018 na kufikia wastani wa miaka 65.5 mwaka 2019. Aidha, Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya mwaka 2019 inaonesha kuwa Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (HDI) imeongezeka na kufikia 0.528 mwaka 2018 kutoka 0.522 mwaka 2017. Hii inaashiria kuimariika kwa kiwango cha maendeleo ya watu nchini.

192. Rushwa hupunguza kasi ya utoaji wa huduma za msingi kwa jamii na hivyo kusababisha kasi ndogo ya kuimarika kwa maendeleo ya watu. Mwaka 2019, Serikali iliendelea na jitihada za kupambana na vitendo vya rushwa katika sekta ya umma ili kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu katika kuboresha maendeleo ya watu. Kutokana na jitihada hizo, Tanzania ilipata alama 37 ya Fahirisi ya Rushwa mwaka 2019 ikilinganishwa na alama 36 mwaka 2018. Hii inaashiria kuimariika kwa jitihada za kupambana na vitendo vya rushwa nchini. Kimataifa, Tanzania ilikuwa nafasi ya 96 ya Fahirisi ya Rushwa mwaka 2019 ikilinganishwa na nafasi ya 99 mwaka 2018.

SEHEMU YA TATU SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

SURA YA 10

SEKTA ISIYO RASMI

Utangulizi

193. Sekta isiyo rasmi inajumuisha shughuli za kiuchumi na kibiashara zilizo nje ya mfumo ulio rasmi. Sekta hiyo huchangia katika uchumi wa Taifa kwa kutoa fursa za kiuchumi kwa watanzania wenyе mtaji mdogo na kuwawezesha kujihusisha na shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujipatia kipato. Sifa kuu za shughuli za kiuchumi au biashara zilizopo kwenye sekta hii ni pamoja na kutokuwa na maeneo rasmi ya kufanyia biashara, kutembeza bidhaa mkononi, kukosekana kwa kumbukumbu za hesabu na taarifa za shughuli zinazofanyika pamoja na kutokuwa na usajili rasmi na hivyo kuleta ugumu kwa mamlaka husika kutoa huduma mbalimbali na ukusanyaji wa mapato. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii katika uchumi, ushirikiano zaidi kati ya Serikali na wadau wengine unahitajika ili kuwawezesha urasimishaji wa biashara zisizo rasmi. Hatua hii itasadidua kupunguza ukosefu wa ajira, kuboresha mazingira ya kazi, kuongeza ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Tafiti Zilizowahi Kufanyika

194. Serikali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali katika sekta isiyo rasmi kwa lengo la kupunguza ukubwa wa sekta hiyo na kuwawezesha wananchi kuendesha shughuli za kiuchumi na kumiliki mali katika mfumo ulio rasmi. Utafiti wa kitaifa uliofanyika mwaka 1991 ulioneshwa kuwa takribani watu 2,369,380 walijihuisha na uzalishaji wa bidhaa na kutoa huduma katika sekta isiyo rasmi. Idadi hiyo ilikuwa sawa na asilimia 9.9 ya watu 23,850,295 waliokuwa wanaishi Tanzania Bara mwaka 1991. Aidha, sekta isiyo rasmi iliendelea kukua kutohana na kufungwa na kubinafsishwa kwa mashirika ya umma mwaka 1992 na kupunguzwa kwa wafanyakazi serikalini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya mageuzi ya kiuchumi. Utekelezaji wa programu hiyo ulisababisha watu kupoteza ajira serikalini na kushindwa kupata ajira mbadala mahali pengine kwa sababu ukuaji wa sekta binafsi ulikuwa mdogo, hivyo kushindwa kupokea walioachishwa kazi pamoja na waliokuwa wanatafuta kazi.

195. Utafiti mwingine wa sekta isiyo rasmi ulifanyika mwaka 1995 na ulikuwa na lengo la kubaini ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika jiji la Dar es Salaam. Hii ilitokana na kasi kubwa ya ongezeko la watu na shughuli nyingi za kiuchumi katika jiji la Dar es Salaam. Idadi ya watu katika jiji la Dar es Salaam iliongezeka

na kufikia 1,840,787 mwaka 1995 kutoka watu 1,549,904 mwaka 1991, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 4.7 kwa mwaka. Kulingana na utafiti huo, idadi ya watu waliojihusisha katika sekta isiyo rasmi katika jiji la Dar es Salaam iliongezeka kwa asilimia 9.5 na kufikia watu 345,869 mwaka 1995 kutoka watu 315,958 mwaka 1991. Hata hivyo, idadi ya watu waliojihusisha katika sekta isiyo rasmi ilipungua na kufikia asilimia 18.8 ya wakazi wote wa Dar es Salaam mwaka 1995 ikilinganishwa na asilimia 20.4 mwaka 1991.

196. Mwaka 2014, Serikali ilifanya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi ambapo matokeo yalionesha kuwa asilimia 42.5 ya kaya nchini ziliwuwa katika sekta isiyo rasmi ikilinganishwa na asilimia 39.5 kulingana na matokeo ya utafiti kama huo ulifanyika mwaka 2006. Hii iliashiria kuwa sekta isiyo rasmi ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi. Aidha, inakadiriwa kuwa asilimia 35 hadi 55 ya kodi haikusanywi kutokana na ugumu wa mazingira ya ukusanyaji kodi katika sekta isiyo rasmi.

197. Mwaka 2019, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya utafiti wa sekta isiyo rasmi katika mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kubaini mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa. Tafsiri iliyotumika kukokotoa viashiria vya ajira katika utafiti huo ilitokana na Mkutano wa 15 wa Watakwimu wa Takwimu za Kazi wa mwaka 1993 ulioandaliwa na Shirika la Kazi Duniani. Kwa mujibu wa tafsiri hiyo, sekta isiyo rasmi inajumuisha biashara zinazomilikiwa na watu binafsi au kaya ambazo haziwezi kutenganishwa na wamiliki wake kisheria, hazina kumbukumbu kamili za fedha na huajiri watu wasiozidi watano. Katika kukidhi mahitaji ya takwimu za Pato la Taifa, utafiti ulitumia kigezo cha usajili wa biashara kisheria kuitambua sekta isiyo rasmi.

Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi wa Mwaka 2019 kwa Mkoa wa Dar es Salaam

198. Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi wa Mwaka 2019 kwa Mkoa wa Dar es Salaam ulikusudia kupata makadirio ya pato ghafi, ongezeko la thamani kutokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma katika shughuli za kilimo na zisizo za kilimo, tija katika uwekezaji, kiwango cha ukuzaji mtaji, thamani ya uzalishaji kwa kila mtu na ajira na mgawanyo wake. Vile vile, utafiti ulilenga kubaini mahusiano kati ya sekta isiyo rasmi na sekta nyingine za kiuchumi pamoja na kutambua mahali biashara zilipo. Utafiti huo ulifanyika kwa mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu ndio mkoa unaoongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa (asilimia 18 mwaka 2018) na idadi kubwa ya watu ambao ni asilimia 10 ya watu

wote nchini kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Utafiti huo ulihusisha kaya 1,322,995 za mkoa wa Dar es Salaam.

Mgawanyiko wa Wamiliki katika Sekta Isiyo Rasmi

199. Matokeo ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi wa Mwaka 2019 yalionesha kuwa, mkoa wa Dar es Salaam una wamiliki wa shughuli za sekta isiyo rasmi takribani 1,023,520 ikilinganishwa na wamiliki 222,915 mwaka 1995. Wamiliki hao ni sawa na asilimia 19.4 ya watu wote wa jiji la Dar es salaam waliokadiriwa kuwa 5,275,315 mwaka 2019. Kati ya hao, wanawake walikuwa 587,234 sawa na asilimia 57.4 na wanaume walikuwa 436,286. Aidha, wamiliki wengi wa shughuli za kiuchumi kwenye sekta isiyo rasmi walikuwa na umri wa miaka 36-59 sawa na asilimia 53.3 wakifuatiwa na vijana wenyе umri wa miaka 15-35 (asilimia 41.9) na wenyе umri wa miaka 60 na kuendelea (asilimia 4.8). Vile vile, asilimia 66.9 ya wamiliki wa sekta isiyo rasmi walikuwa na elimu ya msingi ikifuatiwa na asilimia 23.2 waliokuwa na elimu ya sekondari. **Jedwali Na. 10.1.**

Jedwali 10.1: Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Katika Sekta Isiyo Rasmi (Asilimia)

Makundi ya Umri	Wanaume	Wanawake	Jinsia zote
Chini ya miaka 15	0.1	0.0	0.03
15-24	9.2	11.3	10.4
15-35	41.1	42.5	41.9
25-35	32.0	31.2	31.5
36-44	24.7	29.4	27.4
45-59	28.1	24.2	25.9
60+	6.1	3.9	4.8
Kiwango cha Elimu	Wanaume	Wanawake	Jinsia zote
Hajawahi kwenda shule	2.5	4.8	3.8
Mafunzo ya ufundi	4.1	2.7	3.3
Elimu ya msingi	66.3	67.4	66.9
Elimu ya sekondari	23.4	23.1	23.2
Elimu ya chuo kikuu	3.7	2.1	2.7
Asilimia (Kiwango cha elimu)	100.0	100.0	100.0
Jumla ya Wamiliki Sekta isiyo rasmi	436,286	587,234	1,023,520

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Taktamu

200. Mwaka 2019, kaya 767,904 sawa na asilimia 58.0 ya kaya zote za mkoa wa Dar es Salaam zilizofanyiwa utafiti zilibainika kuwa na angalau mwanakaya mmoja mwenye shughuli ya kiuchumi iliyo kwenye sekta isiyo rasmi ikilinganishwa na asilimia 55.6 ya kaya zilizofanyiwa utafiti mwaka 1995. Aidha,

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikuwa na kiwango kikubwa cha kaya zeny shughuli zilizo kwenye sekta isiyo rasmi kwa asilimia 61.5 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilikuwa na kiwango kidogo cha kaya (asilimia 53.7). **Jedwali Na. 10.2.**

Jedwali 10.2: Mgawanyo wa Kaya katika Sekta Isiyo Rasmi

Halmashauri	Jumla ya kaya kutoka zoezi la uorodhesaji	Kaya zeny shughuli zisizo rasmi	Uwiano wa kaya zeny shughuli zisizo rasmi
Kinondoni	269,806	152,354	56.5
Ilala	371,472	226,091	60.9
Temeke	350,590	207,018	59.0
Ubungo	270,871	145,402	53.7
Kigamboni	60,255	37,039	61.5
Jumla	1,322,994	767,904	58.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

201. Biashara za jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki ziliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wamiliki katika sekta isiyo rasmi (asilimia 47.6). Aidha, shughuli za utoaji huduma mbalimbali ziliwu na kiwango kidogo cha wamiliki wa biashara katika sekta isiyo rasmi (asilimia 0.1). Kwa upande mwingine, matokeo yalionesha kuwa asilimia 55.2 walimiliki shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi kutokana na kutopata kazi nyingine na asilimia 54.3 kutokana na uhitaji wa familia kupata mapato ya ziada. Vile vile, asilimia 20.2 ya wamiliki wa biashara walijihuisha kwenye sekta isiyo rasmi kwa kuwa biashara haihitaji mtaji mkubwa¹. **Jedwali Na. 10.3.**

¹ Jumla ya asilimia sio lazima iwe 100 kwa sababu inaweza kuwa zaidi ya moja

Jedwali 10.3: Sababu za Kujihusisha katika Sekta Isiyo Rasmi (Asilimia)

Sababu za Kujihusisha	Wanaume	Wanawake	Jumla
Sikupata kazi nyingine	55.4	55.1	55.2
Kuachishwa kazi au kupungua muda wa kufanya kazi	6.4	3.1	4.6
Kustaafu kutoka kwenye ajira nyingine	4.3	2.8	3.4
Familia inahitaji mapato ya ziada	48.9	58.4	54.3
Biashara / shughuli inatoa fursa ya mapato mazuri	18.8	14.2	16.2
Biashara / shughuli haihitaji mtaji mkubwa	18.3	21.7	20.2
Nawaza kupunguza gharama za uzalishaji	2.5	2.2	2.4
Nataka kuwa huru kutoka kwa muajiri	17	12.8	14.6
Naweza kuchagua muda na eneo la kufanya kazi	11.8	12.5	12.2
Naweza kuchanganya biashara/shughuli na majukumu ya kaya/kifamilia	16	25.8	21.5
Urasimu wa kurasimisha biashara / shughuli	0.5	0.5	0.5
Ni biashara ya asili ya familia au kabilo	2.3	1.4	1.8
Nyingine	7.4	6.9	7.1
Jumla ya Waendeshaji	463,046	601,952	1,064,998

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

202. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa takribani wamiliki 41,421 wa biashara katika sekta isiyo rasmi katika mkoa wa Dar es Salaam walipokea mikopo ya biashara ikilinganishwa na wamiliki 1,841 mwaka 1995. Kati ya hao, wanawake walikuwa 30,922 na wanaume 10,499. Aidha, wanufaika 23,513 wa mikopo walijihuisha na biashara za jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki wakifuatiwa na wanufaika 9,054 waliojihuisha na huduma za malazi na chakula na wanufaika 3,990 katika shughuli za kilimo, misitu na uvuvi.

Jedwali Na. 10.4.

Jedwali 10.4: Idadi ya Wanufaika wa Mikopo Katika Sekta Isiyo Rasmi

Shughuli za Kiuchumi	Wanaume	Wanawake	Jumla
Shughuli za kilimo, misitu na uvuvi	0	3,990	3,990
Shughuli za uchimbaji wa madini, mchanga na upasuaji wa mawe	514	0	514
Uzalishaji viwandani	0	317	317
Ujenzi	515	0	515
Biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	6,142	17,371	23,513
Usafirishaji na hifadhi	1,038	0	1,038
Huduma za malazi na chakula	494	8,560	9,054
Shughuli za mali isiyohamishika	708	0	708
Sanaa, burudani na starehe	515	0	515
Shughuli nyingine za utoaji huduma	573	684	1,257
Jumla Kuu	10,699	30,922	41,421

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Maeneo ya kufanyia biashara

203. Matokeo ya Utafiti yalionesha kuwa kuna tofauti kubwa ya idadi ya biashara zilizofanyika kwenye maeneo ya kudumu na yasiyo ya kudumu. Kati ya shughuli 1,023,520 za sekta isiyo rasmi zinazofanyika jijini Dar es Salaam, asilimia 76.6 zilifanyika katika maeneo yasiyo ya kudumu na asilimia 40.1 katika maeneo ya kudumu. Vile vile, matokeo yalionesha kuwa asilimia 77.6 ya wanawake waliendesha biashara zao katika maeneo yasiyo ya kudumu ikilinganishwa na asilimia 75.2 ya wanaume.

Uwekezaji wa Mitaji

204. Matokeo ya Utafiti yalionesha kuwa uwekezaji wa mitaji katika sekta isiyo rasmi katika jiji la Dar es Salaam ulikuwa na thamani ya shilingi bilioni 901.5 mwaka 2019. Aidha, shughuli zenyne thamani kubwa ya uwekezaji zilikuwa: biashara za jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki (shilingi bilioni 346.6); kilimo, misitu na uvuvi (shilingi bilioni 188.7); na shughuli za malazi na huduma za chakula (shilingi bilioni 81.1). Vile vile, wastani wa uwekezaji wa mitaji kwa kila mmiliki wa shughuli ya kiuchumi katika sekta isiyo rasmi ni shilingi 880,830. Wastani wa mtaji kwa wanaume ulikuwa shilingi 1,321,688 ikilinganishwa na shilingi 553,293 kwa wanawake. **Jedwali 10.5.**

Jedwali Na. 10.5: Mtaji wa Uwekezaji kwenye Sekta Isiyo Rasmi kwa Shughuli za Kiuchumi


Shughuli za Kiuchumi	Mtaji wa Sasa (Shilingi Bilioni)		
	Wanaume	Wanawake	Jumla
Shughuli za kilimo, misitu na uvuvi	78.1	110.6	188.7
Shughuli za uchimbaji wa madini, uchimbaji wa mchanga upasuaji wa mawe	6.5	0.9	7.4
Uzalishaji wandani	32.5	16.6	49.1
Uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na viyoyozi	5.3	0.4	5.7
Usambazaji wa maji; majitaka na usimamizi wa taka	2.7	1.1	3.8
Ujenzi	16.1	0.3	16.4
Biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	243.6	103.1	346.6
Usafirishaji na hifadhi	58.5	0	58.6
Huduma za malazi na chakula	30.9	50.2	81.1
Habari na mawasiliano	1.3	0.7	2
Shughuli za kifedha na bima	2.6	1.3	3.9
Shughuli za kitaalamu, kisayansi na kiufundi	4.7	2.4	7.2
Shughuli za utoaji wa huduma mbalimbali	1.1	-	1.1
Elimu	23.8	1.3	25.2
Afyya ya binadamu na shughuli za kijamii	6	9.5	15.6
Sanaa, burudani na starehe	17.6	3.1	20.7
Shughuli nyingine za utoaji huduma	45.3	23.4	68.7
Jumla Kuu	576.6	324.9	901.5

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ajira katika Sekta Isiyo Rasmi

206. Matokeo ya Utafiti yalioneshwa kuwa ajira katika sekta isiyo rasmi katika mkoa wa Dar es Salaam kwa watu wenyewe umri wa miaka 15 au zaidi zilipungua kutoka ajira 1,208,250 (asilimia 61.5) mwaka 2014 hadi ajira 1,125,064 (asilimia 55.2) mwaka 2019. Upungufu huo ulichangiwa na juhudini za Serikali kuongeza wigo wa ajira katika sekta rasmi. Aidha, biashara za jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki zilikuwa na kiwango kikubwa cha ajira katika sekta isiyo rasmi (asilimia 44.8). Vile vile, asilimia 44.8 ya watu walio katika sekta isiyo rasmi katika mkoa wa Dar es Salaam walijihuisha na shughuli ndogo ndogo zisizo na ujuzi maalum. **Kielelezo Na. 10.1.**

Kielelezo 10.1: Kiwango cha Ajira katika Sekta Isiyo Rasmi



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

207. Kwa upande mwingine, utafiti unaonesha kuwa asilimia 4.1 ya wamiliki wa biashara katika sekta isiyo rasmi wana mipango ya kuongeza wafanyakazi zaidi kwenvye shughuli zao katika kipindi cha miezi 12 ijayo ambapo jumla ya ajira 114,868 zinatarajiwa kuzalishwa. **Jedwali Na. 10.6** linaonesha mchanganuo wa ajira zitakazozalishwa na sekta isiyo rasmi.

Jedwali Na.10.6: Shughuli za Sekta Isiyo Rasmi na Mipango ya Kuongeza Wafanyakazi

Shughuli za kiuchumi	Asilimia ya wamiliki wenye mpango wa kuongeza wafanyakazi	Idadi ya ajira zitakazozalishwa
Shughuli za kilimo, misitu na uvuvi	6.9	26,211
Uzalishaji viwanda	7	26,748
Ujenzi	3.5	3,435
Biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	2.6	23,117
Huduma za malazi na chakula	6.8	14,195
Sanaa, burudani na starehe	21.4	12,855
Shughuli nyingine za utoaji huduma	4.9	8,309
Jumla	4.1	114,868

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Pato Ghafi na Ongezeko la Thamani

208. Mwaka 2019, jumla ya ongezeko la thamani kwenye bidhaa na huduma zilizozalishwa katika sekta isiyo rasmi katika jiji la Dar es Salaam ilikuwa shilingi bilioni 6,188.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 205.2 mwaka 1995. Aidha, sehemu kubwa ya ongezeko la thamani ilikuwa kwenye biashara za jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki (asilimia 48.0) ikifuatiwa na shughuli za kilimo, misitu na uvuvi (asilimia 9.9). **Jedwali Na. 10.6.**

**Jedwali 10.6: Jumla ya Pato Ghafi la Mwaka na Ongezeko la Thamani
(Shilingi Bilioni) katika Sekta Isiyo Rasmi**

Shughuli za kiuchumi	Pato ghafi	Mali ghafi pamoja na gharama nyingine za uzalishaji	Ongezeko la thamani	Mchango kwenye ongezeko la thamani (Asilimia)
Kilimo, misitu na uvivu	1,601.7	989.7	612	9.9
Uchimbaji madini	255.4	2.0	253.4	4.1
Uzalishaji viwandani	736.4	247.0	489.4	7.9
Shughuli za uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na viyoyozi	11.6	8.8	2.8	0.1
Usambazaji wa maji, majitaka na usimamizi wa taka	182.2	148.8	33.4	0.5
Ujenzi	364.1	81.4	282.7	4.6
Biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na mapikipiki	8,203.8	5233.2	2,970.6 0	48.0
Usafirishaji na uhifadhi	148.0	52.9	95.1	1.5
Huduma za malazi na chakula	1,719.3	1171.0	548.3	8.9
Habari za mawasiliano	22.7	2.8	19.9	0.3
Shughuli za kifedha na bima	39.0	14.6	24.4	0.4
Shughuli za kitaalamu, kisayansi na kiufundi	69.8	37.9	31.9	0.5
Shughuli za utoaji huduma mbalimbali	11.3	1.5	9.8	0.2
Elimu	24.0	3.1	20.9	0.3
Afyya ya binadamu na shughuli za kijamii	34.3	16.4	17.9	0.3
Sanaa, burudani na shughuli za jamii	25.9	5.5	20.4	0.3
Shughuli nyingine za utoaji huduma	955.3	199.8	755.5	12.2
Jumla	14,404.8	8,216.4	6,188.4	100

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Mchango wa Sekta Isiyo Rasmi kwenye Pato la Mkoa wa Dar es Salaam

209. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa pato la sekta isiyo rasmi lilichangia asilimia 22.5 ya pato la mkoa mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 41.2 mwaka 1995. Kupungua kwa mchango kulitokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kurasimisha biashara zilizopo kwenye sekta isiyo rasmi. Wastani wa pato la mtu anayejihusisha na shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi kwa mkoa wa Dar es Salaam kwa mwaka ulikuwa shilingi milioni 11.4 mwaka 2019. **Jedwali Na. 10.7** na **Jedwali Na. 10.8.**

Jedwali 10.7: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi kwenye Pato la Mkoa

Kipengele	Thamani (Shilingi Triliioni)		
	1995	2019	
Kadirio la pato la mkoa wa Dar es Salaam kutokana na Sekta Rasmi na isiyo Rasmi	0.5	25.3	
Kadirio la kiwango cha pato la sasa kutokana na Sekta Isiyo Rasmi	0.2	3.9	
Kiwango halisi cha Sekta Isiyo Rasmi kutokana na utafiti wa mwaka 2019	-	6.2	
Tofauti	-	2.3	
Pato halisi la mkoa wa Dar es salaam	-	27.6	
Mchango wa Sekta isiyo Rasmi kwenye pato la Mkoa wa Dar es salaam	Kadirio la Sekta isiyo Rasmi Uhalisia wa Sekta Isiyo Rasmi	- 41.2	15.4 22.5

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Jedwali 10.8: Wastani wa Pato la Mtu kwa Mwaka (Shilingi Bilioni) katika Sekta Isiyo Rasmi

Shughuli za Kiuchumi	Jumla ya pato	Waajiriwa	Wastani wa pato kwa mtu
Kilimo, misitu na uvuvi	1,601,690.1	140,587	11.4
Uchimbaji madini	255,389.5	16,397	15.6
Uzalishaji viwandani	736,401.4	85,034	8.7
Shughuli za uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke, na vijoyozi	11,639.2	6,422	1.8
Usambazaji wa maji, majitaka na usimamizi wa taka	182,237.1	6,444	28.3
Ujenzi	364,058.7	63,716	5.7
Biashara ya jumla ma rejaraja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	8,203,786.8	568,067	14.4
Usafurishaji na uhifadhi	148,025.6	29,943	4.9
Huduma za malazi na chakula	1,719,279.0	173,971	9.9
Habari na mawasiliano	22,676.6	4,143	5.5
Shughuli za fedha na bima	38,978.7	5,884	6.6
Shughuli za kitaalamu, kisayansi na kiufundi	69,766.8	14,873	4.7
Shughuli za utoaji wa huduma mbalimbali	11,310.1	2,322	4.9
Elimu	23,995.6	7,415	3.2
Afya ya binadamu na shughuli za kijamii	34,318.4	3,812	9.0
Sanaa, burudani na starehe	25,863.9	8,487	3.0
Shughuli nyingine za utoaji huduma	955,308.5	129,565	7.4
Jumla	14,404,726.0	1,267,082	11.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Uhusiano Kati ya Sekta Isiyo Rasmi na Sekta Nyingine

210. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa sehemu kubwa ya bidhaa zinazozalishwa katika shughuli zisizo rasmi kwa Mkoa wa Dar es Salaam ziliuzwa kwa kaya au watu binafsi ambapo asilimia 98.6 zinauzwa bila kuongezwa thamani. **Jedwali Na. 10.9.**


Jedwali 10.9: Bidhaa na Huduma za Sekta Isiyo Rasmi Zilizouzwa kwa Mlaji wa Mwisho

Mlaji wa mwisho	Hali ya bidhaa / huduma		
	Bidhaa zilizouzwa bila kuchakatwa	Bidhaa zilizouzwa baada ya kuchakatwa	Huduma
Serikali au Shirika la Umma	0.1	0.0	0.0
Shirika kubwa la Umma	0.6	0.8	0.0
Shirika dogo Binafsi	0.4	0.5	0.9
Kaya/Mtu binafsi	98.6	98.0	98.7
Kusafirisha nje ya nchi	0.1	0.7	0.0
Matumizi binafsi	0.3	0.0	0.5
Jumla kwa asilimia	100.1	100.0	100.1
Jumla	1,263,857	157,853	325,204.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

211. Kaya au watu binafsi wameonesha kuwa na ushindani mkubwa wa soko la ndani katika shughuli za sekta isiyo rasmi kwa asilimia 95.0. Sekta ya umma na wafanyabiashara wakubwa wameonekana kuwa na ushindani mdogo wa chini ya asilimia moja. Vile vile, matokeo yanaonesha kuwa wamiliki 10,216 wa biashara katika sekta isiyo rasmi walishirikiana au walipokea huduma kutoka taasisi zinazotoa misaada ambapo asilimia 43.8 walipokea huduma kutoka taasisi za sekta binafsi.

Kielelezo 10.2: Washindani Wakubwa wa Soko la Ndani kwenye Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Changamoto Katika Sekta Isiyo Rasmi na Namna ya Kuzitatu

212. Changamoto katika uendeshaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi katika mkoa wa Dar es Salaam ni pamoja na uhaba au ukosefu wa mtaji wa kutosha (asilimia 82.6), kupata soko au wateja (asilimia 72.7), kupata jengo linalofaa (asilimia 35.5) na kupata leseni za biashara (14.4). **Kielelezo Na. 10.3** kinaonesha changamoto za uendeshaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi.


Kielelezo 10.3: Changamoto za Uendeshaji wa Shughuli za Sekta Isiyo Rasmi



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

213. Kwa upande mwingine, utafiti ulionesha kuwa asilimia 61.9 ya wamiliki wa biashara katika sekta isiyo rasmi walihitaji mikopo kama suluhisho la kutatua changamoto za sekta isiyo rasmi ikifuatiwa na upatikanaji wa taarifa za masoko (asilimia 46.4) na upatikanaji wa oda kubwa za biashara (asilimia 45.6). Aidha, mafunzo ya utawala na usimamizi wa fedha katika sekta isiyo rasmi yalionekana kuwa na uhitaji mdogo (asilimia 11.9) katika kutatua changamoto.

Kielelezo 10.4: Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Sekta Isiyo Rasmi (Asilimia)



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Hitimisho

214. Utafiti huu unaonesha kuwa kuna idadi kubwa ya watu wanaojihusisha na shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi. Kutohana na hilo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itazingatia matokeo ya utafiti huu katika kuitia na kutathmini sera, mipango na mikakati ya kimaendeleo kwa lengo la kuweka mazingira rafiki yatakayohamasisha urasimishaji wa shughuli za kiuchumi. Hii itaisaidia Serikali kupanga na kufikia malengo iliyojiwekea ikiwa ni pamoja na kufikia azma ya kupunguza umaskini wa kipato mionganini mwa watanzania kama ilivyobainishwa katika mipango ya maendeleo ya Taifa, Kikanda na Kimataifa.

Jedwali 10.10: Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Mkoa na Halmashauri ya Manispaa	Jumla ya Kaya	Kaya zenye Sekta Isiyo Rasmi	Asilimia ya Kaya zenye Sekta Isiyo Rasmi
Mkoa wa Dar es Salaam	1,322,994	767,904	58.0
Kinondoni	269,806	152,354	56.5
Ilala	371,472	226,091	60.9
Temeke	350,590	207,018	59.0
Ubungo	270,871	145,402	53.7
Kigamboni	60,255	37,039	61.5
Wamiliki wa Sekta Isiyo Rasmi	Jinsi Zote	Me	Ke
Kilimo, Misitu na Uvubi	9.1	9.9	8.6
Uzalishaji Viwandani	7.2	8.7	6.1
Ujenzi	4.2	9.5	0.3
Biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	47.6	41.8	51.8
Huduma za malazi na chakula	12.9	4.3	19.3
Idadi ya Wamiliki	1,023,520	436,286	587,234
Sababu za Kujisughulisha katika Sekta Isiyo Rasmi	Jinsi Zote	Me	Ke
Hawezu kupata kazi nyingine	55.2	55.4	55.1
Familia inahitaji kipato cha ziada	54.3	48.9	58.4
Biashara/shughuli hutoa fursa nzuri za kipato	16.2	18.8	14.2
Biashara/shughuli haihitaji mtaji mkubwa	20.2	18.3	21.7
Kutaka kujitegemea kutoka kwa nwajiri wake	14.6	17	12.8
Idadi ya Biashara	1,064,998	463,046	601,952
Shughuli za Sekta Isiyo Rasmi bila Maeneo ya Kudumu	Jinsi Zote	Me	Ke
Asilimia	76.6	75.2	77.6
Shughuli za Sekta Isiyo Rasmi Maeneo ya Kudumu	Jinsi Zote	Me	Ke
Asilimia	40.1	41.9	38.7
Uwekezaji wa Mitaji katika Sekta Isiyo Rasmi	Jinsi Zote	Me	Ke
Shilingi (bilioni)	901.5	576.6	324.9
Wastani wa Uwekezaji wa Mitaji kwa Kila Mmiliki katika Sekta Isiyo Rasmi	Jinsi Zote	Me	Ke
Shilingi	880,830	1,321,688	553,293
Watu Walioajiriwa katika Sekta Isiyo Rasmi	Jinsi Zote	Me	Ke
Jumla ya Ajira	1,267,082	578,239	688,843
Wamiliki	1,023,520	436,286	587,234
Waajiriwa	243,562	141,953	101,609
Mchango wa Ajira katika Sekta Isiyo Rasmi (Shughuli Kuu) Mkoa wa Dar es Salaam	Jinsi Zote	Me	Ke
2014	61.5	53.4	72.5
2019	55.2	43.6	69.3
Ajira kwa Kundu la Umri wa Wamiliki	Jinsi Zote	Me	Ke
15 – 35	41.9	41.4	42.5
36 – 59	53.3	52.8	53.6
60+	4.8	6.1	3.9
Uzalishaji wa Sekta Isiyo Rasmi (Shilingi Bilioni)	Jinsi Zote	Me	Ke
Mkoa wa Dar es Salaam	14,404.80	8,216.40	6,188.20
Kinondoni	2,372.60	1,289.00	1,083.60
Ilala	4,967.40	2,651.50	2,315.90
Temeke	4,239.60	2,642.20	1,597.40
Ubungo	2,096.60	1,346.10	750.40
Kigamboni	728.60	287.60	440.90
Pato la Mtu kwa Mwaka (Shilingi Bilioni) katika Sekta Isiyo Rasmi	Jumla ya Pato	Waajiriwa	Jumla ya Pato Kwa mtu
Jumla	14,404,725.9	1,267,082.0	11.4
Mchango wa Sekta Isiyo Rasmi kwa Pato Ghafi la Mkoa wa Dar es Salaam (Asilimia)			
1995		41.2	
2019		22.5	
Msaada Unaohitajika kwa Wamiliki wa Shughuli katika Sekta Isiyo Rasmi			
Upatikanaji wa Mikopo		61.9	
Upatikanaji wa Taarifa za Masoko		46.4	
Upatikanaji wa Mauzo Makubwa		45.6	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

SURA YA 11

KILIMO NA USHIRIKA

KILIMO

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

215. Mwaka 2019, uzalishaji wa mazao ya ulezi/mtama, ngano na jamii ya mikunde uliongezeka kwa asilimia 13.1, asilimia 10.5 na asilimia 3.6 mtawalia. Hata hivyo, uzalishaji wa mazao ya mchele, mihogo na mahindi ulipungua ikilinganishwa na mwaka 2018. Hii ilitokana na maeneo yanayozalisha mazao hayo kutopata vipindi vya mvua za kutosha pamoja na mashambulizi ya visumbuvi vikiwemo viwavijeshi vamizi, panya na kweleakwelea. **Jedwali Na.11.1** linaonesha mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula.

Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya chakula (Tani `000)

Zao	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Mahindi	5,908	6,149	6,681	6,273	5,652	-9.9
Mchele	1,937	2,229	1,594	2,220	2,063	-7.1
Ngano	72	76	50	57	63	10.5
Mtama/Ulezi	1,007	1,003	1,064	988	1,117	13.1
Muhogo	1,962	2,205	1,342	2,791	2,728	-2.3
Maharage/Mikunde	1,808	1,959	2,318	1,823	1,888	3.6
Ndizi	1,195	1,061	845	1,132	1,135	0.3
Viazi (Vitamu na mviringo)	1,645	1,491	2,008	1,608	1,644	2.2

Chanzo: Wizara ya Kilimo

216. Kwa mujibu wa tathmini ya uzalishaji wa mazao ya chakula iliyofanyika Desemba 2019, uzalishaji ulikuwa tani 16,293,637 ikilinganishwa na tani 16,891,974 mwaka 2018. Kati ya kiasi hicho, tani 8,896,830 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 7,396,807 mazao yasiyo ya nafaka. Aidha, mahitaji ya chakula yalikuwa tani 13,819,863 (mazao ya nafaka tani 8,730,677 na yasiyo ya nafaka tani 5,089,186). Mahitaji hayo yakilinganishwa na uzalishaji yalionesha kuwa nchi ilikuwa na ziada ya tani 2,473,774 za chakula na hivyo kuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula cha asilimia 118 ikilinganishwa na asilimia 124 mwaka 2018. Kupungua kwa kiwango cha utoshelevu kulitokana na kushuka kwa uzalishaji wa mahindi, mchele na muhogo mwaka 2019.

Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

217. Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka kwa asilimia 19.3 na kufikia tani 1,156,389 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 967,184 mwaka 2018. Hii ilitokana na uwepo wa hali nzuri ya hewa uliochangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya pamba, chai, kahawa, tumbaku na sukari pamoja na matumizi sahihi ya pembejeo katika uzalishaji wa mazao hayo hususan chai na pamba. Kwa upande mwengine, uzalishaji wa zao la korosho ulipungua kwa asilimia 28.3 hadi tani 225,053 mwaka 2019 kutoka tani 313,826 mwaka 2018. Upungufu huo ilitokana na mabadiliko ya hali ya hewa ambapo mvua ilinyesha mfululizo na kuharibu maua ya mikorosho na hivyo kupunguza uzalishaji wa korosho ghafi. Aidha, uzalishaji wa zao la mkonge ulipungua kwa asilimia 18.1 kutokana na kushuka kwa mahitaji ya mkonge katika soko la Mashariki ya Kati hususan Saudi Arabia. Vile vile, uzalishaji wa pareto ulipungua kwa asilimia 16.1 kutokana na hali ya hewa katika maeneo inakolimwa kutokuwa nzuri na kuwepo kwa magonjwa yanayotokana na fungusi. Uzalishaji wa mazao ya biashara ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11.2**.

Jedwali Na. 11.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)

Zao	2016	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Pamba	149,445	132,934	222,039	352,405	58.7
Kahawa	60,921	48,329	45,245	68,147	50.6
Chai	32,629	26,975	34,010	37,193	9.4
Pareto	2,011	2,150	2,400	2,014	-16.1
Tumbaku	60,691	58,639	50,522	79,087	56.5
Korosho	155,416	265,238	313,826	225,053	-28.3
Mkonge	42,314	36,533	40,635	33,271	-18.1
Sukari	293,075	330,843	303,752	359,219	18.3
Jumla	796,502	901,641	967,184	1,156,389	19.6

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uzalishaji wa Mazao ya Bustani

218. Mwaka 2019, uzalishaji wa mazao ya bustani yakiwemo matunda, mboga, maua na viungo ulifikia tani 6,556,102 kutoka tani 5,333,297 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 22.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo kwenye vitalu nyumba (Green house) katika maeneo mbalimbali.

Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11.3.**

Jedwali Na.11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)

Zao	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Matunda	5,243,343	3,703,124	4,576,948	23.6
Mboga	1,298,388	1,595,489	1,926,927	20.8
Maua	11,615	12,622	13,240	4.9
Viungo	22,062	22,062	38,987	76.7
Jumla	6,563,793	5,333,297	6,556,102	22.9

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta

219. Uzalishaji wa mazao ya mafuta ya alizeti, karanga, ufuta, michikichi na soya uliongezeka kwa asilimia 11.0 na kufikia tani 1,230,767 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 1,109,142 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya mbegu za mafuta hususan ufuta katika masoko ya nje na kupanda kwa bei ya ufuta kufuatia zao hilo kuanza kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania. Uzalishaji wa mazao hayo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 11.4.**

Jedwali Na. 11.4: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)

Zao	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Alizeti	352,902	543,261	561,297	3.3
Karanga	216,167	370,356	376,520	1.7
Ufuta	56,846	133,704	227,821	70.4
Mawese	42,277	40,500	42,176	4.1
Soya	6,135	21,321	22,953	7.7
Jumla	674,327	1,109,142	1,230,767	11.0

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Mwenendo wa bei na Masoko ya Mazao ya Kilimo

220. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuboresha mifumo ya masoko ya mazao ya kimkakati kwa kufanya tafiti za mahitaji ya masoko, kuimarisha vyama vya ushirika na kusimamia mikataba baina ya wanunuzi na wakulima. Kufuatia

jitihada hizo, bei za mazao ya kahawa, korosho na kakao katika soko la ndani ziliimarika ikilinganishwa na masoko ya nje. Katika kipindi hicho, bei ya kahawa ya arabika kwa gunia la kilo 50 katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani 109.57 ikilinganishwa na dola 107.04 katika soko la ndani. Bei ya kahawa ya robusta kwa gunia la kilo 50 katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani 67.57 ikilinganishwa na dola 79.04 katika soko la ndani. Vile vile, uuzaji wa kakao kwa mnada kupitia vyama vya ushirika ulichangia kuongezeka kwa bei kutoka wastani wa shilingi 3,000 kwa kilo mwaka 2018 hadi shilingi 5,011 kwa kilo mwaka 2019. Kwa upande mwingine, bei ya korosho ghafi daraja la kwanza ilikuwa shilingi 3,300 kwa kilo na shilingi 2,640 kwa kilo ya korosho ghafi daraja la pili.

Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo

221. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhamasisha matumizi ya zana bora za kilimo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao. Katika kipindi hicho, matrekta makubwa 933 na madogo 314 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na matrekta makubwa 1,476 na madogo 380 mwaka 2018. Upungufu huo ultokana na kukamilika kwa mradi wa kuunganisha matrekta ya URSUS ambao ulichangia uingizaji wa idadi kubwa ya matrekta kutoka Holland.

Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo

222. Serikali kupitia vyuo 14 vya kilimo ilidahili wanafunzi 2,856 kwenye mafunzo ya kilimo katika ngazi ya astashahada na stashahada mwaka 2019 ikilinganishwa na wanafunzi 2,389 mwaka 2018. Kati ya hao, wanafunzi 2,359 walifadhiliwa na Serikali na wanafunzi 497 walijilipia wenyewe. Mafunzo hayo yalitolewa katika vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala. Aidha, Serikali ilidahili wanafunzi 497 wanaojilipia wenyewe katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 338 mwaka 2018. Vile vile, Serikali ilifadhili mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 19 ngazi ya shahada ya uzamili na wanne ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu vya hapa nchini. Halikadhalika, wakufunzi wawili walijiunga na mafunzo ya shahada ya uzamili nje ya nchi na wakufunzi 15 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani - JICA na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa - USAID kupitia *Feed the Future India Triangular Training Programme*.

223. Mwaka 2019, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani - FAO ilijenga vitalu nyumba vitatu na kukarabati bweni moja katika kituo cha

mafunzo kwa wakulima Bihawana Dodoma ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Lutheran World Relief kupitia Mradi wa INVEST ilijenga vituo viwili vyatua ujasiriamali kwa wanafunzi katika chuo cha sukari Kidatu na chuo cha KATRIN kilichopo Ifakara Morogoro kwa lengo la kuwajengea ujuzi wa ujasiriamali.

Utafiti

224. Mwaka 2019, Serikali iliidhinisha na kusambaza mbegu mbalimbali za kilimo zilizogunduliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na taasisi binafsi za kilimo kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji. Katika kipindi hicho, aina 22 za mbegu bora ziligunduliwa na kuidhinishwa ikilinganishwa na mbegu bora aina 25 mwaka 2018. Kati ya hizo, mbegu za muhogo zilikuwa aina tisa (9), alizeti (2), mahindi (2), mpunga (2), ulezi (1) na viazi vitamu (6). Aidha, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa ilizalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 7,284,735 na kugundua aina tatu (3) za mbegu bora za kahawa ya arabika zinazostahimili ukame ambazo ni N39-3, N39-10 na TaCRI 3F.

Mfuko wa Pembejeo

225. Mwaka 2019, Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo ilitoa mikopo ya matrekta makubwa 27 ikilinganishwa na mikopo ya matrekta 26 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, mikopo 10 ya pembejeo mchanganyiko ikiwemo mbolea za viwandani, mbegu bora na madawa ya mifugo ilitolewa ikilinganishwa na mikopo 9 mwaka 2018. Aidha, katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, Mfuko ulitoa mikopo mitano (5) ya zana za umwagiliaji kama ilivyokuwa mwaka 2018.

Umwagiliaji

226. Mwaka 2019, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikamilisha ujenzi wa skimu nane (8) za umwagiliaji za Soko (Moshi), Kituani Mwenzae na Kwemgiriti (Lushoto), Katela - Ntaba (Busokelo), Ngongowele, Nanganga (Ruangwa), Mwalunili (Iguna) na Ngage (Simanjiro). Aidha, Tume ilinunua mitambo 11 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu. Vile vile, Tume kupitia mradi wa USAID - *Feed the Future* ilikamilisha ujenzi wa skimu ya Dakawa yenye ukubwa wa hekta 2,000.

227. Hadi Desemba 2019, idadi ya vyama vyatua ujasiriamali kwa wamwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume ilifikia 169 kutoka vyama 135 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Aidha, Tume ilikamilisha ujenzi wa mabwawa mawili ya Itagata (Itigi - Singida)

na Dongobesh (Mbulu) kwa lengo la kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kunufaika na kilimo cha umwagiliaji.

228. Mwaka 2019, Tume kupitia mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga ilitoa mafunzo kwa wakulima viongozi 135 katika skimu za Mkula na Njange (Kilombero), Rudewa, Chanzuru na Kilangali (Kilosa) na Kigugu (Mvomero). Mafunzo hayo yalihusu uendeshaji na usimamizi wa vyama vyta umwagiliaji pamoja na matunzo ya miundombinu.

MIFUGO

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake

229. Idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia ng'ombe milioni 32.2, mbuzi milioni 20, kondoo milioni 5.5, nguruwe milioni 2.0 na kuku wa asili milioni 38.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 30.5, mbuzi milioni 18.8, kondoo milioni 5.3, nguruwe milioni 1.9 na kuku wa asili milioni 38.2 mwaka 2018. Aidha, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 11.6 na kufikia lita milioni 2,678.4 kutoka lita milioni 2,400.1 mwaka 2018. Kati ya kiasi kilichozaishwa, lita milioni 803.5 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita milioni 1,874.9 zilitokana na ng'ombe wa asili. Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kulitokana na uboreshaji wa mbari za mifugo kupitia uhimilishaji. Kwa upande mwingine, usindikaji wa maziwa ulifikia lita milioni 63.6 kwenye viwanda 90 mwaka 2019 ikilinganishwa na lita milioni 56.2 kwenye viwanda 76 mwaka 2018.

230. Mwaka 2019, uzalishaji wa nyama ulifikia tani 681,501 ikilinganishwa na tani 679,992 mwaka 2018. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 506,798, nyama ya mbuzi na kondoo tani 110,563, nyama ya kuku tani 41,000 na nyama ya nguruwe tani 23,140 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 471,692, nyama ya mbuzi na kondoo tani 92,999, nyama ya kuku tani 78,110 na nyama ya nguruwe tani 37,191 mwaka 2018. Aidha, uzalishaji wa mayai ulifikia milioni 3,575.6 mwaka 2019 ikilinganishwa na mayai milioni 3,156.7 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika mashamba makubwa ya kuzalisha mayai.

Jedwali Na. 11.5: Uzalishaji wa Mazao Yanayotokana na Mifugo

Aina ya Zao	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Uzalishaji Maziwa (Lita `000)						
Ng'ombe wa Asili	1,381,451	1,381,451	1,423,288	1,460,900	1,608,099	1,874,923
Ng'ombe wa Kisasa	650,570	677,275	703,979	626,100	792,044	803,538
Jumla	2,032,021	2,058,726	2,127,267	2,087,000	2,400,134	2,678,461
Uzalishaji Nyama (Tani)						
Ng'ombe	309,086	319,112	323,775	394,604	471,692	506,798
Mbuzi /kondoo	120,199	124,745	129,292	81,064	92,999	110,563
Nguruwe	74,174	54,360	91,451	18,899	37,191	23,140
Kuku	95,292	99,540	104,292	63,597	78,110	41,000
Jumla	598,751	597,757	648,810	558,164	679,992	681,501
Uzalishaji Mayai (000)						
Mayai	3,899,569	4,153,800	4,353,182	2,758,000	3,156,692	3,575,621

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo

231. Mwaka 2019, tani 12.1 za mbegu bora za aina mbalimbali za malisho ya mifugo zilizalishwa kwenye mashamba ya Serikali ikilinganishwa na tani 10 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa hei katika mashamba ya Serikali ulifikia marobota 550,919 ikilinganishwa na marobota 482,247 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.2. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuboresha mashamba ya malisho kwa kuyapatia vitendea kazi ikiwemo matrekta. Aidha, Serikali ilikagua na kusajili maeneo 20 ya kutengeneza vyakula vya mifugo na maeneo 14 ya kuhifadhia vyakula vya mifugo kwa lengo la kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo. Kwa upande mwingine, sekta binafsi ilizalisha tani 600,120 za vyakula vya mifugo mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 776,443 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 22.7. Upungufu huo ulichangiwa na kuongezeka kwa bei za malighafi za kutengeneza chakula cha mifugo.

Biashara ya Mifugo na Mazao Yake

232. Mauzo ya mifugo hai ndani ya nchi yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 947.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,360 mwaka 2018. Kupungua kwa thamani ya mifugo kulitokana na mvua nyingi iliyosababisha wafugaji kushindwa kwenda minadani kuuza mifugo hususan katika minada ya awali. Mauzo hayo yalijumuisha ng'ombe 1,427,212, mbuzi 1,062,324, na kondoo 122,390 ikilinganishwa na ng'ombe 1,614,321, mbuzi 1,340,222, na kondoo 315,636 mwaka 2018. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilifikia ng'ombe 11,670, mbuzi na kondoo 44,790 wenyewe thamani ya shilingi bilioni 22.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na ng'ombe 1,910, mbuzi 2,751, na kondoo 197 wenyewe thamani ya shilingi bilioni 2.7 mwaka 2018. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa nje ya nchi lilitokana na kuimarika kwa bei katika masoko ya nje ya nchi.

233. Mwaka 2019, tani 692.36 za nyama zenyewe thamani ya dola za Marekani bilioni 1.30 ziliuzwa katika nchi za Falme za Kiarabu, Iraq, Oman, Comoro, Hongkong na Vietnam ikilinganishwa na tani 1,207.93 zilizouzwa mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 42.7. Upungufu huo ulichangiwa na kufungwa kwa machinjio ya *Tanzania Meat Company* yaliyopo Dodoma kutokana na kutokidhi viwango vya ubora wa kuchinja mifugo na kusafirisha nyama kwenda Falme za Kiarabu. Kati ya tani za nyama zilizouzwa nje ya nchi, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 142.18, mbuzi tani 36.07, kondoo tani 1.11 na punda tani 513. Aidha, tani 243.65 za nyama zenyewe thamani ya shilingi bilioni 4.07 ziliingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini, Ubelgiji na Uingereza mwaka 2019 ikilinganishwa tani 1,224.55 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 80.1. Upungufu huo ulitokana na kuongezwa kwa tozo kwenye uingizaji wa nyama na bidhaa za nyama zinazotoka nje ya nchi pamoja na kuimarika kwa viwanda vya ndani vya kusindika nyama zenyewe ubora. Kati ya nyama zilizoagizwa kutoka nje, tani 48.53 zilikuwa za nyama ya nguruwe na tani 195.12 nyama ya ng'ombe.

234. Mwaka 2019, ukusanyaji wa ngozi uliongezeka na kufikia vipande 10,435,355 ikilinganishwa na vipande 9,919,704 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vipande 3,010,224 vilikuwa vya ngozi ya ng'ombe na vipande 7,425,131 vya ngozi ya mbuzi na kondoo. Aidha, vipande vya ngozi 665,177 viliuzwa nje ya nchi ambapo vipande 614,743 vilikuwa vya ngozi ya ng'ombe na vipande 50,434 vya ngozi ya mbuzi na kondoo ikilinganishwa na vipande 1,837,180 vilivyouzwa nje ya nchi mwaka 2018. Vile vile, tani 2,871.2 za ngozi ghafi na tani 156 za ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati (wet blue) ziliuzwa nje ikilinganishwa

na tani 3,650 ya ngozi ghafi na tani 4,840 ya ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati mwaka 2018. Mauzo ya ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati nje ya nchi yalipungua kutokana na soko la Ulaya kuzuia bidhaa zilizosindikwa kwa kwa kutumia kemikali aina ya *chrome* kutokana na sababu za kimazingira.

Jedwali Na. 11.6: Ukusanyaji wa Vipande vya Ngozi

Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi na Kondoo	Jumla ya Ngozi za Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo
2009	1,223,668	6,983,998	8,207,666
2010	2,456,540	3,678,294	6,134,834
2011	2,378,235	4,978,000	7,356,235
2012	3,022,400	4,928,000	7,950,400
2013	2,567,340	6,325,525	8,892,865
2014	2,263,472	3,567,321	5,830,793
2015	2,543,914	5,983,210	8,527,124
2016	2,654,400	6,132,212	8,786,612
2017	2,790,561	6,643,998	9,434,559
2018	2,896,796	7,022,908	9,919,704
2019	3,010,224	7,425,131	10,435,355

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jedwali Na. 11.7: Uuzaji wa Vipande vya Ngozi Nje ya Nchi

Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi na Kondoo	Jumla ya Ngozi za Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo
2009	982,668	3,469,936	4,452,604
2010	739,315	2,088,582	2,827,897
2011	1,719,506	1,561,000	3,280,506
2012	2,000,000	3,600,000	5,600,000
2013	1,269,060	2,582,525	3,851,585
2014	1,263,472	2,716,436	3,979,908
2015	1,388,139	1,020,000	2,408,139
2016	1,575,139	1,124,000	2,699,139
2017	1,215,030	928,115	2,143,145
2018	828,079	1,009,101	1,837,180
2019	614,743	50,434	665,177

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jedwali Na. 11.8: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje ya Nchi

Mwaka	Ngozi ghafi		Ngozi zilizoongezwa thamani		Jumla ya thamani (Shilingi Milioni)	Ngozi zilizoongezwa thamani (Asilimia)
	Kiasi Kg (^000)	Thamani (Shilingi Milioni)	Kiasi Kg (^000)	Thamani (Shilingi Milioni)		
2009	1,666	1,433	5,026	6,797	8,230	82.6
2010	3,241	2,438	7,217	8,672	11,110	78.1
2011	8,141	6,831	7,904	17,005	23,836	71.3
2012	2,887	3,445	5,011	17,375	20,820	83.5
2013	2	3	7,061	22,686	22,689	99.9
2014	1,559	2,231	11,186	33,372	35,603	93.7
2015	372	1,185	6,594	20,878	22,063	94.6
2016	1,758	2,397	2,592	5,097	7,494	68.0
2017	4,835	6,592	6,482	9,452	16,044	58.9
2018	3,650	5,064	4,840	8,794	13,858	75.4
2019	2,871.2	4,971.4	156	230	5201.4	4.4

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania

Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo

235. Mwaka 2019, Serikali kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo ilidahili wanafunzi 3,634 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 2,536 mwaka 2018. Mafunzo hayo yalijumuisha fani za afya na uzalishaji mifugo, fundi sanifu wa maabara, utunzaji wa nyanda za malisho na udhibiti wa ndorobo. Aidha, mafunzo yalitolewa katika Kampasi za Morogoro, Tengeru (Arusha), Mpwapwa (Dodoma), Kikulula (Kagera), Madaba (Ruvuma), Mabuki (Mwanza), Temeke (Dar es Salaam) na Buhuri (Tanga). Vile vile, Serikali kupitia Wakala ilitoa mafunzo kwa wafugaji 156 kuhusu uzalishaji bora wa mifugo na malisho.

Utafiti wa Mifugo

236. Mwaka 2019, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ilifanya tafiti zilizohusisha: teknolojia bora za uzalishaji wa mifugo; teknolojia sahihi za mbegu na malisho; teknolojia za kudhibiti magugu vamizi kwenye malisho ya mifugo; na tathmini ya urasimishaji wa mbegu za malisho. Tafiti za uzalishaji wa mifugo ziliwezesha uzalishaji na usambazaji wa ng'ombe chotara wa nyama 93, ng'ombe chotara wa maziwa 48 na mbuzi chotara 134 kwa wadau wa mifugo. Aidha, kuku 642 na mayai 359 ya kuku chotara aina ya SASSO yalisambazwa kwa wafugaji katika Halmashauri ya Mpwapwa kwa lengo la kuongeza tija ya uzalishaji kuku. Vile vile, kilo 6,029 za mbegu bora za malisho na kilo 3,250 za vishina nya malisho zilisambazwa kwa wafugaji.

Huduma za Ugani katika Kilimo na Mifugo

237. Mwaka 2019, Serikali kupitia Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji katika Zao la Mpunga mkoani Morogoro ilianzisha mashamba darasa 644 ambapo wakulima 3,220 walipatiwa mafunzo kuhusu teknolojia ya kilimo shadidi. Mafunzo hayo yalitolewa kwenye skimu 40 za umwagiliaji katika halmashauri za Kilombero, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijini, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro. Aidha, kupitia mradi huo, wakulima 2,461 (Kilosa 1,201, Ulanga 700 na Mvomero 560) katika skimu 22 za umwagiliaji walipewa pembejeo za ruzuku. Kwa upande mwingine, Serikali ilifanya ufuatiliaji na tathmini kwenye vituo 267 nya rasilimali za kilimo nya kata ili kubaini hali halisi na mahitaji ya vituo ambapo vituo 166 vilikuwa vinafanya kazi.

238. Kwa upande wa mifugo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliendelea kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu ufugaji bora wa kisasa ili kuongeza na kuboresha uzalishaji wa mazao ya mifugo sambamba na kukidhi mahitaji ya malighafi ya viwanda. Mwaka 2019, Serikali ilitoa mafunzo kuhusu ufugaji bora, usindikaji wa maziwa na uzalishaji wa malisho kwa maafisa ugani na wafugaji 19,839. Aidha, wadau 1,275 wa mifugo katika halmashauri za Meatu, Mkuranga, Mvomero na Tunduru walipata mafunzo kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mifugo. Vile vile, wafugaji 600 kutoka wilaya za Mvomero, Mkuranga, Meatu, Chato, Rungwe, Rukwa, Mbeya, Katavi na Songwe pamoja na watendaji 116 wa vijiji kutoka wilaya ya Mkuranga walipata mafunzo kuhusu umuhimu wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo.

239. Mwaka 2019, Serikali ilianzisha mashamba darasa 20 ya malisho ya mifugo ambapo mashamba matano (5) yapo katika Halmashauri ya Monduli na 15 katika

Halmashauri za Mji wa Singida, Manispaa ya Singida, Iramba, Mkalama, Itigi na Manyoni. Aidha, wafugaji 260 walipata mafunzo kwa vitendo kuhusu kilimo cha malisho kupitia mashamba darasa hayo.

MAENDELEO YA USHIRIKA

240. Mwaka 2019, Serikali kupitia Tume ya Mendeleo ya Ushirika, iliendelea kudhibiti, kusimamia na kuhamasisha ushirika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Katika kipindi hicho, vyama vya ushirika 11,626 vilisajiliwa ikilinganishwa na vyama 11,331 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vyama 3,835 vilikuwa vya masoko ya mazao; 6,178 vya akiba na mikopo; 238 vya mifugo; na 1,378 vilikuwa vyama vya aina nyingine. Aidha, wanachama wa vyama vya ushirika waliongezeka kwa asilimia 47.1 na kufikia 5,880,736 mwaka 2019 kutoka wanachama 3,998,193 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na juhudzi za kuhabarisha wadau kuhusu mafanikio ya maendeleo ya ushirika kupitia vipindi na makala katika vyombo vya habari.

241. Mwaka 2019, Tume iliendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao na kuzalisha bidhaa. Katika kipindi hicho, viwanda vilivyomilikiwa na vyama vya ushirika viliongezeka na kufikia 379 kutoka viwanda 304 mwaka 2018. Aidha, vyama vya ushirika vilitoa ajira 90,090 zikiwemo ajira za kudumu, mkataba na za msimu mwaka 2019 ikilinganishwa na ajira 32,668 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 ilitolewa kwa wanachama wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 mwaka 2018. Thamani ya hisa na akiba za wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 654 mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 819 mwaka 2019.

UVUVI

242. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kusimamia rasilimali za uvuvi kupitia doria na operesheni maalum kwa lengo la kudhibiti ubora, usalama na viwango vya mazao ya uvuvi. Katika kipindi hicho, sekta ya uvuvi ilitoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 202,053. Aidha, wananchi zaidi ya milioni nne waliendelea kutegemea shughuli mbalimbali za sekta ya uvuvi zikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa samaki na mazao ya uvuvi na utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi.

Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

243. Mwaka 2019, Serikali ilifanya doria na operesheni mbalimbali ikiwemo operesheni maalum chini ya Kikosi Kazi cha *Multi-Agency Task Team* (MATT) kwa lengo la kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Operesheni na doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa nyavu haramu aina ya makila 20,719, timba 2,930, katuli 23, ndoano 11,012, kokoro 1,180, kamba za kokoro zenye urefu wa mita 198,695, nyavu za dududu 51, *ring net* 326, nyavu za dagaa 828 na vyandarua 115. Vile vile, vifaa nya uvuvi vilivyokamatwa vilikuwa mitungi ya gesi 236, mitumbwi 1,141, boti 450, injini za boti 275, kasia 10, viatu nya kuzamia jozi tisa (9), compressor mbili (2), tanki za mafuta 4, magari 13 na pikipiki 24.

244. Kwa upande mwengine, Serikali ilikamata samaki wachanga kilo 35,998, samaki kilo 4,530 walioingizwa nchini bila kufuata utaratibu, kaa wachanga kilo 1,094, pweza wasiofikia uzito unaokubalika kilo 18, kamba koche kilo nane (8), majongoo bahari kilo 26, kambamiti kilo 200, mabondo 89 na makome bahari kilo 60. Kufuatia operesheni na doria hizo, watuhumiwa 2,115 walikamatwa na kesi saba (7) ziliwasilishwa mahakamani ambapo jumla ya shilingi bilioni 3.41 zilikusanywa kama faini.

Uzalishaji wa Samaki, Vifaranga nya Samaki na Viumbe Wakuzwao kwenye Maji

245. Mwaka 2019, samaki wazazi 19,640 walipandikizwa katika vituo nya kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji nya Ruhila (samaki 2,100), Mwamapuli (samaki 5,900) na Kingolwira (samaki 11,640) ili kuzalisha samaki wazazi na vifaranga. Aidha, samaki wazazi 8,000 walipandikizwa katika mabwawa nane (8) ya kituo cha Mtama/Nyegedi mkoani Lindi. Vile vile, vifaranga 17,301,076 (samaki 6,221,076 na kambamiti 11,080,000) vilizalishwa katika vituo vitotoleshi nya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na vifaranga 15,119,757 vilivyozaalishwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Ongezeko hilo lilitokana na uimarishaji wa miundombinu ya kuzalishia vifaranga pamoja na matumizi ya teknolojia sahihi ya uzalishaji wa vifaranga

246. Mwaka 2019, vizimba nya uzalishaji samaki katika maziwa na malambo viliongezeka na kufikia 408 ikilinganishwa na vizimba 315 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vizimba katika Ziwa Victoria vilikuwa 346, Ziwa Tanganyika (9) na malambo (53). Aidha, mabwawa ya kufugia samaki yaliongezeka na kufikia 26,445 mwaka 2019 kutoka mabwawa 24,302 mwaka 2018. Vile vile, uzalishaji

wa samaki (sato na kambale) uliongezeka na kufikia tani 18,288 zenye thamani ya shilingi bilioni 144.7 ikilinganishwa na tani 14,800 zenye thamani ya shilingi bilioni 111.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na ongezeko la mabwawa na vizimba vilivyotumika kupandikiza samaki. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa mwani uliongezeka na kufikia tani 1,449 zenye thamani ya shilingi milioni 869.4 ikilinganishwa na tani 1,329 zenye thamani ya shilingi milioni 664.5 mwaka 2018. Uzalishaji wa kambamiti ulifikia tani 336.4 zenye thamani ya shilingi bilioni 6.7 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 371 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.3 mwaka 2018.

Jedwali Na. 11.9: Uzalishaji wa Samaki wa Maji Baridi (Sato na Kambale) kwenye Mabwawa, Mwani na Kambamiti

Mwaka	Uzalishaji Sato na Kambale (Tani)	Thamani ya Sato na Kambale (Shiling) (Milioni)	Uzalishaji wa Mwani (Tani)	Thamani ya Mwani (shilingi '000)	Uzalishaji wa kambamiti (Tani)	Thamani ya Kambamiti (shilingi Milioni)
2011	959	5,752	689	206,550	290	2,350
2012	972	5,832	651	260,760	350	3,250
2013	2990	17,937	401	160,440	377	3,540
2014	3000	21,000	179	89,650	320	4,000
2015	3118	21,826	223	133,680	391	5,175
2016	3840	26,880	1,177	627,641	407	6,975
2017	11,000	82,500	1,197	598,500	248	3,207
2018	14,800	111,000	1,329	664,500	371	5,275
2019	18,288	144,693	1,449	869,400	336	6,720

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mwenendo wa Uvunaji wa Rasilimali za Uvuvi

247. Mwaka 2019, tani 470,309.2 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.21 zilivunwa ikilinganishwa na tani 376,352.7 zenye thamani ya trilioni 1.78 mwaka 2018. Kati ya hizo, tani 365,104.02 zilivunwa kwenye maji baridi na tani 105,205.21 kwenye maji chumvi. Kuongezeka kwa uvunaji wa samaki kulitokana na kupungua kwa uvuvi haramu.

Jedwali Na. 11.10: Mwenendo wa Uvunaji wa Rasilimali za Uvuvu

Mwaka	Maji baridi			Maji chumvi			Jumla (Maji chumvi na Baridi)		
	Wavuvi	Vyombo	Uzito (tani)	Wavuvi	Vyombo	Uzito (tani)	Wavuvi	Vyombo	Uzito (tani)
2011	141,206	47,635	290,474	36,321	7,664	50,592	177,527	55,299	341,066
2012	147,020	49,721	322,313	36,321	7,664	50,079	182,741	56,985	365,023
2013	147,644	50,120	364,602	36,321	7,664	52,846	183,431	57,385	375,158
2014	147,479	49,627	314,062	36,321	7,664	51,912	183,800	57291	365,974
2015	147,479	49,627	309,922	36,321	7,664	52,723	183,800	57291	362,645
2016	149,018	49,688	308,629	54,511	9,650	53,823	203,529	59,338	362,452
2017	149,018	49,688	332,373	54,511	9,650	55,170	203,529	59,338	387,543
2018	149,018	49,688	323,120	53,035	9,242	53,231	202,053	58,930	376,351
2019	149,018	49,688	365,104.0	53,035	9,242	105,205.21	202,053	58,930	470,309.2

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvu

Udhhibit wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvu

248. Mwaka 2019, Serikali ilifanya kaguzi 3,724 na kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvu kwenye viwanda 18 vya uchakataji samaki, mialo 125 ya kupokelea samaki, masoko 31 ya samaki, maghala 52 ya kuhifadhi mazao ya uvuvu na vyombo 853 vya kusafirisha mazao ya uvuvu. Kufuatia kaguzi hizo, kilo 32,305,630.2 za samaki na samaki hai wa mapambo 182,533 walihakikiwa na kupewa hati ya afya ya kusafirishwa nje ya nchi. Aidha, vibali 5,943 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa ndani na samaki wenyewe uzito wa kilo 93,314,915 walihakikiwa na kuingizwa katika soko la ndani. Vile vile, Serikali kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvu ya Nyegezi ilifanya uchunguzi wa kimaabara wa vimelea na kemikali kwa sampuli 4,608 za mazao ya uvuvu ili kulinda ubora na usalama wa chakula.

Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvu

249. Serikali iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvu ambapo hadi Desemba 2019, jumla ya viwanda vikubwa 15 na vidogo 34 vya kuchakata mazao ya uvuvu, viwanda vinne (4) vya kutengeneza nyavu, vitatu (3) vya kutengeneza boti na maghala 56 ya kuhifadhi mazao ya uvuvu vilianzishwa. Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu iliweza kuvutia uwekezaji katika shughuli za hoteli ambapo hadi Desemba 2019

kulikuwa na hotel 12 za kitalii katika Hifadhi za bahari na maeneo tengefu Mafia na hotel sita (6) katika Hifadhi za bahari na maeneo tengefu Tanga.

Mwenendo wa Uuzaji na uingizaji wa Mazao ya Uvuvi nje ya Nchi

250. Mwaka 2019, tani 45,775 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 136,915 wenyе thamani ya shilingi bilioni 376.76 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 44,939.8 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 63,978 wenyе thamani ya shilingi bilioni 546.99 waliouzwa mwaka 2018. Mauzo hayo yaliliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 25.57 kama mrabaha. Aidha, jumla ya tani 541.5 za mabondo zenyе thamani ya shilingi bilioni 111.47 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2019 na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 3.9 kama mrabaha. Vile vile, tani 6.0 za samaki wenyе thamani ya shilingi milioni 116.59 ziliingizwa nchini na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi milioni 37.01 kama mrabaha ikilinganishwa na tani 22,752.4 za samaki wenyе thamani ya shilingi bilioni 44.90 zilizoingizwa mwaka 2018. Kupungua kwa kiasi cha samaki kilichoagizwa kutoka nje ya nchi kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki nchini.

UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 34

Msimu ¹	Miwa				Sukari		
	Wakulima		Jumla (000 Tani)	Bei ² (Sh./Tani)	Iliyozalishwa Tani	iliyotumika ³	
	Umma (000 Tani)	Binafsi (000 Tani)				Jumla Tani	Kilo kwa kila mtu ⁴
2001/02	1,134	389	1,523	14,700	164,498	142,398	10.10
2002/03	1,402	411	1,813	15,000	190,120	167,300	10.42
2003/04	1,672	670	2,342	16,800	223,839	290,711	10.90
2004/05	1,594	752	2,346	20,568	229,617	328,005	10.90
2005/06	1,545	956	2,501	22,383	263,317	343,292	12.00
2006/07	1,430	611	2,041	29,000	192,095	366,708	12.00
2007/08	1,967	799	2,766	32,767	265,434	382,518	13.00
2008/09	2,056	693	2,749	32,771	279,850	396,113	13.40
2009/10	1,972	598	2,570	42,046	263,461	398,070	13.68
2010/11	2,357	661	3,018	43,865	304,135	410,259	12.00
2011/12	2,036	680	2,716	48,833	262,879	439,307	12.00
2012/13	2,242	711	2,953	52,167	296,698	468,000	12.00
2013/14	2,198	602	2,800	50,500	294,300	434,782	12.00
2014/15	2,466	697	3,163	51,333	304,007	511,680	12.00
2015/16	2,270	569	2,839	59,707	293,075	525,784	12.00
2016/17	2,504	557	3,061	72,667	324,930	456,000	12.75
2017/18	2,550	626	3,175	72,667	303,752	515,004	13.50
2018/19	2,792	797	3,589	72,667	359,219	524,772	13.50
Badiliko (%)							
2017/18-2018/19	9.52	27.38	13.04		18.26	1.90	0.00
Ongezeko (%)							
2001/02-2018/19	146.2	104.9	135.7	394.3	118.4	268.5	33.7

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

- 1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni
- 2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose
- 3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar
- 4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 35

Msimu ¹	Pamba yenye mbegu					Pamba ilioondolewa mbegu					Mauzo nchini	
	Uzalishaji Kiasi (tani)			Bei ya wastani (Shs/Kilo)		Kiasi (tani)			Kiasi (tani)	Bei ya wastani (Shs/tani)		
	AR	BR	Jumla	AR	BR	AR	BR	Jumla	Jumla ²	AR	BR	
2001/02	148,180	-	148,180	165	..	49,668	-	49,668	
2002/03	187,908	781	188,689	180	50	62,983	262	63,245	
2003/04	139,756	213	139,969	280	100	46,843	72	46,915	
2004/05	341,589	-	341,589	250	-	114,496	-	114,496	
2005/06	376,591	-	376,591	220	-	126,228	-	126,228	
2006/07	130,585	-	130,585	350	-	43,770	-	43,770	
2007/08	200,662	-	200,662	450	-	70,773	-	70,773	37,488	
2008/09	368,697	-	368,697	480	-	123,582	-	123,582	66,554	
2009/10	267,644	-	267,644	480	-	54,851	-	54,851	
2010/11	163,518	-	163,518	900	-	54,809	-	54,809	
2011/12	225,938	-	225,938	1,000	-	75,731	-	75,731	
2012/13	351,156	-	351,156	660	-	117,702	-	117,702	
2013/14	245,815	-	245,815	700	-	82,394	-	82,394	
2014/15	202,312	-	202,312	750	-	67,812	-	67,812	
2015/16	149,765	-	149,765	800	-	50,199	-	50,199	525,784	12	..	
2016/17	132,934	-	132,934	1,000	-	42,203	-	42,203	
2017/18	222,790	-	222,790	1,100	-	80,575	-	80,575	39,244	3,667	..	
2018/19	348,901	-	348,901	1,200	-	129,408	-	129,408	51,942	3,123	..	
Badiliko (%) 2017/18-2018/19	56.61		56.61	9.09		60.61		60.61				
Ongezeko (%) 2001/02-2018/19	135.46		135.46	627.27		160.55		160.55				

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba

¹ Msimu ni kati ya Juni na Mei

² Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

Pamba ya Tanzania hainunuliwa wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

ENEO LILIOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 36

Msimu ¹	Eneo liliopandwa (hekta): mashamba			Majani Mabichi yaliyopatikana (tani)						Bei kwa mkulima Shs/Kilo	Mauzo ² Nchini (tani)		
				Kiumilikaji: mashamba			Kikanda: mashamba						
	Makubwa	Madogo	Jumla	Makubwa	Madogo	Jumla	Kaskazini	Kusini	Jumla				
2001/02	10,811	10,364	21,175	97,297	13,999	111,296	22,794	88,502	111,296	80	2,683		
2002/03	11,097	9,762	20,889	100,677	31,718	132,395	28,679	103,716	132,395	85	3,158		
2003/04	11,485	10,801	22,286	95,986	31,993	127,979	26,384	101,595	127,979	86	3,225		
2004/05	11,271	11,442	22,713	94,172	39,246	133,418	20,649	112,769	133,418	86	4,004		
2005/06	11,310	10,977	22,287	91,337	31,881	123,218	29,046	94,172	123,218	93	3,881		
2006/07	11,271	11,956	23,227	109,632	49,024	158,656	39,673	118,983	158,656	100	4,737		
2007/08	11,272	11,449	22,722	97,310	51,160	148,470	33,456	115,015	148,471	111	4,253		
2008/09	11,271	11,449	22,722	100,644	41,167	141,811	31,677	110,134	141,811	118	4,464		
2009/10	11,272	11,449	22,722	106,021	44,716	150,737	33,309	117,428	150,737	124	5,084		
2010/11	11,272	11,449	22,722	95,511	47,616	143,127	112,368	30,759	143,127	152	6,065		
2011/12	11,272	11,449	22,722	88,582	52,359	140,941	27,009	113,932	140,941	200	4,839		
2012/13	11,272	11,449	22,722	113,628	54,872	168,500	30,997	137,503	168,500	206	5,498		
2013/14	11,272	11,449	22,722	101,489	47,001	148,490	27,935	120,555	148,490	225	5,672		
2014/15	11,272	11,449	22,722	100,018	52,467	152,485	23,283	129,202	152,485	176	6,302		
2015/16	11,272	11,449	22,721	96,759	44,605	141,364	25,413	115,915	141,328	230	10,257		
2016/17	11,272	11,449	22,722	78,929	41,495	120,424	20,592	99,832	120,424	285	4,648		
2017/18	11,322	11,705	23,028	97,428	55,620	153,048	31,599	121,449	153,048	299	5,434		
2018/19	12,202	11,449	23,652	105,516	61,851	167,367	36,966	130,401	167,367	313	3,927		
Badiliko (%)													
2017/18-2018/19	7.8	-2.2	2.7	8.3	11.2	9.4	17.0	7.4	9.4	4.7	-27.7		
Ongezeko (%)													
2001/02-2018/19	12.9	10.5	11.7	8.4	341.8	50.4	62.2	47.3	50.4	291.3	46.4		

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 37

Msimu ¹	Iliyonunuliwa (Tani)			Bei (Sh./kilo)			Mauzo nchini ⁺	
	ARABICA		JUMLA	ARABICA		ROBUSTA	KIASI (Tani)	THAMANI (shs'000)
	Laini	Ngumu		Laini	Ngumu			
2001/02	38,000	3,500	12,000	53,500
2002/03	37,294	4,766	34,368	76,428
2003/04	20,716	1,850	16,138	38,704	1,800.0	1,200.0	600.0	38,704.0
2004/05	23,870	888	9,133	33,891	2,593.5	1,976.0	1,235.0	33,891.0
2005/06	24,116	1,362	8,856	34,334	1,200.0	420.0	270.0	33,300.0
2006/07	33,345	2,417	19,076	54,838	2,840.0	1,796.0	1,616.0	548.4
2007/08	26,330	1,588	15,606	43,524	2,995.0	1,875.0	1,734.0	43,523.0
2008/09	37,207	1,727	29,643	68,577	2,887.0	2,172.0	1,836.0	68,577.0
2009/10	22,217	915	11,467	34,599	3,988.0	2,475.0	1,563.0	34,599.0
2010/11	30,309	2,013	24,348	56,670	4,500.0	1,300.0	1,200.0	56,670.0
2011/12	20,775	941	11,590	33,306	8,144.4	5,436.4	3,276.9	33,306.0
2012/13	33,204	1,655	36,150	71,009	4,850.0	3,600.0	3,200.0	71,009.0
2013/14	28,212	1,115	18,875	48,202	4,314.0	3,272.9	3,074.6	48,202.0
2014/15	26,335	810	18,788	45,933	5,848.0	4,515.0	3,848.5	..
2015/16	21,517	460	17,526	39,503	7,249.6	5,943.4	4,092.9	39,503.0
2016/17	27,023	681	19,989	47,693	7,636.0	6,164.0	4,347.0	47,693.0
2017/18	36,551	633	11,897	43,193	2,980.0	2,980.0	2,980.0	43,193.3
2018/19	30,664	2,068	27,927	66,546	2,210.0	2,210.0	2,210.0	66,546.2
Badiliko (%)								
2017/18-2018/19	-16.11	226.94	134.74	54.07	-25.84	-25.84	-25.84	54.07
Ongezeko (%)								
2005/06-2018/19	27.2	51.8	215.3	93.8	84.2	426.2	718.5	99.8
								15,433.3

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

- + Kahawa iliyosafishwa
- 1 Msimu ni kati ya Julai na Juni
- 2 Ni ya muda
- .. Takwimu hazikupatikana

ENEO LILIOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

Jedwali Na. 38

Msimu ¹	Eneo (Hekta)			Katani iliyopatikana		Mauzo nchini ⁺	
	Uliokomaa	Usiokomaa	Jumla	Kiasi (tani)	Bei kwa Mkulima (shs/tani)	Kiasi (tani)	Thamani (Sh. milioni)
2001/02	34,645	11,473	46,118	23,641	337,732	4,947	1,671
2002/03	39,462	10,611	50,073	23,280	450,000	6,300	2,835
2003/04	29,493	12,204	41,697	26,758	540,000	6,370	4,027
2004/05	45,079	14,500	59,579	27,794	617,342	8,213	5,070
2005/06	26,384	13,264	39,648	30,934	810,000	10,767	8,613
2006/07	28,273	13,608	41,882	33,327	975,000	11,010	10,152
2007/08	28,577	15,622	44,199	34,057	1,000,000	16,997	15,800
2008/09	35,751	18,023	53,774	25,996	1,000,000	11,496	10,100
2009/10	30,556	11,849	42,405	24,092	1,200,000	12,761	10,375
2010/11	31,117	12,169	43,286	25,090	1,300,000	11,617	13,154
2011/12	32,601	14,302	46,902	36,600	1,500,000	11,511	14,390
2012/13	33,649	11,994	45,643	34,874	1,600,000	11,466	16,823
2013/14	35,266	11,044	46,310	37,805	1,724,864	9,160	16
2014/15	35,946	12,494	48,440	38,872	2,071,446	8,972	17,513
2015/16	34,723	13,231	47,954	41,795	2,700,000	9,075	20,342
2016/17	41,661	12,850	54,511	36,533	2,700,000	9,559	21,541
2017/18	40,635	14,389	55,024	43,280	3,000,000	12,111	30,803
2018/19	43,406	18,031	61,436	33,271	3,300,000	14,646	43,907
Badiliko (%)							
2017/18-2018/19	6.8	25.3	11.7	-23.1	10.0	20.9	42.5
Ongezeko (%)							
2001/02- 2018/19	25.3	57.2	33.2	40.7	877.1	196.1	2,527.6

Chanzo: Bodi ya Katani

+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

.. Takwimu hazikupatikana

TUMBAKU ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 39

Msimu ¹	Iliyonunuliwa (tani)				Bei (shs/kg)			Mauzo Nchini ⁺			
	Mvuke	Moshi	Hewa	Jumla	Mvuke	Moshi	Hewa	Kiasi (tani)		Thamani (shs.mil.)	
								Mvuke	Moshi	Mvuke	Moshi
2001/02	25,905.0	1,799.0	-	27,704.0	519.0	428.0	-	1,595.0	348.0	4,996.0	-
2002/03	23,074.0	4,798.0	-	27,872.0	563.0	547.0	-	2,325.0	45.0	5,940.0	-
2003/04	30,124.0	3,422.0	-	43,547.0	725.0	680.0	-	2,245.0	136.0	6,862.0	-
2004/05	41,394.0	5,983.0	73.9	47,450.9	918.1	781.9	729.2	3,144.3	252.2	6,881.0	427.0
2005/06	50,494.0	5,228.0	741.0	56,464.0	983.0	735.0	635.0	3,486.0	168.0	9,335.0	392.0
2006/07	49,576.0	1,038.0	170.0	50,784.0	1,264.0	881.0	960.0	3,685.0	-	14,302.0	-
2007/08	52,597.0	2,474.0	286.0	55,357.0	1,144.0	849.0	957.0	4,056.5	230.8	15,392.3	800.9
2008/09	56,663.0	3,641.0	437.0	60,741.0	2,741.5	1,658.9	1,698.5	5,544.0	-	26,167.1	-
2009/10	88,808.0	4,901.0	497.0	94,202.0	2,946.0	1,691.0	1,773.0	2,210.0	148.0	9,699.0	590.0
2010/11	116,886.0	3,685.0	-	120,572.0	1,960.0	1,540.0	-	1,877.0	-	11,815.0	-
2011/12	71,667.0	2,562.0	-	74,239.0	2,784.6	2,370.0	-	3,862.0	-	23,891.0	-
2012/13	84,131.0	2,212.0	-	86,343.0	3,840.0	2,720.0	-	63,967.0	505.0	512,764.0	2,297.0
2013/14	105,001.0	802.4	-	105,803.4	3,686.0	2,182.0	-	43,910.0	1,252.0	363,733.0	5,347.0
2014/15	87,231.0	50.0	-	87,281.0	3,822.0	2,331.0	-	3,081.0	-	12,280.0	-
2015/16	60,691.0	-	-	60,691.0	4,633.0	-	-	4,790.0	267.0	45,143.1	1,584.6
2016/17	85,699.8	160.9	-	85,860.7	3,450.0	3,381.0	-	50,696.4	459.8	500,602.3	1,631.2
2017/18	49,717.2	804.9	-	50,522.1	3,695.5	2,720.0	-	43,511.0	-	393,232.0	-
2018/19	69,576.4	1,247.8	-	70,824.2	3,271.1	3,286.4	-	34,065.0	-	300,496.7	-
Badiliko (%)											
2017/18 - 2018/19	39.94	55.03		40.18	-11.48	20.82		-21.71		-23.58	
Ongezeko (%)											
2001/02-2018/19	168.58	-30.64		155.65	530.28	667.85		2,035.7		5,914.7	

Chanzo: Bodi ya Tumbaku Tanzania

+ Mauzo ya Tumbaku Moshi ni pamoja na Tumbaku Hewa

1 Msimu ni katì ya April na Machi

- Takwimu hazikupatikana

MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

Jedwali Na. 40

Msimu ¹	Maua yaliyonunuliwa (tani)				Mauzo Nchini: Kiasi (tani)			Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000)		
	Kaskazini	Kusini	Jumla	Bei ² (Sh./kg)	Utomvu (Crude Extract)	Poda	Dawa (Dry Mack)	Utomvu (Crude Extract)	Poda	Dawa (Dry Mack)
2001/02	36	1,699.0	1,735.0	420.0	-	-	-	-	-	-
2002/03*	111	979.0	1,090.0	380.0	2.0	90.0	-	106,920.0	99,891.0	-
2003/04	85	751.0	842.0	360.0	-	-	-	-	-	-
2004/05	90	910.0	1,000.0	360.0	-	-	-	-	-	-
2005/06	-	2,800.0	2,800.0	360.0	-	-	-	-	-	-
2006/07	-	1,600.0	1,600.0	700.0	-	-	-	-	-	-
2007/08	-	1,470.0	1,470.0	1,050.0	-	-	-	-	-	-
2008/09	-	1,600.0	1,600.0	1,500.0	36.4	105.0	624.0	-	-	-
2009/10	-	1,780.0	1,780.0	1,500.0	57.0	69.0	1,035.0	37,361.0	1,473.0	248.0
2010/11	-	1,786.8	1,786.8	1,500.0	57.2	69.3	69.3	37,503.7	1,478.6	246.9
2011/12	0	5,700.0	5,700.0	1,700.0	82.0	-	750.0	-	204.0	360,919.0
2012/13	0	6,100.0	6,100.0	2,400.0	84.0	-	2,000.0	-	-	462,000.0
2013/14	34	2,691.8	2,726.2	2,000.0	90.0	60.0	830.0	6,900,000.0	160,500.0	233,000.0
2014/15	31	2,255.0	2,286.0	2,500.0	76.0	30.0	430.0	133.6	116,048.0	235,612.7
2015/16	25	1,987.0	2,012.4	2,100.0	59.9	6.0	480.0	9,450,000.0	30,240.0	282,240.0
2016/17	39	2,111.8	2,151.0	2,050.0	53.2	162.0	727.0	6,782,016.0	651,810.0	436,232.0
2017/18	43	2,355.9	2,400.0	2,500.0	16.0	204.0	700.0	13,932,947.0	869,418.1	390,864.0
2018/19								144,487.0	844,213.9	409,299.4
Badiliko (%)										
2017/18-2018/19	-100.0	-100.0	-100.0	-100.0	-100.0	-100.0	-100.0	-99.0	-2.9	4.7
Ongezeko (%)										
2001/02-2018/19	-100.00	-100.00	-100.00	-100.00	-100.00	-100.00	-100.00	-99.00	-2.9	4.7

Chanzo: Bodii ya Pareto Tanzania

- 1 Msimu ni kati ya Julai na Juni
- 2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano
- Takwimu hazikupatikana
- * Takwimu hizi hadi December 30 2002, Msimu bado unaendelea

KOROSHO ZILIZONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 41

Msimu ¹	Zilizonunuliwa (Tani)			Bei (shs/kilo)		Mauzo Nchini	
	Gredi ya Juu	Gredi ya Chini	Jumla	Gredi ya Juu	Gredi ya Chini	Kiasi (Kg)	Thamani (sh.'000)
2001/02	64,886	14,394	79,280	300	180	2,928	878
2002/03	79,300	15,700	95,000	360	290	5,630	2,122
2003/04	65,000	15,000	80,000	462	370	6,061	2,521
2004/05	59,425	11,575	71,000	750	600	7,013	4,734
2005/06	61,976	15,470	77,446	600	480	10,738	6,354
2006/07	82,154	8,587	90,741	600	480	22,299	13,001
2007/08	89,639	8,633	98,273	610	488	98,273	59,336
2008/09	48,633	-	48,633	700	560	48,633	34,043
2009/10	118,825	355	119,180	1,700	1,200	119,180	202,429
2010/11	65,892	-	65,892	1,865	-	65,892	122,889
2011/12	121,946	-	121,946	1,572	-	84,056	123,856
2012/13	124,723	201	124,924	1,563	850	124,924	195,051
2013/14	174,695	-	174,695	1,440	-	174,695	317,944
2014/15	197,638	295,000	197,933	1,600	1,100	197,933	316,220
2015/16	228,237	3,627	231,864	3,100	2,443	231,864	781,140
2016/17	263,457	1,781	265,238	-	-	265,238	871,463
2017/18	299,265	14,562	313,826	4,128	1,700	313,826	1,191,613
2018/19	207,021	18,095	225,116	3,300	2,640	225,106	730,913
Badiliko (%)							
2017/18-2018/19	-30.8	24.3	-28.3	-20.1	55.3	-28.3	-38.7
Ongezeko (%)							
2001/02-2018/19	219.1	25.7	184.0	1,000.0	1,366.7	7,588.0	83,147.4

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Korosho

- 1 Msimu ni kati ya Oktoba mpaka Septemba
- Takwimu hazikupatikana

MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA

Jedwali Na. 42

(Tani)

Mazao	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	Badiliko % 2017/18 - 2018/19
Katani	36,600	34,874	37,805	38,872	41,795	36,533	43,280	33,271	-23.1
Kahawa	33,306	71,009	48,202	45,933	39,503	47,693	43,193	66,546	54.1
Pamba ¹	225,938	351,156	245,815	202,312	149,765	132,934	222,790	348,901	56.6
Tumbaku	74,239	86,343	105,803	87,281	60,691	85,861	50,522	70,824	40.2
Pareto	5,700	6,100	2,726	2,286	2,011	2,151	2,400		-100.0
Chai ²	140,941	168,500	148,490	152,485	141,328	120,424	153,048	167,367	9.4
Korosho	121,946	124,924	174,695	197,933	231,864	265,238	313,826	225,116	-28.3
Miwa	2,716	2,953	2,800	3,163	2,839	556,522	625,743	797,016	27.4

Chanzo: : Bodi zinazohusika

- 1 Yenye mbegu
- 2 Majani mabichi

UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI 2001-2019

Jedwali Na. 43

Mwaka	Idadi ya Wavuvi	Idadi ya Vyombo			Uzalishaji na Mapato					
		Maji baridi	Maji Chumvi	Jumla ya Vyombo	Maji baridi		Maji Chumvi		Jumla	
					Uzito (tani)	Thamani (Sh..)	Uzito (tani)	Thamani (Sh.)	Uzito (tani)	Thamani (Sh.)
2001	120,266	25,014	4,927	29,941	283,354	47,108,668	52,935	34,113,717	336,289	81,222,385
2002	124,570	31,849	4,927	36,776	273,856	54,771,300	49,675	33,372,136	323,531	88,143,436
2003	124,570	31,225	4,927	36,152	301,855	141,073,500	49,270	34,489,000	351,125	175,562,500
2004	122,514	32,248	4,927	37,175	312,040	147,743,000	50,470	40,376,000	362,510	188,119,000
2005	133,197	32,248	7,190	39,438	320,566	256,452,800	54,969	82,452,930	375,535	338,905,730
2006	156,544	44,362	7,190	51,552	292,519	248,640,904	48,591	37,077,637	341,109	285,718,540
2007	163,037	44,362	7,489	51,851	284,348	252,525,198	43,499	39,210,207	327,847	291,735,405
2008	170,038	44,838	7,489	52,327	281,691	194,725,416	43,130	40,563,641	324,821	235,289,057
2009	172,090	45,234	7,664	52,898	288,059	351,394,073	47,616	56,633,436	335,675	408,027,509
2010	163,601	42,337	7,664	50,001	294,474	684,844,020	52,683	89,639,934	347,157	774,483,954
2011	177,527	47,635	7,664	55,299	290,474	1,031,883,681	50,592	166,954,953	341,066	1,198,838,634
2012	182,741	49,321	7,664	56,985	314,944	1,129,349,925	50,079	177,781,799	365,023	1,307,131,724
2013	183,431	49,721	7,664	57,385	315,008	1,248,903,393	52,846	195,529,127	367,854	1,444,432,520
2014	183,800	49,627	7,664	57,291	314,062	1,287,248,813	51,912	207,649,600	365,974	1,494,898,413
2015	183,800	49,627	7,664	57,291	309,922	1,270,856,680	52,723	210,892,897	362,645	1,481,749,577
2016	203,529	49,688	9,650	59,338	308,772	1,274,485,404	53,823	211,891,899	362,595	1,486,377,303
2017	203,529	49,688	9,650	59,338	332,373	1,495,678,680	55,170	248,262,840	387,543	1,743,941,520
2018	202,053	49,688	9,242	58,930	323,120	1,518,667,619	53,231	250,190,118	376,351	1,768,857,737
2019	202,053	49,688	9,242	58,930	365,104	1,715,988,903	105,205	494,464,498	470,309	2,210,453,400

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

MAUZO YA MAZAO YA UVUVI NCHI ZA NJE KWA MWAKA 2019

Jedwali Na. 44

ZAO	UZITO (TANI)	SAMAKI HAI WA MAPAMBO	THAMANI FOB (USD)	FOB (TSHS)	USHURU (TSHS)
Aquarium Fish/L. Nyasa		50,399	127,109	293,183,086	65,454,141
Aquarium Fish/L. Tang		86,516	352,235	1,576,903,596	160,674,072
Dried chips	15.6		3,320	7,696,248	9,852,236
Dried Daga/L. Vict	9511.7		2,708,175	8,931,916,768	3,682,819,769
Dried Daga/L.Tang	91.9		754,664	1,740,670,870	251,667,678
Dried Daga/Marine	223.5		632,959	1,459,952,115	157,508,367
Dried Daga/L. Nyasa	2.1		6,141	14,124,300	1,240,000
Dried fins	0.0		24	55,200	30,000
Dried Fish (Mgebuka)/L.Tang.	32.3		116,249	269,483,343	63,154,821
Dried Fish Chests	301.6		19,955	45,902,666	36,137,060
Dried fish frame	440.6		63,489	147,176,825	26,493,664
Dried Fish Heads	2992.8		261,347	601,104,181	204,738,832
Dried Fish Meal/L. Manyara	45.0		10,536	24,422,882	2,057,400
Dried Fish Meal/L.Vict	1900.3		69,263	160,317,772	105,234,804
Dried Fish/L. Manyara	5.0		15,000	34,772,203	2,277,000
Dried Fish/L.Rukwa	134.4		464,038	1,075,708,065	158,273,758
Dried Furu / L. Manyara	10.6		31,500	72,450,000	4,842,400
Dried Furu/L.Vict	787.1		469,773	1,146,831,199	292,292,584
Dried Maws	541.5		56,962,299	129,089,603,145	3,925,303,441
Dried Offcuts	153.6		19,047	43,826,437	35,041,800
Dried Sangara/Kayabo	969.3		376,883	881,925,133	761,898,400
Dried shark	0.4		504	1,159,200	1,005,100
Dried Skin	0.0		920	2,116,736	950
Dried Uduvi/L.Vict	245.6		8,795	93,348,726	16,374,441
Farmed Prawns	43.2		330,046	772,323,964	4,775,649
Fish Steaks	0.0		16,380	38,330,913	8,100
Fresh Fillets	7274.2		34,434,016	77,144,723,550	3,860,573,820
Fresh Fish Chest	97.0		17,609	40,508,920	11,157,750
Fresh Fish Frames	79.0		15,400	35,419,072	3,634,151
Fresh Fish heads	84.0		16,561	38,919,956	5,438,243
Fresh Fish/L.Tang.	39.7		90,264	211,221,942	36,592,788
Fresh H&G	724.5		2,564,426	5,896,995,616	585,882,726
Fresh Maws	1.7		15,160	34,876,254	7,608,962
Frozen Fillets	10123.1		56,210,892	127,407,963,164	5,426,578,319
Frozen Fish Chest	1089.9		543,790	1,272,497,506	159,200,602
Frozen Fish Heads	4082.7		534,028	1,249,653,798	235,709,347
Frozen Fish Off cuts	105.3		46,220	108,157,217	24,246,858
Frozen H&G	723.7		2,442,941	7,621,557,431	610,004,261
Frozen Lobster	3.2		35,721	270,944,453	10,442,958
Frozen Maws	294.9		20,994,376	47,093,741,750	1,432,609,981
Frozen Octopus	1048.6		14,164,387	30,830,332,009	1,922,421,200
Frozen Offcuts	613.0		520,404	1,217,773,183	154,640,456
Frozen Prawns	88.0		376,471	4,442,971,292	62,027,393
Frozen Squids	12.7		8,549,283	17,689,530,287	21,667,658
Live Crabs	275.4		11,677,431	27,287,108,957	678,586,446
Live-Lobsters	48.7		914,724	2,796,523,292	264,755,080
Lobsters-Whole Frozen	0.2		632	1,478,515	579,703
Others	0.3		229	536,902	701,775
Prawns H/ON	0.5		8,100	18,630,000	414,178
Prawns Head-on 61 and above	1.9		955	2,183,390	4,196,042
Salted Fillets	0.0		50	114,678	8,000
Sea Shells	514.9		314,043	870,486,267	78,454,310
Smoked Nile Perch	0.5		6,256	14,391,421	311,400
JUMLA	45,776	136,915	218,315,020	502,124,546,395	25,567,600,873

MUHTASARI WA MAUZO YA MAZAO YA UVUVI NCHI ZA NJE - 2002-2019

Jedwali 44A

Mwaka	Uzito Kg	Samaki Hai wa Mapambo Idadi	Thamani		Ushuru Tsh
			Tsh	US \$	
2002	32,662,878	28,301	99,294,249,903	105,779,931	5,957,654,995
2003	42,352,738	24,500	132,862,401,374	129,605,815	7,789,955,963
2004	46,011,033	15,784	121,922,686,607	112,761,195	7,190,356,743
2005	57,289,084	21,025	162,619,492,949	141,597,362	9,142,768,084
2006	44,495,623	21,741	170,184,661,003	138,120,145	6,236,615,179
2007	57,795,514	25,502	213,211,258,838	173,272,670	7,589,576,914
2008	51,426,207	33,066	205,054,092,453	174,409,214	6,629,846,700
2009	41,148,261	53,188	207,447,119,888	161,053,646	6,410,191,232
2010	39,771,834	40,552	263,131,442,028	187,427,054	5,876,103,557
2011	37,996,433	61,215	233,714,590,011	152,973,357	6,153,278,023
2012	41,394,268	45,550	254,901,017,111	163,299,366	6,819,926,007
2013	38,573,606	44,260	234,884,628,956	147,659,779	6,117,769,194
2014	43,354,399	42,100	1,406,120,001,304	832,085,311	7,490,632,355
2015	41,059,452	87,630	547,228,222,096	259,286,762	13,097,411,199
2016	39,691,462	65,841	526,985,019,569	257,257,100	14,302,761,907
2017	36,063,229	101,110	406,568,122,271	182,450,278	10,446,850,539
2018	44,939,793	63,978	546,993,779,393	239,680,015	13,520,367,822
2019	45,775,167	136,915	376,763,802,643	158,657,946	25,567,600,873
JUMLA	998,399,195	992,835	6,410,310,072,541	4,154,608,101	184,658,865,708

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvu - Idara ya Uvuvu

MWELEKEO WA MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI - 2002-2019

Jedwali 44B

Mwaka	Uzito Kg	Thamani		Ushuru T.sh
		T.sh	US \$	
2002	29,479,323	83,005,557,292	88,231,655	4,980,333,438
2003	37,286,859	114,779,736,804	112,049,949	6,707,948,378
2004	30,312,898	82,356,866,789	76,261,406	5,171,324,343
2005	53,675,474	148,785,948,009	129,184,493	8,419,301,970
2006	39,472,978	156,160,190,327	126,829,666	5,491,786,879
2007	50,078,576	195,242,463,550	158,442,059	6,660,034,977
2008	38,721,422	180,366,779,818	153,740,723	5,412,912,979
2009	28,721,577	168,368,910,380	130,644,300	4,628,409,655
2010	27,229,471	194,012,069,314	139,666,995	4,509,670,994
2011	25,426,157	197,899,741,508	127,601,694	4,299,987,312
2012	28,951,095	220,149,518,646	141,189,162	4,967,311,025
2013	33,732,843	197,578,220,799	124,551,585	5,085,642,906
2014	24,473,492	1,131,575,531,076	665,856,773	4,569,314,170
2015	23,000,579	528,534,413,019	250,279,107	11,251,591,352
2016	26,044,656	345,417,803,263	177,338,054	6,964,514,349
2017	26,679,947	376,572,501,425	168,554,019	7,057,407,121
2018	32,166,953	409,654,290,065	179,522,959	9,689,153,198
2019	32,608,425	329,542,681,528	142,057,863	17,622,314,162
JUMLA	761,448,896	5,304,609,892,029	3,448,903,902	138,384,898,638

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvu - Idara ya Uvuvu

SURA YA 12

MALIASILI NA UTALII

Misitu na Nyuki

251. Mwaka 2019, tani za asali zilizovunwa ziliongezeka na kufikia tani 30,622 ikilinganishwa na tani 30,340 mwaka 2018. Kati ya hizo, tani 607.6 zenye thamani ya shilingi milioni 4,860.8 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 1,095.9 zenye thamani ya shilingi milioni 9,342.5 mwaka 2018. Kupungua kwa thamani ya mauzo ya asali kulichangiwa na kushuka kwa bei ya asali katika soko la dunia. Aidha, tani 1,897 za nta zilizalishwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 1,440 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 31.7. Kati ya kiasi kilichozaishwa, tani 179.3 zenye thamani ya shilingi milioni 1,437.9 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 143 zenye thamani ya shilingi milioni 1,287.1 mwaka 2018. Kuongezeka kwa kiasi cha nta kilichouzwa nje ya nchi kulitokana na utulivu wa bei ya nta katika soko la dunia. **Jedwali Na. 12.1.**

Jedwali Na 12.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki (Asali na Nta) Nje ya Nchi

Mwaka	Asali		Nta	
	Uzito (tani)	Thamani (Shs)	Uzito (tani)	Thamani (Shs)
2012	103.8	262,043,582	277.0	2,582,805,057
2013	83.0	287,368,000	384.0	4,659,954,408
2014	108.2	539,927,831	271.0	3,849,466,035
2015	152.6	983,848,159	220.2	3,238,346,723
2016	259.9	1,222,045,655	251.9	4,549,643,832
2017	240.8	1,292,017,450	203.9	6,879,170,450
2018	1,095.9	9,342,538,000	143.0	1,287,099,000
2019	607.6	4,860,834,400	179.3	1,437,865,600

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

252. Mwaka 2019, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania iliotesha miche ya miti milioni 21.8 ikilinganishwa na miche milioni 20.4 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Miche iliyoateshwa ilipandwa katika maeneo mapya yeye hekta 1,893, maeneo yaliyovunwa hekta 615 na maeneo ambayo miti haikuota hekta 251. Katika kipindi hicho, Wakala uliongeza maeneo mapya yeye hekta 6,060 kwa ajili ya upandaji miti. Aidha, hekta 18,101 za

mashamba ya miti zilisafishwa mwaka 2019 ikilinganishwa na hekta 32,499 mwaka 2018. Vile vile, Wakala ulipogoa na kupunguza miti katika mashamba yenye hekta 6,244 na hekta 1,293 mtawalia. Kwa upande mwingine, Wakala ulikusanya shilingi bilioni 129.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 109.1 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Makusanyo hayo yalitokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo ushuru wa huduma za uuzaaji wa mazao ya misitu na nyuki ndani na nje ya nchi, mrabaha wa mazao ya misitu na usajili wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu. Kuongezeka kwa makusanyo kulitokana na kuendelea kuimarika kwa doria katika maeneo ya uvunaji, usafirishaji na masoko ya nta, asali na mazao ya misitu.

Wanyamapori

253. Mwaka 2019, sekta ndogo ya wanyamapori ilikusanya jumla ya shilingi milioni 460,446.9 zilizotokana na ujio wa watalii katika Hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii ikilinganishwa na shilingi milioni 342,746.0 iliyokusanya mwaka 2018. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 292,539.5 zilikusanya na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na shilingi milioni 147,043.4 zilikusanya na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ilipokea wageni wawindaji na wasindikizaji 1,002 ambao waliingizia mapato ya shilingi milioni 20,864.0 kutokana na uwindaji wa kitalii katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapor. **Jedwali Na. 12.2** linaonesha mchanganuo wa mapato katika sekta ndogo ya wanyamapor.

Jedwali Na. 12.2: Mchanganuo wa Mapato yatokanayo na Sekta Ndogo ya Wanyamapor

Mwaka	Hifadhi za Taifa	Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro	Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii (TAWA)	Jumla
2015	149,957,485,000	60,687,703,000	28,802,391,200	239,447,579,200
2016	175,089,696,000	70,863,972,000	29,136,885,800	275,090,553,800
2017	207,587,218,000	103,090,458,000	19,202,957,607	329,880,633,607
2018	214,486,751,736	108,149,417,000	20,109,785,000	342,745,953,736
2019	292,539,502,030	147,043,375,161	20,864,030,536	460,446,907,727

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

254. Katika kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, doria 529,679 zilifanyika mwaka 2019 ikilinganishwa na doria 356,029 mwaka 2018. Kati ya hizo, doria 283,833 zilifanyika katika hifadhi za Taifa; 38,280 Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; na 207,566 katika mapori ya akiba na mapori tengefu. Aidha, doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa nyara mbalimbali za wanyamapori ikiwemo: meno ya tembo yenyeye uzito wa kilogramu 1,161.75, bunduki 461 na risasi 2,240 za aina mbalimbali. Kutokana na juhudhi hizo, idadi ya mizoga ya tembo katika mapori ya akiba, tengefu, ardhhioevu na maeneo ya hifadhi ya wanyamapori ilipungua kutoka 14 mwaka 2018 hadi mizoga mitatu mwaka 2019.

255. Mwaka 2019, Serikali ilianza kutumia mfumo wa Jeshi Usu kwa kada za wanyamapori na misitu kwa taasisi za Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Wakala wa Huduma za Misitu na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori. Mfumo huo unalenga kulinda rasilimali za wanyamapori na misitu dhidi ya ujangili na uvunaji usio endelevu. Hadi Desemba 2019 watumishi 4,556 kutoka katika taasisi hizo walipatiwa mafunzo ya utayari ya Jeshi Usu.

Utalii

256. Mwaka 2019, Serikali iliendelea na jitihada za kutangaza utalii ndani na nje ya nchi, kuboresha huduma za kitalii hususan hoteli na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika huduma ya utalii. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii waliotembelea vivutio mbalimbali nchini yaliongezekwa na kufikia watalii 1,527,230 ikilinganishwa na watalii 1,505,702 mwaka 2018. Aidha, mapato yaliyotokana na utalii yaliongezekwa kwa asilimia 7.1 na kufikia dola za Marekani milioni 2,604.5 mwaka 2019 kutoka dola za Marekani milioni 2,432.8 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wastani wa muda wa watalii kukaa nchini kutoka siku 10 mwaka 2018 hadi siku 13 mwaka 2019 na kuongezeka kwa wastani wa matumizi kwa mtalii kwa siku. Kwa upande mwingine, watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa walikuwa 1,257,952 mwaka 2019 ikilinganishwa na watalii 1,168,546 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Watalii waliotembelea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro walifikia 724,538 mwaka 2019 ikilinganishwa na watalii 679,454 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Kati ya hao, watalii kutoka nje ya nchi walikuwa 445,283 na watanzania 279,255.

Jedwali Na.12.2: Watalii walitembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

Mwezi	2017		2018		2019	
	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Nje ya nchi	Ndani ya nchi
Januari	27,265	22,474	30,000	18,692	32,913	21,348
Februari	32,687	24,180	38,598	19449	41,753	22,215
Machi	20,039	14,503	23,936	15,946	19,506	15,399
Aprili	14,318	14,973	12,497	10,384	14,539	14,519
Mei	15,391	14,092	16,748	12,065	17,150	14,245
Juni	36,044	25,250	33,608	20,954	37,240	24,368
Julai	50,527	22,048	55,513	40,559	69,211	33,100
Agosti	48,756	21,863	59,635	36,394	65,903	34,257
Septemba	31,325	16,178	41,706	25,148	42,693	26,949
Oktoba	34,551	17,066	39,537	23,467	43,396	25,921
Novemba	22,740	15,597	23,507	18,102	24,378	19,167
Desemba	57,387	41,204	35,289	27,720	36,601	27,767
Jumla	391,030	249,428	410,574	268,880	445,283	279,255

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

257. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kutangaza utalii kwa kuboresha *channel* maalum iitwayo Tanzania Safari channel, kuimarisha matumizi ya TEHAMA pamoja na kutumia watu maarufu, mabalozi wa hiari na ofisi za Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Utalii iliandaa jukwaa la uwekezaji katika sekta ya utalii na kushiriki maonesho mbalimbali yaliyofanyika nje ya nchi yakiwemo: Magical Kenya Travel Expo (Kenya); The Pearl of Africa (Uganda); World Travel Market Africa (Afrika Kusini); International French Tourism Market (Ufaransa); International Travel and Tourism Show (Canada); World Travel Market (Uingereza) na New York Times Travel Show (Marekani). Vile vile, Bodi ilipata fursa ya kutangaza vivutio vya utalii kwa washiriki wa mikutano ya Kimataifa iliyofanyika nchini mwaka 2019. Mikutano hiyo ilijumuisha Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi za SADC, Mkutano wa SADC kuhusu Masuala ya Utalii na Uhifadhi na Mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi za Afrika na nchi za Nordic. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wakala wa Utalii wa Kimataifa iliendelea kuhamasisha safari za ndege za moja kwa moja kutoka nje ya nchi ambapo mwaka 2019, Tanzania ilipokea watalii 900 kutoka Israel na 150 kutoka Hong Kong.

258. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kutoa elimu kupitia maonesho na matamasha mbalimbali nchini yakiwemo Wiki ya Utalii Duniani, Sabasaba, Nanenane, Serengeti Cultural Festival, Hydom Tourism Festival, Karibu Kusini, Urithi Festival, East Africa Trade Fair Mwanza, Lamadi Utalii Festival, Onesho la Utalii Nyasa na Kumbukumbu ya Vita vya Maji Maji.

Malikale

259. Mwaka 2019, wageni walitembelea vivutio vya malikale waliongezeka kwa asilimia 60.6 na kufikia wageni 86,095 ikilinganishwa na wageni 53,596 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ziara za mafunzo za wanafunzi. Aidha, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni kwenye vituo vya malikale yaliongezeka hadi shilingi milioni 228.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi milioni 157.2 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 45.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa siku ambazo watalii walikaa nchini. **Jedwali Na. 12.3** linaonesha idadi ya wageni walitembelea vivutio vya malikale na mapato yaliyopatikana.

Jedwali Na. 12.3: Mapato Yatokanayo na Wageni Walitembelea Vivutio vya Malikale

Kituo	2018		2019	
	Wageni	Mapato (shilingi)	Wageni	Mapato (shilingi)
Magomeni	346	75,000	38	94,000
Kaole	13,977	33,344,000	34,226	70,863,000
Isimila	2,772	11,975,000	2,520	7,476,000
Mji Mkongwe	8,474	30,360,200	18,392	50,793,624
Kalenga	2,732	5,074,000	2,258	4,579,300
Kilwa	3,048	14,311,000	3,813	33,389,000
Mbozi	3,147	6,016,000	3,441	6,359,460
Amboni	9,667	19,905,000	9,537	16,627,000
Tongoni	455	1,164,000	238	880,000
Ujiji	3,826	9,054,000	3,429	9,237,340
Kwihiara	362	848,000	506	919,000
Kolo	1,951	17,722,000	2,765	17,543,000
Caravan Serai	2,839	7,344,000	4,932	9,660,160
Jumla	53,596	157,192,200	86,095	228,420,884

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii- Idara ya Mambo ya Kale

260. Mwaka 2019, wageni 67,382 (ndani ya nchi 52,697 na nje ya nchi 14,685) walitembelea vituo vya Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 79,070 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, shilingi milioni 487.3 zilikusanywa ikilinganishwa na shilingi milioni 434.7 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. **Jedwali Na. 12.4.**

Jedwali Na.12.4: Mapato Yatokanayo na Wageni Walitembelea Vivutio vya Makumbusho

Kituo	2018				2019			
	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Jumla	Mapato	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Jumla	Mapato
Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni	7,335	15,111	22,446	322,592,733.2	8,497	15,769	24,266	323,779,084.4
Kijiji cha Makumbusho	3,573	23,464	27,037	36,454,727	3,378	8,363	11,741	76,829,500
Makumbusho ya Azimio la Arusha	347	5,012	5,359	30,454,702	327	5,594	5,921	19,133,900
Makumbusho ya Elimu Viumbe	2,227	7,048	9,275	39,936,147	2,322	6,252	8,574	46,696,700
Makumbusho ya Mwalimu Nyerere	186	7,536	7,722	3,234,440	100	9,104	9,204	12,452,850
Makumbusho ya Vita ya Majimaji	181	7,050	7,231	2,055,614	61	7615	7,676	8,424,000
Jumla	13,849	65,221	79,070	434,728,363.2	14,685	52,697	67,382	487,316,034.4

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA NA MAPATO YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 45

Mwaka				Mapato (Tshs.)
	Nje	Ndani	Jumla	
2015	432,124	526,110	958,234	149,957,485,000
2016	439,119	518,457	957,576	175,089,696,000
2017	386,529	595,811	982,340	207,587,218,000
2018	726,003	442,543	1,168,546	214,486,751,736
2019	763,276	494,676	1,257,952	292,539,502,030
JUMLA KUU	2,747,051	2,577,597	5,324,648	1,039,660,652,766

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Makumbusho ya Taifa

MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NJE - 2019

Jedwali Na. 46

Zao	Kiasi		Thamani (USD)
	Uzito (kg)	Ujazo (Mita za Ujazo)	
Mbao	-	117,049	29,071,481
maji/utomvu wa miwati	2,010,600	-	21,525
Unga wa Msandali		-	
Vinyago	794,947		53,636
Mbao za Mpingo (Clarinets)		160	329,826
Mafuta ya Msandali	72,005		1,172,760
Utomvu wa misindano			
Nguzo za Umeme			
Mafuta ya Ubuyu	31,650	-	51,489
Mkwiniini (Cinchona)	5,649	-	3,088
Maganda Mdalaasini			
Samani	-	80	404
Gundi ya Arabika	569,383	-	134,483
Mirunda (Mithies)		301	17,100
Venia (Veneer)	-	475	31,380
Mafuta ya Msambu	132,000		488,400
Mazao Mengineyo	2,110,189	82	7,078,706
Jumla Kuu	5,726,423	118,145	38,454,278

IDADI NA MAPATO YATOKANAYO NA UWINDAJI WA KITALII

Jedwali Na. 47

Mwaka	Idadi ya Watalii			Mapato (Shs.)
	Wawindaji	Watazamaji	Jumla	
2015	608	393	1,001	28,802,391,200.00
2016	495	297	792	29,136,885,800.00
2017	473	291	764	19,202,957,607.00
2018	503	280	783	20,109,785,000.00
2019	519	483	1,002	20,864,030,536.00
Jumla Kuu	2,598	1,744	4,342	118,116,050,143.00

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Wanyamapori

MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2011-2019

Jedwali Na. 48

Maelezo	Kipimo	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Jumla ya Watalii	Idadi	867,994	1,077,058	1,095,884	1,140,156	1,137,182	1,284,279	1,327,143	1,505,702	1,510,151
Watalii wa hotelini	Idadi	753,818	974,448	1,021,766	1,005,058	1,033,555	1,155,851	1,163,752	1,404,672	1,408,823
Mapato	US \$ Million	1,325	1,713	1,853	1,983	1,902	2,132	2,200	2,433	2,605
Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini	Siku	10	10	10	10	10	10	9	10	13
Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US \$)	Package Tour Non Package Tour	355	384	372	378	305	351	410	331	334
		247	230	201	210	141	145	136	135	136

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii

IDADI YA WATALII WALIOINGIA NCHINI NA KIASI CHA FEDHA ZILIZOPATIKANA

Jedwali Na. 49

Mwaka	Idadi ya Watalii	Ongezeko kwa Mwaka (%)	Mapato (US \$) Milioni	Ongezeko kwa Mwaka (%)
2001	525,122	4.7	725	-1.9
2002	575,000	9.5	730	0.7
2003	576,000	0.2	731	0.1
2004	582,000	1.0	746	2.1
2005	612,754	5.3	823	10.3
2006	644,124	5.1	950	15.4
2007	719,031	11.6	1,198	26.1
2008	770,376	7.1	1,289	7.6
2009	714,367	-7.3	1,160	-10.0
2010	782,699	9.6	1,255	8.2
2011	867,994	10.9	1,325	5.6
2012	1,077,058	24.1	1,713	29.3
2013	1,095,884	1.7	1,853	8.2
2014	1,140,156	4.0	1,983	7.0
2015	1,137,182	-0.3	1,902	-4.1
2016	1,284,279	12.9	2,132	12.1
2017	1,327,143	3.3	2,200	3.2
2018	1,505,702	13.5	2,433	10.6
2019	1,527,230	1.4	2,605	7.1

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO

Jedwali Na. 50

Mwaka	Wageni kutoka Nie	Watanzania	Jumla ya Watalii
2010	281,513	242,133	523,646
2011	281,513	307,086	588,599
2012	310,537	254,730	565,267
2013	350,970	296,763	647,733
2014	332,469	278,221	610,690
2015	289,061	278,922	567,983
2016	284,794	265,845	550,639
2017	391,030	249,428	640,458
2018	410,574	268,880	679,454
2019	445,283	279,255	724,538

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA MWAKA 2015-2019

Jedwali Na. 51

Jina la Hifadhi	2015		2016		2017		2018		2019	
	Wageni kutoka Nje	Watanzania	Wageni kutoka Nje	Watanzania						
ARUSHA	24,708	31,089	26,714	33,463	30,185	33,885	32,790	35,354	22,063	33,504
GOMBE	723	895	956	958	1,002	968	1,194	956	1,208	960
KATAVI	1,200	2,445	1,159	3,066	1,190	1,910	1,482	2,369	1,353	2,925
KILIMANJARO	41,038	3,328	43,893	3,508	47,772	2,731	51,533	2,390	70,580	4,717
KITULO	70	592	95	311	94	432	179	330	262	1,276
LAKE MANYARA	92,341	62,287	103,830	57,855	118,501	56,082	135,098	58,131	147,482	65,913
MAHALE	896	171	690	166	983	151	886	166	969	112
MIKUMI	17,117	35,311	22,923	38,003	19,274	34,413	25,580	33,373	25,265	37,232
MKOMAZI	563	1,905	573	1,482	594	1,700	659	1,464	871	2,886
RUAHA	11,558	7,403	11,233	12,958	11,217	12,161	14,381	13,219	14,459	17,319
RUBONDO	447	501	433	739	558	427	465	793	552	1,083
SAADANI	3,143	19,854	3,548	18,722	2,530	18,603	2,976	15,048	3,247	16,594
SERENGETI	413	13,132	201,728	174,047	474	152,216	270,946	175,084	278,441	194,264
TARANGIRE	167,988	204,998	130,085	78,573	231,756	77,101	183,764	85,935	192,526	96,119
UDZUNGWA	116,590	58,585	2,759	5,557	151,681	5,268	3,420	5,530	3,363	4,379
SAANANE	2,604	6,310	464	11,102	2,617	10,088	650	12,401	635	15,393
Jumla	481,399	448,806	551,083	440,510	620,428	408,136	726,003	442,543	763,276	494,676

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii - Hifadhi za Taifa (TANAPA)

SURA YA 13

MADINI

Utafutaji Madini

261. Mwaka 2019, leseni 3,002 za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini zilitolewa ikilinganishwa na leseni 1,687 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kutoa elimu kwa lengo la kuhamasisha wadau wa sekta ya madini hususan wachimbaji wadogo kuomba leseni za uchimbaji. Kati ya hizo, leseni 120 zilikuwa za utafutaji madini, leseni 23 za uchimbaji wa kati na leseni 2,859 za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, maombi 8,801 ya leseni yalipokelewa na kuidhinishwa mwaka 2019 ikilinganishwa na maombi 8,716 mwaka 2018. Kati ya hayo, maombi 8,181 yalikuwa ya wachimbaji wadogo, maombi 552 ya utafutaji madini na maombi 68 ya uchimbaji wa kati.

Uuzaji wa Madini

262. Thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 2,280.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,624.74 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 40.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na vito vya thamani pamoja na kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini nchini kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017.

Almasi

263. Mwaka 2019, uzalishaji wa madini ya almasi uliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufikia karati 416,749.51 kutoka karati 381,302.06 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa almasi katika mgodi wa Williamson Diamonds Ltd kufuatia kukamilika kwa usimikaji wa mitambo mipya ya uchenjuaji wa almasi katika mgodi huo. Aidha, thamani ya mauzo ya almasi nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 7.0 na kufikia dola za Marekani milioni 89.33 mwaka 2019 kutoka dola za Marekani milioni 96.07 mwaka 2018. Hii ilitokana na kushuka kwa ubora wa almasi iliyozalishwa mwaka 2019.

Dhahabu

264. Uzalishaji wa dhahabu ulifikia kilogramu 48,408 mwaka 2019 ikilinganishwa na kilogramu 39,304 zilizozalishwa mwaka 2018, sawa na

ongezeko la asilimia 23.2. Hii ilitokana na: kuimarika kwa udhibiti katika maeneo ya uzalishaji na uchenjuaji wa dhahabu hasa katika maeneo yenywachimbaji wadogo na wa kati; kuwepo kwa masoko na vituo vyatunuzi na uuzaaji wa madini; na utoaji wa elimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya madini nchini. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 45.9 na kufikia dola za Marekani milioni 2,123.04 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,454.88 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha madini ya dhahabu kilichosafirishwa nje ya nchi na kuimarika kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia ambapo wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia ulifikia dola za Marekani 1,392.5 kwa wakia mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,269.2 mwaka 2018. Thamani ya mauzo ya dhahabu nje ilichangia asilimia 93.1 ya mauzo yote ya madini mwaka 2019.

Vito vya Thamani

265. Mwaka 2019, uzalishaji wa vito vya thamani ulifikia kilogramu 1,929,714 ikilinganishwa na kilogram 284,321.19 zilizozalishwa mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na: kuimarika kwa udhibiti katika maeneo ya uzalishaji ya wachimbaji wadogo na wa kati; kuimarishwa kwa masoko na vituo vyatunuzi na uuzaaji wa madini ya vito; na utoaji wa elimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya madini. Aidha, thamani ya mauzo ya vito nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 2.5 na kufikia dola za Marekani milioni 27.31 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 28.01 mwaka 2018. Hii ilitokana na zuio la usafirishaji madini ghafi ya vito nje ya nchi kwa lengo la kuyaongezea thamani kabla ya kusafirishwa.

Makaa ya Mawe

266. Mwaka 2019, jumla ya tani 712,136.37 za makaa ya mawe zilizalishwa ikilinganishwa na tani 627,652.64 zilizozalishwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji wa makaa ya mawe katika migodi ya TANCOAL, Magamba, Edenvile International (T) Ltd na Kabulo. Aidha, thamani ya mauzo ya makaa ya mawe nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 48.7 na kufikia dola za Marekani milioni 50.95 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 34.26 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wanunuzi kutoka nje na ndani ya nchi kufuatia zuio la uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi.

Tanzanite Ghafi

267. Mwaka 2019, uzalishaji wa madini ya tanzanite ghafi yenyе ubora wa juu na kati ulifikia kilogramu 2,772.2 ikilinganishwa na kilogramu 781.2 zilizozalishwa mwaka 2018. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na kuimarika kwa udhibiti wa madini ya tanzanite kufuatia ujenzi wa ukuta wa Mirerani. Katika kipindi hicho, jumla ya kilogramu 36,013.14 za madini ya tanzanite ghafi yenyе ubora wa chini zilizalishwa. Aidha, mapato yatokanayo na mauzo ya tanzanite ghafi nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 2.15 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.44 mwaka 2018.

Madini mengine

268. Mwaka 2019, uzalishaji wa madini ya fedha uliongezeka kwa asilimia 4.2 hadi kilogramu 12,550 ikilinganishwa na kilogramu 12,041 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa mikuo ya dhahabu (gold bullion) katika migodi ya Shanta, Bulyanhulu, Geita na Buzwagi. Katika kipindi hicho, thamani ya mauzo ya madini ya fedha nje ya nchi ilifikia dola za Marekani milioni 6.54 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6.05 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.1.

269. Uzalishaji wa madini ya chumvi ulifikia tani 99,510.11 ikilinganishwa na tani 36,392.41 mwaka 2018. Aidha, thamani ya mauzo ya chumvi nje ya nchi iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 5.58 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1.21 mwaka 2018. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya chumvi nje kulitokana na kukua kwa soko la madini ya chumvi katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

270. Mwaka 2019, uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 24.32 ikilinganishwa na tani 8.04 mwaka 2018. Ongezeko la uzalishaji wa madini ya bati lilitokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara ya madini ya bati nchini. Aidha, uzalishaji wa madini ya jasi ulifikia tani 256,529 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 241,259.46 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa madini ya kaolini ulipungua hadi tani 15,343 mwaka 2019 kutoka tani 129,382.64 mwaka 2018. Hii ilitokana na wazalishaji wa kaolini katika wilaya ya Kisarawe kuwa na bakaa kubwa ya mwaka 2018 na hivyo kutumia kipindi cha mwaka 2019 kuuza bakaa hiyo.

Uongezaji Thamani Madini

Mwaka 2019, Serikali iliendelea kutilia mkazo uongezaji thamani madini ikiwa ni pamoja na kuzuia usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi na kutoa mafunzo ya kitaalam ya uongezaji thamani madini ya vito na miamba. Katika kipindi hicho, jumla ya karati 160,387.0 za madini ya tanzanite zenye thamani ya dola za Marekani milioni 12.61 zilikatwa na kusanifiwa. Kati ya kiasi hicho, karati 123,613.0 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 8.02 zilisafirishwa kwenda nje ya nchi.

Masoko ya Madini

Mwaka 2019, Serikali ilianzisha masoko na vituo vya uuzaaji wa madini kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa madini, kupata takwimu sahihi za mauzo na kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika na bei stahiki na hivyo, kuongeza mapato ya Serikali. Hadi Desemba 2019, masoko 30 na vituo 27 vilianzishwa katika mikoa mbalimbali nchini. Katika kipindi hicho, kilogramu 8,200 za dhahabu, karati 106,534 za almasi, kilogramu 20,009 za tanzanite, na kilogramu 465,186 za madini ya vito mbalimbali ziliuzwa kupitia masoko hayo na jumla ya shilingi bilioni 58.86 zilikusanywa kama maduhuli.

UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

Jedwali Na.52

MADINI	Kipimo	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Almasi	Carat	28,378	127,174	179,633	252,875	216,491	237,685	304,456	381,302	416,750
Dhahabu	Kg	37,085	39,012	42,534	40,481	43,293	45,155	43,490	39,304	48,408
Gemstones	Kg	1,241,581	1,237,625	1,692,436	3,083,765	1,872,915	2,554,932	1,185,697	284,321	1,929,714
Chumvi	Tani	32,297	34,016	36,032	54,757	92,158	145,718	100,017	36,392	99,510
Phosphate	Tani	848,512	570,626	397,020	738,000	222,800	23,658	1,351	-	-
Limestone	000 Tani	202	1,224	35,529	873	2,945	4,170	3,301	2,944	5,527
Tin Ore	Tani	-	-	2	79	179	138	91	8	24
Gypsum	Tani	9,288	91,610	171,567	200,179	239,302	213,744	123,645	241,260	256,529
Makaa ya mawe	Tani	80,710	78,672	84,772	246,128	257,321	276,030	563,053	627,652	712,136
Pozolana	Tani	113,489	75,193	79,452	68,925	342,628	230,045	79,085	91,645	263,064
Kaolin	Tani	178	1,422	907	3,809	1,953	656	13,816	129,383	15,343
Madini ya fedha	Kg	10,399	11,227	12,159	14,493	15,569	17,984	10,911	12,041	12,550
Shaba	Pound	7,531,164	12,426,025	12,749,548	14,027,008	14,252,341	15,762,430	2,933,941	-	-
Bauxite	Tani	29,520,000	28,433,930	39,977,300	25,641,201	204,956	72,779	12,090	7,140	-
Madini ya Ujenzi	000 Tani			5,470	10,480	12,960	15,460	5,601	10,375	20,188

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

Carat = 0.205 gm

MADINI YALIYOUZWA NCHI ZA NJE 2015 - 2019

Jedwali Na. 53

Aina ya madini	Kipimo	Kiasi kilichouzwa					Thamani ('000 US \$)				
		2015	2016	2017	2018	2,019	2015	2016	2017	2018	2019
Almasi (Rough)	'000 Carats	216,491	239,305	304,456	383,391	416,750	56,003	85,090	67,510	96,066	89,335
Almasi (iliyokatwa)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Almasi (Contract goods)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Dhahabu	'000 Gramu	43,358	45,155	43,490	35,864	48,408	1,609,392	1,824,815	1,636,575	1,454,879	2,123,035
Mawe ya thamani	'000 Gramu	1,872,915	2,944,107	1,185,697	284,321	761,814	46,067	60,483	53,596	28,006	27,314
Chumvi	Tani	92,158	145,718	100,017	36,392	99,510	5,071	4,806	3,803	1,207	5,576
Phosphate	Tani	222,800	23,658	1,351	-	-	126	721	585	-	-
Bati	Tani	179	138	91	8	-	959	1,499	1,037	-	-
Jasi	Tani	235,920	213,744	123,645	241,260	2,916	4,445	6,279	3,187	-	317
Grafiti	Tani	30	1,180	128	27,810	9,271	5	2,132	18	2,418	4,420
Fedha	000Grams	15,569	17,984	10,911	12,041	12,550	7,626	9,901	5,850	6,045	6,537
Shaba	0001b	14,252	16,247	2,934	-	-	35,658	35,421	7,741	-	-
Madini ya viwandani	Tani	151,297	4,769,577	708,047	783,180	336,844	3,254	78,491	29,896	35,783	23,994
Bauxite	Tani	204,956	74,660	12,090	7,140	-	325	1,242	898	335	-
Jumla ('000 Us \$)							1,768,930	2,110,877	1,810,697	1,624,739	2,280,529

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 14

VIWANDA NA BIASHARA

Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini

271. Mwaka 2019, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani kuendelea kuongezeka kutokana na uhitaji mkubwa katika soko la ndani na nje. Bidhaa ambazo uzalishaji wake uliongezeka ziliwu: saruji (asilimia 36.7), rangi (asilimia 21.1), bati (asilimia 20.0), kamba za katani (asilimia 14.0), tabaka za mbaao (asilimia 12.5), nyavi za uvuvi (asilimia 11.4), konyagi (asilimia 10.3), biskuti na tambi (asilimia 7.1), sigara (asilimia 5.7), betri (asilimia 4.4), dawa za pareto (asilimia 4.3) na unga wa ngano (asilimia 2.6). Kwa upande mwingine, uzalishaji ulipungua kwa bidhaa za nguo (asilimia 13.7), bia (asilimia 5.2), chuma (asilimia 3.3) na chibuku (asilimia 2.3). Gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka kwa asilimia 10.0 na kufikia shilingi bilioni 8,696.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7,905.6 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa bei za malighafi za viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na ghamama za mishahara ya wafanyakazi.

Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

272. Mwaka 2019, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ilitoa mafunzo kuhusu usimamizi wa fedha na upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali 91,584 ikilinganishwa na wajasiriamali 71,794 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 27.6. Aidha, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) lilitoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali 17,831 ikilinganishwa na wajasiriamali 14,885 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Mafunzo yaliyotolewa yalijumuisha: usindikaji wa mazao ya kilimo; utengenezaji wa bidhaa za ngozi; usindikaji wa mazao ya nyuki; ubunifu wa mavazi na ushonaji; kuzuia upotevu wa mazao shambani; na utengenezaji wa mashine, zana na bidhaa mbalimbali. Kuongezeka kwa wajasiriamali waliopewa mafunzo kulitokana na jitihada mbalimbali za Serikali katika kuhamasisha wananchi kuanzisha biashara na viwanda vidogo.

273. Mwaka 2019, SIDO kupitia vituo vya maendeleo ya teknolojia ilitengeneza na kusambaza mashine 338 ikilinganishwa na mashine 293 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Hii ilichangwa na kuongezeka kwa ushiriki wa

wananchi katika shughuli za uchumi wa viwanda. Mashine zilizotengenezwa zilijumuisha: mashine za kusindika mazao ya kilimo, mifugo na bidhaa zake; mashine za uvunaji na uhifadhi wa mazao; mashine za kupunguza matumizi ya miti na mazao yake kama vyanzo vya nishati; mashine za kufungashia vyakula vilivyoindikwa; na mashine za kutengeneza matofali.

274. Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.35 kwa wajasiriamali 2,763 mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.87 zilizotolewa kwa wajasiriamali 3,368 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Upungufu huo ilitokana na wajasiriamali kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati. Aidha, mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 7,594 mwaka 2019 ikilinganishwa na fursa 7,477 mwaka 2018. Vile vile, Chuo cha Elimu ya Biashara kilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 98 ikilinganishwa na wajasiriamali 21 mwaka 2018.

275. Mwaka 2019, Serikali iliendelea na mkakati wa kuwezesha sekta ndogo ya biashara kuongeza tija na ufanisi katika biashara ili kujiendesha kiushindani. Katika kipindi hicho, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ulitoa mafunzo kwa wadau 1,897 ikilinganishwa na wadau 691 mwaka 2018. Mafunzo hayo yalijumuisha wajasiriamali, wasindikaji wa viungo na wanafunzi wa sekondari kwa lengo la kuwajengea uelewa wa biashara, mbinu za upatikanaji wa masoko na usindikaji bora wa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Miundombinu ya Masoko ya Bidhaa za Mazao na Mifugo

276. Mwaka 2019, idadi ya vibaraza vya machinjio, bucha na maghala iliongezeka na kufikia vibaraza 6,082, bucha 9,546 na maghala 678 ikilinganishwa na vibaraza 2,297, bucha 8,280 na maghala 612 mwaka 2018. Aidha, minada ya upili ilikuwa 17 mwaka 2019 ikilinganishwa na minada 12 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeza kwa mahitaji kulikosababishwa na kuhamasika kwa wananchi na wazalishaji kutumia miundombinu hiyo. Mchanganuo wa miundombinu ya masoko ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 14.1.**

Jedwali Na. 14.1: Mchanganuo wa Miundombinu ya Masoko

Miundombinu ya Masoko	2018	2019	Ongezeko (Asilimia)
Vibaraza vya Machinjio (Slaughter slab)	2297	6,082	164.8
Bucha	8280	9,546	15.3
Banda la ngozi	750	226	-69.9
Nyumba za Machinjio (Slaughter house)	394	566	43.7
Maghala	612	678	10.8
Machinjio (Abattoir)	59	78	32.2
Minada ya Awali	442	330	-25.3
Minada ya Upili	12	17	41.7
Minada ya Mipakani	9	6	-33.3
Mashine za Kuchakata Nyama	86	84	-2.3
Mashine za Kuchakata Maziwa	35	30	-14.3
Mashine za Kuchakata Samaki	11	13	18.2
Vituo vya Kukusanya Maziwa	150	133	-11.3

Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara - *Agricultural Routine Data System*

Usajili wa Biashara na Viwanda

277. Mwaka 2019, Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilitoa leseni 240 za kuanzisha viwanda vipyta ikilinganishwa na leseni 194 mwaka 2018. Aidha, BRELA ilisajili kampuni mpya 8,846 mwaka 2019 ikilinganishwa na kampuni 6,762 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Ongezeko hilo lilitokana na juhudhi mahsusizi za Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya usajili kwa njia ya mtandao sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kusajili kampuni au/na biashara zao.

Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa

278. Mwaka 2019, kampuni 3,250 za ndani na kampuni 520 za nje ya nchi zilishiriki maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyoandalifiwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ikilinganishwa na kampuni 2,956 za ndani na 508 za nje zilizoshiriki maonesho ya 42 mwaka 2018. Aidha, nchi 35 zilishiriki mwaka 2019 ikilinganishwa na nchi 33 zilizoshiriki mwaka 2018. Kuongezeka kwa ushiriki kulichangiwa na kampuni kutambua umuhimu wa maonesho katika kutangaza bidhaa zao na kuwafikia wateja wengi kwa wakati mmoja. Vile vile, TanTrade

iliratibu mikutano minne ya kibiashara iliyohusisha wadau 520 kutoka sekta mbalimbali ambapo mikataba 64 isiyo fungani ya mauzo yenye thamani ya shilingi milioni 13,220 ilisainiwa. Mikataba hiyo ilihuhsisha sekta ndogo ya matunda na mboga (milioni 6,090); sekta ndogo ya asali na mazao ya misitu (milioni 4,240); muhogo, nafaka na mazao ya mikunde (milioni 2,060) na bidhaa za ngozi na vifaa vya shule (milioni 830).

279. Mwaka 2019, Serikali kupitia TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni 18 za Tanzania katika maonesho ya *Fruit Logistica* yaliyofanyika nchini Ujerumani. Kupitia maonesho hayo, kampuni 20 za Ujerumani ziliunganishwa na kampuni za Tanzania zinazofanya biashara ya matunda. Vile vile, kampuni 20 za teknolojia kutoka mataifa mbalimbali ya Ulaya na Amerika ziliunganishwa na kampuni tano (5) za Tanzania ili kufanya ubia wa kibiashara.

Udhibiti wa Ubora wa Viwango na Vipimo

280. Mwaka 2019, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilitoa leseni 358 za ubora ikilinganishwa na leseni 259 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 38.2. Ongezeko hilo lilitokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wazalishaji mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuzingatia ubora wa bidhaa. Aidha, mafunzo 108 ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 7,464 ikilinganishwa na mafunzo 59 yaliyotolewa kwa washiriki 4,208 mwaka 2018.

281. Mwaka 2019, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo iliendelea kutoa huduma za kuhakiki usahihi wa vipimo na mifumo ya upimaji katika sekta ya biashara, afya, usalama na mazingira kwa lengo la kumlinda mlaji. Katika kipindi hicho, Wakala ulikagua vipimo 841,518 ikilinganishwa na vipimo 732,912 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi vikiwemo magari na vifaa vya kisasa vya kupima dira za maji na mizani ya kuhakiki usahihi wa vipimo vya madini. Vile vile, Wakala ulitoa leseni za ufundi na uundaji wa vipimo kwa wadau 300 mwaka 2019 ikilinganishwa na wadau 200 mwaka 2018.

282. Mwaka 2019, Wakala uliongeza uwezo wa kuhakiki magari yanayobeba mafuta kutoka wastani wa magari nane (8) na kufikia magari 70 kwa siku. Hii ilitokana na kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kisasa cha uhakiki wa magari kilichopo Misugusugu-Kibaha. Aidha, Wakala uliongeza kituo cha Tarakea

mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha udhibiti wa bidhaa zinazofungashwa mipakani na hivyo kuwa na jumla ya vituo nane (8).

Udhibiti wa Bidhaa Bandia

283. Mwaka 2019, Serikali kupitia Tume ya Ushindani ilikagua makasha 3,260 ya kusafirishia mizigo ambapo makasha 114 yalibainika kuwa na bidhaa bandia. Bidhaa bandia zilizokamatwa ziliwu na alama zilizogushiwa pamoja na kukosa alama za utambulisho wa bidhaa, anuani ya mzalishaji na nchi ya uasili ilipotengenezwa. Aidha, Tume ilifanya kaguzi 32 za kushtukiza katika maghala na maduka mbalimbali kwa lengo la kubaini bidhaa bandia. Tume ilifanikiwa kukamata bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi (pisi 12,571); mafuta na vipodozi (pisi 850); vifaa vya ofisi (pisi 6,652); vipuri na vilainishi (dazani 129); nguo na viatu (jozi 6,906) pamoja na vifaa vya elektroniki (pisi 3,750).

Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

284. Mwaka 2019, uzalishaji wa mpira mkavu katika mashamba ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) ulifikia tani 40.3 ikilinganishwa na tani 21.2 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 90.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa usimamizi katika mashamba hayo.

285. Mwaka 2019, matrekta 421 yaliunganishwa katika kiwanda cha URSSUS kilichopo Kibaha ikilinganishwa na matrekta 282 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 49.29. Hii ilitokana na ongezeko la mtaji kutoka shilingi bilioni 1.22 mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 2.48 mwaka 2019, kuwepo kwa fursa ya kununua matrekta kwa njia ya mkopo na uhamasishaji kwa umma kupitia vyombo vya habari na maonesho.

Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji

286. Mwaka 2019, Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA) ilisajili kampuni mpya sita (6) ikilinganishwa na kampuni tano (5) mwaka 2018. Kampuni zilizosajiliwa ni *H&J Fibres Investment*, Tembo Mfalme, *Third Man Limited*, *Gravita Tanzania Limited*, *One Belt Electrical Technology Group Ltd* na *Metalord Impex Limited*. Kuongezeka kwa usajili wa kampuni kulitokana na Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji. Katika kipindi hicho, mtaji wa dola za Marekani bilioni 2,376 uliwekezwa kwenye maeneo maalumu ya uwekezaji (EPZ/SEZ) ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2,196 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Aidha,

ajira 57,342 zilizalishwa mwaka 2019 ikilinganishwa na ajira 55,497 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na juhudzi za Serikali kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji.

MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 54

Mwaka	Kutoka Nje	Uuzaji nje	Uzalishaji wa Ndani	Tani	
				Matumizi Tani	Badiliko %
2001	56,395	53,517	900,430	903,308	11.5
2002	149,079	37,203	1,026,082	1,137,958	26.0
2003	166,446	34,396	1,186,434	1,318,484	15.9
2004	125,007	37,655	1,280,851	1,368,203	3.8
2005	120,200	40,430	1,375,222	1,454,992	6.3
2006	92,711	98	1,421,460	1,514,073	4.1
2007	101,827	52,170	1,629,890	1,679,547	10.9
2008	356,468	99,688	1,755,862	2,012,642	19.8
2009	516,182	57,569	1,940,845	2,399,458	19.2
2010	566,828	189,321	2,312,055	2,689,562	12.1
2011	768,343	217,944	2,408,765	2,959,164	10.0
2012	1,013,986	145,793	2,557,798	3,425,991	15.8
2013	1,218,453	154,481	2,369,819	3,433,791	0.2
2014	1,428,995	142,001	2,795,687	4,082,681	18.9
2015	1,257,578	126,391	3,273,000	4,404,187	7.9
2016	1,306,732	194,338	4,916,400	6,028,794	36.9
2017	188,067	226,588	4,397,684	4,359,163	-27.7
2018	17,259	206,234	4,766,092	4,577,117	5.0
2019	0	410,607	6,514,715	6,104,108	33.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa Takwimu

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.55

Aina ya Bidhaa	Kipimo	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (%) 2018/19
Biskuti & tambi	Tani	12,053	16,423	17,440	18,225	19,204	15,890	16,451	16,911	18,113	7.1
Unga wa ngano	Tani	439,926	442,345	516,778	529,797	533,257	498,940	606,432	662,967	680,393	2.6
Konyagi	000 Lita	15,432	16,229	20,680	31,963	29,491	28,754	25,555	29,335	32,366	10.3
Bia	000 Lita	323,393	338,041	374,238	379,913	386,310	383,251	396,864	412,555	391,299	-5.2
Chibuku	000 Lita	23,474	22,359	19,935	20,301	23,028	26,513	22,624	20,819	20,350	-2.3
Sigara	Milioni	6,630	7,723	7,710	8,028	7,837	8,091	7,412	7,921	8,369	5.7
Nguo	000 M ²	101,820	81,437	97,522	119,458	100,491	76,436	52,052	52,613	45,415	-13.7
Kamba za katani	Tani	6,976	7,927	7,542	7,871	8,851	9,216	8,188	8,148	9,287	14.0
Nyavu za uvuvi	Tani	164	272	297	279	311	312	196	228	254	11.4
Mazulia	000 M ²	-	-	-	-	0	0	-	-	-	-
Tabaka za mbao	M ²	30,589	38,871	36,935	38,913	36,317	34,983	37,302	37,849	42,563	12.5
Dawa za pareto	Tani	53	70	83	136	118	126	134	139	145	4.3
Mbolea	Tani	11,200	-	-	-	0	0	-	-	-	-
Rangi	000 Lita	31,211	35,025	36,623	38,308	38,372	35,096	40,146	47,928	58,024	21.1
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	-	-	-	0	0	-	-	-	-
Saruji	000 Tani	2,409	2,558	2,369	2,795	3,135	4,572	4,398	4,766	6,514	36.7
Chuma*	Tani	39,955	46,690	48,500	56,752	62,612	65,686	231,591	275,267	266,314	-3.3
Bati	Tani	76,912	81,427	85,314	86,825	91,385	91,421	84,541	84,132	100,963	20.0
Aluminium	Tani	33	23	37	27	32	14	-	-	-	-
Radio	000 namba	-	-	-	-	0	0	-	-	-	-
Betri	Milioni	89	68	75	93	87	69	122	115	120	4.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

* Takwimu za uzalishaji wa chuma kuanzia mwaka 2008 - 2018 zimerekebishwa

VIWANDA - IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 56

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Walioajiriwa			Wengine			Jumla		
		2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
151-4	Vyakula	77,625	84,611	93,072	26,092	28,441	31,285	103,718	113,052	124,357
155	Vinywaji	8,410	9,167	10,084	103	112	123	8,513	9,279	10,207
160	Tumbaku na Sigara	6,203	6,761	7,437	7	8	9	6,210	6,769	7,446
171-2,	Ufumaji na Ushonaji	32,942	35,907	39,498	25,709	28,023	30,825	58,651	63,930	70,323
181	Ngozi, bidhaa za ngozi	1,713	1,868	2,055	384	419	461	2,097	2,286	2,516
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	8,763	9,551	10,506	2,685	2,926	3,219	11,448	12,478	13,725
210-221-	Karatasi, Uchapishaji	6,553	7,142	7,856	244	266	293	6,797	7,409	8,149
222	Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya serikali	8,762	9,551	10,506	276	301	331	9,038	9,852	10,837
241-2	Bidhaa za mpira na Plastiki	5,209	5,678	6,246	69	75	82	5,278	5,753	6,328
251	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	9,837	10,722	11,794	1,570	1,712	1,883	11,407	12,434	13,677
261-9	Nyinginezo	36,833	40,148	44,163	20,908	22,790	25,069	57,741	62,938	69,232
	Jumla	202,852	221,108	243,217	78,047	85,072	93,580	280,899	306,180	336,797

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa L

Viwanda vilivyo husika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA - GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 57

(Sh.milioni)

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Mishahara			Malipo Mengine			Jumla		
		2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
151-4	Vyakula	431636	435952	479547	79023	79813	87794	510659	515765	567341
155	Vinywaji	264531	267177	293895	112426	113550	124905	376957	380727	418800
160	Tumbaku na Sigara	117834	119013	130914	32955	33284	36612	150789	152297	167527
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	131297	132610	145871	69302	69995	76994	200600	202605	222865
191	Ngozi, Bidhaa za ngozi	7461	7535	8288	754	762	838	8215	8297	9127
201- 202	Mbao, Bidhaa za Mbao	34732	35079	38587	4918	4967	5464	39650	40047	44051
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya Binadamu	63114	63745	70119	13994	14134	15547	77108	77879	85667
241-2	Bidhaa za Mpira na Plastiki	85682	86538	95192	13390	13524	14876	99072	100062	110068
251	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	44031	44471	48918	6475	6540	7194	50506	51011	56112
261-9	Nyinginezo	115986	117146	128861	35155	35506	39057	151141	152652	167917
271-369	Jumla	1487646	1502522	1652773	408210	412292	453521	1895856	1914814	2106294

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uza
Viwanda vilivyo husika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 58

ISIC (Rev 3)	Shughuli	PATO			GHARAMA			nani Iliyoongezeka (Value Ad)		
		2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
151-4	Vyakula	6549583	6615079	7276587	3010077	3040178	3344196	3539505	3574901	3932391
155	Vinywaji	2701037	2728047	3000852	808786	816874	898561	1892251	1911174	2102290
160	Tumbaku na Sigara	1015002	1025152	1127667	254737	257285	283013	760265	767867	844654
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	792579	800505	880556	362835	366463	403109	429744	434041	477446
191	Ngozi, bidhaaa za ngozi	88957	89846	98831	60388	60992	67091	28569	28855	31739
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	240805	243213	267534	79878	80677	88745	160927	162536	178790
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji Utengenezaji wa Kemikali na madawa ya Binadamu	435327	439681	483649	269555	272251	299476	165772	167430	184173
241-2	Bidhaa za mpira na Plastiki	953497	963032	1059335	596655	602621	662883	356842	360411	396452
251	Bidhaa za Madini yasiyo	979423	989217	1088139	633295	639628	703591	346128	349590	384548
261-9	Chuma	1250627	1263134	1389447	634686	641032	705135	615942	622101	684312
271-369	Nyinginezo	1922793	1942021	2136223	1116457	1127622	1240384	806336	814399	895839
	Jumla	16929630	17098926	18808820	7827349	7905622	8696185	9102281	9193304	10112635

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 59

Jina la mkoa	Idadi ya Wafanyakazi			Idadi ya Waajiriwa			shahara (TShs. Milioni)			Ni Iliyoongezeka (TShs.)		
	2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
Dodoma	3039	3313	3644	2195	2392	2631	18616	18802	20682	115042	116192	126546
Arusha	23840	25986	28585	17216	18766	20643	63206	63838	70222	390599	394505	429659
Kilimanjaro	17901	19512	21463	12927	14091	15500	80059	80860	88946	494748	499696	544223
Tanga	13513	14729	16202	9758	10637	11701	99765	100762	110838	616523	622689	678176
Morogoro	42347	46159	50775	30581	33333	36666	42324	42748	47023	261555	264170	287711
Pwani,	13181	14368	15805	9519	10376	11414	60048	60649	66714	371086	374796	408195
Dar es Salaam	90635	98793	108672	65453	71343	78477	854210	862752	949027	5278818	5331606	5806701
Lindi	1352	1474	1621	977	1065	1172	380	384	422	2349	2373	2585
Mtwara	3919	4272	4699	2830	3085	3394	14165	14307	15738	87536	88411	96290
Ruvuma	2529	2756	3032	1826	1991	2190	2857	2885	3173	17655	17831	19420
Iringa	6740	7346	8081	4867	5305	5836	33790	34128	37541	208815	210903	229696
Mbeya	8072	8798	9678	5829	6353	6988	68745	69433	76376	424829	429078	467312
Singida	3123	3404	3744	2256	2459	2705	2472	2497	2747	15276	15429	16804
Tabora	994	1084	1192	718	782	860	13635	13772	15149	84262	85105	92688
Rukwa	2080	2267	2494	1502	1637	1801	7876	7955	8750	48671	49157	53538
Kigoma	2532	2760	3036	1828	1993	2192	1327	1341	1475	8204	8286	9024
Shinyanga	3724	4059	4465	2689	2932	3225	13543	13679	15047	83695	84531	92063
Kagera	4851	5288	5817	3504	3819	4201	6306	6369	7006	38970	39359	42867
Mwanza	14856	16193	17812	10728	11694	12863	79185	79976	87974	489342	494235	538276
Mara	4760	5188	5707	3437	3746	4121	6918	6988	7687	42754	43182	47030
Manyara	6924	7547	8302	5000	5450	5995	3294	3327	3660	20359	20563	22395
Njombe	3705	4039	4443	2676	2917	3209	6288	6350	6985	38856	39244	42741
Katavi	1920	2093	2302	1387	1511	1662	1352	1366	1503	8358	8441	9194
Simiyu	2361	2573	2830	1705	1858	2044	5050	5100	5610	31207	31519	34328
Geita	810	883	971	585	638	702	249	251	276	1536	1551	1690
Songwe	1189	1296	1426	859	936	1030	1984	2004	2204	12259	12381	13484
Jumla	280899	306180	336798	202852	221108	243220	1487646	1502522	1652775	9193302	9285235	10112636

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiria kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani Viwanda viliyohusika ni vyenye ajira ya mtu

VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA (Asilimia)

Jedwali Na. 60

Mwaka	Mchango katika Pato la Taifa (Bei za miaka husika)	Ukuaji wa Sekta (Bei za Mwaka 2015)	Mchango katika mauzo nje	Mchango katika mauzo nje yasiyo asilia	Badiliko katika mauzo nje ya bidhaa za viwanda
2013	9.11	3.7	20.4	28.95	3.4
2014	9.12	10.0	23.9	32.63	15.6
2015	7.86	7.1	24.0	31.61	3.0
2016	7.81	10.8	14.4	20.18	-44.1
2017	7.67	8.2	15.3	22.44	-2.9
2018	8.07	8.3	18.1	24.76	14.5
2019	8.49	5.8	16.9	23.29	3.9

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SURA YA 15

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

UJENZI

Mtandao wa Barabara Nchini

287. Tanzania ina mtandao wa barabara wenge urefu wa kilometra 86,472. Mtandao huo unajumuisha kilometra 12,176 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilometra 24,082 za barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu na kilometra 50,214 ni barabara za wilaya zinazounganisha wilaya, kata na vijiji.

288. Mwaka 2019, barabara kuu na barabara za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometra 33,178 ikilinganishwa na kilometra 32,852 kwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 1.0. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya barabara za wilaya kupandishwa hadhi na kuwa barabara za mikoa. Kati ya barabara zilizofanyiwa tathmini, kilometra 3,618 zilikuwa na hali mbaya, kilometra 16,693 zilikuwa katika kiwango cha wastani na kilometra 12,867 zilikuwa katika hali nzuri mwaka 2019 ikilinganishwa na kilometra 4,217, kilometra 17,592 na kilometra 11,043 mwaka 2018 mtawalia. Aidha, barabara zenye hali ya wastani na zenye hali mbaya zilipungua kutokana na kuongezeka kwa barabara zenye hali nzuri zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

289. Hadi Desemba 2019, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometra 10,482 sawa na asilimia 31.6 ya mtandao wa barabara kuu na za mikoa zilizofanyiwa thathmini ikilinganishwa na kilometra 10,490 mwaka 2018. Kati ya hizo, kilometra 1,164 zilikuwa katika hali mbaya ikilinganishwa na kilometra 1,214 mwaka 2018, kilometra 2,789 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometra 2,951 mwaka 2018 na kilometra 6,529 zilikuwa na hali nzuri ikilinganishwa na kilometra 6,325 mwaka 2018. Aidha, kupungua kwa barabara zenye hali mbaya kulitokana na kuongezeka kwa barabara zenye hali nzuri zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

290. Hadi kufikia Desemba 2019, barabara za mikoa zilizokuwa na kiwango cha lami na changarawe zilizofanyiwa tathmini ziliikuwa na urefu wa kilometra 22,696 ikilinganishwa na kilometra 22,362 mwaka 2018. Kati ya barabara zilizofanyiwa tathmini, kilometra 2,454 ziliikuwa na hali mbaya, kilometra 13,904 ziliikuwa na hali ya wastani na kilometra 6,338 ziliikuwa na hali nzuri mwaka 2019 ikilinganishwa na kilometra 3,003, kilometra 14,641 na kilometra 4,718 mwaka 2018 mtawalia. Kupungua kwa barabara zenye hali ya wastani na mbaya kulitokana na kuongezeka kwa barabara zenye hali nzuri zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. **Jedwali Na. 15.1** linaonesha hali ya mtandao wa barabara hadi Desemba 2019.

Jedwali Na. 15.1: Hali Ya Mtandao wa Barabara Hadi Desemba, 2019

Aina ya Barabara	Hali ya Mtandao wa barabara						Jumla	
	Nzuri		Wastani		Mbaya			
	Km	%	km	%	km	%		
Barabara kuu (lami)	5,771	72.2	1,248	15.6	971	12.2	7,990	
Barabara kuu (changarawe/udongo)	758	30.4	1,541	61.8	193	7.7	2,492	
Jumla ndogo	6,529	62.3	2,789	26.6	1,164	11.1	10,482	
Barabara za Mkoa (lami)	754	49.7	314	20.7	449	29.6	1,517	
Barabara za Mkoa (changarawe/udongo)	5,584	26.4	13,590	64.2	2,005	9.5	21,179	
Jumla ndogo	6,338	27.9	13,904	61.3	2,454	10.8	22,696	
Jumla kuu	12,867	38.8	16,693	50.3	3,618	10.9	33,178	

Chanzo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Matengenezo ya Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari

291. Mwaka 2019, jumla ya kilometra 35,813.7 za barabara kuu na za mikoa zilifanyiwa matengenezo kupitia TANROADS ikilinganishwa na kilometra 29,084.6 mwaka 2018. Aidha, madaraja 3,310 yalitengenezwa ikilinganishwa na madaraja 2,679 mwaka 2018. Kuongezeka kwa barabara na madaraja yaliyotengenezwa katika kipindi hicho kulitokana na azma ya Serikali kuendelea kuweka mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji.

292. Mwaka 2019, Serikali kupitia Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania – TEMESA ilinunua kivuko kipy cha MV Ilemela chenye uwezo wa kubeba tani 100 (sawa na abiria 200 na magari madogo 6) kwa lengo la kutoa huduma ya usafiri katika eneo la Kayenze – Bezi mkoani Mwanza. Katika kipindi hicho, abiria 26,837,846, magari 1,140,885 na mizigo kilogramu 3,585,117 ilivushwa ikilinganishwa na abiria 25,458,445, magari 1,065,970 na mizigo kilogramu 3,253,166 iliyovushwa mwaka 2018.

293. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kufanya matengenezo ya vivuko vilivyopo, kuboresha miundombinu ya maegesho ya vivuko, kujenga maegesho mapya na kukarabati karakana za magari za Mwanza na Singida. Aidha, Serikali kupitia TEMESA ilianzisha karakana ya magari katika wilaya ya Kilombero kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wateja. Vile vile, TEMESA ilitengeneza magari 29,707 ikilinganishwa na magari 29,083 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa huduma zinazotolewa na Wakala pamoja na kuongezeka kwa karakana mpya ya Kilombero.

Mtandao wa Barabara Zilizo Chini ya TARURA

294. Hadi Desemba 2019, mtandao wa barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) ulikuwa na urefu wa kilometra 108,946.2. Kati ya hizo, barabara za wilaya zenye kiwango cha lami zilikuwa na urefu wa kilometra 2,025.0, changarawe kilometra 24,493.02 na udongo kilometra 82,428.19 ikilinganishwa na kilometra 1,449.55, kilometra 24,405.40 na kilometra 83,091.24 mwaka 2018 mtawalia. **Jedwali Na.15.2** linaonesha hali ya mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA.

Jedwali Na.15.2: Hali ya mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA mwaka 2019

Aina ya Barabara	Hali ya mtandao wa Barabara (Tarura)			Jumla	Asili mia
	Nzuri	Inaridhisha	Hairidhishi		
Barabara za Lami	1,173.66	751.776	99.56	2,025.00	1.9
Barabara za Changarawe	10,309.25	9,288.20	4,895.57	24,493.02	22.5
Barabara za Udongo	13,916.49	27,747.52	40,764.18	82,428.19	75.7
Jumla	25,399.40	37,787.50	45,759.31	108,946.21	100.0

Chanzo: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

295. Hadi Desemba 2019, TARURA ilifanya matengenezo ya barabara za wilaya zenyе urefu wa kilometa 17,688.15 ikilinganishwa na kilometa 19,917.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Matengenezo hayo yalijumuisha ujenzi na ukarabati wa barabara zenyе urefu wa kilometa 39.19 kwa kiwango cha lami, kilometa 235.13 kwa kiwango cha changarawe na kilometa 17,413.83 za matengenezo maalumu na ya mara kwa mara pamoja na maeneo korofи. Katika kipindi hicho, TARURA ilijenga madaraja makubwa manne (4), madaraja madogo na makalavati 1,782, mifereji ya maji yenye urefu wa mita 44,122.72 pamoja na kukarabati madaraja 101. Vile vile, Wakala kuitia miradi ya uendelezaji wa miji na majiji iliwezesha ujenzi wa masoko ya kisasa manne, vituo vya mabasi na daladala vinne, vituo vya malori vinne, madampo ya kisasa manne, madaraja ya watembea kwa miguu 48, maeneo matatu ya mapumziko na mifereji mikubwa yenye urefu wa mita 32,940 kwa ajili ya kukabiliana na mafuriko.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

296. Mwaka 2019, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 841.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 745.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha dizeli na petroli (kinachotozwа tozo) kilichoagizwa kwa matumizi ya ndani pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na tozo za magari ya kigeni kufuatia kuongezeka kwa mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam. Aidha, Bodi ilikagua miradi ya barabara 606 ikilinganishwa na miradi 523 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa halmashauri zilizofanyiwa ukaguzi wa kiufundi kutoka halmashauri 65 mwaka 2018 hadi halmashauri 71 mwaka 2019.

Wakala wa Nyumba na Majengo ya Serikali

297. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kusimamia miradi 485 ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali ikilinganishwa na miradi 420 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa hospitali katika wilaya mbalimbali pamoja na ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba – Dodoma. Katika kipindi hicho, miradi 117 ya ukarabati wa nyumba na majengo ilisimamiwa ikilinganishwa na miradi 168 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 30.4. Upungufu huo ilitokana na idadi kubwa ya nyumba kukarabatiwa mwaka 2018, hivyo kupunguza idadi ya nyumba zilizohitaji ukarabati mwaka 2019. Aidha,

nyumba 1,499 zilipangishwa kwa watumishi wa Serikali mwaka 2019 ikilinganishwa na nyumba 1,210 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.9. Vile vile, nyumba 4,802 za biashara zilipangishwa kwa watu mbalimbali ikilinganishwa na nyumba 4,782 mwaka 2018. Kuongezeka kwa nyumba za makazi na biashara zilizopangishwa kulitokana na nyumba zilizokuwa wazi kupata wapangaji baada ya Wakala kufanya ukarabati wa nyumba na mapitio ya kodi.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

298. Mwaka 2019, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili makandarasi 925 wa fani na madaraja mbalimbali ikilinganishwa na makandarasi 832 mwaka 2018. Kutokana na usajili huo, idadi ya makandarasi waliosajiliwa hadi Desemba 2019 ilifikia 10,822 ikilinganishwa na makandarasi 9,897 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Ongezeko hilo lilitokana na Bodi kutoa elimu kuhusu umuhimu wa makandarasi kujisajili pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa makandarasi wanaofanya kazi kwenye kampuni zisizosajiliwa. Aidha, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 3,155 ikilinganishwa na miradi 3,575 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 11.7. Hii ilitokana na Bodi kutosajili miradi ambayo haifanywi na makandarasi.

299. Mwaka 2019, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi 3,717 ambapo miradi 2,633 sawa na asilimia 70.8 haikuwa na mapungufu na miradi 1,084 (asilimia 29.2) ilikuwa na mapungufu. Mapungufu hayo yalijumuisha: miradi kutekelezwa na watu ambao hawajasajiliwa; miradi kutosajiliwa; kutowekwa bango la mradi; kutozingatia sheria ya afya na usalama wa wafanyakazi; na makandarasi kutekeleza miradi ambayo haiendani na fani na madaraja yao. Hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya makandarasi wa miradi iliyokuwa na mapungufu ni pamoja na kutozwa faini, kusimamishwa kwa muda na wahusika kushtakiwa. Aidha, Bodi iliwaapeleka mahakamani watuhumiwa 72 waliokuwa na makosa mbalimbali ikiwemo kutekeleza miradi kwa kutumia kampuni au watu wasio makandarasi ikilinganishwa na watuhumiwa 52 mwaka 2018.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

300. Mwaka 2019, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili jumla ya wahandisi 26,918 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 23,416 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu wengi

kujisajili kufuatia kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi zinazohusu taaluma ya uhandisi hasa viwanda vya uzalishaji, ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kati ya wahandisi waliosajiliwa, 24,638 sawa na asilimia 91.5 walikuwa watanzania na wahandisi 2,280 walikuwa wageni. Aidha, mafundi sanifu waliosajiliwa na Bodi waliongezeka na kufikia 359 kutoka mafundi 333 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa miradi mikubwa inayotekelizwa na Serikali pamoja na Bodi kuendelea kudhibiti mafundi sanifu wasiokuwa na usajili kufanya kazi kwenye miradi.

301. Mwaka 2019, Bodi ilisajili kampuni za ushauri 354 ikilinganishwa na kampuni 333 mwaka 2018. Kati ya hizo, kampuni 242 zilikuwa za kitanzania na kampuni 112 za kigeni. Aidha, Wahandisi washauri 578 walisajiliwa na Bodi mwaka 2019 ikilinganishwa na wahandisi washauri 556 mwaka 2018. Kati ya hao, wahandisi washauri 439 walikuwa watanzania na 139 walikuwa wageni. Kuongezeka kwa usajili wa kampuni na wahandisi washauri kulitokana na kuongezeka kwa miradi ya kiuhandisi na kampuni za kigeni ambazo huja na wahandisi washauri. Kwa upande mwingine, Bodi ilisajili maabara 34 za vifaa vya ujenzi na uhandisi mwaka 2019 ikilinganishwa na maabara 29 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuanzishwa kwa utaratibu unaozitaka kampuni zinazotoa huduma za maabara ya vifaa vya ujenzi na uhandisi kujisajili.

302. Mwaka 2019, wahandisi 7,259 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 5,814 mwaka 2018. Kati ya hao, wahandisi 3,551 walihitimu na kusajiliwa kama wahandisi wataalamu ikilinganishwa na wahandisi 3,253 mwaka 2018. Aidha, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 649 na kukagua miradi 88 mwaka 2019 ikilinganishwa na usajili wa miradi 769 na ukaguzi wa miradi 124 mwaka 2018.

Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

303. Mwaka 2019, Bodi ilisajili wataalamu 1,098 ikilinganishwa na wataalamu 1,021 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Kati ya wataalamu waliosajiliwa, 1,064 walikuwa watanzania na 34 walikuwa wageni. Aidha, Bodi ilisajili kampuni 387 za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi (378 za kitanzania na 9 za kigeni) ikilinganishwa na kampuni 368 mwaka 2018, sawa na

ongezeko la asilimia 5.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na waendelezaji majengo kuendelea kutumia huduma za wataalamu waliosajiliwa na Bodi.

304. Mwaka 2019, Bodi ilikagua miradi ya majengo 1,617 ikilinganishwa na miradi 1,666 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Aidha, miradi 816 ya ujenzi wa majengo ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 885 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 7.8. Kupungua kwa usajili na ukaguzi miradi ya majengo kulitokana na waendelezaji majengo wengi kutoelewa faida ya kutumia wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika kuendeleza miradi ya ujenzi. Kwa upande mwingine, wahitimu 47 walihudhuria mafunzo kwa vitendo katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ikilinganishwa na wahitimu 106 mwaka 2018. Kupungua kwa wahitimu waliohudhuria mafunzo kulitokana na baadhi ya wahitimu kupata ajira za kudumu na wengine kwenda masomoni.

Baraza la Taifa la Ujenzi

305. Mwaka 2019, Baraza la Taifa la Ujenzi lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 43 ikilinganishwa na miradi 199 mwaka 2018. Upungufu wa miradi iliyokaguliwa ultokana na kuwepo kwa mikataba michache ya miradi iliyopatikana mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Baraza lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau nane (8) wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau sita (6) mwaka 2018. Aidha, Baraza lilifanya usuluhishi wa migogoro ya ujenzi 78 ikilinganishwa na migogoro 153 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 49.0. Kupungua kwa usuluhishi wa migogoro kulitokana na Taasisi ya Usuluhishi Tanzania na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakaridiaji Majenzi kuanza kutoa huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ujenzi. Vile vile, Baraza lilitoa mafunzo kwa wadau 69 wa sekta ya ujenzi mwaka 2019 ikilinganishwa na wadau 36 mwaka 2018. Mafunzo hayo yalijumuisha fani mbalimbali za ujenzi zikiwemo usimamizi wa mikataba, usuluhishi wa migogoro na ukaguzi wa kiufundi wa miradi. Kupungua kwa wadau waliopata mafunzo kulitokana na mwitikio mdogo wa kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na Baraza.

MAENDELEO YA ARDHI

Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi, na Uhakiki Milki

306. Mwaka 2019, Serikali iliandaa hatimiliki 53,872 za viwanja na mashamba ikilinganishwa na hatimiliki 61,987 mwaka 2018. Aidha, ilani za ubatilisho zilizotumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji zilipungua hadi

2,598 kutoka ilani 3,500 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, hatimiliki za kimila 238,839 zilitolewa mwaka 2019 ikilinganishwa na hatimiliki 186,186 mwaka 2018. Kuongezeka kwa utoaji wa hatimiliki za kimila kulitokana na utekelezaji madhubuti wa programu ya kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria

307. Mwaka 2019, Serikali ilisajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 92,512 ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 93,706 mwaka 2018. Kati ya hizo, hati za kumiliki ardhi 47,948 zilisajiliwa ikilinganishwa na hati za kumiliki ardhi 41,522 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kusajili hatimiliki. Aidha, nyaraka 15,018 za kisheria zilisajiliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na nyaraka 27,716 mwaka 2018.

Jedwali Na.15.3: Usajili wa Hati Miliki na Nyaraka za Kisheria

Hati na Nyarakazilizosajiliwa	2015	2016	2017	2018	2019
Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334)	31,254	33,257	21,743	41,522	47,948
Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (<i>Unit Title Act No.17/2008</i>).	1,541	1,410	827	844	321
Nyaraka za Kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura Na. 334).	29,546	34,682	13,821	27,716	15,018
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura. 117).	13,041	20,525	13,027	21,807	26,096
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika (Sura 210).	2,082	1,313	310	1,817	3,129
Jumla	77,464	91,187	49,728	93,706	92,512

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Uthamini wa Mali kwa Madhumuni Mbalimbali

308. Mwaka 2019, taarifa 19,669 za uthamini ziliidhinishwa ikilinganishwa na taarifa 26,096 mwaka 2018. Idadi hii ilijumuisha taarifa zilizopokelewa kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kampuni binafsi za uthamini pamoja na taarifa za tathmini zilizofanywa na Serikali Kuu. Madhumuni ya uthamini huo yalijumuisha: kuwezesha ulipaji wa fidia; utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali; utozaji wa malipo ya awali wakati wa kutoa miliki; kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo; upatikanaji wa mirathi; kinga ya bima; na utozaji wa kodi ya pango la ardhi.

Upimaji wa Mashamba na Viwanja

309. Mwaka 2019, ramani zenye viwanja 322,709 na mashamba 717 ziliidhinishwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 235,752 na mashamba 2,159 mwaka 2018. Kuongezeka kwa ramani zenye viwanja zilizoidhinishwa kulitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa programu ya kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. **Jedwali Na. 15.4** linaonesha mchanganuo wa viwanja na mashamba yaliyoidhinishwa katika mikoa.

Jedwali Na.15.4: Milki ya Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa

Mikoa	2017		2018		2019	
	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba
Arusha	1,392	18	3,547	17	4,193	25
Pwani	36,974	107	18,108	1,010	12,706	41
DSM	28,079	0	19,096	0	23,617	0
Dodoma	3,622	5	38,230	0	105,809	0
Geita	5,279	0	4,176	0	13,659	4
Iringa	4,531	26	4,222	9	2,825	4
Kagera	2,959	2	6,160	25	4,420	18
Katavi	2,858	1	1,912	0	2,599	
Kigoma	1,893	2	3,201	835	1,946	9
Kilimanjaro	1,532	36	1,612	20	1,963	13
Lindi	7,253	0	3,113	15	8,530	0
Manyara	1,668	86	3,375	4	3,439	0
Mara	2,326	16	3,003	5	6,299	1
Mbeya	3,473	17	5,015	9	1,493	5
Morogoro	5,298	73	12,050	138	11,936	7
Mtwara	4,737	1	4,413	0	9,325	3
Mwanza	22,910	0	45,494	8	33,288	0
Njombe	2,870	6	5,088	60	4,316	9
Ruvuma	1,112	0	2,513	0	6,967	0
Rukwa	2,388	9	792	4	2,184	59
Simiyu	2,720	14	3,521	0	8,948	1
Singida	8,934	8	7,233	0	8,942	0
Songwe	98	1	4,489	0	4,381	3
Shinyanga	5,028	0	22,128	0	17,366	0
Tabora	4,265	1	3,047	0	6,516	0
Tanga	6,223	26	10,214	0	15,042	515
Jumla	170,422	455	235,752	2,159	322,709	717

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mipango ya Matumizi ya Ardhi

310. Mwaka 2019, Serikali iliandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 431 katika wilaya 67 ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 125 ilioandaliwa katika wilaya 23 mwaka 2018. Idadi ya vijiji kwa mikoa husika ni kama ifuatavyo: Arusha vijiji 38, Kagera (29), Manyara (23), Njombe (6), Ruvuma (18), Tanga (36), Tabora (20), Singida (24), Mwanza (3), Geita (32), Iringa (6), Shinyanga (2), Dodoma (26), Simiyu (16), Mara (34), Kigoma (11), Mbeya (13), Morogoro (68), Pwani (4), Lindi (18) na Mtwara (4).

Urasimishaji Makazi Holela

311. Mwaka 2019, michoro ya mipangomiji 1,188 iliandaliwa na kuidhinishwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara ikilinganishwa na michoro 1,285 mwaka 2018. Aidha, vipande 232,717 vya ardhi vilirasimishwa katika halmashauri mbalimbali kupitia Programu ya Urasimishaji na Udhibiti wa Makazi holela ikilinganishwa na vipande 126,504 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 84.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kampuni za upangaji na upimaji ardhi zilizosajiliwa.

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

312. Mwaka 2019, mashauri mapya 24,428 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 23,002 mwaka 2018. Idadi hiyo inafanya jumla ya mashauri yaliyokuwa yanafanyiwa kazi hadi Desemba 2019 kufikia 51,951. Kati ya hayo, mashauri 26,090 yaliamuliwa na mashauri 25,861 yaliendelea kusikilizwa. Katika kipindi hicho, migogoro 4,186 ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kiutawala ikilinganishwa na migogoro 6,499 mwaka 2018. Aidha, vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa ndani ya maeneo ya hifadhi na mapori vilihalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

MAENDELEO YA MAKAZI

Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara

313. Hadi Desemba 2019, nyumba 6,112 zilijengwa na Shirika la Nyumba la Taifa katika halmashauri mbalimbali nchini ambapo nyumba 1,617 zilijengwa kwa ajili ya ofisi na biashara, nyumba 3,036 za makazi na biashara na nyumba 1,459 za makazi. Kati ya nyumba za makazi zilizojengwa, nyumba 1,185 zilikuwa za gharama nafuu na nyumba 274 zilikuwa za gharama ya kati na juu. Aidha, Watumishi Housing Company ilijenga nyumba 845 mwaka 2019 ikilinganishwa na nyumba 98 mwaka 2018. Ongezeko la nyumba zilizojengwa lilitokana na kukamilika kwa miradi ya ujenzi iliyokuwa ikitekelezwa tangu mwaka 2015.

SURA YA 16

MAWASILIANO NA UCHUKUZI

UCHUKUZI

Usafiri wa Barabara

314. Mwaka 2019, idadi ya leseni za vyombo vya usafirishaji zilizotolewa ziliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia 202,149 ikilinganishwa na leseni 176,282 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutumia mfumo wa TEHAMA katika utoaji leseni, kutoa adhabu kwa watoa huduma wasio na leseni/wenye leseni zilizoisha muda wa matumizi na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni. Mchanganuo wa leseni zilizotolewa ni kama unavyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 16.1**.

Jedwali Na. 16. 1: Mchanganuo wa Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa

Leseni	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Mabasi ya Abiria	46,612	46,449	60,344	29.9
Magari ya Mizigo	99,484	113,345	123,460	8.9
Bajaji/Pikipiki	14,819	16,488	18,345	11.3
Jumla	160,915	176,282	202,149	14.7

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu

315. Mwaka 2019, ajali za vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa upande wa barabara zilikuwa 1,340 ikilinganishwa na ajali 1,965 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 31.8. Upungufu huo ulichangiwa na matumizi ya mfumo wa udhibiti mwendo wa mabasi, upimaji ulevi kwa madereva, matumizi ya madereva wawili kwa safari zilizozidi masaa nane na kaguzi za mara kwa mara zilizoambatana na kufungiwa kwa mabasi yasiyo na ubora wa kutembea barabarani. **Jedwali Na. 16.2** linaonesha mchanganuo wa idadi ya ajali kwa vyombo vya usafiri.

Jedwali Na.16.2: Mchanganuo wa Ajali za Barabarani

Ajali	2017	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Mabasi	842	620	442	-28.7
Malori	607	469	331	-29.4
Pikipiki/Bajaji	1,459	876	567	-35.3
Jumla	2,908	1,965	1,340	-31.8

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu

Usafiri wa Majini

316. Mwaka 2019, leseni 824 za uwakala wa ugomboaji wa shehena zilitolewa ikilinganishwa na leseni 662 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 24.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa fursa za utoaji wa huduma pamoja na mawakala kuzingatia vigezo na masharti ya kujisajili. Aidha, leseni za uwakala wa meli zilipungua kutoka 29 mwaka 2018 hadi leseni 27 mwaka 2019. Kupungua kwa idadi ya leseni za uwakala wa meli kulitokana na baadhi ya waombaji wa leseni kutotimiza masharti yaliyowekwa.

Jedwali Na. 16.3: Utoaji Leseni

Aina ya leseni	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Ugomboaji wa shehena	662	824	24.5
Uwakala wa Meli	29	27	-6.9
Wakusanyaji mizigo	29	28	-3.4
Bandari Kavu	28	27	-3.6

Chanzo: Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

317. Mwaka 2019, hali ya usalama wa huduma za usafiri na usafirishaji majini iliendelea kuimarika ambapo ajali za majini zilipungua hadi 15 kutoka ajali 18 mwaka 2018. Kupungua kwa ajali kulichangiwa na utoaji wa elimu ya usalama kwa wamiliki na watumiaji wa vyombo vya majini kuititia mikutano mbalimbali na uzingatiaji wa masharti ya usalama wa utoaji wa huduma za usafiri wa majini. Katika kipindi hicho, mikutano 149 ya uelimishaji kuhusu usalama wa vyombo vya majini ilifanyika ikilinganishwa na mikutano 138 mwaka 2018. Aidha, kagazi 369 zilifanyika kwa meli zenye ukubwa wa zaidi ya tani 50 na kagazi 6,539 kwa meli zenye ukubwa wa chini ya tani 50 mwaka 2019 ikilinganishwa na

kaguzi 290 kwa meli zenyenye ukubwa wa zaidi ya tani 50 na kaguzi 6,127 kwa meli zenyenye ukubwa wa chini ya tani 50 mwaka 2018.

Usafiri wa Reli

Shirika la Reli Tanzania

318. Mwaka 2019, Shirika la Reli Tanzania lilisafirisha shehena ya mizigo tani 355,079 kwa umbali wa kilometra 366,119,797 ikilinganishwa na tani 379,321 kwa umbali wa kilometra 375,901,609 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 6.4. Katika kipindi hicho, abiria 492,423 walisafirishwa kwa umbali wa kilometra 428,739,684 ikilinganishwa na abiria 589,608 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometra 404,296,156 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 16.5. Upungufu wa usafirishaji wa shehena za mizigo na abiria ulitokana na ukarabati wa njia ya reli ya kati uliosababisha kupungua kwa safari za treni kwa wiki.

319. Mwaka 2019, Shirika lilisafirisha abiria 3,577,313 kwa umbali wa kilometra 114,474,016 katika Jiji la Dar es Salaam ikilinganishwa na abiria 5,382,497 kwa umbali wa kilometra 172,239,904 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 33.5. Upungufu huo ulitokana na kuanza kutumika kwa daraja la juu la Mfugale lililochangia kupunguza foleni ya magari na hivyo watu kuhamasika kutumia magari binafsi na usafiri wa umma.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

320. Mwaka 2018/19, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ilisafirisha tani 175,599 za mizigo ikilinganishwa na tani 220,818 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 20.5. Upungufu huo ulitokana na nchi ya Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuanzisha kodi mpya ya kusafirisha madini kulikosababisha wafanyabiashara wengi kusitisha biashara ya kusafirisha baadhi ya madini yakiwemo *manganese* na shaba.

Jedwali Na.16.4: Shehena ya Mizigo iliyosafirishwa Mwaka 2019

Aina ya Mizigo	2017/18	2018/19	Badiliko (Asilimia)
Kwenda nje ya nchi	99,491	68,253	-31.4
Kutoka nje ya nchi	88,067	86,240	-2.1
Ndani ya TAZARA	33,260	21,106	-36.54
Jumla	220,818	175,599	-20.5

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia


321. Mwaka 2018/19, TAZARA ilisafirisha jumla ya abiria 494,059 wa njia kuu ikilinganishwa na abiria 543,196 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 9.0. Aidha, treni ya Udzungwa ilisafirisha abiria 396,895 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na abiria 393,570 mwaka 2017/18. Kwa upande wa treni ya Jijini Dar es Salaam, TAZARA ilisafirisha abiria 2,155,048 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na abiria 2,418,807 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 10.9. Upungufu huo ilitokana na uchache wa mabehewa ya abiria, kuongezeka kwa ushindani baada ya Shirika la Reli Tanzania kuanzisha safari ya kwenda Pugu ambayo ni sambamba na safari ya TAZARA ya kwenda Mwakanga.

Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga

322. Mwaka 2019, ndege 15 zilisajiliwa kwa mara ya kwanza ikilinganishwa na ndege 13 zilizosajiliwa mwaka 2018. Katika kipindi hicho, ndege 49 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora ikilinganishwa na ndege 36 mwaka 2018. Hadi Desemba 2019, mashirika 22 ya ndege ya kimataifa yalikuwa yanatoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine ikilinganishwa na mashirika 28 mwaka 2018. Upungufu huo ilitokana na baadhi ya mashirika ya ndege kutohuisha leseni zao. Aidha, idadi ya abiria waliowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege nchini iliongezeka hadi abiria 5,487,679 mwaka 2019 kutoka abiria 5,187,662 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa miruko ya ndege kwa wiki, uimarishwaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege na kuongezeka kwa shughuli za utalii nchini.


Kielelezo Na.16.1: Idadi ya Abiria Waliowasili na Kuondoka Nchini



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga


323. Mwaka 2019, safari za ndege ziliongezeka kwa asilimia 18.7 na kufikia 292,105 kutoka safari 246,072 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ndege za Shirika la ATCL. Aidha, mizigo iliyosafirishwa iliongezeka na kufikia tani 28,202 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 27,910 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilichangiwa na uingizaji wa mitambo ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu ikiwemo reli ya kati ya kisasa pamoja na biashara ya mboga na maua kwenda nje ya nchi.

Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga

Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga

Kampuni ya Ndege Tanzania

324. Mwaka 2019, Kampuni ya Ndege Tanzania ilikuwa na vituo 13 vya kutolea huduma ndani ya nchi ikilinganishwa na vituo 11 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, kampuni ilifanya safari katika vituo vya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Tabora, Zanzibar, Iringa na Mpanda. Kwa upande mwingine, safari za ndege za ATCL kwenda nje ya nchi ziliongezeka na kufikia vituo sita mwaka 2019 ikilinganishwa na vituo vitatu

mwaka 2018. Vituo hivyo vilikuwa Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Lusaka (Zambia), Bujumbura (Burundi), Harare (Zimbabwe) na Mumbai (India). Vile vile, abiria waliosafiri kwa ndege za ATCL waliongezeka na kufikia 703,610 mwaka 2019 ikilinganishwa na abiria 338,286 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuboreshwa kwa huduma za Kampuni pamoja na kuongezeka kwa miruko na idadi ya ndege katika vituo vya kikanda.

325. Mwaka 2019, Kampuni ilisafirisha mizigo tani 1,710.2 ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 453.8 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilichangiwa na uanzishwaji wa safari za vituo vya nje ya nchi ikiwemo Mumbai. Aidha, ATCL ilitoa huduma ya usafiri wa anga kwa kutumia ndege nane (8) mwaka 2019 ikilinganishwa na ndege tano (5) mwaka 2018.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

326. Mwaka 2018/19, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena ya mizigo tani milioni 17.1 ikilinganishwa na tani milioni 16.2 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Ongezeko hilo lilitokana na Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia mizigo mingi ya miradi ya maendeleo. **Jedwali Na. 16.5** linaonesha shehena iliyohudumiwa na Mamlaka.

Jedwali Na. 16.5: Shehena Zilizosafirishwa (Tani `000)

Kituo (Bandari)	2016/17	2017/18	2018/19	Badiliko (Asilimia)
Bandari Kuu za Mwambao				
Dar es Salaam	13,561.00	14,863.00	15,950.00	7.3
Tanga	486	646.7	668	3.3
Mtwara	378	363.3	106	-70.8
Jumla ndogo	14,425.00	15,873.00	16,724.00	5.4
Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu				
Kilwa, Lindi na Mafia	41	17.6	32.1	82.4
Mwanza	124	84.6	158	86.8
Kigoma	137	196.8	199.9	1.6
Kyela	6	0.4	5.7	1325.0
Jumla ndogo	308	299.5	395.7	32.1
Jumla Kuu	14,733.00	16,172.50	17,119.70	5.9

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

327. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kupitia kitengo cha mizigo ya kawaida ilihudumia kontena zenyne urefu wa futi ishirini 120,904 (TEUs) mwaka 2018/19 ikilinganishwa na kontena 117,529 (TEUs) mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Aidha, kitengo cha kontena cha TICTS kilihudumia kontena 584,157 (TEUs) mwaka 2019 ikilinganishwa na kontena 535,515 (TEUs) zilizohudumiwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Kuongezeka kwa kontena zilizohudumiwa na Mamlaka kulitokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo hutumia kontena kusafirishia vifaa na mitambo ya ujenzi.

Jedwali Na. 16.6: Shehena ya Kontena (TEUs) - Bandari ya Dar es Salaam

	2016/17	2017/18	2018/19	Badiliko (Asilimia)
TICTS	445,493	535,515	584,157	9.1
General Cargo	108,088	117,529	120,904	2.9
Jumla Ndogo	553,581	653,044	705,061	8.0
Tanga	8,048	7,158	6,259	-12.6
Mtvara	30,371	35,778	4,064	-88.6
Jumla Ndogo	38,419	42,936	10,323	-76.0
Jumla Kuu	592,000	695,980	715,384	2.8

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

328. Mwaka 2018/19, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia abiria 2,521,512 ikilinganishwa na abiria 2,185,084 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Katika kipindi hicho, abiria waliohudumiwa na Mamlaka waliongezeka katika bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza na Kyela wakati abiria waliohudumiwa katika bandari ya Kigoma walipungua kutokana na meli ya abiria ya Mv. Liemba kuwa kwenye matengenezo.

Jedwali Na. 16.7: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa

Bandari	2016/17	2017/18	2018/19	Badiliko (Asilimia)
Dar es Salaam	1,848,937	1,884,125	1,950,487	3.5
Tanga	10508	45820	60,241	31.5
Mwanza	165,098	246,462	504,481	104.7
Kigoma	9,895	7,710	4,628	-40.0
Kyela	3,415	967	1,675	73.2
Jumla	2,037,853	2,185,084	2,521,512	15.4

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Muda wa Meli Kukaa Bandarini

329. Muda wa meli kukaa bandarini kwa kitengo cha kontena uliongezeka na kufikia siku 2.5 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na siku 1.8 mwaka 2017/18. Hii ilitokana na ujenzi unaoendelea wa gati namba 5 na namba 7 katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo kusababisha meli kusubiriana. Kwa upande wa mizigo ya kawaida, muda wa meli kukaa bandarini ulipungua na kufikia siku 2.7 ikilinganishwa na siku 3.3 mwaka 2017/18. Katika kitengo cha mafuta, muda wa meli kukaa bandarini uliongezeka na kufikia siku 5.3 mwaka 2018/19 ikilinganishwa na siku 3.3 mwaka 2017/18. Aidha, muda wa mizigo ya kontena kukaa bandarini baada ya kupakuliwa kutoka melini na kabla ya mteja kuchukua ulikuwa wastani wa siku 10.5 mwaka 2018/19 kama ilivyokuwa mwaka 2017/18.

Shehena za Nchi Jirani

330. Mwaka 2018/19, shehena ya mizigo kwenda nchi jirani iliyohudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ilikuwa tani 5,576,367 ikilinganishwa na tani 5,604,605 mwaka 2017/18. Kupungua kwa shehena ya mizigo kulitokana na hali ya uchumi wa Zambia iliyochangia kupungua kwa usafirishaji wa shaba na uagizaji wa mbolea. Hata hivyo, shehena ya mizigo kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo iliongezeka kwa asilimia 42.7 na Rwanda kwa asilimia 15.0. Mchanganuo wa shehena kwenda nchi jirani ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na.16.8.**

Jedwali Na.16.8: Shehena ya Mizigo kwenda Nchi Jirani (Tani)

Nchi	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	Badiliko (Asilimia)
Zambia	1,819,069	1,705,659	2,053,174	1,663,499	-19.0
J.D. Kongo	1,464,847	1,141,611	1,370,078	1,954,626	42.7
Burundi	351,044	363,060	425,300	378,874	-10.9
Rwanda	839,826	1,012,889	922,134	1,060,809	15.0
Malawi	106,883	217,852	258,271	320,399	24.1
Uganda	156,105	239,953	215,878	167,270	-22.5
Nyinginezo	101,693	104,195	359,770	30,889	-91.4
Jumla	4,839,467	4,785,219	5,604,605	5,576,367	-0.5

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Uchukuzi Kwenye Maziwa

Kampuni ya Huduma za Meli

331. Abiria waliosafirishwa na Kampuni ya Huduma za Meli walipungua kwa asilimia 13.7 na kufikia 96,892 mwaka 2019 kutoka abiria 112,222 mwaka 2018. Hii ilitokana na meli ya MV. Liemba kusimama kutoa huduma na idadi kubwa ya meli zikiwa katika mpango wa kufanyiwa ukarabati mkubwa. Aidha, tani 34,304.4 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 25,081 zilizosafirishwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 36.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na MV. Umoja kuanza kusafirisha shehena za mizigo kutoka Mwanza kwenda Sudan Kusini kupitia Uganda na MT. Sangara kusafirisha mafuta kutoka Kigoma kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kampuni ya Meli ya China na Tanzania

332. Kampuni ya Meli ya China na Tanzania - SINOTASHIP ilisafirisha shehena ya mizigo tani 600,000 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 598,000 mwaka 2018. Kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyosafirishwa kulitokana na SINOTASHIP kuendelea kushirikiana na Kampuni ya COSCO Bulk Carrier yenyeye uzoefu na uwezo mkubwa katika masuala ya usafirishaji wa shehena duniani. Aidha, makasha 47,000 yalihudumiwa na Kampuni katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na makasha 41,000 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Ongezeko hilo lilitokana na Kampuni kuendelea kujitangaza na kutafuta masoko ya mizigo inayosafirishwa nje ya Tanzania.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

333. Mwaka 2019, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliendelea kutumia mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma ya hali ya hewa kwa sekta mbalimbali ikiwemo usafiri wa maji na anga. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilitoa huduma ya hali ya hewa katika Bahari ya Hindi kwa meli na boti 4,285 ikilinganishwa na meli na boti 3,167 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 35.3. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia huduma ya hali ya hewa kwa ajili ya usalama wa usafiri wa majini. Wateja na watumiaji wa huduma ya hali ya hewa waliongezeka na kufikia 50,882 mwaka 2019 ikilinganishwa na wateja na watumiaji 48,075 mwaka 2018. Aidha, kiwango cha usahidi wa utabiri kilifiki asilimia 84.5 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 89.8 mwaka 2018. Hicho ni kiwango cha zaidi ya asilimia 70 kinachokubalika kimataifa.

Jedwali Na. 16.9: Viashiria vya Ufanisi katika Sekta ya Hali ya Hewa

Viashiria vya Ufanisi	Mwaka		
	Maelezo	2018	2019
Kiwango cha usahihi wa utabiri wa siku na msimu (asilimia)	Usahihi wa utabiri	89.8	84.5
Idadi ya wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa	Sekta ya usafiri wa anga	44,287	45,966
	Meli na boti	3,167	4,285
	Huduma mahsusii	621	631
Kiwango cha watumiaji na wateja wanaoridhika na huduma za hali ya hewa (asilimia)	Kiwango cha kuridhika	89.0	90.0

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Udhibiti wa Mionzi

334. Mwaka 2019, Serikali kuitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 439 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi 376 mwaka 2018. Kati ya hayo, maombi 435 yalipata vibali baada ya kukidhi matakwa na vigezo vya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003 ikilinganishwa na maombi 371 mwaka 2018. Aidha, Tume ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 1,213 kutoka katika vituo 390 mwaka 2019 ikilinganishwa na wafanyakazi 1,100 kutoka vituo 320 mwaka 2018. Matokeo ya upimaji huo yalionesha kuwa kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi ndani ya miezi mitatu kilikuwa chini ya *mSv* 5 ambacho kinakubalika kimataifa. Hadi Desemba 2019, vituo vinavyotumia mionzi vilifikia 952 kutoka vituo 900 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kwa upande mwingine, Tume ilikagua vituo 650 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira mwaka 2019 ikilinganishwa na vituo 546 vilivyokaguliwa mwaka 2018.

335. Mwaka 2019, Tume iliendelea kudhibiti usalama wa mionzi katika bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi. Katika kipindi hicho, Tume ilipima viwango vya mionzi kwenye sampuli 7,873 ambapo sampuli za mbolea zilikuwa 143, sigara 220, wanyama 751 na chakula 6,759. Kati ya sampuli za chakula zilizopimwa, sampuli 2,883 ziliingizwa nchini na sampuli 3,876 zilisafirishwa nje ya nchi.

HUDUMA ZA MAWASILIANO

Huduma za Posta

336. Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 6,855,626 ndani ya nchi mwaka 2019 ikilinganishwa na barua 12,059,221 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 43.2. Aidha, barua 2,187,254 zilisafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na barua 3,737,816 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 41.5. Kupungua kwa barua zilizosafirishwa kulitokana na kuongezeka kwa ushindani katika usafirishaji wa barua pamoja na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

337. Idadi ya vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi ilikuwa 40,629 mwaka 2019 ikilinganishwa na vifurushi 72,433 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 43.9. Aidha, vifurushi 3,304 vilitumwa nje ya nchi ikilinganishwa na vifurushi 6,623 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 50.1. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa kampuni zinazosafirisha vifurushi ndani na nje ya nchi. Kwa upande mwingine, rejestra 160,290 zilisafirishwa nchini mwaka 2019 ikilinganishwa na rejestra 464,377 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 65.5. Rejestra zilizotumwa nje ya nchi ziliwuwa 17,490 ikilinganishwa na rejestra 40,453 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 56.8. Hii ilitokana na kupungua kwa taasisi zinazotumia huduma ya posta kutokana na utumiaji wa teknolojia mbadala.

338. Idadi ya nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka (EMS) nchini ilikuwa 615,663 mwaka 2019 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 753,278 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 18.3. Aidha, nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka vilipungua kwa asilimia 15.5 na kufikia 14,206 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 16,803 mwaka 2018. Barua na nyaraka 57,716 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua kwa haraka ndani ya majiji na miji ikilinganishwa na barua na nyaraka 67,193 mwaka 2018.

339. Mwaka 2019, miamala ya fedha iliyohaulishwa kwa njia ya kielektroniki iliongezeka kwa asilimia 28.5 na kufikia 808 ikilinganishwa na miamala 629 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, miamala ya fedha iliyotumwa kwa mfumo wa kimataifa wa utumaji fedha ilikuwa 1,211 ikilinganishwa na miamala 704 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 72.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vituo vya utumaji fedha na kufikia 168 mwaka 2019 kutoka vituo 46 mwaka 2018.

Aidha, wateja 18,198 walihudumiwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ndani ya nchi kwa njia ya *PostGiro* ikilinganishwa na wateja 170,606 mwaka 2018. Kupungua kwa wateja kulitokana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kusitisha kutumia huduma ya *PostGiro* kulipa pensheni kwa wastaaifu.

Huduma za Simu

340. Idadi ya kadi za simu za kiganjani ilifikia 47,761,520 mwaka 2019 ikilinganishwa na kadi 43,621,499 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Hii ilitokana na kukua kwa huduma za mtandao ya kijamii na kuongezeka kwa matumizi ya simu katika kufanya miamala ya kifedha. Aidha, kadi za simu za mezani zilipungua kwa asilimia 38.6 na kufikia 76,288 kutoka kadi 124,238 mwaka 2018. Hadi Desemba 2019, kadi za simu za kiganjani zilizosajiliwa kwa alama za vidole ziliwu 24,021,757.

341. Mwaka 2019, ghamama za kupiga simu ndani ya mtandao zilipungua kwa asilimia 65.1 na kufikia shilingi 87 kwa dakika kutoka shilingi 249 mwaka 2018. Ghamama za kupiga simu nje ya mtandao zilipungua kwa asilimia 70.6 na kufikia shilingi 94 kwa dakika mwaka 2019 kutoka shilingi 320 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, ghamama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki ilikuwa shilingi 732 kwa dakika mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi 731 mwaka 2018. Ghamama za kupiga simu kwenda mataifa mengine ziliwu shilingi 1,439 kwa dakika mwaka 2019 ikilinganishwa na shilingi 1,443 mwaka 2018.

Huduma za Intaneti

342. Watumiaji wa huduma za intaneti waliongezeka kwa asilimia 11.5 na kufikia milioni 25.8 mwaka 2019 kutoka watumiaji milioni 23.1 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa utoaji wa huduma mbalimbali kwa njia ya intaneti.

Jedwali Na. 16.10: Matumizi ya Intaneti Nchini

Aina ya huduma	2018	2019	Badiliko (asilimia)
Fixed wireless	135,954	773,837	469.2
Mobile wireless	22,281,727	24,762,778	11.1
Fixed wired	725,279	257,946	-64.4
Jumla	23,142,960	25,794,561	11.5

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Huduma za Utangazaji

343. Watumiaji wa huduma za utangazaji kwa kutumia ving'amuzi walifikia 2,683,513 mwaka 2019 ikilinganishwa na watumiaji 2,769,841 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 3.1. Aidha, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia *Satellite* waliongezeka kwa asilimia 10.9 mwaka 2019 na kufikia 1,092,891 kutoka watumiaji 985,594 mwaka 2018. Mchanganuo wa watumiaji wa huduma za utangazaji ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 16.11**

Jedwali Na. 16.11: Watumiaji wa Huduma za Utangazaji

Aina	2018	2019	Badiliko (Asilimia)
Digital Terrestrial Television	1,626,023	1,432,398	-11.9
Satellite	985,594	1,092,891	10.9
Cable	158,224	158,224	0
Jumla	2,769,841	2,683,513	-3.1

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Utoaji wa Leseni za Mawasiliano

344. Mamlaka ya Mawasiliano ilitoa leseni 1,507 za huduma mbalimbali za mawasiliano mwaka 2019 ikilinganishwa na leseni 583 mwaka 2018. Kuongezeka kwa utoaji wa leseni kulitokana na uhitaji mkubwa wa leseni zinazotoa kibali cha kutumia ungo ndogo kupokea mawasiliano kupitia jukwaa la *Satellite* (V-SAT) pamoja na kuongezeka kwa huduma mbalimbali za kidigitali. **Jedwali Na. 16.12** linaonesha mchanganuo wa aina za leseni kwa huduma mbalimbali za mawasiliano.

Jedwali Na. 16.12: Leseni Zilizotolewa Mwaka 2019

Aina ya Leseni	2018	2019
Leseni za kusimika vifaa vya mawasiliano	0	1
Leseni za huduma za mawasiliano	3	15
Leseni za maudhui ya redio	9	22
Leseni za maudhui ya televisheni	2	6
Leseni za ufungaji na utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki	25	67
Leseni za kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki	12	42
Leseni za kusambaza nchini vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki	5	23
Leseni za kuuza vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki	266	321
Leseni za huduma ya msingi ya posta	0	1
Leseni za huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto	5	90
Leseni za V-SAT	3	571
Leseni ya maudhui ya mtandaoni	231	330
<i>Content by subscription (cable)</i>	22	18
Jumla	583	1,507

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

345. Hadi Desemba 2019, viji ni mitaa 14,257 iliunganishwa na huduma ya mawasiliano ikilinganishwa na viji ni mitaa 13,432 mwaka 2018. Aidha, kuitia watoa huduma binafsi, miundombinu ya mawasiliano ilifikishwa katika ofisi 150 za halmashauri mwaka 2019. Maeneo mengine ambayo yalishafikishiwa miundombinu ya mawasiliano ni pamoja na vituo 66 vya posta; vituo 121 vya polisi; hospitali za wilaya 150; mahakama 26; na shule za sekondari. Vile vile, Serikali iliendelea kuboresha uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu (Dar es Salaam) na kuendelea na kazi ya usanifu wa ujenzi wa vituo viwili vya Taifa vya kuhifadhi kumbukumbu katika maeneo ya Dodoma na Zanzibar.

Sekta ya Habari

346. Hadi Desemba 2019, kulikuwa na magazeti 226, vituo vya redio 183 na vituo vya televisheni 43 ikilinganishwa na magazeti 201, vituo vya redio 162 na vituo vya televisheni 35 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Magazeti na majarida yaliyopewa leseni yalipungua kwa asilimia 45.2 na kufikia 23 mwaka 2019 ikilinganishwa na magazeti na majarida 42 mwaka 2018. Aidha, vituo vya

redio 25 na vituo vya televisheni saba (7) vilisajiliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na vituo nane (8) vya redio na vituo vitatu vya televisheni vilivyosajiliwa mwaka 2018. Kuongezeka kwa vituo vya redio vilivyosajiliwa kulichangiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuhamasisha uanzishwaji wa vituo hivyo katika maeneo yasiyofikiwa na matangazo pamoja na kupanua wigo wa masafa. Kwa upande mwingine, blogu 78 zilisajiliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2019.

Maendeleo ya Sanaa

347. Mwaka 2018/19, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 168 vya kutengeneza filamu na picha jongevu ikilinganishwa na vibali 183 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 8.2. Kati ya hivyo, vibali 34 vilitolewa kwa kampuni za ndani za utengenezaji makala za filamu na picha jongevu na vibali 134 kwa kampuni za nje ya nchi. Kupungua kwa utoaji vibali kulichangiwa na baadhi ya watengenezaji filamu hususan wa ndani kutozingatia taratibu za utengenezaji wa filamu

Jedwali 16.13: Idadi ya Vibali vya Kutengeneza Filamu Vilivyotolewa Nchini

Mwaka	Vibali vya Wageni	Vibali vya Watanzania	Jumla
2014/15	133	36	169
2015/16	137	31	168
2016/17	123	30	153
2017/18	137	46	183
2018/19	134	34	168

Chanzo: Bodi ya Filamu Tanzania

Baraza la Kiswahili la Taifa

348. Mwaka 2018/19, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lilirusha vipindi 780 kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 847 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 7.9. Vipindi hivyo vilihusu sarufi na fasihi ya kiswahili pamoja na teknolojia inayohusiana na lugha. Aidha, BAKITA ilipitia miswada 38 kwa lengo la kutoa ithibati ya lugha kwa vitabu vinavyokusudiwa kutumika shuleni ikilinganishwa na miswada 63 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 39.7. Upungufu huo ultokana na waandishi na wachapishaji kutowasilisha miswada ili kupata ithibati ya lugha kabla ya kuchapisha vitabu hivyo.

349. Mwaka 2018/19, BAKITA ilitafsiri nyaraka 5,061 na kuhariri nyaraka saba (7) ikilinganishwa na nyaraka 1,607 zilizotafsiriwa na nyaraka 39 zilizohaririwa mwaka 2017/18. Kuongezeka kwa nyaraka zilizotafsiriwa kulitokana na ujio wa wageni wengi hasa wachina ambao vyeti vyao vya kitaaluma huandikwa kwa lugha ya kichina na hivyo kuhitaji tafsiri. Aidha, BAKITA ilitoa huduma mbili (2) za ukalimani ikilinganishwa na huduma tatu (3) mwaka 2017/18. Kwa upande mwingine, BAKITA ilibainisha makosa 1,081 yanayofanywa na vyombo vya habari nchini mwaka 2018/19 ikilinganishwa na makosa 848 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 27.5. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya waandishi wa habari kutotumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 16.14: Mchanganuo wa Huduma Zilizotolewa

Mwaka	Vipindi vya redio na runinga	Huduma ya ithibati	Huduma ya tafsiri	Huduma ya ukalimani	Huduma ya uhariri	Makosa yaliyobainika kutumiwa katika vyombo vya habari
2014	156	24	410	3	7	1,010
2015	118	121	320	3	8	1,200
2016	110	60	350	2	20	1,048
2017	87	61	268	3	10	805
2018	847	63	1,607	3	39	848
2019	780	38	5,061	2	7	1,081

Chanzo: Baraza la Kiswahili la Taifa

Maendeleo ya Michezo

Mwaka 2019, vilabu vya michezo vilivyosajiliwa vilikuwa 231 ikilinganishwa na vilabu 212 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Ongezeko hilo lilitokana na wananchi kuendelea kuhamasika kushiriki michezo kutokana na fursa zake ikiwemo ajira. Aidha, vyama 18 vya michezo vilisajiliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na vyama 23 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 21.7. Upungufu huo ultokana na idadi ndogo ya vyama vya michezo kujitokeza kuomba usajili. Vile vile, vituo 21 vya michezo vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 18 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Ongezeko hilo

lilitokana na wadau wengi kuanzisha vituo vya michezo nchini. Kwa upande mwagine, wakuzaji na mawakala 19 wa michezo walisajiliwa ikilinganishwa na wakuzaji na mawakala 29 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 34.5. Upungufu huo ultokana na kutojitokeza kwa Mawakala/Wakuzaji wa michezo katika mikoa mingine ikilinganishwa na Dar es Salaam ambako zoezi la uhamasishaji lilanza kufanyika.

Jedwali Na. 16.15: Usajili wa Vilabu, Vyama, Vituo na Wakuzaji na Mawakala wa Michezo

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo vya Michezo	Wakuzaji /Mawakala wa Michezo
2014	464	17	7	-
2015	224	15	12	-
2016	331	9	15	-
2017	288	29	13	14
2018	212	23	18	29
2019	231	18	21	19

Chanzo: Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 61

Maelezo	Kipimo	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Urefu wa Reli	KM	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707
Magari ya Moshi:	Namba	22	20	45	45	30	44	44	30	30
Mvuke	Namba	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Dizeli:	Namba	22	20	45	45	30	44	44	30	30
Mainlain		19	16	38	38	21	40	40	28	28
Shunting		3	4	7	7	9	4	4	2	2
Jumla ya mabehewa:	Namba	1,326	1,162	1,200	1,214	1,155	426	426	327	327
Abiria	Namba	53	36	91	91	56	56	56	71	71
Mizigo ya kawaida	Namba	658	635	681	590	561	22	22	18	18
Mafuta	Namba	335	208	178	203	196	123	123	95	95
Mifugo	Namba	88	80	39	64	64	27	27	27	27
Mengineyo	Namba	192	203	211	266	278	198	198	116	116
Uchukuzi	Namba									
Abiria	000	227	339	373	170	196	1,707	2,150	6,012	445
Mizigo	Tani'000	138	154	185	127	283	102	170	357	374

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 62

Maelezo	Kipimo	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Urefu wa Reli Kuu	Km	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860
Magari ya Moshi	Namba	15	13	13	15	16	17	21	21	18	18
Reli Kuu	Namba	10	9	9	11	13	12	14	12	13	13
Ya kujongeza	Namba	5	4	5	4	3	6	7	7	5	5
Mabehewa ya abiria	Namba	36	36	35	52	50	51	56	49	60	61
Abiria	Namba	31	30	30	45	44	43	48	40	51	52
Chakula	Namba	2	3	2	3	3	3	4	4	4	4
Vifurushi	Namba	3	3	3	4	3	5	4	5	5	5
Mabehewa ya mizigo	Namba	1,620	930	858	1,391	1,101	1,142	1,221	1,033	1,068	1,054
Mizigo ya kawaida	Namba	1,381	795	765	1,229	966	1,007	1,077	972	998	992
Mifugo	Namba	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mafuta	Namba	197	93	59	104	82	82	89	26	70	72
Barafu	Namba	7	7	-	5	5	5	5	-	-	-
Mengineyo	Namba	2	2	1	1	1	1	1	1	1	1
Breki	Namba	16	16	16	35	30	30	32	30	34	34
Ballast	Namba	17	17	17	17	17	17	17	4	15	14
Uchukuzi mizigo (Tani)	000	540	248	259	245	33	81	96	171	268	155
Abiria	000	758	414	678	654	287	327	440	443	154	510

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

USA FIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 63A

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Jumla ya meli	Namba	1,298	1,600	1,617	1,684	1,688	1,744	1,516
Uwezo wa kubeba mizigo	000 Tani	27,805	31,936	31,614	31,278	31,287	32,513	31,200
Jumla ya abiria	000 Namba	1,472	1,433	1,612	1,735	1,874	1,901	2,035
Jumla ya bidhaa zote	000 Dwt	13,510	14,476	14,601	13,580	13,761	14,401	16,405
Bidhaa zilizopakuliwa	000 Dwt	11,380	11,763	11,901	11,260	11,460	11,682	13,836
Za kawaida	000 Dwt	6,642	7,100	6,657	6,087	6,376	6,199	7,876
Saruji	000 Dwt	-	-	-	-	-	-	-
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000 Dwt	4,471	4,357	4,882	4,772	4,740	5,483	5,959
Mengineyo1	000 Dwt	267	306	362	401	344	-	-
Bidhaa zilizopakiwa	000 Dwt	2,130	2,713	2,700	2,320	2,301	2,719	2,550
Za kawaida	000 Dwt	1,892	2,232	2,137	1,915	1,986	2,353	2,422
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000 Dwt	37	66	362	116	59	99	82
Mengineyo1	000 Dwt	14	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano (<i>Transhipment</i>)	000 Dwt	187	415	201	289	256	267	46

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, molasses, tallow fats n.k

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 63B

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Jumla ya meli	Namba	86	68	63	87	72	144	120
Uwezo wa kubeba mizigo	000	1,456	1,403	1,018	1,258	1,041	780	568
Jumla ya abiria	000 Namba	-	-	-	-	-	45,820	68
Jumla ya bidhaa zote	000Dwt	458	368	645	677	486	647	619
Bidhaa zilizopakuliwa	000Dwt	345	265	561	614	436	502	511
Za kawaida	000Dwt	334	259	483	398	141	183	181
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000Dwt	11	6	78	216	295	319	331
Bidhaa zilizopakiwa	000Dwt	113	103	83	63	50	144	108
Za kawaida	000Dwt	113	103	83	63	50	144	108
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000Dwt	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano (<i>Transhipment</i>)	000Dwt	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USA FIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 63C

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Jumla ya meli	Namba	41	65	46	113	105	69	132
Uwezo wa kubeba mizigo	000	540	841	593	460	457	589	598
Jumla ya abiria	000	-	-	-	-	-	-	-
Jumla ya bidhaa zote	000 DWt	277	365	248	375	378	363	270
Bidhaa zilizopakuliwa	000 DWt	157	249	109	158	91	40	
Za kawaida	000 DWt	141	249	108	147	91	69	2
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000 DWt	16	-	1	10	-	-	37
Bidhaa zilizopakiwa	000 DWt	120	117	139	218	286	230	
Za kawaida	000 DWt	120	116	139	218	286	294	230
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000 DWt	-	0	-	-	-	-	-
Mabadilishano (<i>Transhipment</i>)	000 DWt	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 64

Maelezo	Kipimo	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Ofisi Ndogo Posta	Namba	171	105	65	74	74	65	65	66	57	46
Franchised Post Offices	Namba	81	151	112	89	89	90	90	87	87	79
Ofisi Kubwa	Namba	170	163	147	160	160	158	158	154	157	139
Jumla	Namba	422	419	324	323	323	313	313	307	301	264
Masanduku Binafsi	000		146	162	173	142	160	160	161	161	145
Masanduku Yaliokodishwa	000	120	130	140	148	128	138	138	143	157	126
Maombi Yasiotimizwa	000	-	21	28	25	18	4	1	1	3	1
Mifuko Pekee Iliyokodishwa	Namba	183	361	278	212	260	180	180	342	675	442
Barua Zilizotumwa bila Vifurushi	Mill.	29	27	15	26	15	10	4	5	9	11
Regista na Barua za Amana	000	480	347	397	568	455	402	297	269	280	186
Vifurushi Nchini	000	15	10	15	29	12	17	36	51	63	32
Vifurushi Nje	000	7	11	12	9	5	9	2	3	4	3
Leseni za kuuza stamp	Namba	25,145	28,257	33,311	2,637	3,715	-	-	4,635	6,027	5,570
Huduma za Haraka, barua na vifurushi	"										
Ndani ya Nchi	"	283,711	501,635	404,453	620,478	406,732	416,007	452,827	560,710	655,927	511,274
Nje ya Nchi	"	18,766	16,965	24,347	17,130	20,564	308,288	6,364	9,534	14,346	13,742
EMS Money Fax	"	82,002	36,357	2,940	550	745	748	272	18	-	-
EMS Fax (Fax message received)	"	31,594	1,595	876,187	544	1,194	3,844	2,518	129	-	-
Overnight Mail Services	"			9,963	115,126	-	-	-	-	-	-
Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	76,983	115,403	50,082	87,051	46,652	53,639	57,605	24,966	14,553	19,598
Vifurushi vya magazeti vilivyo safirishwa	"	2,752	12,040	10,652	18,784	8,700	9,130	113,448	2,120	5,346	7,800
Huduma za gari ndogo											
Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	-	193	24,095	849	714	9,576	-	-	2,919	2,518
Amna za Haraka Zilizotolewa	"	8,169	4,717	3,087	2,034	845	58,423	272	127	104	109
Amna za Haraka Zilizolipwa	"	11,881	17,397	516	555	-	-	-	-	-	-
Amna za Haraka za Nje ya Nchi											
Zilizotumwa	"	1,027	998	369	478	325	221	220	8	11	26
Zilizopokelewa	"	150	217	77	83	227	283	116	43	37	-
Amna za Posta zilizouzwa	"	1,924	633	414	684	261	251	107	45	2	-
Amna za Posta Zilizolipwa	"	3,262	1,662	252	166	67	25	18	8	-	-
Benki ya Akiba (Transaction)											
Uwekaji Amna (Deposit)	"	18,863	13,438	6,260	21,491	12,732	21,541	261,423	59,249	108,972	91,567
Uchukujaji Amna (Withdrawal)	"	23,025	72,358	17,527	37,556	12,807	18,098	45,449	76,926	133,531	103,958

Chanzo: Shirika la Posta

IDADI YA WANAOUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI

Jedwali Na. 65

Kampuni	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	Badiliko (%)
A. Simu za Kiganjani										
Mobitel/Tigo	5,450,766	6,244,050	6,297,288	8,624,638	10,639,610	11,677,344	11,044,520	12,583,640	12,572,826	-0.1
Vodacom	11,625,773	8,967,269	10,288,972	11,810,064	12,520,645	12,419,425	12,714,297	14,143,657	15,672,390	10.8
Airtel	6,993,418	8,001,689	8,995,824	9,551,977	10,887,742	10,456,117	10,571,110	10,954,621	12,722,224	16.1
Zantel	1,524,601	2,479,505	1,814,444	1,730,105	1,563,503	1,083,157	934,991	1,153,623	1,170,085	1.4
Benson/Smart	1,558	924	528	528	528	803,251	131,501	132,292		
TTCL Mobile	225,578	60,887	210,766	296,618	165,460	166,383	175,717	587,191	981,072	67.1
Sasatel	5,824	4,810								
Smile										1,222
Hallotel						3,438,509	3,799,691	3,942,237	4,641,701	17.7
Jumla Ndogo	25,827,518	25,759,134	27,607,822	32,013,930	35,777,488	40,044,186	39,371,827	43,497,261	47,761,520	9.8
B. Simu za Mezani										
TTCL	159,364	160,012	158,935	140,391	140,391	127,112	127,009	124,220	76,288	-38.6
Zantel	1,699	8,953	6,064	10,833	10,833	24,585	85	18		
Jumla Ndogo	161,063	168,965	164,999	151,224	151,224	151,697	127,094	124,238	76,288	-38.6
Jumla Kuu	25,988,581	25,928,099	27,772,821	32,165,154	35,928,712	40,195,883	39,498,921	43,621,499	47,837,808	9.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)⁺

Jedwali Na.66

Maelezo	Kipimo	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Tani-Kilometa:										
Zilizokuwepo	000	1,662	1,932	6,154	3,052	60,042	3,937	863,107	32,095	32,927
Zilizotumika	000	268	815	2,503	117	30,889	1,756	89,092	17,526	18,944
Matumizi	%	16	42	41	4	54	47	10	55	58
Viti-kilometa:										
Vilivyokuwepo	000	7,140	15,131	54,665	3,680	21,693	37,877	225,259	231,943	321,771
Vilivyotumika	000	2,946	10,209	27,279	946	11,472	20,692	122,532	158,203	220,433
Matumizi	%	41	67	50	26	53	56	54	68	69
Abiria ++	000	9	11	35	56	31	28	129	279	627
Mizigo ya ziada	Tani	2	0	45	-	53	1	41	55	96
Mizigo mingine	Tani	4	5	35	45	42	7	50	220	696
Shehena za Posta	Tani	-	-	25	405	4	-	32	119	295

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 17

NISHATI

Ufuaji wa Umeme

350. Uwezo wa uzalishaji umeme uliongezeka na kufikia MW 1,601.03 mwaka 2019 ikilinganishwa na MW 1,600.86 mwaka 2018. Umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali uliongezeka kwa asilimia 6.1 na kufikia saa za gigawati 7,804.93 mwaka 2019 kutoka saa za gigawati 7,354.79 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji umeme kwa kutumia mitambo ya Kinyerezi II. Kati ya umeme uliozalishwa mwaka 2019, saa za gigawati 7,513.83 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa; saa za gigawati 176.55 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa; na saa za gigawati 114.55 ziliingizwa kwenye gridi ya Taifa kutoka nje ya nchi. Kwa upande mwingine, mahitaji ya juu ya umeme yalifika MW 1,120.12 mwaka 2019 ikilinganishwa na MW 1,116.58 mwaka 2018.

351. Mchanganuo wa umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa mwaka 2019 ulikuwa kama ifuatavyo: umeme wa mitambo ya nguvu za maji saa za gigawati 2,477.24; gesi saa za gigawati 5,035.79; na mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 0.8. Umeme wa mafuta mazito na dizeli uliozalishwa mwaka 2019 ulikuwa saa za gigawati 177.40. Kati ya huo, saa za gigawati 0.8 zilizalishwa katika gridi ya Taifa. Aidha, uzalishaji umeme kwa kampuni binafsi ulifikia saa za gigawati 1,531.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,483.0 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme ya Songas. Vile vile, umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani ulikuwa saa za gigawati 114.55 mwaka 2019 ikilinganishwa na saa za gigawati 117.53 mwaka 2018, sawa na asilimia 1.5 ya umeme wote uliozalishwa mwaka 2019.

352. Mwaka 2019, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali uliongezeka kwa asilimia 5.6 na kufikia saa za gigawati 6,642.78 kutoka saa za gigawati 6,290.74 mwaka 2018. Aidha, umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ulikuwa saa za gigawati 1,162.15 (sawa na asilimia 14.9 ya umeme uliozalishwa mwaka 2019) ikilinganishwa na saa za gigawati 1,064.1 sawa na asilimia 14.5 ya umeme uliozalishwa mwaka 2018.

**UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME ULIOZALISHWA KWA VITUO
MWAKA 2019**


Jedwali Na. 67

Kituo	2019	
	Uwezo (MW)	Umeme Uliozalishwa (GWh)
Kidatu	204.0	820.7
Kihansi	180.0	956.0
Mtera	80.0	242.4
New Pangani Falls	68.0	328.2
Hale	21.0	49.3
Nyumba ya Mungu	8.0	33.5
Uwemba	0.8	1.8
Mwenga	4.0	13.4
Yovi	1.0	5.4
Matembwe	0.6	0.6
Darakuta	0.3	2.2
Matawi Mengine	6.0	23.9
Jumla Ndogo - Hydro	573.7	2,477.2
Ubungo Gas Plant I	102.0	585.9
Tegeta Gas Plant	45.0	217.8
Ubungo Gas Plant II	129.0	860.6
Zuzu	7.4	0.1
Nyakato	63.0	0.7
Kinyerezi I	150.0	719.5
Kinyerezi II	248.2	1,120.8
Jumla Thermal	744.6	3,505.5
IPTL		
Songas	189.0	1,513.9
Imports from SPPs	11.0	17.1
Jumla Wazalishaji Binafsi	200.0	1,531.1
Jumla Grid	1,518.3	7,513.8
MATAWI MENGINE (ISOLATED STATIONS)		
Kigoma	8.3	29.7
Songea	7.7	0.3
Mpanda	3.8	13.6
Mbinga	2.0	0.1
Ngara	2.5	3.7
Biharamuro	4.1	2.8
Mafia	3.2	5.6
Tunduru	2.9	7.6
Ludewa	1.3	0.2
Liwale	0.8	0.7
Somanga	7.5	3.3
Sumbawanga	5.0	0.4
Kasulu	2.5	9.3
Kibondo	2.5	5.5
Loliondo	3.8	1.6
Namtumbo	0.3	-
Mtwara	22.0	92.3
Bukoba	2.6	0
Umeme kutoka nchi jirani		114.5
Jumla Nje ya Gridi	82.7	291.1
Jumla Kuu ya Umeme – Nchi Nzima	1,601.0	7,804.9

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

Kielelezo Na 17.1: Mchanganuo wa Umeme Ulizalishwa Mwaka 2019 (Saa za gigawati)



MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 68

Mwaka	Tanzania Bara			Zanzibar T5+T7	Jumla	Umeme uliopotea	Jumla ya umeme uliotengenezwa GWH
	Wateja wadogo (D1)	Wateja wa Kati (T1)	Wateja Wakubwa (T2,T3 & T8)				
2012	320.8	1,480.1	2,301.8	298.6	4,401.4	1,048.3	5,449.6
2013	280.6	1,747.0	2,560.4	218.7	4,806.7	1,139.6	5,946.2
2014	217.0	1,891.0	2,595.0	348.5	5,051.5	1,135.3	6,186.8
2015	148.8	2,082.7	2,721.1	344.6	5,297.1	1,119.8	6,416.9
2016	345.3	2,263.4	2,887.2	375.6	5,871.5	1,220.7	7,092.2
2017	301.5	2,371.0	2,893.3	390.4	5,956.2	1,159.1	7,115.3
2018	319.8	2,481.9	3,075.0	414.0	6,290.7	1,064.1	7,354.8
2019	307.2	2,655.9	3,198.1	481.5	6,642.8	1,162.2	7,804.9

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 69

Mkoa	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Dodoma	94.0	104.9	110.5	115.9	136.7	150.4	161.0	179.7
Arusha	286.0	315.8	325.5	311.2	356.9	365.9	383.3	406.3
Manyara	23.0	24.2	25.2	25.8	29.5	31.9	32.4	34.8
Kilimanjaro	138.0	144.1	153.6	150.9	181.8	179.4	181.7	185.2
Tanga	245.0	264.2	265.8	299.9	321.7	330.4	353.9	374.2
Morogoro	207.0	221.0	232.2	212.2	239.8	242.8	274.9	268.0
Coast	142.0	170.7	199.2	220.1	260.1	302.1	393.1	450.7
Dar-es-Salaam	1,548.0	1,931.5	2,118.1	2,229.4	2,397.9	2,412.5	2,481.6	2,573.8
Lindi	14.6	18.2	22.6	21.5	24.0	22.9	25.8	29.7
Mtwara	34.0	35.0	8.5	50.7	49.4	48.3	52.8	55.9
Ruvuma	23.6	26.8	27.6	30.6	33.7	35.4	41.9	50.3
Iringa	102.0	105.3	106.5	111.5	106.9	98.4	103.7	108.9
Mbeya	149.6	153.2	169.9	163.8	177.4	177.6	186.9	201.6
Singida	29.4	32.0	35.2	47.3	42.6	43.8	45.7	49.5
Tabora	103.2	108.7	60.4	51.5	56.9	55.9	60.7	68.4
Rukwa	19.3	20.1	22.2	23.3	28.4	27.0	25.9	27.3
Kigoma	20.5	23.1	24.9	27.6	28.5	34.8	40.2	40.3
Shinyanga	279.3	280.4	359.0	416.9	428.2	371.9	339.5	354.1
Kagera	55.0	52.7	54.2	60.5	72.3	76.9	90.6	80.3
Mwanza	224.0	231.1	241.3	235.9	262.1	283.2	287.7	295.2
Mara	108.0	125.0	134.0	134.6	141.7	156.9	165.8	163.9
Njombe				-	69.1	35.6	35.4	39.1
Katavi				-	3.8	10.8	11.2	13.6
Geita				-	33.5	42.7	49.2	53.0
Simiyu				-	8.3	18.2	22.4	24.2
Songwe			6.4	11.4	4.9	10.1	29.3	33.2
Jumla Tanzania Bara	3,845.5	4,388.0	4,702.8	4,952.6	5,495.9	5,565.8	5,876.7	6,161.3
Zanzibar	298.6	218.7	348.5	344.6	375.6	390.4	414.0	481.5
JUMLA	4,144.1	4,606.7	5,051.3	5,297.1	5,871.5	5,956.2	6,290.7	6,642.8

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

Utafutaji Mafuta na Gesi

Gesi Asilia

353. Mwaka 2019, uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songsosongo na Mnazi Bay ulifikia futi za ujazo milioni 63,821.3 kutoka futi za ujazo milioni 58,950.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Ongezeko hilo lilitokana na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha gesi katika visima vya Songsosongo. Aidha, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia katika visima vya Songsosongo na

Mnazi Bay yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 64.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola milioni 63.1 mwaka 2018.

Jedwali Na. 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia katika Visima vya SongoSongo na Mnazi Bay

Mwaka	Futi za Ujazo (SCF)			Jumla
	Songo Songo	Mnazi Bay	Kiliwani North	
2019	37,619,760,000	26,201,516,247	-	63,821,276,247
2018	28,510,280,000	30,412,535,066	27,784, 935	58,950,600,001
2017	29,496,560,000	17,960,300,000	3,597,578,168	51,054,438,168
2016	29,747,400,000	15,792,127,458	2,783,497,464	48,323,024,922
2015	31,384,100,000	5,792,141,976	-	37,176,241,976
2014	33,061,500,000	783,595,488	-	33,845,095,488
2013	35,217,410,596	715,942,883	-	35,933,353,479
2012	36,233,010,000	673,870,408	-	36,906,880,408
2011	30,970,500,000	664,980,487	-	31,635,480,487
2010	27,633,000,000	454,123,320	-	28,087,123,320

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Jedwali Na. 17.2: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Gesi Asilia katika Visima vya SongoSongo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)

Mwaka	Songo Songo	Mnazi Bay na Kiliwani	Jumla
2019	28,097,086	35,952,953	64,050,040
2018	22,406,171	40,683,088	63,089,259
2017	22,795,142	19,466,121	42,261,263
2016	38,172,718	13,818,715	51,991,433
2015	43,854,236	1,921,965	45,776,201
2014	58,761,119	1,762,977	60,524,096
2013	50,582,385	1,592,879	52,175,264
2012	35,026,145	1,525,251	36,551,396
2011	38,337,903	1,444,856	39,782,759
2010	25,607,621	1,080,131	26,687,753

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Uagizaji Mafuta

354. Mafuta yaliyoingizwa nchini yaliongezeka kwa asilimia 7.8 na kufikia lita za ujazo milioni 6,152.0 mwaka 2019 kutoka lita za ujazo milioni 5,704.8 mwaka 2018. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani hususan katika usafiri na miradi mikubwa ya maendeleo. Katika kipindi hicho, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani yaliongezeka kwa asilimia 8.4 na kufikia lita za ujazo milioni 3,537.9 kutoka lita za ujazo milioni 3,264.8 mwaka 2018. Hata hivyo, uagizaji wa mafuta ya taa ulipungua kutokana na kuongezeka kwa vijiji vilivyounganishwa na umeme, matumizi ya nishati mbadala maeneo ya vijijini ikiwemo umeme wa juu na udhibiti wa uchakachuaji wa mafuta.

355. Mwaka 2019, mafuta yaliyopitishwa nchini kwenda nchi jirani yaliongezeka kwa asilimia 7.1 na kufikia lita za ujazo milioni 2,614.1 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 2,440.0 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam na unafuu wa gharama za uingizaji wa mafuta nchini kufuatia ufanisi wa mfumo wa uagizaji mafuta.

Jedwali Na.17.3: Mafuta Yaliyoingizwa kwa Matumizi ya Ndani Mwaka 2019 (Lita `000)

	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Taa	Mafuta ya Ndege	Mafuta Mazito	Jumla
Januari	107,747.8	164,422.3	3,803.3	11,771.0	-	287,744.4
Februari	228,055.2	92,909.5	1,752.8	13,857.8	2,009.2	338,584.6
Machi	135,843.5	81,199.8	-	-	4,576.2	221,619.4
Aprili	158,198.0	75,736.8	1,346.8	12,805.4	-	248,087.0
Mei	142,273.2	79,844.7	3,655.0	23,054.9	-	248,827.8
Juni	154,402.2	97,255.0	2,635.7	14,491.4	-	268,784.3
Julai	156,915.9	98,840.3	6,872.3	19,357.6	9,046.9	291,033.0
Agosti	167,784.5	98,129.5	1,905.9	18,971.7	-	286,791.6
Septemba	151,994.3	84,436.9	1,423.6	20,943.0	2,590.5	261,388.3
Oktoba	186,090.5	127,072.5	1,832.8	23,005.9	-	338,001.7
Novemba	205,912.8	139,336.4	3,345.3	23,749.7	-	372,344.1
Desemba	157,632.2	88,370.9	-	-	-	246,003.2
Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit)	68,183.5	51,748.0	6,924.0	211.7	1,615.3	128,682.6
Jumla Kuu	2,021,033.6	1,279,302.6	35,497.5	182,220.1	19,838.1	3,537,891.9

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 17.4: Mafuta Yaliyopitishwa Nchini Kwenda Nchi Jirani
Mwaka 2019 (Lita `000)**

	Dizeli	Petroli	Mafuta ya taa / mafuta ya ndege	Mafuta mazito	Jumla
Januari	90,930.10	109,509.10	14,657.70		215,096.90
Februari	205,448.7	92,956.0	15,290.2	6,830.3	320,525.20
Machi	142,473.6	83,098.4			225,572.00
Aprili	122,028.5	66,013.7	18,731.3		206,773.50
Mei	140,815.1	54,227.6	26,361.9		221,404.60
Juni	91,986.6	66,205.1	9,553.2		167,744.90
Julai	105,487.1	63,041.3	11,005.9	1,030.8	180,565.10
Agosti	122,609.8	79,948.3	12,066.0		214,624.10
Septemba	127,332.5	70,482.2	14,737.1		212,551.80
Oktoba	181,926.0	89,546.6	18,086.3		289,558.90
Novemba	154,278.4	89,992.8	15,268.9		259,540.10
Desemba	159,888.7	68,901.1			228,789.80
Jumla ya mafuta yaliyobadilishwa matumizi (Localized transit)	-68,183.5	-51,748.0	-7,135.7	-1,615.3	-128,682.50
Jumla Kuu	1,577,021.6	882,174.2	148,622.8	6,245.8	2,614,064.4

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Mwenendo wa Bei za Mafuta

356. Mwaka 2019, wastani wa bei ya mafuta ya petroli kwa tani ulikuwa dola za Marekani 593, mafuta ya dizeli dola za Marekani 570 na mafuta ya taa dola za Marekani 589 ikilinganishwa na dola 661, dola 622 na dola 645 mwaka 2018 mtawalia. Bei hizo zilipungua kwa asilimia 10.3 kwa mafuta ya petroli, asilimia 8.4 mafuta ya dizeli na asilimia 8.7 mafuta ya taa. Upungufu huo ilitokana na kushuka kwa bei za mafuta ghafi kwenye soko la dunia. Kiwango cha juu cha wastani wa bei ya mafuta ya petroli na dizeli kilikuwa mwezi Juni na kwa mafuta ya taa kilikuwa mwezi Januari. Kwa upande wa mafuta ghafi, wastani wa bei ulipungua kwa asilimia 10.5 na kufikia dola za Marekani 63.9 kwa pipa kutoka wastani wa dola 71.4 kwa pipa mwaka 2018. Hii ilitokana na ongezeko la uzalishaji wa mafuta katika nchi za Marekani, Brazil, Canada, Norway na Guyana.

Jedwali Na. 17.5: Bei za Mafuta katika Soko la Dunia (f.o.b) - Dola za Marekani kwa tani za Ujazo

Aina ya mafuta	Petroli			Dizeli			Mafuta ya taa		
	2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
Mwezi/Mwaka	2017	2018	2019	2017	2018	2019	2017	2018	2019
Januari	497	574	635	421	530	606	442	570	644
Februari	502	600	520	468	549	501	499	587	542
Machi	542	599	496	485	581	516	504	587	543
Aprili	557	646	543	505	607	582	510	624	543
Mei	531	615	610	470	573	600	476	624	605
Juni	555	632	677	480	580	618	497	633	625
Julai	521	718	658	455	674	610	474	633	634
Agosti	503	710	597	454	655	546	464	691	570
Septemba	510	710	639	462	639	576	485	673	601
Oktoba	560	711	576	516	653	552	529	673	584
Novemba	600	712	596	546	699	572	570	693	602
Desemba	599	707	574	549	721	560	587	756	574
Wastani wa Bei	540	661	593	484	622	570	503	645	589
Badiliko (Asilimia)		22.4	-10.3		28.5	-8.4		28.2	-8.7

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

357. Mwaka 2019, bei za mafuta katika soko la ndani ziliwa zikibadilika kulingana na mabadiliko ya bei katika soko la dunia pamoja na gharama za usafirishaji wa mafuta hayo. Katika kipindi hicho, wastani wa bei za ukomo kwa mafuta ya petroli mwaka 2019 ulikuwa shilingi 2,200 kwa lita, dizeli shilingi 2,159 kwa lita na mafuta ya taa shilingi 2,114 kwa lita ikilinganishwa na shilingi 2,318, shilingi 2,229 na shilingi 2,188 mwaka 2018 kwa mtiririko huo. Mwenendo huo ni sawa na upungufu wa bei wa asilimia 5.1 kwa mafuta ya petroli, asilimia 3.1 mafuta ya dizeli na asilimia 3.4 mafuta ya taa. Hii ilitokana na ufanisi wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia mwaka 2019.

Jedwali Na. 17.6: Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani, Mwaka 2019

Mwezi/ Mwaka	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/Lita)	Mafuta ya taa (Sh/Lita)
Januari	2,295	2,224	2,202
Februari	2,120	2,080	2,046
Machi	2,098	2,131	2,096
Aprili	2,147	2,192	2,096
Mei	2,233	2,181	2,109
Juni	2,353	2,220	2,180
Julai	2,312	2,210	2,167
Agosti	2,153	2,107	2,086
Septemba	2,236	2,168	2,132
Oktoba	2,094	2,109	2,056
Novemba	2,192	2,158	2,117
Desemba	2,161	2,125	2,075
Wastani Mwaka 2019	2,200	2,159	2,114
Wastani Mwaka 2018	2,318	2,229	2,188
Badiliko (Asilimia)	-5.1	-3.1	-3.4

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Nishati Jadidifu

Nishati Mbadala ya LPG

358. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati ya kupikia ikiwemo gesi ya kupikia majumbani -LPG kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa ya gesi inayotokana na petroli (LPG) uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2018. Kiasi cha gesi kilichoagizwa kilikuwa tani 166,436 mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 142,939 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 16.4. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi hiyo katika soko la ndani kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kuchomea vyuma na kupikia sambamba na juhudhi za Serikali na kampuni zinazouza gesi hiyo kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia nishati mbadala na hivyo kupunguza matumizi ya mkaa, kuni na mafuta ya taa.

Nishati ya Mionzi ya Jua

359. Uzalishaji wa umeme jua kwa mfumo wa gridi ndogo katika maeneo yaliyo nje ya mfumo wa gridi ya Taifa ulifiki megawati 7.4 mwaka 2019 ikilinganishwa na megawati 7.0 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa miradi mipy ya umeme wa jua katika mikoa ya Kagera na Lindi iliyoteklezwa na Kampuni za Jumeme na Powercorner. Aidha, matumizi ya nishati ya mionzi ya jua majumbani (*Solar Home System*) yalionezeka kwa asilimia 8.3 na kufikia megawati 19.5 kutoka megawati 18 mwaka 2018. Mwaka 2019, umeme wa mionzi ya jua ulichangia katika maendeleo ya sekta ya kilimo ambapo kilowati 70 zilitumika katika shughuli za umwagiliaji mazao ya matunda.

SURA YA 18

MAJI

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

360. Mwaka 2019, Serikali ilifanya utafiti kuhusu hali ya rasilimali za maji nchini ambapo utafiti ulionesha kuwa rasilimali za maji zilizopo na zinazofaa kwa matumizi ziliwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka. Kati ya hizo, mita za ujazo bilioni 105 zilikadiriwa kuwa ni maji juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 ni maji chini ya ardhi. Aidha, kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kilikuwa wastani wa mita za ujazo 2,300 kwa mwaka. Kiasi hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

361. Mwaka 2019, Serikali iliendelea na jitihada za kuvitambua, kuvivekea mipaka, kuandaa ramani na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Na. 221 la tarehe 22 Julai 2016 vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha rasilimali za maji zinakuwa endelevu. Katika kipindi hicho, vyanzo vya maji 575 vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vyanzo 298 mwaka 2018. Vyanzo hivyo vilijumuisha mabwawa 33, chemichemi 280, maeneo ya visima 36, mito 185, maeneo ya ardhi oevu 22 na maziwa 19. Aidha, vyanzo 18 vilihifadhiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu na vyanzo 120 viliwekewa mipaka kama hatua ya awali ya kuvihifadhi ikilinganishwa na vyanzo 91 mwaka 2018.

362. Hadi Desemba 2019, kulikuwa na jumla ya vituo 996 vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na vituo 1,067 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 6.7. Upungufu huo ultokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya vituo kusombwa na mafuriko pamoja na wizi na uharibifu wa miundombinu katika vituo vya kufatilia mwenendo wa maji. Kati ya hivyo, vituo kwa ajili ya kukusanya takwimu za mvua vilikuwa 154, hali ya hewa (86), mtiririko wa maji katika mito (264), kina cha maji katika maziwa (10), kina cha maji katika mabwawa (14), kiasi cha tope katika mito (33), maji chini ya ardhi (81) na ubora wa maji (354). Aidha, vituo sita (6) katika bonde la Ziwa Victoria na kituo kimoja

(1) katika bonde la mto Rufiji vilijengwa kwa ajili ya kukusanya takwimu na kufuatalia mwenendo wa maji. Vile vile, vituo 19 vya kufuatalia hali ya hewa vilijengwa katika Bonde la Mto Rufiji. Kwa upande mwengine, vituo 100 vya kufuatalia mwenendo wa maji mitoni vilikarabatiwa ambapo katika bonde la Ziwa Victoria vilikarabatiwa vituo tisa (9), bonde la Ziwa Rukwa (22), bonde la Ziwa Nyasa (11), bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini (31), bonde la Ziwa Tanganyika (5), bonde la Wami/Ruvu (3), bonde la Mto Rufiji (8) na bonde la Kati (11).

363. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji wa maji ambapo sampuli 5,252 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ikilinganishwa na sampuli 5,668 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 7.3. Kati ya hizo, sampuli kwa matumizi ya majumbani ziliwu 4,218, viwandani (268), umwagiliaji (60), ujenzi (56), utafiti (116) na sampuli 534 kwa ajili ya kubaini mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli za maji 3,832 kwa ajili ya matumizi ya majumbani sawa na asilimia 90.8 zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika ikilinganishwa na asilimia 86.3 mwaka 2018. Aidha, sampuli 386 za maji sawa na asilimia 9.2 hazikukidhi viwango vinavyokubalika kutokana na kuwepo kwa viwango vikubwa vya madini ya chuma, *Manganese* na chumvichumvi kwa mikoa ya Lindi na Mtwara, *Fluoride* kwa mikoa ya Arusha na Singida, *Nitrate* na chumvi katika mkoa wa Dodoma. Vile vile, sampuli 384 za maji kwa ajili ya shughuli za viwandani, ujenzi na umwagiliaji zilizofanyiwa uchunguzi zilikidhi viwango vinavyokubalika. Kwa upande mwengine, sampuli 387 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ambapo asilimia 60 ya sampuli hizo zilikidhi viwango vya kurudishwa kwenye mazingira ikilinganishwa na asilimia 16.3 mwaka 2018. Kuongezeka kwa sampuli zilizokidhi viwango kulitokana na utekelezaji wa ushauri uliotolewa na wataalamu wa maabara za ubora wa maji kwa mamlaka za maji na viwanda kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji taka.

Huduma ya Maji Vijini

364. Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji vijini ambapo hadi Desemba 2019 miradi 1,753 ya maji vijini ilikamilika ikilinganishwa na miradi 1,659 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Miundombinu ya maji iliyojengwa ilikuwa na vituo vya kuchotea maji 138,987 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 34,746,750 kati ya wananchi 36,328,023 sawa na asilimia 95.6 ya wananchi waishio vijijini ikilinganishwa na vituo 131,370 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 32,842,500 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vituo 96,952 vinafanya kazi na kutoa huduma kwa asilimia 70.1 ya wananchi wote waishio vijijini ikilinganishwa na vituo 86,780 vilivyokuwa vinafanya kazi mwaka 2018 na kutoa huduma kwa asilimia 64.8 ya wananchi..

Huduma za Maji Mijini

365. Mwaka 2019, wastani wa upatikanaji wa huduma ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa ulikuwa asilimia 84 ikilinganishwa na asilimia 80 mwaka 2018. Hadi Desemba 2019, wateja 943,074 waliunganishwa na huduma ya majisafi ikilinganishwa na wateja 743,765 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 26.8. Aidha, uzalishaji wa majisafi na salama uliongezeka hadi kufikia mita za ujazo milioni 345.9 ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 338.2 mwaka 2018², sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Hii ilitokana na kukamilika kwa miradi ya maji na ukarabati wa miundombinu. Kwa upande mwingine, wastani wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa jiji la Dar es Salaam ulikuwa asilimia 85 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa ulikuwa asilimia 64 mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018.

Uchimbaji wa Visima

366. Mwaka 2019, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliendelea na uchimbaji wa visima katika maeneo ya mijini na vijijini ili kuboresha huduma za maji. Katika kipindi hicho, visima 2,053 vilichimbwa katika mikoa mbalimbali ambapo Dar es Salaam vilichimbwa visima 736, Pwani (137), Morogoro (113), Njombe (1), Iringa (22), Ruvuma (16), Mtwara (11), Lindi (45), Kigoma (50), Tanga (45), Tabora (33), Songwe (39), Singida (60), Simiyu (11), Shinyanga (27), Rukwa (1), Geita (56), Mwanza (27), Mbeya (72), Mara (30), Manyara (27), Kilimanjaro (93), Katavi (5), Kagera (65), Dodoma (210) na Arusha (121).

² Uzalishaji wa maji mijini kwa mwaka 2018 na 2019 umejumuisha takwimu za Mamlaka za uzalishaji maji za Dar es salaam, Kahama, na Vwawa-Mlowo.

Uondoaji wa Majitaka

367. Mwaka 2019, huduma ya uondoaji wa majitaka kwa kutumia mtandao wa uondoaji majitaka kutoka kwa wateja ilikuwa asilimia 13.0 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2018. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kujenga, kukarabati na kupanua mifumo ya uondoaji majitaka. Aidha, wateja wa majitaka waliongezeka na kufikia 50,408 mwaka 2019 kutoka wateja 48,566 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Vile vile, mtandao wa majitaka uliongezeka kutoka kilomita 823.32 mwaka 2018 hadi kilomita 878.77 mwaka 2019.

UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI

Jedwali Na. 70

Mamlaka	Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	Mapato (TShs)
	2018		2019	
Arusha	15,855,281	14,217,491,604	15,207,609	17,147,472,138
Dar es Salaam	183,960,000	110,011,241,199	183,960,000	140,781,910,096
Babati	2,171,167	2,081,921,523	2,196,128	2,504,075,166
Bukoba	3,108,330	2,155,596,478	2,288,913	2,674,430,314
Dodoma	14,133,296	14,432,195,493	15,993,293	18,793,945,336
Iringa	4,816,026	7,438,654,131	4,850,334	9,128,422,716
Kigoma	2,899,655	1,401,397,427	3,542,157	1,856,673,611
Kahama	4,146,954	5,519,409,689	4,283,787	9,086,230,528
Lindi	782,362	428,571,295	817,153	804,163,655
Mbeya	13,799,430	10,283,182,014	16,219,782	13,437,635,472
Morogoro	11,503,479	9,648,877,386	11,477,281	9,586,393,334
Moshi	11,504,048	8,710,378,486	12,288,705	9,850,398,091
MtWARA	3,414,928	3,195,032,315	3,569,872	3,722,963,282
Musoma	6,500,625	2,595,585,907	6,484,529	3,106,769,854
Mwanza	28,143,030	23,110,801,495	29,138,375	26,762,495,979
Shinyanga	3,844,976	5,358,301,189	4,339,482	6,697,549,150
Singida	2,506,742	2,655,530,728	2,618,508	3,176,653,742
Songea	2,821,306	2,745,616,563	2,862,762	3,212,818,561
Sumbawanga	2,623,216	1,227,268,381	2,873,643	1,511,067,307
Tabora	4,935,898	4,065,238,488	5,249,105	4,789,917,115
Tanga	10,259,291	12,347,980,872	10,732,719	14,451,964,945
Mpanda	943,574	568,916,237	1,013,665	593,542,631
Bariadi	186,667	165,347,800	214,128	182,050,541
Njombe	1,184,152	954,726,211	1,263,582	993,794,522
Geita	1,412,883	649,172,951	1,744,633	1,624,701,489
Vwawa Mlowo	738,531	84,584,708	677,435	87,585,517
Jumla	338,195,847	246,053,020,570	345,907,580	306,565,625,092

Chanzo: Wizara ya Maji

MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI
Jedwali Na. 71

Mamlaka	Mahitaji ya Maji kwa Mwaka	Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa mwaka 2019
Arusha	38,420,000	81%
Dar es Salaam	207,970,000	85%
Babati	2,970,000	83%
Bukoba	4,780,000	85%
Dodoma	16,790,000	86%
Iringa	6,350,000	98%
Njombe	2,440,000	88%
Mpanda	3,590,000	75%
Kigoma	8,280,000	76%
Kahama	6,200,000	80%
Lindi	1,760,000	78%
Mbeya	21,900,000	80%
Morogoro	21,630,000	85%
Moshi	18,770,000	100%
Mtwara	5,170,000	85%
Musoma	6,760,000	88%
Mwanza	40,950,000	95%
Geita	5,730,000	82%
Bariadi	2,080,000	49%
Shinyanga	9,630,000	83%
Singida	4,310,000	80%
Songea	5,260,000	94%
Sumbawanga	4,830,000	88%
Tabora	10,740,000	92%
Tanga	11,870,000	100%
Vwawa - Mlowo	3,490,000	58%
Jumla	472,670,000	84%

Chanzo: Wizara ya Maji

SURA YA 19

ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA

Elimu ya Awali

368. Mwaka 2019, wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya awali walikuwa 1,429,169 ikilinganishwa na wanafunzi 1,422,868 mwaka 2018. Kati ya hao, wasichana walikuwa 706,547, sawa na asilimia 49.4 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 722,622. Ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi lilitokana na utekelezaji wa Sera ya elimumsingi bila ada. Aidha, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 1,334,992 mwaka 2019 ikilinganishwa na wanafunzi 1,334,726 mwaka 2018. Kati ya hao, wasichana walikuwa 660,127 sawa na asilimia 49.4 na wavulana walikuwa 674,865. Katika kipindi hicho, shule zisizo za Serikali zilikuwa na wanafunzi 94,177 ikilinganishwa na wanafunzi 88,142 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Mwaka 2019, mkoa wa Mwanza uliendelea kuwa na kiwango kikubwa cha uandikishaji wa wanafunzi cha asilimia 7.6 wakati mkoa wa Katavi ulikuwa na kiwango kidogo cha asilimia 1.3.

Elimu ya Msingi

369. Mwaka 2019, idadi ya shule za msingi ilikuwa 17,804 ikilinganishwa na shule 17,562 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 16,223 ikilinganishwa na shule 16,149 mwaka 2018. Ongezeko la shule za msingi lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuhakikisha uwepo wa shule ya msingi katika kila kata. Aidha, idadi ya shule zisizo za Serikali iliongezeka kwa asilimia 11.9 na kufikia 1,581 mwaka 2019 kutoka shule 1,413 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya elimu.

370. Mwaka 2019, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi ilikuwa 10,605,430 ikilinganishwa na wanafunzi 10,111,671 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Kati ya hao, wasichana walikuwa 5,304,648 na wavulana walikuwa 5,300,782 ikilinganishwa na wasichana 5,065,100 na wavulana 5,046,571 mwaka 2018. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka kwa asilimia 4.7 na kufikia wanafunzi 10,174,237 mwaka 2019 kutoka wanafunzi 9,717,309 mwaka 2018. Hii ilitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ugharamiaji wa elimu ya msingi bila ada

pamoja na ujenzi wa miundombinu kama vile madarasa na vyoo. Vile vile, Serikali iliendelea kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo ya nchi kwa kuhakikisha wanafunzi wanaotakiwa kuwa shuleni wanakuwa shuleni wakati wa masomo.

371. Mwaka 2019, watahiniwa 933,369 walifanya mtihani wa darasa la saba ambapo watahiniwa 759,737 walifaalu (wasichana 395,738 na wavulana 363,999), sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 81.40 ya watahiniwa wote ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 77.7 mwaka 2018.

Elimu ya Sekondari

372. Mwaka 2019, idadi ya shule za sekondari ilikuwa 5,001 ikilinganishwa na shule 4,883 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kati ya hizo, shule 3,742 zilikuwa za Serikali na shule 1,259 zisizo za Serikali. Aidha, wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita walikuwa 2,338,457 ikilinganishwa na wanafunzi 2,148,466 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Katika kipindi hicho, wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne walikuwa 2,185,037 ikilinganishwa na wanafunzi 1,991,021 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa Sera ya Elimumsingi bila Ada iliyowezesha wanafunzi wengi kujiunga na elimu ya sekondari.

373. Mwaka 2019, watahiniwa 473,755 walifanya mtihani wa kidato cha nne ikilinganishwa na watahiniwa 358,427 mwaka 2018. Kati ya hao, watahiniwa 371,301 walifaalu (wanawake 192,037 na wanaume 179,264), sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 78.4. Aidha, watahiniwa 91,001 walifanya mtihani wa kidato cha sita mwaka 2019 ikilinganishwa na watahiniwa 62,233 mwaka 2018, kati ya hao watahiniwa 88,069 walifaalu (wanawake 37,219 na wanaume 50,850), sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 96.8.

Elimu katika Vyuo vya Ualimu

374. Mwaka 2018/19, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu ilikuwa 23,396 ikilinganishwa na wanachuo 20,962 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Kati ya hao, wanawake walikuwa 7,081 na wanaume walikuwa 16,315. Kuongezeka kwa idadi ya wanachuo kulitokana na: ujenzi na ukarabati wa vyuo vya ualimu; uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA; na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara za sayansi.

Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu

375. Mwaka 2018/19, Serikali iliendelea kufanya ukaguzi katika taasisi za elimu ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakuwa na ubora na viwango vinavyostahili. Katika kipindi hicho, jumla ya taasisi 8,966 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 11,870 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 24.5. Upungufu huu ulichangiwa na uwepo wa wathibiti ubora wachache na hivyo ukaguzi kufanyika kwenye taasisi zenye changamoto ya uzingatiaji wa miongozo ya utoaji elimu. Aidha, idadi ya taasisi za elimu zilizokaguliwa mwaka 2018/19 ni sawa na asilimia 79.2 ya lengo la mwaka la kukagua taasisi 11,327. **Jedwali Na. 19.1** linaonesha mchanganuo wa taasisi zilizokaguliwa mwaka 2018/19.

Jedwali 19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu mwaka 2018/19

Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo	Idadi iliyolengwa kukaguliwa (2018/19)	Idadi halisi iliyokaguliwa (2018/19)	Kiwango cha utekelezaji (Asilimia ya idadi iliyokaguliwa)
Shule za Awali na Msingi	8,785	7,288	83
Shule/Vituo vya Elimu Maalum	-	197	
Shule za Sekondari	2,480	1,436	58
Vyuo vya Ualimu	62	45	73
Jumla	11,327	8,966	79.2

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Elimu ya Ufundzi na Mafunzo

376. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundzi na mafunzo ilipungua hadi wanafunzi 113,427 mwaka 2018/19 kutoka wanafunzi 128,940 mwaka 2017/18. Kati ya hao, wanawake walikuwa 56,052, sawa na asilimia 49.4 na wanaume walikuwa 57,375. Kupungua kwa idadi ya wanafunzi kulitokana na kusitishwa kwa baadhi ya programu.

Elimu ya Ufundzi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

377. Mwaka 2018/19, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundzi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi ilikuwa 226,767 ikilinganishwa na wanafunzi 119,184 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 90.3. Kati ya hao, wanawake walikuwa 104,693 (asilimia 46.2) na wanaume walikuwa 122,074.

Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa na kuboreshwa kwa programu zinazoendana na soko la ajira. Aidha, Serikali iliendelea kufanya upanuzi na ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya wananchi ambapo vyuo 20 vilikarabatiwa mwaka 2018/19 na kufanya idadi ya vyuo vilivyokarabatiwa kufikia 40 kati ya vyuo 54.

Elimu ya Juu

378. Mwaka 2018/19, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu nchini ilikuwa 181,897 ikilinganishwa na wanafunzi 230,339 mwaka 2017/18, sawa na upungufu wa asilimia 21.0. Kati ya hao, wanawake walikuwa 73,242 (asilimia 40.3) na wanaume walikuwa 108,655. Upungufu huo ultokana na baadhi ya programu kusitishwa katika baadhi ya vyuo kwa kutokidhi vigezo na viwango vya utoaji wa elimu ya juu vilivyowekwa na Tume ya Vyuo Vikuu.

379. Mwaka 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliendelea kuratibu utoaji wa mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 450 kwa wanafunzi 132,030. Kati ya wanufaika hao, wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa 49,710 ambapo wanafunzi yatima walikuwa 1,344, wenye mzazi mmoja 9,049, wenye ulemavu 415 na kutoka kaya maskini 38,902. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ilipanga kukusanya shilingi bilioni 221.5 mwaka 2019/20 kutoka kwa wanufaika ambapo hadi Machi 2020, shilingi bilioni 144.3 zilikuwa zimekusanywa.

Teknolojia na Ubunifu

380. Mwaka 2019, Serikali iliendelea na juhudhi za kujenga uwezo na kuongeza rasilimali watu katika sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Katika kipindi hicho, wanafunzi 602 (wanaume 402 na wanawake 200) walidahiliwa katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (Arusha) ikilinganishwa na wanafunzi 486 (wanaume 328 na wanawake 158) mwaka 2018. Wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya walikuwa 5,320 (wanaume 4,199 na wanawake 1,121) ikilinganishwa na wanafunzi 4,630 (wanaume 3,746 na wanawanke 884) mwaka 2018. Aidha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi wapya 1,951 (wanaume 1,318 na wanawake 633) mwaka 2019 ikilinganishwa na wanafunzi 1,499 (wanaume 1,203 na wanawake 296) mwaka 2018. Kwa upande mwingine, Serikali ilianzisha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuchochea

ubunifu na ugunduzi nchini ambapo wabunifu na wagunduzi 415 walitambuliwa. Kati ya hao, wabunifu na wagunduzi 60 waliendelezwa ili kufikia hatua ya ubiasharishaji. Vile vile, Serikali ilianzisha kituo cha ubunifu na ujasiriamali katika fani ya TEHAMA katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO							(Namba)
Jedwali Na. 72	I	II	III	IV	V	VI	
Mwaka							Jumla
2001	47,204	45,078	30,531	29,188	7,198	6,601	165,800
2002	56,101	50,371	36,989	29,045	7,711	7,126	187,343
2003	52,863	60,643	36,906	35,653	7,780	6,885	200,730
2004	98,738	67,294	46,546	36,385	8,353	7,572	264,888
2005	134,963	109,398	46,188	46,489	9,710	8,444	355,192
2006	196,391	151,448	72,167	42,584	18,211	9,691	490,492
2007	401,011	218,060	105,770	70,796	21,789	11,668	829,094
2008	395,930	332,393	175,353	95,214	25,240	11,743	1,035,873
2009	480,529	308,131	159,789	167,355	31,201	12,695	1,159,700
2010	382,207	398,870	293,519	279,995	26,065	20,674	1,401,330
2011	403,873	396,724	380,528	279,117	30,265	25,164	1,515,671
2012	457,321	386,250	355,740	343,376	31,206	28,859	1,602,752
2013	444,532	506,036	193,901	302,963	30,581	26,698	1,504,711
2014	479,089	506,170	356,787	178,246	33,619	26,899	1,580,810
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	467,982	366,396	263,981	278,690	45,533	47,007	1,469,589
2017	491,535	443,614	296,034	236,775	53,749	43,494	1,565,201
2018	587,186	480,327	358,960	278,239	57,287	52,687	1,814,686
2019	637,335	555,087	388,029	334,284	52,428	56,042	2,023,205
Badiliko (%)							
2018 - 2019	8.5	15.6	8.1	20.1	-8.5	6.4	11.5

Chanzo: Wizara ya Elimu,Sayansi naTeknolojia

IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali Na.72A

	2018			2019		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
Elimu ya msingi						
Jumla ya wanafunzi wate walioandikishwa Darasa la I-VII	5,046,571	5,065,100	10,111,671	5,304,782	5,304,648	10,605,430
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa	4,848,367	4,868,942	9,717,309	5,084,434	5,089,803	10,174,237
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa	198,204	196,158	394,362	216,348	214,845	431,193
Jumla ya walimu katika shule za msingi	-	-	-			192,889
Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali	-	-	-			173,851
Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi	-	-	-			19,038
Elimu ya Sekondari						
Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI	1,056,498	1,091,968	2,148,466	1,133,088	1,205,369	2,338,457
Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-V	894,647	920,039	1,814,686	982,220	1,040,985	2,023,205
Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI	161,851	171,929	333,780	150,868	164,384	315,252
Idadi ya walimu katika shule za Serikali	-	-	-			84,106
Idadi ya walimu katika shule za binafsi	-	-	-			21,140
Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari	-	-	-			105,246

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali Na. 72B

Aina ya Taasisi	2018			2019		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Shule za Msingi	16,109	1,065	17,174	16,223	1,581	17,804
Shule za Sekondari	3,614	1,145	4,759	3,742	1,259	5,001
Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari)	-	-	-	-	-	-
Elimu ya Ufundu na Mafunzo	-	-	-	-	-	-
Jumla	19,723	2,210	21,933	19,965	2,840	22,805

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu hazikupatikana

MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

Jedwali Na. 72C

Aina	Mwaka wa Kwanza			Mwaka wa Pili			Jumla		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Masomo ya Art									
Cheti (pre services)	2,206	1,397	3,603	822	492	1,314	3,028	1,889	4,917
Astashahada(in services)	286	198	484	786	445	1,231	1,072	643	1,715
Astashahada(pre services)	1,421	715	2,136	2,822	1,513	4,335	4,243	2,228	6,471
Masomo ya Sayansi									
Cheti (pre services)	164	115	279	-	-	-	164	115	279
Astashahada(in services)	175	112	287	423	243	666	598	355	953
Astashahada(pre services)	4,558	1,089	5,647	2,051	756	2,807	6,609	1,845	8,454
Elimu Maalum									
Astashahada(pre services)	60	41	101	299	207	506	359	248	607
Jumla	8,870	3,667	12,537	7,203	3,656	10,859	16,073	7,323	23,396

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

IDADI YA WANAFUNZI WANAOSOMA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA JINSI KWA MWAKA 2019

Jedwali Na. 72D

Jina la Chuo	Idadi ya Wanafunzi			Idadi ya Walimu		
	Ke	Me	Jumla	Ke	Me	Jumla
UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM (UDSM)	4534	5940	10474	305	832	1137
IRINGA UNIVERSITY	1160	1349	2509	29	80	109
MKWAWA UNIVERSITY OF COLLEGE EDUCATION	1014	1651	2665	52	118	170
UNIVERSITY OF DODOMA INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING (MIPANGO)	3975	4128	8103	35	92	127
MADINI INSTITUTE- DODOMA	124	30	154	6	45	51
DODOMA UNIVERSITY (UDOM)	4768	6959	11727	225	595	820
ARUSHA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY	835	789	1624	21	84	105
ARUSHA UNIVERSITY	482	628	1110	18	51	69
ARUSHA TECHNICAL COLLEGE	524	2174	2698	14	88	102
ST. JOHN UNIVERSITY OF TANZANIA	309	500	809	70	37	107
LOCAL GOVERNMENT TRAINING INSTITUTE (LGTI)	2198	1244	3442	22	65	87
KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL UNIVERSITY COLLEGE (KCMC)	220	123	343	70	110	180
CENTRE FOR EDUCATION DEVELOPMENT IN HEALTH ARUSHA (CEDHA)	36	71	107	6	10	16
LIVESTOCK TRAINING (LITA TENTERU)	164	260	424	7	21	28
HORTICULTURE RESEARCH AND TRAINING INSTITUTE (TENTERU)	14	31	45	5	10	15
ST. AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA-ARUSHA BRANCH	147	162	309	13	26	39
TENTERU INSTITUTE OF COMMUNITY DEVELOPMENT (TICD)	840	328	1168	13	28	41
TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA	396	396	792	21	41	62
NELSON MANDELA AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	31	75	106	28	44	72
SEBASTIAN KOLOWA UNIVERSITY	-	-	-	11	18	29
THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA	5340	9015	14355	111	212	323
JUMLA	27111	35853	62964	1082	2607	3689

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Takwimu hazikupatikana

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 73

(Namba)

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2001	36,305	30,820	25,004	20,762	5,892	5,116	123,899
2002	41,593	34,209	27,540	20,681	6,418	5,534	135,975
2003	46,891	38,506	26,385	21,650	6,430	4,859	144,721
2004	48,752	46,167	33,240	24,476	8,847	6,229	167,711
2005	45,276	46,321	32,063	29,248	9,183	7,046	169,137
2006	46,968	48,013	42,878	29,796	9,569	7,956	185,180
2007	47,437	46,927	41,340	35,746	11,299	8,667	191,416
2008	42,971	43,232	43,177	35,980	12,576	8,594	186,530
2009	44,255	36,384	37,064	34,061	11,851	9,096	172,711
2010	56,620	57,876	50,778	46,820	12,269	13,006	237,369
2011	63,282	67,205	65,859	54,521	11,083	11,926	273,876
2012	65,058	69,403	64,453	61,209	9,684	11,713	281,520
2013	70,060	77,407	67,998	65,637	8,592	9,651	299,345
2014	109,784	96,732	76,574	66,898	8,865	7,686	366,539
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	70,844	81,499	72,970	73,231	21,091	17,731	337,366
2017	71,160	79,548	77,168	72,056	24,146	19,578	343,656
2018	64,844	71,685	74,932	74,848	24,030	23,441	333,780
2019	63,629	64,488	68,064	74,121	22,050	22,900	315,252
Badiliko (%)							
2018 - 2019	-1.9	-10.0	-9.2	-1.0	-8.2	-2.3	-5.6

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 20

AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

AFYA

Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

381. Serikali iliendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ambapo mwaka 2019 vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka na kufikia 9,104 kutoka vituo 8,119 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Kati ya hivyo, hospitali, zahanati na vituo vya afya vilikuwa 8,446 mwaka 2019 ikilinganishwa na hospitali, zahanati na vituo vya afya 7,819 mwaka 2018. Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya lilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji wa Serikali, mashirika ya dini na sekta binafsi katika ujenzi wa hospitali na vituo vya afya. Aidha, Serikali ilikuwa inamiliki asilimia 64.2 ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya, mashirika ya dini asilimia 17.5 na vituo binafsi asilimia 18.3. Vile vile, hospitali ziliikuwa asilimia 3.2, vituo vya afya asilimia 10.0 na zahanati asilimia 79.5.

382. Mwaka 2019, wagonjwa wa nje waliongezeka kwa asilimia 15.0 na kufikia 47,197,905 ikilinganishwa na wagonjwa 41,052,012 mwaka 2018. Aidha, wagonjwa wa kulazwa walifikia 1,852,720 ikilinganishwa na wagonjwa 1,359,264 mwaka 2018. Kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa waliohudumiwa kulichangiwa na Serikali kuendelea kujenga na kukarabati hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati pamoja na kuboresha mazingira ya utoaji huduma za afya na kuhamasisha matumizi ya bima za afya. Kwa upande mwingine, idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka na kufikia 80,164 mwaka 2019 ikilinganishwa na vitanda 61,203 mwaka 2018.

Huduma za Afya kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja

383. Watoto 1,794,856 walizaliwa mwaka 2019 ikilinganishwa na watoto 1,568,832 mwaka 2018. Watoto hao walipata huduma za chanjo ili kuzuia magonjwa ya kupooza, kuharisha, pepopunda, pneumonia, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, surua, polio na dondakoo. Chanjo zilizotolewa ziliijumuisha OPV ambayo ilichanjwa kwa asilimia 103.9, PENTA 3 asilimia 98, PV3 asilimia 99 na Rota2 asilimia 97.5. Kutokana na ufanisi wa utoaji wa chanjo hizo, Tanzania

iliweza kukidhi vigezo vya Shirika la Afya Duniani vinavyotaka kuhakikisha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watoto wanapata chanjo zote.

Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

384. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi hicho, upatikanaji wa dawa muhimu zinazofuatiliwa (tracer medicine) katika vituo vya kutolea huduma za afya uliendelea kuwa asilimia 94.4 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Aidha, hali ya upatikanaji wa aina 312 za dawa muhimu na za kipaumbele ilifikia asilimia 84 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 76 mwaka 2018.

385. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za uchunguzi katika Hospitali za Rufaa kwa kununua vifaa tiba. Vifaa hivyo vilijumuisha: kifaa cha MRI kilichopelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili; CT-Scan, MRI, digital X-ray na Ultrasound (Taasisi ya Mifupa Muhimbili); CT-Scan na MRI (Hospitali ya KCMC); na CT-scan, Digital X-ray na Ultrasound (Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya). Aidha, Serikali ilinunua mashine za X-ray za kidigitali nane (8) zilizopelekwa katika hospitali za rufaa za mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Singida, Njombe, Kagera, Dar es Salaam (Amana) na Katavi.

Afyaya Uzazi na Mtoto

386. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhamasisha wajawazito kuanza huduma ya afya ya uzazi na mtoto kabla ya majuma 12 ya ujauzito na kuhudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito. Katika kipindi hicho, wajawazito 2,320,559 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,260,120 mwaka 2018. Aidha, asilimia 34 ya wajawazito walifanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 28 mwaka 2018. Wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne waliongezeka kutoka asilimia 63.7 mwaka 2018 hadi asilimia 80.4 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, huduma ya kumkinga mama mjamzito dhidi ya malaria iliimarika ambapo asilimia 83.7 ya wajawazito walipatiwa kinga mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 81.1 mwaka 2018. Mwaka 2019, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi Vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 99 ikilinganishwa na asilimia 97.2 mwaka 2018. Kati ya wajawazito waliopima VVU, asilimia 3.7 waligundulika kuwa na

VVU na asilimia 99.2 ya waliogundulika na VVU walianzishiwa matibabu ya ART (Antiretoviral therapy).

387. Mwaka 2019, vituo 352 vya kutoa huduma ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni vilikarabatiwa ikilinganishwa na vituo 304 mwaka 2018. Kati ya hivyo, vituo vya afya vilikuwa 304, zahanati 39 na hospitali 9. Katika kipindi hicho, vifaa tiba vilisambazwa katika vituo vya afya 100 vinavyotoa huduma ya dharura ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Aidha, vituo vya uchunguzi na tiba ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi viliongezeka na kufikia 176 mwaka 2019 ikilinganishwa na vituo 108 mwaka 2018.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa

388. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, hospitali maalumu na hospitali za rufaa za kanda na hivyo kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Huduma zilizotolewa zilijumuisha upandikizaji wa figo, upasuaji wa moyo na mishipa ya fahamu, ubadilishaji wa nyonga, upandikizaji wa vifaa vya usikivu na tiba ya saratani. Aidha, wagonjwa saba (7) walipandikizwa figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na wagonjwa nane (8) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na hivyo kuendelea kuipunguzia Serikali gharama za upandikizaji wa figo nje ya nchi.

389. Mwaka 2019, Taasisi ya Tiba ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilihudumia wagonjwa 57,453 ikiwemo wagonjwa 289 waliofanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo na wagonjwa 610 waliofanyiwa upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo. Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) ilihudumia wagonjwa 138,583 ikiwemo wagonjwa 101 waliobadilishwa nyonga, wagonjwa 106 waliofanyiwa upasuaji wa kichwa na wagonjwa 276 waliofanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo. Aidha, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ilihudumia wagonjwa 118,204 mwaka 2019 kwa kutumia mashine za kisasa za LINAC na Gamma Camera. Matumizi ya mashine hizo yalipunguza wastani wa muda wa mgonjwa kusubiri huduma ya tiba ya saratani kwa njia ya mionzi kutoka wiki 12 mwaka 2018 hadi wiki 4 mwaka 2019.

390. Mwaka 2019, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilitoa huduma ya upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto tisa (9) na kufanya jumla ya watoto 30 kunufaika tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo. Kutolewa kwa huduma hiyo

nchini kumeipunguzia Serikali gharama za upandikizaji wa vifaa hivyo nje ya nchi kutoka wastani wa shilingi milioni 100 na kufikia wastani wa shilingi milioni 40. Aidha, wagonjwa 133 walipata huduma za tiba ya radiolojia (interventional radiology) ili kuruhusu upasuaji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingo, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziba, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo.

Udhibiti wa Malaria

391. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa vipimo vya malaria vinapatiwana katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi hicho, vipimo 25,699,500 vya vitendanishi vya malaria, dozi 10,668,600 za dawa ya mseto na vichupa 1,205,876 vya dawa ya malaria ya sindano vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vipimo 23,545,575, dozi 8,662,590 na vichupa 891,862 mwaka 2018. Aidha, vyandarua 3,266,260 vilinunuliwa na kusambazwa ikilinganishwa na vyandarua 3,286,774 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, kiwango cha ugonjwa wa malaria kwa watoto chini ya miaka mitano mwaka 2019 kilikuwa asilimia 7.3 kama ilivyokuwa mwaka 2018 na kwa wajawazito kilikuwa asilimia 6.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.6 mwaka 2018. Vile vile, Serikali iliendelea kudhibiti malaria kwa kusambaza takribani lita 60,000 za viuadudu kupitia Bohari Kuu ya Dawa kwenye halmashauri za mikoa ya Lindi, Mtwara, Geita, Kigoma na Kagera ambazo zilikuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria. Utekelezaji wa afua hiyo ulisaidia kudhibiti magonjwa mengine yakiwemo homa ya dengue, zika, matende, homa ya manjano, chikungunya na homa ya bonde la ufa.

Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu

392. Mwaka 2019, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya iliendelea kuimarisha huduma za ugunduzi wa maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu kwa kuongeza mashine 28 za GeneXpert katika mikoa ya Pwani, Singida, Mbeya, Songwe, Dodoma na Manyara. Idadi hiyo inafanya jumla ya mashine za GeneXpert kufikia 238 mwaka 2019 ikilinganishwa na mashine 210 mwaka 2018. Mashine hizo ziliongeza ufanisi wa uchunguzi wa kifua kikuu kwa kupunguza muda wa kutoa majibu kutoka masaa 48 hadi masaa mawili. Aidha, vituo vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya kifua kikuu viliongezeka na kufikia 1,201 mwaka 2019 kutoka vituo 662 mwaka 2018. Vile vile, Serikali ilianzisha afua ya kuboresha huduma za kuzuia maambukizi ya kifua kikuu kwa kutoa

mafunzo kwa watumishi 1,326 wa magereza mbalimbali nchini mwaka 2019. Afua hiyo ilienda sambamba na uchunguzi wa kifua kikuu ambapo wafungwa 38 waligunduliwa kuwa na maambukizi na kuanzishiwa matibabu.

Lishe

393. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe (2016/17 - 2020/21) ili kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji mzuri wa mwili na akili kwa mtoto. Aidha, Serikali ilifanikisha utoaji wa matone ya Vitamini A na dawa za kutibu maambukizi ya minyoo kwa watoto walio chini ya miaka mitano ambapo zaidi ya asilimia 95 ya watoto milioni 8.5 walipatiwa matone ya Vitamini A na zaidi ya asilimia 95 ya watoto milioni 7.5 walipatiwa dawa za minyoo.

Mafunzo kwa Watumishi wa Kada ya Afya

394. Wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya walifikia 25,077 mwaka 2019 ikilinganishwa na wanafunzi 18,996 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 32.0. Ongezeko hilo lilitokana na upanuzi na ukarabati wa vyuo vya afya vya Serikali pamoja na uanzishwaji wa vyuo vypya vya afya vya binafsi. Kati ya hao, wanafunzi 5,682 walijiunga kwenye vyuo vya Serikali na wanafunzi 19,395 kwenye vyuo binafsi katika programu za uuguzi na ukunga, sayansi shirikishi za afya na wahudumu wa afya ya jamii.

MAENDELEO YA JAMII

Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

395. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyuo vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli. Wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya maendeleo ya jamii walikuwa 3,986 (wanawake 2,438 na wanaume 1,548) ikilinganishwa na wanafunzi 3,414 (wanawake 2,277 na wanaume 1,137) waliodahiliwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji wa miundombinu ya vyuo ikiwemo madarasa na mabweni. Aidha, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ilianzisha kituo cha kidigitali cha utafiti wa kijamii kwa lengo la kuibua na kuboresha vipaji na ubunifu utakaoweza kutatua changamoto zilizoko katika jamii hususan ukosefu wa ajira kwa vijana. Vile vile, Taasisi ilidahili wanafunzi 1,971 (wanawake 1,350 na wanaume 621)

ikilinganishwa na wanafunzi 1,183 (wanawake 827 na wanaume 356) waliodahiliwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 66.6. Ongezeko hili lilitokana na uboreshaji wa miundombinu katika taasisi hiyo ikiwemo ukarabati wa karakana ya ufundi seremala, mabomba ya maji safi, ofisi ya kituo cha ubunifu, miundombinu ya umeme na miundombinu ya TEHAMA.

396. Mwaka 2019, Serikali kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama iliendelea kutoa mafunzo ya ustawi wa jamii katika ngazi ya astashahada, stashahada, shahada, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamili. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,799 (wanawake 1,275 na wanaume 524) walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 1,064 (wanawake 614 na wanaume 450) mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 69.1. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii ikiwemo ujenzi wa maktaba ya kisasa. Aidha, Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara kilidahili wanafunzi 169 (wanawake 123 na wanaume 46) mwaka 2019 ikilinganishwa na wanafunzi 158 (wanawake 115 na wanaume 43) mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Wanafunzi hao walidahiliwa katika ngazi za astashahada na stashahada na kupatiwa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Maendeleo ya Wanawake

397. Mwaka 2019, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kuweka mazingira wezeshi katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa ili kuleta usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake nchini. Katika kipindi hicho, wanawake wajasiriamali 11,833 kutoka mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Songwe, Dodoma, Iringa, Kigoma, Kagera, Mtwara, Singida, Simiyu, Pwani, Manyara, Dar es Salaam na Tanga walishiriki katika maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ikilinganishwa na wanawake 1,286 walioshiriki mwaka 2018. Maonesho hayo yaliwawezesha wanawake wajasiriamali kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha bidhaa na kupata uzoefu kuhusu upatikanaji wa masoko.

398. Serikali kupitia Benki ya Posta Tanzania katika Dirisha la Wanawake iliendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wanawake. Jumla ya shilingi bilioni 3.58 zilitolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.05 zilizotolewa kwa wanawake wajasiriamali

3,035 mwaka 2018. Aidha, wajasiriamali 718 (wanawake 334 na wanaume 384) kutoka katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Geita na Dodoma walipatiwa mafunzo ya uongezaji thamani wa bidhaa, uwekezaji na uratibu wa masuala ya fedha.

399. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa wahanga wa ukatili wa kijinsia wanapata huduma kwa kuanzisha madawati ya kijinsia. Katika kipindi hicho, Jeshi la Magereza lilianzisha madawati ya jinsia 162 ili kuhakikisha uwepo wa fursa sawa za kijinsia pamoja na kupambana na vitendo vyta ukatili kwa wafungwa wakiwemo watoto walio kwenye magereza. Aidha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilianzisha dawati la jinsia mwaka 2019 kwa ajili ya kushughulikia masuala ya rushwa ya ngono.

Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto

400. Mwaka 2019, watoto 114 (wasichana 58 na wavulana 56) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za kuasili na malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 54 (wasichana 30 na wavulana 24) mwaka 2018. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi na msaada wa kisheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Watoto 250 (wasichana 19 na wavulana 231) walio katika mkinzano na sheria walipata huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na elimu ikilinganishwa na watoto 354 (wasichana 34 na wavulana 320) mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 29.4. Upungufu huo ulitokana na juhudini za kuboresha malezi ya watoto kuitia afua mbalimbali ikiwemo uanzishwaji wa vikundi vyta malezi na utekelezaji wa programu ya marekebisho ya tabia kwa watoto walio katika mkinzano na sheria.

401. Mwaka 2019, watoto 148 (wasichana 59 na wavulana 89) walio katika mkinzano na sheria walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 64 (wasichana 7 na wavulana 57) waliochepushwa mwaka 2018. Aidha, watoto 32 (wasichana 2 na wavulana 30) walihukumiwa na kupelekwa katika shule ya maadilisho Irambo (Mbeya) ikilinganishwa na watoto 30 mwaka 2018. Vile vile, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanapata huduma za msingi zikiwemo chakula, mavazi, malazi, elimu na afya katika makao ya watoto. Mwaka 2019, makao 72 ya watoto yalisajiliwa na kufanya jumla ya makao ya watoto kufikia 213. Watoto 15,365 (wasichana 7,095

na wavulana 8,270) walio katika mazingira hatarishi walipatiwa huduma za msingi katika makao ya watoto ikilinganishwa na watoto 13,420 (wasichana 6,651 na wavulana 6,769) mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Kati ya hao, watoto 75 (wasichana 42 na wavulana 33) walipata huduma katika makao ya watoto ya Taifa yaliyopo Kurasini (Dar es Salaam).

Huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

402. Mwaka 2019, watoto wenyе umri chini ya miaka mitano waliendelea kupata huduma za malezi na makuzi kupitia vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Katika kipindi hicho, vituo 373 vya kulelea watoto wadogo mchana vilisajiliwa na kufanya idadi ya vituo vilivyosajiliwa nchini kufikia 1,543. Idadi ya watoto walioandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana iliongezeka kwa asilimia 7.0 na kufikia watoto 159,479 (wasichana 82,539 na wavulana 76,940) mwaka 2019 ikilinganishwa na watoto 149,093 (wasichana 76,094 na wavulana 72,999) mwaka 2018. Aidha, idadi ya walezi wa watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana iliongezeka kutoka walezi 2,482 mwaka 2018 na kufikia walezi 2,563 mwaka 2019. Wanafunzi 748 walidahiliwa katika vyuo 21 vya Serikali na binafsi vinavyotoa mafunzo ya malezi ya watoto. Vile vile, Serikali iliendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi wa watoto kwa kuunda vikundi vya malezi chanya ambapo hadi Desemba 2019, vikundi 1,186 viliundwa.

Huduma za Ustawi kwa Wazee

403. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kuwezesha utoaji wa huduma za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza katika makazi 17 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali. Katika kipindi hicho, wazee 383 (wanawake 179 na wanaume 204) walipatiwa huduma za msingi katika makazi hayo ikilinganishwa na wazee 510 (wanawake 234 na wanaume 276) mwaka 2018. Katika kuhakikisha wazee walio katika mazingira hatarishi wanapata huduma za matibabu bila malipo, wazee 167,566 (wanawake 95,765 na wanaume 71,801) walipatiwa vitambulisho vya matibabu mwaka 2019 ikilinganishwa na wazee 247,771 (wanawake 160,043 na wanaume 87,728) mwaka 2018.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

404. Mwaka 2019, Serikali iliendelea kusajili mashirika yasiyo ya kiserikali kulingana na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 na mwaka 2019. Katika kipindi hicho,

mashirika yasiyo ya kiserikali 1,402 yalisajiliwa ikilinganishwa na mashirika 516 mwaka 2018. Kuongezeka kwa usajili kulitokana na utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002 na mabadiliko yake ya mwaka 2019 ambayo yanaelekeza mashirika yote yanayofanya kazi za kijamii pamoja na mashirika yaliyosajiliwa katika sheria nyingine kujisajili chini ya Sheria hiyo. Kati ya mashirika yaliyosajiliwa, mashirika 133 yalisajiliwa katika ngazi ya kimataifa, mashirika 1,251 ngazi ya kitaifa, mashirika tisa (9) ngazi ya mkoa na mashirika tisa (9) ngazi ya wilaya.

IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 74

Aina ya Vituo	2016			2017			2018				2019			
	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Dini	Jumla	Binafsi	Serikali	Dini	Jumla
Zahanati	1,421	4,789	6,210	1,435	4,925	6,360	986	5,055	659	6,700	1,235	5,136	871	7,242
Vituo vya Afya	259	508	767	277	527	804	127	551	156	834	153	587	170	910
Hospitali	146	119	265	150	123	273	50	127	108	285	57	121	116	294
Nyinginezo*	39	15	54	182	8	190	225	21		246	168	4	434	606
Maternity/Nursing Homes			50	50	1	51	52	2		54	49	1	2	52
Jumla	1,865	5,431	7,346	2,094	5,584	7,678	1,440	5,756	923	8,119	1,662	5,849	1,593	9,104

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

* Ni pamoja na kliniki

IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 75

Mwaka	Wagonjwa wa Nje			Jumla ya Wagonjwa waliolazwa
	Hospitali	Zahanati	Vituo vya Afya	
1999	812,891	10,321,654	1,242,354	626,700
2000	989,101	13,697,988	1,874,346	626,700
2001	1,167,139	17,218,371	2,511,624	680,263
2002	1,328,395	19,695,356	3,258,520	701,568
2003	1,491,909	22,935,688	3,659,615	1,390,273
2004	1,532,028	23,552,460	3,758,027	2,125,388
2005	1,619,700	24,900,276	3,973,085	2,237,146
2006	1,754,925	26,979,136	4,304,787	2,837,252
2007	1,842,671	28,328,093	4,520,026	2,979,115
2008	1,934,805	29,744,498	4,746,027	3,128,071
2009	2,128,286	32,718,948	5,220,630	3,440,870
2010	2,341,114	35,990,843	5,742,693	3,784,957
2011	2,622,048	39,917,117	6,431,816	4,239,152
2012	2,815,529	41,333,522	6,657,817	4,388,108
2013	2,903,275	42,682,479	6,873,056	4,529,971
2014	5,910,725	14,008,692	475,295	1,665,935
2015	4,480,781	25,072,487	6,006,466	1,858,956
2016	4,984,645	20,859,281	6,515,219	1,775,835
2017	5,266,252	21,115,639	7,050,725	1,650,224
2018	4,675,045	27,473,506	8,903,461	1,359,264
2019	9,821,148	26,500,182	10,153,322	1,852,720

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI

Jedwali Na. 76

Aina ya Huduma	2018			Jumla	2019			Jumla
	Serikali	Shirika la Kujitolea/Dini	Binafsi		Serikali	Shirika la Kujitolea/Dini	Binafsi	
Hospital za Mkoa	7,523	0	0	7,523	6,692	1,033	480	8,205
Hospitali za Wilaya	6,802	6,750	0	13,552	9,919	6,154	2,911	18,984
Hospitali nyingine	336	2,889	710	3,935	1,420	6,865	1,108	9,393
Vituo vya Afya	9,794	3,868	2,205	15,867	15,221	5,373	3,674	24,268
Zahanati	13,602	4,160	3,564	21,326	11,818	4,979	2,517	19,314
Jumla	38,057	17,667	6,479	62,203	45,070	24,404	10,690	80,164

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto